

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Thelathini na Tano - Tarehe 30 Julai, 2003

(Mkutano Ulianiza Saa Tatuh Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Tume ya Taifa ya Mionzi pamoja na Hesabu Zilizokaguliwa kwa Mwaka 2000/2001 (*The Annual Report on the Activities of the National Radiation Commission and Audited Accounts for the Year 2000/2001*)

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu na Hesabu Zilizokaguliwa kwa Mwaka 2001/2002 (*The Annual Report on the Activities of the Higher Education Accreditation Council and Audited Accounts for the year 2001/2002*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2003/2004.

MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 339

**Watumishi Kukaa Kwenye Kituo Kimoja cha Kazi
kwa Muda Mrefu**

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA aliuliza:-

Kwa kuwa inaaminika kwamba mtumishi wa umma akikaa kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu hujisahau kutokana na kutawaliwa na mazingira ya aina moja; na kwa kuwa hali hiyo imejitokeza kwa baadhi ya watumishi kukaa kwenye kituo kimoja cha kazi kati ya miaka 10 hadi 25 au zaidi; na kwa kuwa hali hiyo huwa mbaya sana kiufanisi hasa pale ambapo mtumishi wa aina hiyo ndiye Mkuu wa Taasisi au Kituo husika:-

(a) Licha ya tatizo la fedha za uhamisho kuwa kikwazo kwa watumishi hao; je, Serikali haioni kwamba taratibu za utumishi zinakiukwa; na kuwa athari zake ni kubwa kiufanisi jambo ambalo husababisha kero na chuki mionganoni mwa watumishi na Jumuiya kwa ujumla?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kitendo hicho kinatoa upendeleo kwa baadhi ya watumishi na adhabu kwa wengine?

(c) Je, Serikali ina msimamo gani juu ya hali hiyo, ambayo sasa inawafanya watumishi wengine kukataa uhamisho wa kwenda kwenye sehemu nyingine?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi uhamisho wa watumishi wa umma kutoka kituo kimoja kwenda kingine hutawaliwa na kanuni, taratibu na sheria za kiutumishi. Kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Serikali Na. 1 wa mwaka 1978, muda wa chini kwa mtumishi kukaa katika kituo kimoja cha kazi ni miaka mitatu na muda wa juu ni miaka mitano. Hata hivyo, uamuzi huu hauna maana kwamba muda huu ukifika mtumishi anayehusika ni lazima ahame. Hivyo mtumishi kutohamishwa kwa msingi wa muda haukiuki taratibu. Pamoja na muda uhamisho wa watumishi uzingatie pia vigezo ifuatavyo, umuhimu wa kazi, kuwepo fedha za kugharamia uhamisho, kuwepo nafasi wazi kwenye kituo kipyaa, kuwepo kwa mtumishi mbadala kwenye kituo anachohama mtumishi na kuwepo kwa manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, si mara zote mtumishi kukaa katika kituo kimoja cha kazi kunasababisha kero na chuki mionganoni mwa watumishi na jumuiya kwa ujumla. Kiini cha kero hii kinaweza kuwa uongozi mbovu, uhaba wa raslimali, watumishi kutoridhika hivyo kusababisha tofauti za mahusiano kati ya mtu na mtu. Hata hivyo, pale ambapo inathibitika kuwa kukaa kwa muda mrefu kumesababisha mtumishi kuleta kero na chuki kwa wananchi, uhamisho hufanyika kwa manufaa ya pande zote zinazohusika.

(b) Mheshimiwa Spika, uhamisho siyo adhabu, ni moja ya hatua za kuimarisha menejimenti na utendaji wa watumishi ili kuongeza ufani. Ufinyu wa Bajeti ndilo tatizo kubwa katika kutekeleza uhamisho wa watumishi. Pale ambapo Bajeti inaruhusu uhamisho hutekelezwa kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zilizopo kama nilivyoeleza hapo juu.

(c) Mheshimiwa Spika, kadri hali ya Bajeti inavyozidi kuwa nzuri Serikali itaendelea kushughulikia uhamisho pale ambapo zipo sababu za msingi na kwa maslahi ya Taifa. Kiutaratibu uhamisho wowote wa kawaada unapaswa kutekelezwa katika kipindi cha siku kumi na nne tangu mtumishi anapopata barua ya uhamisho. Mtumishi yeoyote anayekataa uhamisho bila sababu ya msingi anapaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na msimamizi wake wa kazi mara baada ya muda huo kupita.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza, wapo watumishi ambaa ndani ya mwaka mmoja au miwili anahama kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine, anakaa siku mbili, tatu anahama, anakaa sehemu mwaka mmoja au miwili anahama na imekuwa kero sana kwake yeeye na familia yake na hata kwa watoto wanaosoma, lakini wakati huo huo kuna watumishi ambaa wanakaa miaka 10 mpaka 25, je, hawa wanaohama kila baada ya miwili au mitatu hela zinatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, ukishaweka kanuni kwamba ni kati ya miaka miwili mpaka mitano sasa inakuwa miaka 10 mpaka 25 mtu alikwenda hana mke anaoa, anazaa na watoto wanaolewa hapo, je, hiyo ndio kanuni uliyoiweka, unaiheshimu au unafanya mchezo tu na kazi? (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwamba kuna watumishi wengine huhamishwa baada ya muda mfupi kutoptana na vigezo vile vingine

ambavyo nimeviorodhesha katika majibu yangu ya msingi na inawezekana vile vile wengine wakaka miaka mingi kutokana na vigezo hivyo hivyo nilivyovisema kwa mfano, kwamba hakuna mtu mbadala atakayeletwa sehemu hiyo au hakuna nafasi ambayo anaweza akahamishiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la fedha ni kigezo muhimu kwa sababu bila fedha huwezi kumhamisha, lakini vigezo vingine na mahitaji mengine ya uhamisho vile vile ni muhimu. Ila nimesema kwamba pale ambapo inatokea mtumishi anakuwa kero, Serikali imekuwa ikiwahamisha wale ambao wanaleta kero na kwa hiyo suala la fedha haliwezi likawa kigezo peke yake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali ndiyo iliyoweka kupitia Waraka wake, utaratibu wa kati ya miaka mitatu na miaka mitano. Lakini napenda kurudia tena kusema kwamba, kigezo cha muda siyo peke yake, nimeorodhesha vigezo vingine. Lakini napenda kusema kwamba kwa kadri hali ya fedha na makusanyo ya Serikali yanavyokuwa bora, basi uhamisho utafuata taratibu hizi ambazo zimewekwa ikiwa ni pamoja na huo muda ambao nimeuelezea. (*Makofsi*)

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba wafanyakazi wanapokaa mahali pamoja hujilimbikizia mali, mashamba na ufugaji wa ng'ombe wengi na kusahau kazi; je, hili wameliona? (*Makofsi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwa watumishi wenyewe fursa kuweza kujijengea maisha mazuri na inawezekana kabisa vile vile kuna wengine ambao wanakosa fursa, wakawa hawana nafasi ya kujijengea maisha mazuri na kwa hiyo, napenda kurudia kusema tena kwamba, pale ambapo mtumishi anakuwa kero mahala pake pa kazi na pale ambapo panakuwa na nafasi ya kumhamishia, tunapopata taarifa na kwa kutumia utaratibu wetu wa Serikali kujua kwamba utumishi wake hauwi wa ufanisi pale, Serikali itachukua hatua mara moja kwa kadri inavyowezekana.

Na. 340

Mkataba wa Huduma kwa Mteja

MHE. MARIA D. WATONDOHA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilizindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja katika Mkutano wa Tisa wa Bunge; na kwa kuwa uzinduzi huo umewapa ari watumishi na wananchi ambao wanategemea kwamba huduma itakuwa ya haraka na ya uhakika:-

(a) Je, watumishi wa Idara mbalimbali za Serikali walishirikishwa vipi katika kuandaa Mkataba wa Idara zao?

(b) Kama hawakushirikishwa, je, wanaandaliwa vipi kuufahamu Mkataba vizuri?

(c) Je, Serikali imefanya tathmini ya awali katika miezi mitatu ya kwanza kuona ufanisi wa utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu sehemu (a) na (b) kwa pamoja.

(a) Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Idara mbalimbali za Serikali walishirikishwa kikamilifu katika kuandaa Mikataba ya Idara zao kwa njia ya kuwa na mikutano na warsha. Warsha hizo zililhusu mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kupokea hii dhana ambayo ni mpya, kuwaelimisha

juu ya nadharia ya Mkataba wa kazi kwa mteja, kuainisha maeneo ya kuwasiliana na mteja na kutamka wenyewe ubora na muda wa kutoa huduma kwa mteja.

Aidha, watumishi walipata fursa ya kuwashirikisha baadhi ya wateja wao katika maandalizi ya mikataba ya huduma kwa mteja ili kuafikiana ubora na muda wa kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya ushirikishwaji wa pande hizi mbili, mto huduma na mpokeaji, ni kusaidia kuainisha maeneo ya kuboresha katika huduma inayotolewa siku hadi siku.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hatujafanya tathmini ya awali katika miezi mitatu ya mwanzo. Sababu za msingi ni tatu. Kwanza, kufanya tathmini katika muda mfupi namna hiyo ni ghali sana kwa Serikali. Pili, baadhi ya mihadi iliyowekwa inachukuwa zaidi ya miezi mitatu kuona matokeo na mwisho, kulingana na dhana hii ya Mkataba wa huduma kwa mteja, tathmini inashauriwa ifanyike kila mwaka mara moja ili kuhakikisha kuwa watumishi wawe wamepata uzoefu wa kutosha katika kuwasiliana na kupokea malalamiko ya wateja ili kubaini eneo la kuboresha. Nia ni kuboresha kazi siku hadi siku ili huduma zitolewazo na watumishi ziwe bora kwa wananchi.

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa kuwa baadhi ya huduma zimedhihirika kwamba hazitekelezeki kwa mfano, kuna walimu wameajiriwa na wana zaidi ya mwaka hawajalipwa mshahara, je, Serikali inasema nini juu ya hilo wakati walimu wanafanya kazi na wanahitaji kuishi?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa baadhi ya wafanyakazi wako Vijijini na hawa nao wana wateja ambaa wanawapa huduma hizo, wafanyakazi walio katika ngazi ya Kata na Tarafa walishirikishwa vipi ili wafahamu wajibu wao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Huduma kwa Wateja hauwahuwananchi peke yao, unahusu vile vile kero za watumishi na kwa hiyo, Mkataba huu unawapa fursa watumishi wa Serikali, pale ambapo wana kero ambazo zinakwamisha ufanisi wao wa kazi, waweze kutoa kero hizo na yule anayehusika achukue hatua thabiti ili huduma ziwe bora.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa walimu ambaa hawajalipwa kwa mwaka, basi anayehusika anapaswa kuhakikisha kwamba walimu hao wamelipwa ili waweze kutenda kazi zao vizuri na watoe huduma kama inavyotegemewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la pili la Mheshimiwa Maria Watondoha, katika kuwahamasisha na kuwaelimisha watumishi hakuna ngazi ambayo imeachwa, ngazi zote zimeshirikishwa ikiwa ni pamoja na ngazi za Vijijini, Kata, Tarafa na Wilaya. Ni kazi ya sekta husika kwa kushirikiana na utumishi kuhakikisha kwamba watumishi wote wameelewa dhana hii na kwamba tunaingiza sasa demokrasia ndani ya utumishi wa umma ili wananchi waweze kusema kero zao pale ambapo hawatendewi ipasavyo na pale ambapo watumishi hawatendewi vile vile ipasavyo kama kutokuwa na nyenzo za kufanyia kazi, wamweleze msimamizi wao wa kazi ili hatua thabiti ichukuliwe na kwa nia moja niliyoisema katika jibu langu la msingi, kuboresha huduma kwa wananchi.

Na. 341

Misaada Inayotolewa kwa Tanzania

MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. DR. WILLBROD P. SLAA) aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania inasemekana kwamba ni moja kati ya nchi zilizopata misaada mingi sana katika Afrika; na kwa kuwa chini ya Mpango wa *HIPC* Tanzania imefutiwa/kusamehewa sehemu ya madeni yake:-

(a) Je, kuanzia mwaka 1990 Tanzania imepokea mikopo na misaada kiasi gani na kutoka nchi zipo?

(b) Je, mikopo au misaada hiyo ilikuwa kwa ajili ya miradi ipi na ni miradi mingapi kati ya hiyo imekamilika sasa au inategemea kukamilika lini?

(c) Baada ya kufutiwa madeni na nchi kadhaa rafiki; je, hadi sasa ni nchi ngapi zimetufutia madeni hadi tarehe 31 Desemba, 2002 na tumbakiwa na madeni ya shilingi ngapi hadi sasa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo mafupi kwamba ushirikiano wa nchi yetu na wahisani mbalimbali umekuwa mzuri tangu Tanzania ilipopata uhuru wake mwaka 1961. Mikopo na misaada tunayopata inatusaidia katika kutekeleza mipango yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mikopo na misaada hiyo imekuwa kichocheo katika kuleta maendeleo hapa nchini kwa kuchangia pale ambapo Serikali imeshindwa kufanya hivyo kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha. Pamoja na misaada ya wahisani hao, sote tunafahamu kuwa juhudzi za wananchi katika kujitafutia maendeleo ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kuanzia mwaka 1990 jumla ya misaada na mikopo iliyopatikana kwa miradi mbalimbali ya maendeleo inafikia dola za Kimarekani milioni 8,121.0 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 6,903. Kati ya hizo jumla ya dola za Kimarekani milioni 4,451.6 sawa na shilingi bilioni 3,784 ni mikopo.

(b) Mikopo na misaada hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 917 katika sekta mbalimbali za uchumi. Kati ya miradi hiyo, miradi 596 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 4,251.5 sawa na shilingi bilioni 3,614 imekamilika, miradi 321 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 3,869.5 sawa na shilingi bilioni 3,289 ipo katika hatua mbalimbali ya utekelezaji.

(c) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2001 jumla ya nchi 14 ambazo ni wanachama wa kundi la Paris (*Paris Club*) zilitoa misamaha ya madeni kwa Tanzania yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,305 sawa na shilingi bilioni 1,175.

Aidha, Tanzania imepata unafuu wa madeni yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,804 sawa na shilingi bilioni 2,383 kwa kuongezewa muda wa kulipa (*Re-scheduled Debt*). Nchi zilizotusamehe madeni ni pamoja na Canada, Brazil, Japan, Austria, Uhlanzi, Ubeligiji, Finland, Norway, Sweden, Ujeruman, Uingereza, Marekani, Ufaransa na Urusi. Tunategemea kufutiwa madeni pia na Italia ambapo Uswisi na Denmark zimesogeza mbele muda wa madeni kulipwa (*Re-scheduled Debt*). Aidha, Serikali inaendelea kuzungumza na nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris ili kutupunguzia madeni yao.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2001 deni la nje la Taifa ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 6,080 ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 5,168.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, baada ya kufutiwa madeni kwa kiasi gani tumeweza kupunguza Bajeti yetu kuwa tegemezi ambayo hivi sasa ni asilimia 47?

Mheshimiwa Spika, pili, ni vigezo gani vinavyotumika katika kutoa kipaumbele katika miradi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Bajeti yetu bado ni tegemezi kwa asilimia alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. Lakini niseme tu kwamba, msamaha ambao tumeupata umesaidia sana kuziba mapengo ambayo tulikuwa nayo katika makusanyo ya fedha za ndani.

Kiasi cha fedha tulizosamehewa jumla kama nilivyotaja ni Dola za Kimarekani bilioni tatu, lakini hizi hatuzipati kwa mara moja, kadri deni linavyoiva tunasamehewa. Katika kila mwaka kwa hiyo, tunapata ule msamaha ambao tulitakiwa tuzilipe fedha nje, fedha hizo kwa nchi na mashirika yanayotudai.

Kwa hiyo, tegemezi ya Bajeti katika uchumi wetu itaendelea kuwepo. Lakini ni dhana na dhamira ya Serikali kwamba tupunguze kadri miaka inavyokwenda na hiyo iko pia kwenye Bajeti ama kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ni nia thabiti ya Serikali kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele katika miradi inatokana na Bajeti ya Serikali na miradi mbalimbali ambayo inawasilishwa katika Bunge lako Tukufu. Baada ya Kamati mbalimbali kupitia miradi ya sekta ya Wizara mbalimbali hivyo ndiyo vipaumbele na wafadhili wanapitishia fedha zao kwenye Bajeti ya Serikali kupitia utaratibu wa *Tanzania Assistant Strategy (TAS)*. Kwa hiyo, vipaumbele vyote vinatokana na vinawekwa na Bunge lako Tukufu.

Na. 342

Mikopo Inayotolewa na *National Microfinance Bank*

MHE. KHALID S. SURU aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya 1994 Serikali ilianzisha Mifuko maalum kwa madhumuni ya kuwawezesha wananchi wa makundi mbalimbali kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi; na kwa kuwa Mifuko kama ule wa wafanyabiashara wa vijana na akina mama ni mionganoni mwa Mifuko maalum; na kwa kuwa *National Microfinance Bank* ambayo Serikali kwa makusudi ilianzisha Benki maalum kwa ajili ya kutoa mikopo midogo midogo kwa makundi hayo na wananchi wa kawaida kwa ujumla; na pia Serikali iliandaa sera maalum ya mitaji midogo (*Microfinance*) kwa wananchi wavuja jasho ili iwasaidee kuondokana na umaskini:-

(a) Je, *National Microfinance Bank* imewakopesha wananchi wavuja jasho kiasi gani cha fedha kuanzia mwaka 1998 hadi 2003?

(b) Je, ni Matawi yapi na mangapi huko Mikoani na Wilayani ambayo yametoa mikopo na ni mangapi hayakutoa mikopo na ni kwa nini?

(c) Je, iwapo Benki kama hiyo ikikosekana kwenye maeneo hususan ya Wilaya, ni athari gani zinazoweza kuwakumba wananchi; na kwa Sheria za Ubinafsishaji zinalenga katika kubinafsishwa kwa Taasisi zote za Umma?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Benki ya *National Microfinance* ilianza kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wananchi wenyewe kipato cha chini mwezi Agosti, 2000 katika Tawi la Barabara ya Kenyatta lililopo Jijini Mwanza. *NMB* imekuwa ikiongoza shughuli zake za mikopo kwa utaratibu wa kuandaa kwanza mazingira muhimu ambayo yatafanikisha ufuutiliaji wa mikopo hiyo midogo midogo. Maandalizi hayo ni pamoa na kuajiri wafanyakazi wenyewe ujuzi, kutoa mafunzo kwa watumishi,

kujenga mtaji na kadhalika. Hivyo, mpaka mwezi Machi, 2003, idadi ya mikopo midogo midogo iliyotolewa na *NMB* ilikuwa 24,941 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 14.18.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 25 Julai, 2003 jumla ya Matawi 58 ya *NMB* yalikuwa yanatoa mikopo katika Matawi 104 na Wakala (*Agencies*) wanne .

Matawi hayo ni *Clock Tower* (Arusha Mjini), Ilala, Kariakoo, *Bank House*, *Morogoro Road* na Muhimbili katika Wilaya ya Ilala, *Kenyatta Road*, Jijini Mwanza, Magomeni Wilaya ya Kinondoni, Nelson Mandela, Moshi Mjini, Temeke (Temeke), Wami (Morogoro Mjini), *Mbalizi Road* (Mbeya Mjini), Mkwawa (Iringa Mjini), Geita (Geita), Kilombero (Kilombero) Makambako huko Njombe, Manonga (Shinyanga Mjini), Kahama (Kahama), Mihayo (Tabora Mjini), Mtendeni (Dodoma Mjini) ambayo sasa linaitwa Tawi la Dodoma, Ifaraka (Ulanga), Babati (Babati), Songea (Songea Mjini), Singida (Singida Mjini), Karatu (Karatu), Bukoba (Bukoba), Kayanga huko Karagwe na Madaraka (Tanga Mjini).

Mheshimiwa Spika, matawi mengine ni Mbozi (Mbozi), Korogwe (Korogwe) Muleba (Muleba) Mpanda (Mpanda), Sumbawanga (Sumbawanga Mjini), Musoma (Musoma), Tarime (Tarime) Kyela (Kyela), Bunda (Bunda), Nzega (Nzega), Tukuyu huko Rungwe, Kigoma (Kigoma Mjini), Masasi (Masasi), Lushoto (Lushoto), Tunduma (Mbozi), *University Agency* (Kinondoni), Mtwara (Mtwara Mjini), *Kibaha Agency* (Kibaha) Chalinze na Bagamoyo (Bagamoyo), Kilosa (Kilosa), Sengerema (Sengerema), Hai (Hai), Muheza (Muheza), Magu (Magu), *Njombe Agency* (Njombe), Rombo (Rombo), Mombo (Korogwe), Mafinga (Mufindi) na Mpwapwa (Mpwapwa). Mheshimiwa Mbunge alikuwa ameuliza tuyataje kwa majina ndiyo maana nimehitaji kuyataja kama alivyoomba kwenye swali lake. (*Kicheko/Makofi*)

Kama ilivyoelezwa hapo awali, Matawi yalianza kutoa mikopo yake pale tu matayarisho yote yalipokamila. Hivyo, Benki inaendelea na maandalizi ya kuyafanya Matawi mengine kuweza kutoa mikopo kwa kuwa utaalami wa utoaji wa mikopo midogo midogo ni tofauti na ule wa utoaji wa mikopo ya kawaida, hasa kwa sababu hii ni mikopo isiyo na dhamana za kawaida za Kibenki.

Mheshimiwa Spika, Matawi 46 ya *NMB* hayatoi mikopo kwa sababu tatu zifuatazo:-

(i) Kutokuwepo kwa mtandao wa umeme wa Gridi ya Taifa katika Wilaya ambako baadhi ya Matawi ya *NMB* yapo, kumeisababishia Benki kushindwa kupeleka huduma muhimu ya Kompyuta katika Matawi husika ambayo ni nguzo muhimu katika utoaji huduma za Kibenki hususan katika mfumo wa utoaji na ufuatiliaji wa mikopo.

(ii) Katika kuifikisha huduma hii muhimu ya mikopo kwa wananchi, *NMB* imekuwa ikifanya hivyo hatua kwa hatua ikizingatia utoaji wa mafunzo sahihi kwa wafanyakazi sambamba na upanuaji wa huduma hiyo. Mafunzo ya usambazwaji wa huduma hiyo yanaendelea kufanyika kwa awamu mpaka hapo huduma hii itakapofikishwa kwa Matawi yote nchini na mwisho ni kutokuwa na mtaji wa kutosha.

(c) Mheshimiwa Spika, kuna athari mbalimbali ambazo zinaweza kuwakumba wananchi iwapo Benki kama *NMB* ikikosekana kwenye maeneo ya Wilayani. Athari hizo ni pamoja na wananchi kukosa huduma kama vile za kutunza amana na kupata mikopo (*Deposits and Loans*), njia za kutuma na kupokea fedha (*Money Transfers*) na shughuli za malipo (*payment*) na kadhalika.

Hivyo, Serikali kwa kuzingatia athari hizo katika maeneo ambayo yatakosa huduma za Kibenki, inaweka mazingira bora ya kiuchumi na kisera ili wananchi waweze kujianzishia Benki za Wananchi (*Community Banks*), Vyama vya Kuweka na Kukopa na kadhalika. Mazingira hayo bora pia yatayafanya Mabenki yaliyopo sasa kufikisha huduma zao katika maeneo ya Wilayani, pale ambapo wataona panafaa kama nilivyoeleza. Hata hivyo, Benki na vyombo vya fedha vitahamasika zaidi pale ambapo wananchi watavitumia ipasavyo, kwani Benki ni biashara kama nyingine zozote ambazo msingi na uhai wake ni kujipatia faida katika kutoa huduma.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, kwa majibu mazuri katika swali langu la msingi lakini nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa kuwa suala la Benki hii ya Wananchi (*NMB*) limekuwa na utata, wananchi hawaelewi msimamo wa Serikali na kadhalika; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atatumia nafasi ya swali hili kuwaeleza wananchi msimamo wa Serikali juu ya *NMB?* (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa sasa kuna Benki hii ya Posta ambayo inatoa huduma vizuri sana, mimi ningekuwa ndiyo Serikali ningeimarisha Posta zote za Vijijini na kuziwezesha ili ziweze kuwakopesha wananchi wa maeneo hayo; je, yeye kama Serikali anasemaje? (*Kicheko/Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu msimamo wa Serikali. Mheshimiwa Waziri wa Fedha alijibu katika Bunge lako Tukufu hili linaloendelea la Bajeti swali la nyongeza akafafanua kwamba, napenda nirudie, kwamba Serikali inakusanya maoni mbalimbali kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuona namna muafaka na ya manufaa zaidi jinsi itakavyofanya ama kubinafsisha *NMB*.

Mheshimiwa Spika, pia yalitolewa mawazo na Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa nini usitumike utaratibu kama uliotumika *CRDB*, nafikiri suala hilo tulilijibu lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema kwamba utaratibu uliotumika kubinafsisha *CRDB* ulikuwa ni wa kizamani na kwa sababu sasa hivi tuna soko la hisa tutumie utaratibu wa kisasa zaidi. Kwa hiyo, mara taratibu na maoni yote yatakapokuwa yamekusanya, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ataleta mapendekezo Bungeni kwa ajili ya utaratibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimariswa kwa Benki ya Posta ili ifike vijijini, tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, lakini nia ya Serikali ni kwamba isifanye biashara. Benki ya Posta ni kati ya Benki ambazo bado zinashikiliwa na Serikali kwa asilimia 100 na taratibu zinaendelea kufanyika kuiimariswa ili hatimaye iweze kupitia utaratibu kama ambao umetumika kwa *CRDB* na ambao unaandaliwa kwa ajili ya *NMB* ili na yenye we iweze kubinafsishwa kwa maana ya kwamba Serikali inajitoa kwenye shughuli za uendeshaji wa biashara.

Kwa hiyo, taratibu zitakapokamilika, Serikali italeta mapendekezo yake lakini kwa sasa kinachofanyika ni kuimariswa Benki hii na kuhakikisha kwamba inakuwa imara na inaweza kutoa faida kwa Serikali na hatimaye kwa wadau watakaokuwa wanashiriki katika kuiendesha kama *owners*.

SPIKA: Bado nusu saa tu kufikia mwisho wa maswali na nina maswali sita kwa hiyo, tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga!

Na. 343

Mpango wa Kukamilisha Mradi wa Umeme Vijijini

MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Magu hususan Jimbo la Busega, limo katika mpango mzima wa ukamilishaji mradi wa kipeleka umeme wa Gridi ya Taifa Vijijini; na kwa kuwa mradi huo ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ahadi ya uwekiwa wa umeme katika Hospitali ya Mkula, vinu vyta kuchambulia Pamba vyta Ngasamo na Aquva, Hoteli za Kitalii za *Speke Bay* na *Kijereshi Tented Camp*, miji midogo ya Nyamikoma, Kalemera, Lamadi na Shighala?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuchelewesha mpango huo kunaathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji mali na maendeleo kwa maeneo hayo kwa ujumla?

tu?
(c) Je, Serikali inatoa ahadi gani inayoweza kutekelezeka badala ya kuendelea na ahadi ya mpango

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika mji mdogo wa Lamadi Jimboni Busega. Mradi wa kupeleka umeme katika eneo hilo unaghanamu shilingi milioni 560.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi nguzo zote za laini zimeshawekwa za kilovolti 33 na taarifa nilizopipata asubuhi hii ni kwamba na waya zote zimeshafungwa.

Mheshimiwa Spika, awamu ya sasa, umeme utafika Lamadi, Aquva na Hoteli *Speke Bay*. Maeneo mengine aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yataingizwa katika awamu ya pili ya mradi mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, Hospitali ya Mkula bado haijafikishiwa umeme lakini inatarajiwa kwamba katika awamu itakayofuata Hospitali hii itapatiwa umeme.

(b) Serikali inatambua sana umuhimu wa umeme katika kuleta maendeleo. Hivi sasa pamoja na juhudu kubwa ambayo *TANESCO* inafanya lakini pia tunafanya majadiliano na baadhi ya wafadhili ili kuongeza nguvu ya kifedha *TANESCO* kwenye utekelezaji wa mradi huu ili maeneo mengine aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ya miji midogo ya Nyamikoma, Kalemra na Shighala pia ipatiwe umeme.

(c) Napenda kusema kwamba awamu hiyo ambayo bado haijapatiwa umeme tutakopofanikiwa kupata fedha hizi basi awamu hiyo ya mradi itapatiwa umeme.

MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye kwa kweli amejibu swal langu la msingi kwa usahihi na takwimu zilizo sahihi, napenda nimpongeze lakini nina swal moja la nyongeza.

Kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo ambapo tayari umeme umeshapatikana lakini kunakuwa na matatizo ya upatikanaji wa mita, je, Serikali inasemaje kuhusu ufungaji wa umeme kwenda sambamba na upatikanaji wa mita?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika maeneo kadhaa pamekuwa na matatizo ya vifaa. Nilishawahi kutoa taarifa hapa Bungeni kwa njia ya majibu ya Bunge kwamba *TANESCO* wamekuwa wakiagiza vifaa hivi lakini uingiaji wake umekuwa ukifanyika kwa awamu.

Kwa maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, nadhani ni vizuri pengine baada ya maswali akanipa kwa kina zaidi maeneo ambayo anayoyazungumzia ili mimi na yeye tuweze kuwasiliana na wenzetu wa *TANESCO* ili kuhakikisha kwamba maeneo aliyoyataja na ambayo tayari waya zimeshafungwa basi vifaa hivyo ambavyo vinakosekana vipatikane.

Na. 344

Umeme - Kata ya Malangali

MHE. BENITO W. MALANGALILA aliuliza:-

Kwa kuwa Menejimenti mpya ya Shirika la Ugavi wa Umeme (*TANESCO*) linakusanya madeni yake kwa nguvu na fedha nyingi zinapatikana; na kwa kuwa Serikali nayo ina mpango wa kukopa fedha toka Benki ya Maendeleo Afrika (*ADB*) kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini na vile vile upo mpango wa kuanzisha mfuko wa kusaidia nishati ya umeme (*energy fund*):-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye Kata ya Malangali ambayo ina vijiji vya Mwilavila, Isimilanyi, Itengule, Kingege na Tambalang'ombe na taasisi kama *Malangali Sec, Itengule Sec, Itengule Mission*, Kituo cha Afya Malangali, Chuo cha Ufundii Itengule na kadhalika?

(b) Kwa kuwa Kata ya Malangali ina taasisi nyingi za elimu; je, Serikali ipo tayari kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili kuona namna ya kupeleka umeme katika taasisi hizo na kuboresha taaluma kwa wanafunzi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Benito Malangalila, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kusambaza umeme kwenye vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, ndiyo maana katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, *TANESCO* ilisambaza umeme katika maeneo mengi ya Mufindi Kusini kwa gharama ya takribani shilingi bilioni 1.6 kama vile Mgololo, Sawala A. Kibao, Mashamba ya Chai ya *Brooke Bond*, Viwanda vitatu vya Kusindika Chai ya *Brooke Bond*, Ugowole na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali bado haijapata fedha za kusambaza umeme katika vijiji hivi vingine ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini iko tayari na kwa kweli ni utaratibu wa kawaada wa Serikali kushirikiana baina ya Wizara na Wizara lakini kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameuliza nataka niseme kwamba tuko tayari kushirikiana na Wizara ya Elimu kwa kuzingatia maelezo ambayo nimeyatoa hapo awali juu ya uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya miradi hii ya kuweka umeme ambayo imeitaja.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa swalii langu la msingi limegusia mpango huu wa Serikali wa kukopa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikizungumzia jambo hili na wananchi wa vijijini wanatarajia kupata umeme kutegemea pesa hizi je, upatikanaji wa mkopo huo mpaka sasa umefikia wapi sambamba na uanzishwaji wa *Rural Energy Fund* ambayo imekuwa ikizungumziwa na Serikali?

(b) Wakati Serikali inazindua mradi wa umeme katika Kijiji cha Ugowole ilisema kwamba kulikuwa na mazungumzo na Serikali ya Sweden juu ya kuteremsha umeme mkuu (*High Tension*) pale Makambako na umeme huo ungeweza kusaidia upatikanaji wa umeme katika vijiji na Kata za Itandula, Mbalamaziwa pamoja na Malangali na Kata nyingine. Je, mazungumzo haya na Serikali ya Sweden yamefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la upatikanaji wa fedha na uanzishwaji wa taasisi na mfuko maalum wa kusambaza umeme vijijini, napenda kutoa taarifa kwamba *consultant* wa mradi huo wa uanzishaji wa taasisi na namna ya kupata fedha hizi tayari ameshawasili nichini na ameshaanza kazi. Tunatarajia mpaka bajeti ijayo mfumo kamili juu ya suala hili utakuwa umefikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makambako, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba pamekuwa na majadiliano na wenzetu wa Sweden, nataka niseme tu kwamba majadiliano haya yanaendelea vizuri.

Na. 345

Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Wananchi

MHE. EDSON M. HALINGA (k.n.y. MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA) aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi letu la Ulinzi lina Kikosi cha Ujenzi chenye uwezo mkubwa katika fani hiyo; na kwa kuwa mara nyingi kimetumika katika ujenzi na katika maafa; na kwa kuwa nchi yetu ni ya amani; je isingekuwa busara kutumia ujuzi na uwezo huo usiotumika ili kikosi hicho kipewe kazi za ujenzi wa barabara na madaraja kibiashara?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria ya Ulinzi wa Taifa Na.24 ya mwaka 1966 Kifungu cha 5 na kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2000 Sura ya 9 Ibara ya 148, jukumu kubwa la msingi la Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania ni ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, jukumu hilo pia hujumuisha kulinda uhuru wa nchi yetu pamoja na watu wake; kuhalikisha ulinzi imara wa mipaka yetu katika nchi kavu, anga na majini; kutoa mafunzo ya ulinzi kwa wananchi na kutoa misaada ya dhararu kwa kushirikiana na vyombo vingine vinavyohusika wakati wa dharura na maafa mbalimbali yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili la msingi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kutumia Wahandisi wa medani na kwa kushirikiana na Wahandisi wa Mikoa mbalimbali wamefanya kazi kubwa katika kujenga madaraja na miundo mbinu ya dharura, katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kama vile wakati wa mafuriko ya 1980 Lindi na Mtware, wakati wa mvua za *El-Nino* na ukarabati wa daraja la Msata mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, kama ifuatavyo.

Nilipokuwa nikimjibu Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mbunge wa Viti Maalum, CCM katika swalii lake Na.293, nilisitisiza kuwa haitakuwa sahihi kulihusisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ujenzi wa barabara na madaraja kibiashara, kwani jukumu hili ni la Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali (*SUMAJKT*) lililoundwa mwaka 1984 chini ya Sheria Na.23 ya mwaka 1974 inayohusu Mashirika ya Umma.

Katika sekta ya ujenzi, tangu kuundwa *SUMAJKT* imeshiriki kikamilifu katika miradi ya kusanifu na kusimamia ujenzi wa barabara nyingi mbalimbali nchini. Kuanzia Oktoba 2001 hadi Oktoba 2002, *SUMAJKT* imepata miradi 17 ya kujenga na kukarabati majengo mbalimbali yenye thamani ya shilingi 723,548,677/=.

Mheshimiwa Spika, lengo la kufanya biashara hizi ni kulipunguzia Taifa mzigo wa uendeshaji JKT na kupata tija kwa lengo la kuuza ziada katika soko la ndani na nje ya nchi na vile vile kutumia ujuzi na uwezo mkubwa walionao katika fani hizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kupitia Bunge lako Tukufu, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, wananchi na Taasisi mbalimbali kuitumia JKT katika miradi ya ujenzi wa nyumba na majengo ya taasisi. Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa sana Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kwa ushauri na mapendekezo yake kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu uboreshaji na uimarishaji wa Jeshi letu kwa manufaa ya ulinzi wa Taifa letu.

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Kwa kuwa Jeshi linafanya kazi nzuri na kwa nidhamu ya kutosha kuliko Wakandarasi wa kawaida na halina usumbufu kwa Serikali yake na wananchi wake katika utekelezaji wa miradi hiyo, je,

Serikali haioni hapa ndio mahali pa kuwezesha kazi kufanyika kwa uaminifu na ukamilifu zaidi kuliko kutafuta Wakandarasi wasioaminika sana? (*Makofî*)

(b) Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba Jeshi lingeweza kujipatia mapato ya nyongeza na kuinua mapato yake na kupunguza Bajeti isiyotosheleza shughuli za Kijeshi? (*Makofî*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Jeshi linaendeshwa chini ya kanuni, taratibu, sheria na *doctrine* maana yake ni kwamba kazi ambazo Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linafanya ziko chini ya sheria na utaratibu kinyume chake wataadhibiya kwa sababu msingi imara wa Jeshi ni utiifu. Kama nilivyooleza katika jibu langu la msingi kwamba hiyo sio kazi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kuitumia Jeshi katika shughuli za ujenzi kwa sababu ya utaratibu mzuri walionao Jeshini, napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba JKT kwa kupertia Wizara ya Ujenzi imeweza kupata tenda ya kujenga nyumba 150 za wafanyakazi wa Serikali na nyumba hizo zitakamilika mwezi ujao kwa muda uliopangwa. Jibu hili linajibu swalilake la pili kwamba tukiendelea kupata miradi kutoka Wizara mbalimbali na vyombo vyaya Serikali itaiongezea Jeshi uwezo wa kibajeti wa kuweza kujitegemea.

Na. 346

Zuio la Muda Mahakamani

MHE. PAUL E. NTWINA aliuliza:-

Kwa kuwa upo udhaifu na usumbufu wa kusikilizwa kwa mtu anayeomba zuio la muda Mahakamani; je, ni kwa misingi gani zuio hilo linawenza kutoa hisia kwa anayeomba zuio hilo awe mdaiwa au mdai?

WAZIRI WA SHERIA YA MAMBO YA KATIBA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalilaki la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kesi yoyote ya madai huwa na pande mbili na aghalabu huhusisha mali au kitu chochote ambacho kila upande hudai kuwa na haki nacho. Mara nyangi upande mmoja ndio huwa na umiliki mali hiyo wakati kesi inaendelea na hivyo upande huo unaweza kuitumia mali hiyo katika namna ambayo inaathiri mali hiyo kiasi kuwa kama upande mwingine utashinda, utakosa mali hiyo na hautakuwa na mahali pa kukimbilia.

Mheshimiwa Spika, amri ya zuio huombwa na upande wowote kuitaka Mahakama kuuzuia upande mwingine kufanya vitendo fulani vinyoweza kuathiri mali au kitu kinachogombewa na pande husika.

Mheshimiwa Spika, lengo ni mali au kitu hicho kiwepo na kibaki katika hali kiliyo nayo hadi kesi itakavyomalizika au hadi muda fulani. Maombi ya amri ya zuio hushughulikiwa sawa na kwa taratibu zile zile zilizoainishwa na sheria na hivyo haupo udhaifu au usumbufu wowote mahsus kwa wanaoomba amri hizi tofauti na wenye kesi nyngine.

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Kwa kuwa inaonekana kuwa wakati mlalamikaji anazuiwa na mlalamikiwa bila kuwepo mlalamikaji inaonyesha kuna hisia ipo pale; je, Waziri haioni kwamba hisia hiyo inaweza kufanya kesi hiyo ikaonyesha kuwa haina haki ndani yake?

(b) Kuwepo na Hakimu na mlalamikiwa kukubaliana zuio la kuendeshwa kwa kesi hiyo pasipo kuwepo na yule aliyepeleka kesi hiyo Mahakamani haoni inatoa upenyo kwa haki ambayo ingetendeka Mahakamani isitendeke? (*Makofsi*)

WAZIRI WA SHERIA YA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba utaratibu huu upo kila mahali na suala ambalo pengine ni tatizo ni wakati mlalamikaji anakawa amepeleka ombi lake Mahakamani na wakati huo huo Hakimu kutoa *Court Injunction*, kwa kweli utaratibu ni kwamba wote wawili inabidi wawepo Mahakamani. Sasa hisia hiyo ya kutoa maamuzi wakati anayelalamikiwa hayupo hujenga hisia kwamba pengine kuna kitu fulani lakini kwa kweli kiutaratibu ni kwamba wote wanatakiwa wawepo Mahakamani waweze kujieleza na kujitetea na haki kutendeka.

Na. 347

Kuendeleza Ubongo wa Mtoto

MHE. JENISTA J. MHAGAMA aliuliza:-

Kwa kuwa Taifa lolote lile ili liweze kuondokana na umaskini na kuwa Taifa bora linalojitegemea linahitaji watu wabunifu, watendaji wenyewe afya bora na elimu bora iliyojengwa kwa msingi imara na hasa inayotokana na makuzi bora ya ubongo toka utotonii; na kwa kuwa taarifa za utafiti na kitaalam huonyesha kuwa katika umri wa miezi 18 ya mwanzo ya maisha ya binadamu ubongo huwa na uzani wa gramu 400, binadamu huyo afikiapo umri wa miaka 3 uzani huo wa ubongo hufikia ongezeko la gramu 1,100 na hatimaye kutoka umri wa miaka 3 mpaka utu uzima uzani huo huongezeka kwa gramu 1,300 mpaka 1,400:-

(a) Je, Serikali inaweka umuhimu gani katika maendeleo haya ya ubongo wa watoto kwa kuandaa Taifa la baadaye lililo bora?

(b) Kwa kuwa Shule za Awali (*Day Care Centers*) ndizo hasa zinazofaa kukuza akili, utashi na vipaji kwa watoto; je, ni nini mkakati wa Serikali wa uboreshaji wa shule hizo kimazingira, majengo, vifaa vya kufundishia na kadhalika?

(c) Je, ni Wizara gani hasa inawajibika katika malezi na makuzi ya kielimu na vipaji vya watoto chini ya miaka minne?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa sehemu kubwa ya uwezo wa mtoto kujifunza hukamilika kabla hajaanza darasa la kwanza akiwa na miaka 7. Kutokana na ukweli huo, Serikali kupitia Wizara yangu na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Afya, zimeandaa Sera zinazoendana na makuzi na maendeleo ya mtoto kimwili, kiakili na kimaono.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 kuhusu Elimu ya Awali inaelekeza kuwa Elimu ya Awali itolewe kwa watoto wa miaka 5 hadi 6 ili kuwaandaa kuanza Darasa la Kwanza wakiwa na miaka 7. Katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka huu nimetaarifu kuhusu upanuaji wa elimu ya awali na elimu ya msingi unaoendelea vizuri kuelekea kwenye lengo la elimu ya msingi kwa wote.

(b) Kulingana na mabadiliko ya uendeshaji wa Serikali za Mitaa (*Local Government Reforms*) uendeshaji wa shule za awali ni jukumu la Wizara ya Elimu na Utamaduni, kupitia Halmashauri za Serikali za Mitaa pamoja na mashirika na madhehebu yanayojitolea. Wizara yangu ina jukumu la kutoa mafunzo kwa Walimu na maelekezo muhimu ya kisera na miongozo ya utekelezaji wa sera hizo.

Aidha, Wizara yangu inahamasisha mashirika yasiyo ya Kiserikali na watu binafsi kuanzisha, kumiliki na kuziendesha shule hizo. Wizara pia hutoa huduma za usajili, ukaguzi na kutahini ili kuhakiki ubora wa shule hizo kwa mazingira ya shule, majengo, vifaa vya shule na elimu inayotolewa.

(c) Vituo vya kulelea watoto wenye umri wa chini ya miaka 4 ambavyo hupewa majina kama *Day Care Centers, Nursery Schools* na *Kindergarten* vinasimamiwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mujibu wa Sheria Na.17 mwaka 1981 ya kuanzisha Vituo vya Kulelea Watoto wadogo.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa idadi kubwa ya wananchi wa Tanzania ni wanawake na watoto wadogo na kwa kuwa watoto hao wadogo chini ya miaka 5 wamekuwa wakirandaranda na kuzurura tu kwa kukosa vituo vingi vya kuwalea wakiwa wadogo na kuwapa makuzi bora ya maandalizi ya kuingia katika elimu ya msingi ambayo Wizara ya Elimu huanza kuwachukua na umri wa miaka 5 na kuendelea; je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa uko umuhimu wa kutengeneza mkakati maalum wa kusaidia kuanzisha vituo hivyo na hasa katika maeneo ya vijijini ambako haviko?

(b) Kwa kuwa suala zima la kuwahudumia watoto hawa wadogo chini ya miaka mitano limekuwa likihusisha Wizara nyingi na hakuna Wizara maalum inayohusika moja kwa moja, je, Mheshimiwa Waziri atapokea ushauri wangu kwamba sasa Wizara hizo zikae pamoja ili watoto hawa waeleweke watakuwa wakihudumiwa moja kwa moja na Wizara gani ili kupunguza matatizo yao? (*Makofî*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba wanawake na watoto wadogo ni wengi sana katika jamii asilimia yao ni kubwa sana tukitazama katika idadi ya watu na kwa namna ya muundo wa idadi ya watu katika nchi yetu watoto wadogo ni wengi sana kulinganisha na watu wakubwa. Hili ni jambo la kweli kabisa. Nakubaliana naye kwamba iko haja ya Serikali pamoja na wadau wote katika suala hili la elimu kujiiamarisha zaidi kutoa huduma hii ya elimu ya awali pamoja na elimu ya watoto wadogo.

Mheshimiwa Spika, tunachofanya hivi sasa tunapanua elimu ya msingi, tunaongeza shule lakini pia mkakati tunaofuata ni kwamba kila palipo na shule ya msingi pawe pana shule ya awali. Kwa namna hii tutaweza kufikia sehemu kubwa ya watoto kupertia katika elimu ya awali.

Mheshimiwa Spika, pia alisema kuna haja ya kukaa pamoja kwa sababu jambo hili la watoto wadogo linasimamiwa kwa maana ya elimu kwa ujumla na Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa maana ya shule za chekechea ni Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, lakini pale pale tuna Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Kwa hiyo, pengine kuna haja ya kukaa pamoja kwa sababu inawezekana mgawanyo huu wa kazi ulikuwa umetengenezwa wakati hatujawa na hii Wizara nilioitaja mwisho. Napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo haja tukae pamoja tulitazame upya jambo hili la elimu ya watoto tuweze kulipa *focus* kubwa na yenye maana zaidi kwa malengo ya Tanzania ya leo.

Marekebisho ya Mishahara ya Walimu

MHE. MARGARETH A. MKANGA aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja, Serikali ilifafanua kuwa imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya mishahara ya Walimu wa Shule za Sekondari kama jitihada ya kuwavutia Walimu hao kuendelea kufundisha kwenye shule hizo za Serikali:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kama marekebisheso hayo yatawahusu Walimu wa Shule za Sekondari peke yake itakuwa imewabagua Walimu wengine wa Shule za Msingi ambao nao wameanza kupenda kufundisha kwenye Shule za Binafsi?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba wakati sasa umefika wa kubuni mikakati mipy ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi hasa Walimu ili maboresho ya elimu yaliyoanza yawe ya mafanikio katika ngazi zote za elimu?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Margaret Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa marekebisheso hayo ya mishahara kama yalivytangazwa Bungeni na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi hayatawahusu Walimu wa Shule za Sekondari peke yao bali yatawahusu pia Walimu wa Shule za Msingi na Vyuo vya Walimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 imetenga kiasi cha shilingi bilioni 34.5 kwa ajili ya marekebisheso ya viwango vya mishahara ya watumishi wakiwemo Walimu kwa kuwapa nyongenza ya kati ya asilimia 6 hadi 10.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba maboresho tunayoyafanya katika utoaji wa elimu lazima yaambatane na Serikali kujitahidi kufanya kila linalowezakana kuboresha hali ya walimu kwa ujumla wake ikiwa ni pamoa na kuongeza mishahara ya walimu kama nilivyosema kwa kati ya asilimia sita hadi kumi, kuendelea kujenga nyumba za walimu ambazo kazi hii tunaifanya kwa kiwango kikubwa sana, kuajiri walimu 15,000 waliokuwa hawajaajirwa. Sasa wameajiriwa wote. Kupanua mafunzo ya elimu ya walimu na kuajiri walimu moja kwa moja kutoka Vyuo vya Ualimu hadi kufikia uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40 katika kila Wilaya na hatimaye katika kila shule.

Hata hivyo ni muhimu kuzingatia kuwa mishahara ya walimu haiwezekani ikawa zaidi ya uwezo wa Bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, maboresho zaidi ya mishahara ya watumishi wa Serikali wakiwemo walimu yatategemea kuongezeka kwa mapato ya Serikali yatakayotokana na ufanisi wa ukusanyaji wa kodi na kukua kwa uchumi wa Taifa.

SPIKA: Mheshimiwa Margaret Mkanga, ameridhika na muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, tunaendelea na shughuli nyingine. Vikao vya leo, Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Njelu Kasaka, anaomba wajumbe wake wakutane leo tarehe 30 Julai, 2003 saa 5.00 asubuhi chumba Na. 54.

Kamati ya pili ni Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anaomba wajumbe wake wakutane leo tarehe 30 Julai, 2003 saa 5.00 asubuhi chumba Na. 58. Ni hizo Kamati mbili ambazo zimepanga kukutana.

Tangazo lingine linahusu uchaguzi wa Wajumbe wetu wanaowakilisha Bunge katika Bodi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Muda wa wajumbe waliopo sasa unakwisha kesho tarehe 31. Wajumbe waliopo sasa tuliowichagua ni Profesa David Mwakyusa, Profesa Henry Mgombelo na Mheshimiwa Monica Mbega, wanatakiwa watatu. Sasa muda wao unakwisha, kwa hiyo, inabidi tufanye uchaguzi mwagine ama wa kuwarudisha hao hao au wa kuchagua wengine.

WABUNGE FULANI: Hao hao. (*Makofit*)

SPIKA: Mimi nawajibika kutoa tangazo hilo kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, natoa taarifa kwamba uchaguzi utafanyika Jumatano ijayo tarehe 6 Agosti, 2003 baada ya maswali. Kwa hiyo, wanaotaka kugombea wawasilishe majina yao kwa Katibu wa Bunge wakati wowote kabla ya Jumatano ijayo. Ni kwa mujibu wa taratibu tu, kama mnataka waendelee mtasema hivyo siku ya tarehe 6.

Mwisho wa matangazo. Katibu endelea na *Order Paper*.

KAULI ZA MAWAZIRI

KAULI YA SERIKALI JUU YA UTARATIBU WA FEDHA ZA STABEX

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kauli hii ya Serikali juu ya utaratibu wa fedha za *STABEX* ya kahawa inatolewa chini ya Kanuni namba 39 ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano ya hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula, katika vikao vya 14 na 15 vya Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge lako Tukufu vilivyoofanyika tarehe 30 Juni na tarehe 1 Julai, 2003 baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliitaka Serikali kueleza kwa nini wakulima wa Kahawa wasilipwe malipo ya fedha taslimu kutohana na fedha za *STABEX* ili kufidia hasara waliyoipata kutohana na kushuka sana kwa bei ya kahawa kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilijitahidi kutoa maelezo juu ya matumizi ya fedha hizo, lakini kutohana na ufinyu wa muda uliokuwepo Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, aliahidi kuwa Serikali ingetoa kauli juu ya *STABEX* chini ya Kanuni ya 39 ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kabla Serikali haijatoa maelezo yake ya kina kama ilivyoahidi, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa, katika kikao cha 34 cha Mkutano huu wa Kumi na Mbili, akataka maelezo ya Serikali juu ya jambo lile lile. Ingependeza sana kama Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, angesubiri maelezo ya Serikali kwanza na kama asingeridhika nayo ndiyo akatoa maelezo yake. Hivyo kwa maelezo yangu ninatekeleza ahadi ya Serikali aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu na nitajitahidi pia kujibu hoja za Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi.

Mheshimiwa Spika, lengo la maelezo nitakayotoa ni kufafanua maelezo na matumizi ya fedha za *STABEX* kwa kipindi cha miaka ya 1990 hadi 2003. Natoa maelezo haya nikijua kwamba sehemu kubwa ya maelezo haya imewahi kutolewa katika ukumbi huu mara nyingi na katika vipindi mbalimbali. Natambua pia kwamba suala hili litaendelea kujadiliwa na kuhojiwa ndani na nje ya Bunge hadi fedha zilizopo zitakapotumika. Tutajitahidi kuendelea kutoa maelezo na ufanuzi hata kama itabidi kujirudia rudia kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Ulaya ilianzisha utaratibu wa *STABEX* chini ya Mkataba wa Kwanza wa Lome kama ulivyoorekeblishwa na Mkataba wa George Saung Ayana mwaka 1975 kwa lengo la kupunguza athari zinatokana na kushuka kwa mapato ya fedha za kigeni ya nchi za Afrika, Caribbean na Pacific yanayotokana na mauzo ya mazao ya nchi hizo nje. Jumuiya ya Ulaya ililitambua tatizo hili kuwa ni moja kati ya vikwazo vya amani na utilivu, upatikanaji wa ziada na ukuaji endelevu wa uchumi wa nchi hizo. Lengo la *STABEX* ni kusaidia juhudhi za maendeleo ya nchi za *ACP* na kwa njia hiyo kuziwezesha kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa watu wa nchi hizo kwa kulinda uwemo wao wa kujikumu.

Mheshimiwa Spika, fidia ya *STABEX* imekuwa ikitolewa pale Jumuiya ya Ulaya iliporidhika kuwa mapato yaliyotokana na mauzo ya mazao nje yameshuka kutohana na matatizo ya uzalishaji na soko na siyo kutohana na utekelezaji wa sera zisizokuwa sahihi. Ni muhimu kuzingatia kwamba fidia ya *STABEX* hutolewa kusaidia nchi iliyoathirika inayohusika. Ibara ya 187 ya Mkataba wa Nne wa Lome imenorodhesha mazao yanayoweza kufidiwa chini ya utaratibu wa *STABEX*. Kwa upande wa Tanzania mazao yaliyopo kwenye orodha hiyo na yaliyowahi kunufaika na fedha za *STABEX* ni Kahawa, Pamba, Chai, Mkonge, Korosho na Karafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 186 ya Mkataba wa Nne wa Lome fedha zinazopatikana chini ya utaratibu wa *STABEX* zinaweza kutumiwa kuongeza tija katika sekta iliyoathirika au katika maeneo mengine ya uzalishaji ya sekta ya nchi. Kwa mfano, fedha hizo zinaweza kutumika

kugharamia utekelezaji wa miundombinu kama barabara, ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao na maeneo mengine ya uzalishaji hususan katika sekta ya kilimo. Aidha, fedha hizo zinaweza kutumika kuendeleza maeneo yasiyo na uhusiano wa moja kwa moja na sekta iliyojalisha zao ambalo ndilo chanzo cha fidia kama elimu, ujenzi wa barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kabla fedha za *STABEX* hazijatumika, nchi inayohusika hukubaliana na Jumuiya ya Ulaya namna fedha hizo zitakavyotumika. Kigezo kikuu cha makubaliano ni sera za kiuchumi za nchi zinazohusika kukubaliwa na Jumuiya ya Ulaya. Kwa mfano, katika kutoa fedha za *STABEX* za miaka ya 1994 na 1996 kigezo kikuu ni utekelezaji wa sera za mikakati ya kuondoa umaskini. Makubaliano kati ya nchi inayohusika na Jumuiya ya Ulaya huwekwa kwenye Mkataba ambaa unajulikana kama *Framework of Mutual Obligation* kwa kifupi *FMO*.

Baada ya kusaini Mkataba huo nchi inayohusika hutakiwa kuandaa mpango wa utekelezaji. Mpango huo unapaswa uandaliwe kwa utaratibu utakaofanywa ukubaliwe na Jumuiya ya Ulaya. Mchakato wa kuandaa mpango huo huchukua muda mrefu na unawenza kuchelewesha kutolewa kwa fedha za *STABEX*. Kwa mfano, taarifa ya upatikanaji wa fedha za *STABEX* za miaka ya 1994 na 1996 iliwasilishwa Serikalini na Jumuiya ya Ulaya mwaka 2000. Mkataba wa makubaliano wa matumizi ya fedha hizo ulisainiwa tarehe 10 Februari, 2003. Mipango ya kutumia fedha hizo inaandaliwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 1988, nchi wanachama wa Shirika la Kahawa la Kimataifa linalojulikana kama *ICO* zilikuwa na utaratibu wa kuuza kahawa kwa viwango maalum walivyokubaliana yaani walikuwa na *a quarter system*. Chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa mwaka 1962 utaratibu huo ulisaidia kulinda bei ya kahawa katika soko isiyumbe ulivunjika mwaka 1989 na hivyo kusababisha bei ya kahawa kushuka kutoka dola za Kimarekani 2500 kwa tani kwa mwaka 1989 hadi dola za Kimarekani 1050 mwaka wa 1991/1992. Aidha, katika kipindi kilichofuata na hasa katika miaka ya 1993, 1997 na 1998 uzalishaji wa kahawa ulishuka kwa sababu mbalimbali hususan kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kushuka kwa mapato ya Taifa yaliyotokana na mauzo ya kahawa Jumuiya ya Ulaya ilitulipa fedha za *STABEX* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1993 tulilipwa *Euro* milioni 19.178 za *STABEX* ya mwaka 1990, mwaka 1995 tulilipwa *Euro* milioni 13.04 za *STABEX* ya mwaka 1991, mwaka 1997 tulilipwa *Euro* milioni 12.528 na *Euro* milioni 8.3 za *STABEX* ya miaka ya 1992 na 1993 zililipwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya makubaliano na Jumuiya ya Ulaya pesa hizo za *STABEX* zilitumika kwa shughuli mbalimbali zikiwa ni pamoja na kuwalipa wakulima, kununua vipuri vya mitambo ya kumenyea kahawa inayojulikana kama *Central Pulparies*, kugharamia utafiti wa zao la kahawa, kutoa mafunzo kwa wakulima, wanaushirika na wataalam, kununua pembejeo, kuzalisha miche ya kahawa, kuchimba visima ili kupata maji safi ya kusafishia kahawa, kutengeneza miundombinu hasa barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, takwimu zetu zinaonyesha kwamba asilimia 64 ya fedha zote za *STABEX* zilizopokelewa katika mwaka wa 1990 na 1993 ambazo ni jumla ya *Euro* milioni 53.04 zililipwa kwa wakulima kama fedha taslimu. Ukweli huu unadhihirisha nia njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kwaongeza wananchi mapato kila kunapokuwepo na uwezekano wa kufanya hivyo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa tulizonazo zinaonyesha kwamba ni Tanzania peke yake ambayo imekuwa na utaratibu wa kuwalipa wananchi wake fedha taslimu kutokana na fedha za *STABEX* ili kuwafidia kutokana na kushuka kwa bei za mazao wanayozalisha. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, fedha ambazo hazikutumika kumlipa mkulima fedha taslimu zilitumika kumpatia mafunzo, kujenga miundombinu ambayo ilimwezesha kuzalisha kwa ufanisi zaidi, kusindika mazao yake, kuyasafirisha kwa urahisi na kugharamia usafiri.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuboreshwa kwa huduma hizo ni kumsaidia mkulima wa zao husika aweze kuzalisha mazao mengi na bora zaidi na kwa hiyo kupata kipato kikubwa zaidi na kwa utaratibu endelevu.

Mheshimiwa Spika, fedha za *STABEX* za miaka ya 1994 na 1996 zimejumuisha fedha zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, *Euro* milioni 2.8 za *STABEX* ya mwaka 1994, *Euro* milioni 26.18 za *STABEX* ya mwaka wa 1996, *Euro* milioni 8.278 ambazo ni nyongeza na riba ya fedha za *STABEX* ya miaka ya 1990, 1991, 1992 na 1993, *Euro* milioni 1.0 kama nyongeza iliyotokana na albaki ya miaka ya 1990 na 1993 na *Euro* milioni 1.178 ambazo zimehifadhiwa katika akaunti ya pamoja kati ya Serikali ya Jumuiya ya Ulaya iliyopo Dar es Salaam. Hivyo jumla ya fedha zote zilizolipwa kama *STABEX* ya miaka ya 1994 na 1996 pamoja na nyongeza mbalimbali ni *Euro* milioni 38.44 ambazo ndizo zilizopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, majadiliano kati ya Serikali na wawakilishi wa Jumuiya ya Ulaya kuhusu magawanyo wa matumizi ya fedha za *STABEX* kwa miaka ya 1994 na 1996 yalianza mwezi Novemba mwaka 2000 kwa kuwashirikisha wadau wa zao la kahawa wakiwa ni pamoja na wawakilishi wa wakulima wadogo na wakubwa wa zao la kahawa, wawakilishi wa Vyama Vikuu vya Ushirika vya Arusha, Karagwe, Kagera, *KNCU* na *VACU* vya Kilimanjaro, *MBOCU* na *IKISAYULA* vya Mbozi na wadau wengine walitoka Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Lyamungo, Bodi ya Kahawa Tanzania, Mamlaka ya Mapato, Wawakilishi wa Viwanda vya kukobia kahawa na wawakilishi wa mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. Wawakilishi wa Jumuiya ya Ulaya walihuduria kama watazamaji tu.

Mheshimiwa Spika, hivyo madai ya Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwamba wadau wa kahawa hawakushirikishwa katika kupanga mgawanyo wa fedha za *STABEX* ya miaka ya 1994 na 1996 hayana hata chembe ya ukweli. Wadau hao walipendekeza fedha za *STABEX* za miaka ya 1994 na 1996 zitumike kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, fidia kwa wakulima *Euro* milioni 17.0, pili, kukarabati na kujenga barabara katika maeneo yanayolima kahawa *Euro* milioni 8.0, tatu, utafiti wa zao la kahawa *Euro* milioni 3.0, nne, kuimarisha ubora wa kahawa *Euro* milioni 5.4, tano, huduma za fedha kuitia *SACCOS* *Euro* milioni 0.2 na sita, gharama za maandalizi, usimamizi, taaluma, ukaguzi na tathmini *Euro* milioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mgawanyo huu ni dhahiri kwamba hata wadau wenyewe waliona umuhimu wa kutenga fedha zilizopo kwa ajili ya kujenga miundombinu, kufanya utafiti, kuweka mfumo wa kuwezesha uzalishaji wa kahawa bora na kuimarisha Vyama vya Kuweka na Kukopa. Serikali kuitia barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ya tarehe 20 Februari, 2001 iliwasilisha mapendekezo ya wadau kwenye Jumuiya ya Ulaya. Kwa kuitia barua yake ya tarehe 13 Machi, 2001 Jumuiya ya Ulaya ilijibu kuwa pendekezo la fidia ya fedha kwa wakulima halikubaliki kwa sababu kuu tatu.

(a) Kwamba kuwalipa wakulima fedha taslimu siyo moja kati ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mkakati wa kupunguza umaskini.

(b) Kwamba isingekuwa rahisi kupata takwimu za uhakika zinazoonyesha mauzo ya kila mkulima. Hali hii inatokana na kutokuwepo kwa utaratibu wa ukusanyaji wa takwimu na taarifa za uuzaji na ununuzi wa kahawa wa wakulima chini ya mfumo wa sasa wa soko huru.

(c) Kwamba kutokana na tatizo la kutokuwepo kwa takwimu kulikuwepo na uwezekano mkubwa kwa fedha hizo kulipwa kwa watu wasiokuwa walengwa na hivyo kupotosha madhumuni ya kuwafidia wakulima.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo Jumuiya ya Ulaya ilishauri kwamba fedha hizo zitumie kugharamia programu ya kuendeleza sekta ya kilimo (*Agricultural Sector Development Programme*).

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002, Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba, alifanya majadiliano zaidi ya Jumuiya ya Ulaya huko Brussel, Ubelgiji yaliyokuwa na lengo la kuwataka

wakubaliane na pendekezo la kuwafidia wakulima kwa fedha taslimu. Kamishna wa Jumuiya ya Ulaya anayeshughulikia maendeleo ya nchi za Afrika, Caribbean na Pacific, Bwana Paul Lingston alieleza kuwa uamuzi wa kutolipa fedha za *STABEX* kwa mkulima mmoja mmoja ulikuwa ni wa Bunge la Ulaya ina inabidi uheshimiwe. Bunge la Jumuiya ya Ulaya hawakukubali fedha za walipa kodi wao kunufaisha wasiokuwa walengwa badala ya wakulima waliohusika.

Baada ya majadiliano haya kushindikana na kupata majibu tuliyopata Serikali iliondoa kipengele cha fidia ya fedha taslimu kwa wakulima na badala yake kuweka kipengele au shughuli ambazo zitakuwa na matokeo ya kumufaisha mkulima katika kilimo chake cha kahawa. Naamini Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na Serikali kuwa utaratibu huo ni endelevu na una manufaa zaidi kwa mkulima na Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Serikali ingeweza kulazimisha Jumuiya ya Ulaya kulipa fedha za *STABEX* kwa mkulima mmoja mmoja kama anavyodai Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. Serikali inastahili pongezi kwa juhudzi zake za kuwatetea wakulima kwa mfano, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, anapendekeza wakulima walipwe asilimia 20 ya fedha za *STABEX* zilizopo wakati Serikali ilipendekeza walipwe asilimia 44. Aidha, kwa lengo la kupotosha ukweli uliopo kwenye barua ya Waziri wa Fedha kwenda kwa aliyekuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou ya tarehe 8 Julai, 2002, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, alinukuu sehemu tu ya aya moja ya barua hiyo. Aya kamili ya barua ya Waziri wa Fedha, inasema kama ifuatavyo na naomba kunukuu:

"As to whether the EU Commission as directed that Stabex Fund should not be paid directly to farmers. I wish to assure you that this is not a case."

Hiyo ndiyo sehemu aliyonukuu Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. Sasa inaendelea: *"As reflected above the aim of the scheme goes beyond direct payment, they include investment in widest possible sense including diversification to approximate productive sectors with the aim of minimizing the effect of loss of revenue to the economy. For instance, the Government was just concluded discussion with EC on the utilization of Stabex fund for 1994 -1999 application year, including balances of the previous Stabex totalling Euro 38.4 million. And the agreed arrears are consist inventions, technology and support Euro 9.0 million, Support to Agricultural Sector Development Programme Euro 18.0 million, rehabilitation of priority regional roads 10.0 million, CA that is coordination, monitoring and evaluation 1.4 million, total 38.4 million. The agreed arrears seek to address the problems of low hubs caused by inadequate genetic material, crop losses due to coffee disease and limited access to services in particular market access. It also makes contributions to finance priority areas identified under ASDB,"* mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hivyo kama Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, angesoma aya kamili angeona kuwa barua ya Waziri wa Fedha inasema kwamba fedha hizo zitafikishwa katika miradi na shughuli zitakazowasaidia wakulima kuinua na kuboresha uzalishaji wa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, ninaamini Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, sasa ameelewa maudhui ya barua hiyo. Aidha, madai ya Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwamba majibu ya Serikali ni ya kujikanganya hayana msingi na kujikanganya anakoona kunatokana na yeze mwenyewe kutokusoma kikamilifu kumbukumbu anazopata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2001 wakulima 18,706 wa chai walilipwa Euro milioni 1.15 kutokana na fedha za *STABEX* za mwaka wa 1999. Tofauti ya utaratibu wa soko la chai na kahawa ni kwamba hata chini ya mfumo wa soko huru chai inaendelea kuuzwa viwandani na kwa utaratibu unaowezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za wakulima wa chai.

Mheshimiwa Spika, kufuatia makubaliano ya maeneo ya matumizi ya fedha za *STABEX* za mwaka 1994 na 1996, Mkataba wa makubaliano yaani *Framework of Mutual Obligation* kati ya Serikali na Jumuiya ya Ulaya ulitiwa saini na Serikali na Jumuiya ya Ulaya tarehe 10 Februari, 2003 na utatekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka huu.

Aidha, kwa mujibu wa Mkataba huo kabla ya utekelezaji utafanyika upembuzi yakinifu kutathmini na kuainisha barabara na maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa mpango. Mkataba huo unabana pande zote mbili na hauna kipengele kinachoruhusu majadiliano ya kuubadilisha. Mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya inayoandaliwa kuwashirikisha wadau wa sekta ya kilimo katika Halmashauri za Wilaya itaainisha maeneo ya utekelezaji. Hilo ndilo eneo pekee ambalo Halmashauri za Wilaya pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanaweza kushawishi ulekezaji wa fedha za *STABEX* katika maeneo wanayoona ni muhimu.

Namshauri Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kutumia nafasi hii kushawishi utengenezaji wa barabara za Jimbo lake la Kyerwa kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya mpango wa maendeleo ya Halmashauri za Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Cotonuo wa mwaka 2000 ambao umefuta Mkataba wa Nne wa Lome una mwelekeo mpya wa utoaji wa fedha za misaada kutoka Jumuiya za Ulaya kwa lengo la kupunguza kuyumba kwa mapato ya nchi za *ACP* kutokana na mauzo ya mazao yao nchi za nje. Mkataba wa Cotonuo unalenga kuzisaidia nchi hizo kuwekeza katika maeneo yatakayoleta maendeleo endelevu. Mwelekeo huo unakubaliana na mkakati wa Taifa wa kuondo umaskini, mkakati wa maendeleo Vijijini na mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo. Kwa mujibu wa Ibara ya 68 ya Mkataba wa Cotonuo fedha za kupunguza kuyumba kwa mapato ya nchi za *ACP* kutokana na mauzo ya mazao yao nchi za Jumuiya ya Ulaya zitaelekezwa katika kuimarisha bajeti za nchi za *ACP* zinazohusika. Mkataba wa Nne wa Lome ulifkia mwisho mwezi Juni, 2000 na fedha za *STABEX* zilizopo sasa hivi na ambazo zinasubiri kutumiwa ndiyo za mwisho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, ameuliza iwapo Serikali inaweza kuwafidia wakulima wa kahawa angalau shilingi bilioni tano tu baada ya utaratibu wa *STABEX* kushindikana. Pamoja na kwamba Serikali ingependa sana kuwafidia wakulima wote nchini wakiwemo wakulima wa kahawa kila wanapopata hasara hivi sasa Serikali haina uwezo wa kufanya hivyo kutokana na uwezo mdogo wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi siku zote inawathamini sana wakulima na inafanya kila linalowezekana kutafuta njia za kuwaongezea kipato. Mara tatu mfululizo Serikali ilitetea na kukubaliwa kutumia fedha za *STABEX* kuwalipa wakulima wa kahawa fidia kwa fedha taslimu. Malipo haya ya fidia kwa wakulima yalifanywa mwaka 1993, 1994 na 1997. Malipo ya fedha taslimu kwa wakulima wa kahawa yalifikia jumla ya shilingi 17,070,152,700/= ambazo ni asilimia 64 ya fedha zilizotolewa ambazo zilikuwa shilingi 26,685,189,352.

Mheshimiwa Spika, mara zote ambapo fedha za *STABEX* zinatolewa Serikali imekuwa ikiwashirikisha wadau wa sekta husika ili kupata maoni yao na kupanga matumizi ya fedha hizo. Hata katika majadiliano ya matumizi ya fedha za *STABEX* za miaka ya 1994 na 1996 Serikali ilishirikisha wadau hawa. Hivyo Serikali haioni sababu ya kwenda katika Wilaya zote au hata baadhi ya Wilaya zinazolima kahawa kuwauliza wakulima mahitaji yao kwa sababu mahitaji yao yanaeleweka na wamewahi kuyajadili katika vikao vya wadau. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kama nilivyoeleza chini ya mipango ya maendeleo ya Halmashauri za Wilaya Serikali itawashirikisha wakulima wakiwemo wakulima wa kahawa ikiwa ni pamoja na kuhamasisha katika uandaaji na utekelezaji wa mipango hiyo. Baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha. Pia nitampa Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, nakala ya maelezo haya. (*Makofii*)

SPIKA: Hata usipompa yatakuwa kwenye *Hansard* kwa hiyo, wote watapata. Waheshimiwa Wabunge, kabla sjamwita mtoa hoja nilisahau kuwatambulisha Makamanda wa Majeshi yetu ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wapo kwenye *Gallery* ya Spika wamekuja kusikiliza mjadala wetu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi inayohusu Wizara yangu naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa likubali kupitia makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nami naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini; Mheshimiwa Edward Ndeka, Mbunge wa Kigoma Kusini, Mheshimiwa Sumri Abdallah Salum Mohamed, Mbunge wa Mpanda, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatibu, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Ali Said Salum, Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni na Mheshimiwa Salum Omar Ali, Mbunge wa Tumbe.

Wengine ni Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mbunge wa Konde, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mbunge wa Mgogoni, Mheshimiwa Mohamed Ali Saidi, Mbunge wa Wingwi, Mheshimiwa Khalif Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mbunge wa Utaani, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mbunge wa Kojani na Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mbunge wa Pandani. Wote nawapongeza kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge baada ya kufanya chaguzi ndogo za Wabunge katika Majimbo yao tarehe 18 Mei, 2003. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuongoza, kusimamia, kudhibiti na kuratibu utekelezaji wa majukumu katika maeneo makuu matatu. Eneo la kwanza ni shughuli ya msingi ya Wizara ya kudhibiti ulinzi wa mipaka ya nchi yetu dhidi ya uvamizi wa maadui kutoka nje ili Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iendelee kuwa na amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni la kuwaandaa vijana wa Tanzania ili wawe raia wema watakoasimamia Umoja, Utaifa na watakaokuwa na silika ya kufanya kazi za mikono na kujitegemea kwa kuwapatia mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, ulinzi, ufundi stadi na uzalishaji mali. Katika eneo hili pia tumeendelea kupata mafanikio tangu mafunzo hayo yaliporejeshwa mwaka 2001 baada ya kusitishwa mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni la shughuli za utafiti na uendelezaji wa teknolojia ya kijeshi pamoja na uzalishaji mali kibashara. Madhumuni ya shughuli hizi ni kupata teknolojia itakayoongeza uwezo wa Jeshi letu kimapigano pamoja na kuingiza mapato yatakayotumika katika kutekeleza miradi ya kuimarisha vyombo vya kiulinzi. Katika eneo hili mafanikio ni madogo kutokana na ufinyu wa Bajeti na upungufu wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu kwa mwaka 2002/2003 kwa wastani ilikuwa shwari isipokuwa katika mpaka wa Magharibi na nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*). Mapigano ya kikabilo kati ya vikundi vya Waasi na Majeshi ya Serikali ya nchi hizo yamesababisha matukio mengi ya kuhatarisha usalama wa watu na mali zao katika maeneo yaliyo karibu na mpaka huo. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lenye dhamana ya kulinda Uhuru wa nchi yetu, wananchi wetu pamoja na mali zao ili amani na utulivu uendelee kudumishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limeendelea kudhibiti ipasavyo ulinzi wa mipaka yote ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, JWTZ kwa kushirikiana na wananchi na vyombo vingine vya usalama limeikabili hali ya kuhatarisha usalama katika mpaka huo wa Magharibi na kuweza kudhibiti vikundi vya wahalifu vilivyohatarisha maisha ya wananchi na mali zao kama ifuatavyo:-

(a) Matukio ya ujambazi wa kutumia silaha katika Vijiji vya Wilaya za Kibondo, Kigoma Vijijini, Kasulu, Mpanda na Nkasi. Katika baadhi ya matukio hayo doria ya JWTZ ilipambana na majambazi, kuwaua baadhi yao na kufanikiwa kukamata silaha na mabomu yaliyotumiwa na majambazi hayo.

(b) Katika kipindi cha Julai, 2002 hadi Mei, 2003 askari wa JWTZ wanaolinda mpaka waliweza kukamata kutoka kwa Waasi wa Serikali ya *DRC* na Burundi silaha ndogo aina ya *SMG* idadi 34, *G3* idadi nne, risasi 1,782 na mabomu ya mkono 12.

(c) Mwezi Novemba, 2002 wapiganaji wanane wa *CNDD -FDD* wakiwa na silaha walikamatwa na doria ya JWTZ katika eneo la Kililani katika hifadhi ya wanyamaporu ya Mahale. Walikuwa na silaha aina ya *SMG* 8 idadi nane, risasi za silaha hiyo 538 na *Magazine* 23.

(d) Mwezi Januari, 2003 Askari 40 wa jeshi la Burundi walivuka mpaka na kuingia katika ardhi ya Tanzania. Askari hao walikuwa wanaafutilia waasi wa Serikali ya Burundi waliodaiwa kukimbilia Tanzania kutafuta maficho. Doria ya JWTZ ilifanikiwa kudhibiti askari hao baada ya kurushiana risasi. Katika tukio hilo la kurushiana risasi raia mmoja wa Tanzania alifariki.

(e) Mwezi Januari, 2003 kiasi cha askari 40 wa Jeshi la Burundi wakiwa upande wa Burundi waliirushia risasi doria ya JWTZ iliyopo eneo la Manyara. Hata hivyo, askari wa JWTZ walijibu mapigo na hakuna madhara yaliyotokea.

(f) Kulikuwepo na askari wachache wa *DRC* walikamatwa na doria ya JWTZ wakiingia Tanzania huku baadhi wakiwa na silaha. Waliingia nchini kukimbia mapigano na hali mbaya ya maisha iliyopo nchini mwao.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama ya mpaka mmoja ilikuwa kama ifuatavyo:-

Kwanza, mpaka wa Magharibi (*Zambia*, *DRC*, Burundi na *Rwanda*) na pili, mpaka na nchi ya *Zambia*. Katika mpaka wa nchi ya *Zambia* hali ya ulinzi iliendelea kuwa shwari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpaka na nchi ya *DRC*. Hali ya ulinzi katika mpaka na nchi ya *DRC* ilitawaliwa na kuingia nchini kwa wakimbizi na wahamiaji haramu kutoka nchi hiyo na huku wengine wakiwa na silaha. Pia kumekuwepo na matukio ya utekaji wa boti za wavuvi kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika, ujambazi wa kutumia silaha zinazoingizwa nchini kinyemela na baadhi ya wakimbizi na wahamiaji haramu. Aidha, kulikuwepo na matukio ya kujisalimisha kwa askari wa Serikali ya *DRC*, wengine wakiwa na silaha, wanaokimbia mapigano nchini mwao.

Kuhusu mpaka wa Burundi, hali ya ulinzi katika mpaka na nchi ya Burundi ilikuwa shwari kwa wastani kutokana na hali ya mapigano ilivyokuwa ndani ya nchi hiyo. Katika mpaka huo askari wa Jeshi la Burundi waliwarushia risasi askari wa JWTZ waliokuwa katika doria, walifanya vitendo vya ujambazi wa kutumia silaha pia wakimbizi kutoka Burundi waliingia nchini. Pia yalikuwepo matukio ya kukamatwa au kuokotwa kwa silaha na risasi, kukamatwa kwa waasi wa Serikali ya Burundi walioingia nchini kutafuta maficho na askari wa Jeshi la Burundi kuvuka mpaka na kuingia nchini na kufanya vitendo vya kiharamia kama vile kupora mifugo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpaka wa nchi ya *Rwanda*, hali ya ulinzi katika mpaka na nchi ya *Rwanda* ilikuwa shwari. Hapakuwepo na matukio yenye kuhatarisha usalama kwenye eneo hilo. Tatizo la wakimbizi lililokuwepo katika miaka ya nyuma limezungu baada ya wengi wa wakimbizi kutoka nchi ya *Rwanda* waliokuwa Wilayani Ngara kurudi makwao kwa hiari. Tatizo lililopo katika eneo hilo ni kuwepo kwa wahamiaji haramu wa Kinyarwanda wanaoishi katika Vijiji mbalimbali Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpaka wa Kaskazini (*Uganda* na *Kenya*), hali ya ulinzi na usalama katika mipaka na nchi za *Uganda* na *Kenya* ilikuwa shwari, hapakuwepo na matukio yanayohatarisha usalama wa wananchi, mali na nchi kwa ujumla.

Kuhusu mpaka wa Mashariki (Bahari ya Hindi), hali ya ulinzi na usalama katika mpaka wa eneo la Bahari ya Hindi ilikuwa shwari na mpaka wa *Kusini* (*Msumbiji* na *Malawi*), hali ya ulinzi katika mpaka na nchi za *Msumbiji* na *Malawi* ilikuwa shwari katika kipindi cha 2002/2003. Hapakuwepo na matukio ya kuhatarisha usalama wa wananchi na mali. Hata hivyo, matatizo ya mpaka katika *Mto Songwe* na Ziwa

Nyasa, kwenye mpaka na nchi ya Malawi bado yanashughulikiwa katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, nilipowasilisha Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mwaka wa fedha 2002/2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Makadirio hayo ya Bajeti yalilenga kutekeleza mipango ifuatayo:-

Mipango hiyo ni kuwapatia wanajeshi na vijana wa JKT huduma muhimu kama sare, michezo na huduma za afya, kutoa mafunzo, mazoezi ya kijeshi na kitaaluma, kufanya matengenezo ya magari, mitambo na vifaa vingine vya kijeshi, kufanya matengenezo/kukarabati baadhi ya majengo katika makambi, kukamilisha viporo vya miradi ya ujenzi wa nyumba za kuishi wanajeshi katika makambi na huduma za maji safi, maji taka na umeme, kuendeleza utafiti na teknolojia ya kijeshi na hivyo kuongeza uwezo wa Jeshi kimapigano, kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kupata vitendea kazi bora na vya kisasa na kulipa mishahara na chakula kwa wanajeshi na mishahara ya watumishi raia.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na taasisi zake pamoja na kukabiliwa na ufinyu wa Bajeti upungufu wa vitendea kazi na mahitaji mengine muhimu, imetekeliza vilivyo, kwa juhudni na ufanisi mipango ya bajeti ya mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kufanikisha mipango ya Bajeti hiyo Bunge lako Tukufu liliidhinisha Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida, Fungu 38 - Ngome, mishahara shilingi 58,896,249,300/= sawa na asilimia 50. Chakula shilingi 19,400,000,000/= sawa na asilimia 16. Matumizi mengineyo shilingi 40,191,536,100/= ambayo ni sawa na asilimia 34. Jumla ni shilingi 118,487,785,400/= sawa na asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, Fungu 39 - JKT, mishahara ni shilingi 8,722,603,200/= sawa na asilimia 43, chakula shilingi 4,513,176,000/= sawa na asilimia 22 na matumizi mengineyo shilingi 7,193,783,600/= sawa na asilimia 35. Jumla ni shilingi 20,429,560,800 sawa na asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Fungu 57 - Wizara na Mashirika, mishahara shilingi 167,726,800/= ambayo ni asilimia tano, Ruzuku kwa Mashirika na Majenerali Wastaafu shilingi 3,018,855,200/= ambayo ni sawa na asilimia 78 na Matumizi Mengine shilingi 672,312,800/= sawa na asilimia 17. Jumla ni shilingi 3,858,894,800/= ambayo ni sawa na asilimia 100.

Mwelekeo wa matumizi kwa ujumla hadi mwisho wa mwezi Juni, 2003 kwa mafungu haya ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mhehsimiwa Fungu 38 - shilingi 118,487,785,400/= sawa na asilimia mia moja, Fungu 39 - shilingi 20,429,560,800/=sawa na asilimia mia moja na Fungu 57 - shilingi 3,858,894,800/= sawa na 100%.

Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika kipindi cha 2002/2003 ni shilingi 9,084,513,300/. Hadi ilipofika mwezi Mei, 2003, fedha zote zilizoidhinishwa zilikuwa zimetumika kwa utekelezaji wa miradi kadhaa iliyopewa kipaumbele kama vile Mtandao wa Mawasiliano ya Kipekee (*ITN*). Ujenzi wa Nyumba za makazi katika makambi ya Jeshi na malipo ya awali ya ndege ya usafirishaji ya JWTZ.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha Jeshi, hususan utekelezaji wa mpango wa Maendeleo wa Miaka 15 wa JWTZ (2002 - 2017). Mpango huo unaoinishwa mahitaji yake katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kulingana na uwezo wa Serikali kifedha, unalenga katika kuimarisha

uwezo wa JWTZ kwa kulipatia vifaa na zana bora za kisasa kwa ajili ya ulinzi wa nchi na kuwapatia wanajeshi mafunzo na mazoezi ya mbinu za kisasa za kimapigano na mafunzo ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya mkakati huo inayotekelawa sasa inaweka mkazo katika kurekebisha na kuimariswa upatikanaji wa huduma muhimu ya chakula, sare, tiba, makazi, usafiri na usafirishaji.

Katika mwaka 2002/2003, huduma ya chakula na mabwalo vikosini imeendelea kuboreshwa. Utaratibu wa kutumia kantini kuwalisha wanajeshi vikosini unaendelea kuimariswa kwani kwa kiasi kikubwa umewezesha kudhibiti kasi ya malimbikizo ya madeni. Hali ya upatikanaji wa sare za kawaida na za medani imeendelea kuwa ya kuridhisha na kwa wakati uliopangwa.

Aidha, huduma ya tiba Jeshini imeendelea kuimariswa ambapo katika mwaka 2002/2003, hatua muhimu zifuatazo zimeweza kufanikishwa:-

Hatua hizo ni uimarisaji wa Hospitali Kuu ya Jeshi na Hospitali za Kanda za JWTZ, hospitali Kuu ya Jeshi iliyopo Lugalo, Dar es Salaam imeendelea kuimariswa kwa kufanyiwa ukarabati na kuwekwa vifaa muhimu vya kisasa. Hii ikiwa pamoja na kujengwa kwa chumba cha wagonjwa mahututi (*Intensive Care Unit*), hospitali ya Kanda ya Mbeya imefanyiwa ukarabati kwa ghamama ya shilingi milioni 116 zilizotolewa na Serikali ya Ujerumani kama msaada kwa Serikali ya Tanzania. Ukarabati huo umekamilika na hospitali ya Kanda ya Mwanza imefanyiwa ukarabati kwa ghamama ya shilingi milioni 200 zilizotolewa na Serikali ya Ujerumani kama msaada kwa Serikali ya Tanzania.

Pia hospitali ya Kanda ya Bububu, Zanzibar imeimarishwa kwa kufanyiwa ukarabati wa wodi mbili, moja ya wanawake na nyingine ya wanaume. Aidha, jengo la chumba cha maiti linaendelea kukarabatiwa. Ukarabati huo umehusisha kubomoa majengo ya mbaao na kujenga ya matofali na hadi mwisho wa mwezi Mei, 2003 shilingi milioni 11 kutoka bajeti ya Serikali ilikwishatumika kwa ajili hiyo na hospitali ya Kanda ya Monduli, Arusha imefanyiwa ukarabati katika maeneo ya *X-Ray*, chumba cha meno, chumba cha upasuaji, chumba cha kuzalia na wodi yake. Ukarabati huo umefanyika kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, pia kufundisha wataalam ili wawe na kiwango cha juu cha utaalam katika fani mbalimbali na kuimariswa upatikanaji wa dawa kwa ajili ya wagonjwa pamoja na vifaa vya kisasa vya hospitali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea na utekelezaji wa programu inayolenga kutanzua tatizo la uhaba wa nyumba za makazi Jeshini. Utekelezaji huo unahusisha ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi katika makambi mbalimbali ya Jeshi.

Baada ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za kuishi familia 90 katika Kambi ya Ihumwa - Dodoma uliogharimu shilingi milioni 443.4, juhudzi zimeelekezwa katika kukamilisha nyumba zilizoko katika kambi ya Sofa - Arusha. Katika mwaka huo nyumba za kuishi familia 28 zilikamilishwa kwa ghamama ya shilingi milioni 358.8 na hivi sasa zinakaliwa na askari. Nyumba zingine za kuishi familia 38 ujenzi wake unaendelea na zinatarajia kukamilishwa ifikapo mwezi Agosti, 2003. Nyumba hizo zitagharimu shilingi milioni 673. Baada ya kukamilisha ujenzi wa nyumba 38, ujenzi wa nyumba 28 zilizokamilishwa mwaka 2002/2003, pamoja na nyumba 24 zilizokamilishwa mwaka 1996, kambi hiyo ya Sofa - Arusha itakuwa na nyumba za kuishi familia 90.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kufanya juhudzi kuhakikisha kuwa tatizo la usafiri na usafirishaji wa anga, majini na nchi kavu linapatiwa ufumbuzi.

Katika mwaka 2002/2003 juhudzi zimefanywa kulinunulia JWTZ ndege mbili kubwa za usafirishaji aina ya Y-8 kwa ajili ya kusafirisha wanajeshi wakati wa amani na wakati wa dharura au maafa. Ndege hizo zitagharimu shilingi bilioni 30.8. Malipo ya awali ya shilingi bilioni 3.0

yamekwishafanya na katika mwaka 2003/2004 shilingi bilioni 13.5 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za kutatua tatizo la usafiri na usafirishaji zimehusisha pia programu ya kuvifanya matengenezo, kuvifufua na kuvikarabati vifaa vilivyoaribika ili viweze kutumika. Chini ya programu hiyo JWTZ limeweza kufufua meli yake moja katika Ziwa Tanganyika iliyokuwa haifanyi kazi kwa muda mrefu. Hivi sasa meli hiyo inatumika katika majukumu ya kiulinzi katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na mazoezi kwa maafisa na askari yameendelea kutolewa. Maafisa na askari wamefanya kozi na mafunzo katika fani zao katika vyuo vya kijeshi hapa nchini na baadhi yao wameshiriki katika mazoezi ya kulinda amani pamoja na majeshi ya nchi zingine nje ya nchi. Katika kipindi cha 2002/2003 pamoja na maafisa na askari kufanya mazoezi binafsi, JWTZ liliendesha mazoezi ya vikundi na mazoezi ya *Brigade*. Mazoezi ya Brigade yalifanyika Arusha, Songea, Tabora na Zanzibar. Mazoezi hayo yameendelea kuvizoeza vikundi vya fani mbalimbali ndani ya JWTZ kufanya kazi za medani pamoja kuwapatia wanajeshi nafasi ya kuelimishana juu ya matumizi ya bora ya vifaa na zana pamoja na kuwajenga ukakamavu.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya rasimu ya Sera ya Ulinzi wa Taifa yalikamilika katika kipindi cha 2002/2003 baada ya kupokea na kuzingatia maoni kutoka Taasisi mbalimbali zinazohusika moja kwa moja na suala la ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Hata hivyo, kabla ya rasimu hiyo haijaweza kuwasilishwa kwa vyombo husika kwa ajili ya kupata idhini, ilionekana kwamba ipo haja kwa sera hiyo kuwa na matamko kuhusu shughuli za Ulinzi wa Umma au Mgambo na pia shughuli za Viwanda na Karakana za Kijeshi.

Kwa hiyo, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliitisha warsha mbili tofauti zilizohusisha wadau mbalimbali kwa lengo la kupata maoni yao kuhusu maeneo hayo mawili. Kazi ya kuainisha maoni hayo ili kupata matamko hayo yatakayojumuishwa katika rasimu ya Sera ya Ulinzi wa Taifa inakamilishwa na zoezi la kuandaa sera hiyo linategemewa kukamilika katika kipindi cha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 27(1), (2) na Ibara ya 28 (1) kila mwananchi ana jukumu la ulinzi na usalama wa mali na Taifa. Kutokana na wajibu huo, sera yetu ya ulinzi inabainisha kwamba umma wa Tanzania utaandaliwa ili kupata nguvu za kiulinzi (Mgambo) wakati wa vita na dharura. Jukumu hilo la kuandaa umma wa Tanzania ili kupata nguvu hiyo ni la JWTZ kwa kutoa mafunzo kuhusu kulinda, kutetea na kuhifadhi umoja, uhuru na mshikamano wa Taifa. Kwa maandalizi hayo umma wa Tanzania uliopatiwa mafunzo hayo umetoa mchango mkubwa katika jukumu la ulinzi wa nchi, wananchi pamoja na mali zao. Mchango huo umedhihirika katika ulinzi wa maeneo mbalimbali katika nchi yetu hasa katika kukabiliana na wimbi la ujambazi na uhalifu wa kila aina unaotokea hapa nchini hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, JWTZ imeendesha mafunzo ya mgambo katika Kanda za Kusini (Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma), Kanda ya Mashariki (Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Morogoro, Mtwara na Pwani), Kanda ya Zanzibar (Mikoa yote ya Tanzania Visiwani), Kanda ya Kaskazini (Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida na Tanga) na Kanda ya Magharibi (Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza, Shinyanga na Tabora). Mafunzo hayo yameendeshwa katika ngazi ya mafunzo ya awali, mafunzo ya kujikumbushia, kozi ya uongozi mdogo na kozi ya uongozi mkubwa. Malengo yaliyowekwa kuhusu mafunzo hayo yalifikiwa. Aidha, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, kuitia JWTZ, katika kipindi cha 2002/2003 imefanya uteuzi wa Maafisa wa Mgambo katika baadhi ya Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano katika nyanja ya kiulinzi na nchi nyingine ni muhimu kwa Tanzania ili kuweza kujiletea maendeleo ya Kijeshi, kuzidisha maelewano ya kidiplomasia, kudumisha amani na utulivu ndani ya nchi, katika ukanda wetu huu wa Afrika na duniani kwa ujumla. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kuenga Taifa imeendelea kufanya juhudzi kupanua na kuimarisha ushirikiano na Serikali

za nchi mbalimbali uliojengeka juu ya misingi inayotambua, kuheshimu na kulinda haki na uhuru wa kila nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, katika mwaka 2002/2003, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imefikia makubaliano ya kushirikiana na Serikali za nchi kadhaa katika maeneo mbalimbali. Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imetoa nafasi za kozi za mafunzo katika Vyuo vya Kijeshi vya China kwa Maafisa wa JWTZ.

Pia Serikali ya China katika mwaka 2002/2003 imetoa msaada wa Dola za Kimarekani milioni 9.8 kwa ajili ya kununulia vifaa na zana za Kijeshi kwa JWTZ. Aidha, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa Tanzania Jenerali George Waitara, alifanya ziara nchini China mwezi Agosti, 2002 na Mkuu wa Jeshi la Ukombozi la Watu wa China (*PLA*) Jenerali Liang Guanglie, alifanya ziara nchini Tanzania mwezi Mei, 2003.

Serikali ya Ujerumani katika mwaka 2002/2003 imetoa nafasi za kozi za mafunzo katika Vyuo vya Kijeshi nchini Ujerumani kwa Maafisa wa JWTZ na kutoa msaada wa kukarabati Hospitali Kuu ya Kijeshi, Hospitali za Kanda za JWTZ zilizoko Mbeya, Mwanza na Arusha pamoja na kukarabati karakana Kuu ya Kijeshi.

Vile vile Serikali ya Ujerumani imetoa msaada wa matibabu nchini Ujerumani kwa baadhi ya Maafisa na Askari wa JWTZ pamoja na familia zao. Serikali za Canada, India, Ufaransa, Uingereza na Marekani katika mwaka 2002/2003 zimetoa nafasi za kozi za mafunzo kwa maafisa wa JWTZ katika Vyuo vya Kijeshi nya nchi zao pamoja na misaada ya kibinadamu kwa JWTZ.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki umeendelea kuratibiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mpango wa utekelezaji wa mkataba huo ulisainiwa na Mawaziri wa Ulinzi huko Nairobi, Kenya tarehe 7 Machi, 2003. Mpango huo umelenga ushirikiano katika maeneo ya mafunzo, operesheni za pamoja za kulinda amani na kukabiliana na maafa, ushirikiano katika nyanja za kiufundi (*Technical Assistance*) pamoja na michezo na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa kiulinzi na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) umeendelea kuimashwa katika maeneo mbalimbali. Majeshi ya nchi hizo yameendelea kushirikiana katika kutoa nafasi za kozi za mafunzo katika vyuo vyao ili kubadilishana ujuzi na kupata uzoefu wa kuimashwa utendaji wao. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa makubaliano ya kiulinzi ya Jumuiya hiyo ikiwa pamoja na kushiriki katika vikao kwenvye ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napenda kuchukua nafasi hii, kuzishukuru Serikali za nchi zote tulizoshirikiana nazo katika maeneo hayo katika kipindi cha 2002/2003. Aidha, napenda kutoa shukrani maalum kwa Serikali za Jamhuri ya Watu wa China kwa misaada yao kwa JWTZ na JKT. Tunathamini sana ushirikiano na misaada yao ya kirafiki na ya kihistoria.

Napenda pia kutoa shukrani kwa Serikali za Ujerumani, Ufaransa na nchi zingine ambazo zimetupatia misaada. Misaada ya Serikali hizo imekuwa na mchango mkubwa katika kuliimashwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushirikiano na Serikali za nchi moja moja na ushirikiano wa kikanda katika maeneo mbalimbali, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika kipindi cha 2002/2003 imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa ushirikiano na nchi za Falme za Nchi za Kiarabu, Ghana, Indonesia, Italia, Misri, Nigeria, Nchi za *Nordic* na Urusi. Napenda pia kuzishukuru Serikali za nchi hizo kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, JWTZ imeendelea na utekelezaji wa jukumu lake lingine la kusaidia Mamlaka za kiraia na ilitekeleza shughuli zifuatazo, Operesheni Uvuvi Haramu. Ikishirikiana na Idara ya Maliasili na Polisi, JWTZ imeendelea kuendesha operesheni ya kupambana na

majambazi yanayojihusisha na uvuvi haramu katika maeneo ya nchi katika Bahari ya Hindi na kusindikiza Meli za Kiraia na kufanya doria katika Ziwa Tanganyika. Ili kudhibiti vitendo vyatujambazi vinavyofanywa katika Ziwa Tanganyika dhidi ya wananchi (hasa wavuvi) pamoja na mashambulizi dhidi ya meli za kibashara kati ya nchi za Zambia, DRC, Burundi na Tanzania, JWTZ kwa kusaidiana na Polisi pamoja na Idara ya Maliasili imeendelea kufanya doria katika ziwa hilo na pia kusindikiza meli hizo za kibashara pale ilipobidi kufanya hivyo.

Pia Operesheni Kamata Majambazi Mko wa Kagera (KAMAKA). Operesheni KAMAKA iliyofanyika tarehe 25 hadi 29 Julai, 2002 kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama Mkoani Kagera bado inaendelea kuendeshwa na JWTZ kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo mbalimbali, matembezi ya Kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

JWTZ ilitoa vijana walioshiriki katika matembezi ya Kumuenzi Baba wa Taifa yaliyofanyika mnamo tarehe 14 hadi 28 Oktoba, 2003. Matembezi hayo yalianzai Dar es Salaam na kupokelewa na Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa katika Ikulu ya Chamwino, Dodoma tarehe 28 Oktoba, 2002. Katika sherehe ya mapokezi ya matembezi hayo, Amiri Jeshi Mkuu alitoa hati maalum ya ponezi kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Makuu wa Jeshi la Kujenga Taifa kama ishara ya utambulisho kwa michango ya maafisa na wapiganaji katika matembezi hayo.

Mheshimiwa Spika, pia Operesheni Shinda Malaria, JWTZ ilishiriki katika maadhimisho ya siku ya Malaria Afrika (*Malaria Day*) kwa kusindikiza msafara maalum wa nchi za SADC kutoka Tunduma hadi Dar es Salaam kwa kutoa huduma za utawala ikiwemo ujenzi wa mahema, huduma za afya na mawasiliano na Operesheni za kulinda amani ambayo JWTZ imeendelea kushiriki katika Operesheni za Umoja wa Mataifa za kulinda amani katika nchi mbalimbali za Afrika ambazo zimekumbwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Katika mwaka 2002/2003, JWTZ lilipeleka Maafisa katika nchi za Siera Leone, Ethipoia na Eritrea kama waangalizi katika Jeshi la Umoja wa Mataifa (*UNMIL*)s) katika operesheni za kulinda amani.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuelimisha na kuandaa vijana wa Tanzania, kielimu, kimaadili na kinidhamu kuwa raia wema, kuipenda, kuitumikia na kuilinda nchi yao, kuwapenda, kuwatumikia na kuwalinda Watanzania wenzao na kuwa na silika ya kupenda kazi za mikono na kujitegemea limeendelea kutekelezwa katika makamby ya JKT. Yamekuwepo mafanikio makubwa tangu mafunzo hayo yarejeshwe tena mwaka 2001. Umakini unaoonyeshwa na vijana wa Operesheni Mkapa, kundi la kwanza la vijana kuijunga na mafunzo ya JKT tangu yarejeshwe, katika ushiriki wao kwenye shughuli za kiulinzi, uokoaji wa maisha ya watu na mali, urejeshwaji wa huduma baada ya kutokea maafa, uaminifu na upendo kwa raia wenzao umedhiihirisha umuhimu wa mafunzo hayo kwa jamii yetu kama ilivydhamiriwa na Waasisi wa mafunzo ya JKT chini ya uongozi wa Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Vijana hao wamekuwa mfano wa kuigwa na vijana wenzao ambao hawakupata mafunzo hayo hasa wakati huu ambapo kuna dalili ya jamii yetu kutikisika kimwenendo na kimaadili. Tunampongeza na kumshukuru Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa kwa kukubali kurejeshwa kwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tunaadhimisha miaka 40 ya Jeshi la Kujenga Taifa lenye dhamana ya kuendesha mafunzo hayo katika makambi yake. Sherehe za kuadhimisha miaka 40 ya JKT zilifanyika tarehe 4 Julai, 2003 katika Kambi ya JKT, Ruvu na kuzinduliwa na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Rais Benjamin Wiliam Mkapa na kuhudhuriwa na Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mabalozi, Waasisi na Wakuu wa zamani wa JKT, viongozi wastaafu na umati mkubwa wa Wananchi wa Mkoa wa Pwani.

Aidha, kilele cha sherehe za miaka 40 ya JKT zilifungwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, tarehe 10 Julai, 2003 katika Kambi ya JKT, Mgulani. Katika kipindi cha miaka 40, JKT, ilioanzishwa tarehe 10 Julai, 1963, mionganoni mwa Taasisi za awali za matunda ya Uhuru wa nchi yetu,

imedhihirisha kuwa ni chombo muhimu kwa jamii yetu kwa kutoa mchango mkubwa katika shughuli za Kitaifa za ujenzi, ulinzi, uzalishaji mali, umoja, mshikamano na amani katika nchi yetu.

Watanzania wengi wamenufaika na mafunzo ya JKT ambapo baadhi yao sasa ni wataalam na wengine ni viongozi wetu katika Serikali, asasi, Mashirika, Makampuni na sehemu nyingine. Inatia moyo kuona kuwa vijana wetu wengi nao wameendelea kuvutiwa na kuthamini umuhimu wa mafunzo hayo. Hii imejidhihirisha katika idadi kubwa ya vijana wanaojitokeza kutaka kujiunga na mafunzo hayo tangu uliporejeshwa utaratibu wa uchukua ji wa vijana katika makambi ya JKT mwaka 2001.

Hata hivyo, kikwazo kimekuwa nafasi finyu zilizopo za vijana wanaoweza kuchukuliwa. Kwa mfano, katika mwaka 2001 vijana 200,000 walijitokeza kutaka kujiunga na mafunzo ya JKT ambapo ni vijana 2,488 tu walioweza kupata nafasi na mwaka huu vijana 570,000 walijitokeza lakini walioweza kupata nafasi ni vijana 2600 tu. Serikali inaendelea kuangalia namna bora ya kukidhi utashi huo kwa kutafuta uwezo wa kuongeza nafasi za vijana wa kujiunga na mafunzo ya JKT. Kudhihirisha dhamira ya Serikali juu ya suala hili napenda kumukuu Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa wakati alipozindua sherehe za miaka 40 ya JKT kwamba: "Jeshi la Kujenga Taifa litadumishwa kwa faida ya vijana wetu wa leo, na kwa faida ya vizazi vijavyo."

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na kupitia Bunge hili kuwafahamisha wananchi kwamba vijana 1,611 waliojiunga na JKT mwezi Oktoba, 2001 wa Kundi la Operesheni Mkapa, sasa wamechukuliwa na JWTZ. Kati ya vijana hao asilimia 70 ni wavulana na asilimia 30 ni wasichana. Vijana wengine 50 (wavulana) wa kundi hilo wamechukuliwa na *TANAPA* na vijana 40 wamechukuliwa na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

Napenda kuwapongeza wakuu wa vyombo vyote vilivyowachukua vijana hao. Maamuzi yao ni mfano wa wazi wa utekelezaji wa sera ya Serikali iliyositisizwa na Mheshimiwa Rais alipozindua sherehe za kuadhimisha miaka 40 ya JKT kwamba "Jeshi la Kujenga Taifa litaendelea kuwa chemchem ya ajira ya kudumu kwa vyombo vyote vya ulinzi na usalama". Ninawaomba wakuu wengine wa vyombo vya ulinzi na usalama vilivyobaki nao waige mfano huo.

Mheshimiwa Spika, vijana wengine walibakia wa Operesheni Mkapa wamegawanywa na kupatiwa mafunzo ya uzalishaji mali katika makambi ya Makutopora ambako wanajifunza kilimo cha zabibu na bustani za mboga, Ruvu wanajifunza ufugaji kuku na ushonaji nguo na Maramba wanajifunza kilimo cha kakau. Mafunzo ya ufundi stadi kwa mitaala ya *VETA* yalitegemewa kuanza kutolewa kwa vijana walio katika makambi baada ya kupatikana kwa vifaa vya mafunzo hayo vilivyonunuliwa kwa gharama ya shilingi milioni 450. Vifaa hivyo vinaendelea kufungwa katika makambi ya Makutopora – Dodoma, Mgulani – Dar es Salaam, Maramba – Tanga, Ruvu – Pwani na Mlale – Ruvuma. Kazi ya kufunga vifaa hivyo inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa makambi ya JKT umeendelea kufanya katika mwaka 2002/2003 huku msisitizo ukiwekwa katika kuyakamilisha makambi yaliyotengwa kwa ajili ya mafunzo ya awali kwa vijana yaani *Central Training Schools*. Katika mwaka huo makambi ya Mafinga na Oljoro yalikarabatiwa. Hatua hiyo iliwezesha, pamoja na kuendelea kuendesha mafunzo kwa vijana wa Operesheni Mkapa, kuchukuliwa kwa vijana 2600 wa Operesheni Miaka 40 ya JKT katika kambi za Makutopora, Oljoro na Ruvu mwezi Februari, 2003. Vijana hao wanatarajiwa kumaliza mafunzo ya awali ya kijeshi ya miezi sita mwezi Agosti mwaka huo kabla ya kuendelea na awamu ya pili ya mafunzo yatakayojumuisha ufundi stadi, kilimo na ufugaji.

Kambi ya Mafinga imetengwa kwa ajili kuendesha mafunzo ya awali ya askari wapya wa JWTZ kutokana na vijana waliochukuliwa kutoka JKT. Makambi mengine ya Maramba, Itende na Mlale ambayo yanaendesha mafunzo ya awamu ya pili ya uzalishaji mali na ufundi stadi yanaendelea kukarabatiwa ili yaweze kuchukua vijana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (*SUMA JKT*) imeendelea kuboresha shughuli zake za uzalishaji mali na kujipanga vizuri zaidi. *SUMA JKT* limefanya upembuzi yakinifu, limepanga vizuri kwa upande wa muundo, menejimenti na utaalam na kufanya tathmini ya raslimali zake.

Lengo ni kuiwezesha *SUMA JKT* kupanua na kuendesha miradi yake kibiashara ili kupata faida kubwa zaidi. Aidha, hatua hizo zimelelenga kuliwezesha *SUMA JKT* kupata mikopo ya mitaji kutoka Mabenki pamoja na kuingia ubia na wawekezaji wengine katika miradi yake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, *SUMA JKT* limefanya yafuatayo, shirika lilitkeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji mali na kuingiza mapato ya shilingi bilioni 1.2 kwa kutumia gharama ya shilingi milioni 964.0, Kati ya mapato hayo miradi ya ujenzi iliingiza shilingi milioni 843.3, miradi ya kilimo, ufugaji na uvuvi shilingi milioni 164.1 na miradi ya viwanda shilingi milioni 156.5. Mapato na matumizi hayo ni nje ya yale yatakayopatikana kutokana na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba 150 za makazi ya wafanyakazi wa Serikali wenye thamani ya shilingi bilioni 3 huko Mbweni, Dar es Salaam. Mkataba kuhusu mradi huo umeishasainiwa na utekelezaji unaendelea. Napenda kutoa shukrani zangu na za viongozi na wapiganaji wetu kwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli kwa kuiwezesha *SUMA JKT* kupata mradi huo. Namshukuru kwa uamu wake wa kimapinduzi.

Pia kiwanda cha ubia cha kutengeneza dawa za binadamu cha Mgulani, Dar es Salaam (*TANZANSINO*) kilichoanza kwa kutengeneza aina mbili za dawa (*Paracetamol* na *Aspirin*), hivi sasa kinatengeneza dawa zifuatazo, *Paracetamol*, *Aspirin*, *Metronidazole*, *Diclofenac*, *Ibuprofen Compound*, *Magnesium Trisilicate*, *Sulphadoxine (SP)* na *Pyimethamine*, *Indomethacin Capsules*). Dawa nyingine ya kutibu malaria inayoitwa *Artemec* tayari imeanza kutengenezwa kwa majaribio.

Aidha, kiwango cha uzalishaji wa dawa kiwandani kimepanda kutoka vidonge 400,000 hadi 1,400,000 kwa siku. Kiwanda cha *TANZANSINO* kimepata tuzo ya Kimataifa inayoitwa “*The 17th International Quality Summit Award for Excellency and Business Prestige in Gold Category*” ambayo imetolewa huko New York, Marekani tarehe 14 Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, hatua za awali za kuanzishwa kwa kiwanda cha ushonaji nguo na viatu kati ya *SUMA JKT* na Kampuni ya kibiashara kutoka China zinaendelea kuchukuliwa na zoezi la kutenganisha mali za *SUMA JKT* na zilizo za Serikali limekamilika na kinachoendelea sasa ni kufanya tathmini ya mali hizo. Pia zoezi la upimaji wa maeneo ya JKT ili kuwezesha upatikanaji wa hati miliki za maeneo hayo linaendelea. Upatikanaji wa hati hizo ni hitajio muhimu la kuiwezesha *SUMA JKT* kuingia ubia na wawekezaji wengine wanaoonyesha nia hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha hayo, *SUMA JKT* litatekeleza kuwa sekta ya Kilimo na Ufugaji. Kutumia zana na mbinu bora za kitaalam bila kutegemea sana mvua. Aidha, hatua zitachukuliwa za kusindika mazao badala ya kuyauza yakiwa ghafi, hivyo kuongeza thamani ya mazao hayo kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo, sekta ya Ujenzi. Kuongeza kiwango cha utaalami pamoja na kuweka utaratibu na mipango mizuri iliyo endelevu ya ufuatiliaji na uendeshaji miradi na miundombinu kwa kuwatumia wataalam waliopo na kushirikiana na wawekezaji wengine wa ndani na nje ya nchi na sekta ya Viwanda kuvipatia Viwanda uwezo wa kutengeneza bidhaa za aina mbalimbali vyenye ubora wa viwango vya juu ili kukidhi mahitaji na ushindani katika soko. Aidha, unaangaliwa uwezekano wa kuanzisha na kuimarisha shughuli nyingine kama vile biashara za hoteli na utalii, usafiri na usafirishaji, uchapishaji na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuridhia utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa mtandao wa *ITN*, maandalizi yamekuwa yakifanywa ili kuweza kuutumia mtandao huu kikamilifu kwa kutekeleza programu mbalimbali za Serikali. Pamoja na kuimarisha huduma ya mawasiliano katika Jeshi, awamu ya tatu ya mtandao huu una lengo la kutekeleza Sera ya *Taifa ya Information and Communication Technology (ICT)* kwa kujenga muundombinu wa Serikali elektroni (*E-Government*) pamoja na kuhudumia watumiaji wengine.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Serikali elektroni utaunganisha mitambo ya mawasiliano ya sauti, video na kompyuta ya Serikali hadi ngazi ya Wilaya. Aidha, Hospitali Kuu zote za Mikoa na Rufaa pamoja na Ofisi za Mamlaka ya Mapato (*TRA*) zitaunganishwa katika muundombinu mmoja. Serikali inaangalia uwezekano wa muundo mbinu huu kutumika katika kurusha matangazo ya televisheni ili nayo yaweze kuonekana nchi nzima.

Utekelezaji wa mradi huu unategemewa kuanza katika mwaka 2003/2004 na utagharimu dola za Marekani milioni 54. Gharama hii itachangiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Ubelgiji ambayo itachangia asilimia 60 kama mkopo nafuu kwa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Tanzania ambayo itachangia asilimia 40. Mfumo huu utakuwa wa kwanza wa aina yake katika Afrika na utaliweka Taifa katika hali bora zaidi ya kushiriki katika utandawazi na kwa gharama nafuu zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kampuni ya MEREMETA imesitisha shughuli zake za Geita, Tembo na Nyamahuna ili iweke nguvu zake zote kwenye kukamilisha mradi wa mgodi wa Buhembba.

Nafurahi kueleza kwamba uzalishaji wa dhahabu kwenye mgodi wa Buhembba, ulianza mwezi Januari, 2003 na ilipofikia mwezi Juni, 2003 dhahabu iliyochimbwa ilikuwa ya wakia 32,265.3. Madini mengine yenye thamani yaliyoweza kupatikana wakati wa kusafisha dhahabu hiyo ni wakia 1,500 za madini ya fedha (*silver*) ambayo nayo yatauzwa. Dhahabu hiyo baada ya kusafishwa iliuza na kuipatia Serikali ya Tanzania jumla ya Dola za Marekani 10,646,291.

Mheshimiwa Spika, gharama za uchimbaji, usafishaji na uuzaji wa dhahabu hiyo ilikuwa Dola za Marekani 9,075,626. Fedha zilizobaki yaani Dola za Marekani 1,570,665 zimetumiwa na MEREMETA kwa kulipia sehemu ya mkopo uliotumika kununulia radio zinazotumiwa sasa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na vifaa vya huduma kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa mradi wa Mgodi wa Buhembba unaendesha shughuli zake chini ya Kampuni ya MEREMETA ambayo imeundwa kwa sababu maalum ya kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo amba kwa kukosa soko rasmi, wanaauza dhahabu nyingi kwa walanguzi wasiojali maendeleo ya wachimbaji hao wala uchumi ipasavyo Kampuni ya MEREMETA imeingia Mkatuba na Kampuni ya *Jeffares and Green* ya Afrika Kusini ambayo kwa utaratibu wa *Sub- Contract* inasaidiana na Kampuni ya *WBHO – Construction (Pty) Limited* kwa ajili ya uchimbaji wa mgodi na kampuni ya *Time mining (Pty) limited* kwa ajili ya usimamizi wa mitambo ya kutenganisha dhahabu kutoka kwenye udongo kutoka kwenye mgodi. Makampuni haya hayamo kwenye ubia wala uwakala na Kampuni ya MEREMETA bali ni makandarasi tu wanaohusika katika utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mapato yatakayopatikana kutokana na uuzaji wa dhahabu katika Mgodi wa Buhembba yatatumika kwa kugharamia shughuli zote za uendeshaji na uchimbaji dhahabu katika mgodi wa Buhembba, kulipia mikopo iliyochukuliwa hapo awali na Kampuni ya MEREMETA kwa ajili ya Redio Maalum zinazotumiwa na JWTZ hivi sasa, vifaa mbalimbali vinavyotumiwa na wachimbaji wadogo katika maeneo mengi ya Wilaya ya Geita yanayosaidiwa na mradi wa MEREMETA, mtambo (*hub*) wa kusindika udongo wenye dhahabu utakaosimikwa huko Nyamahuma Geita, mitambo ya Mgodi wa Buhembba ambayo hivi sasa imeanza kuzalisha dhahabu, ujenzi wa bomba la maji kutoka Bwawa la Kyarano hadi Buhembba na ujenzi wa huduma mbalimbali kwa jamii kama vile shule na kadhalika katika maeneo yaliyo karibu na mradi huo.

Pia kufanya uchunguzi (*exploration*) zaidi katika maeneo yaliyo karibu na Mgodi wa Buhembba kwa lengo la kuupatia mradi huo maeneo zaidi ya kuchimba dhahabu.

Mheshimiwa Spika, ni vema Bunge lako Tukufu lifahamu kwamba Mgodi wa Buhembba unatarajiwa kuendelea na uzalishaji katika kipindi cha miaka kumi hadi kumi na mbili. Mambo yakienda kama yaliivyoangwa mgodi huu utaweza katika kipindi cha miaka sita hadi saba, kulipia mikopo yote iliyotajwa hapo juu iliyochukuliwa na Kampuni ya MEREMETA kutoka Benki ya Afrika Kusini iitwayo *NEDBANK*. Baada ya hapo faida itakayotokana na shughuli za mgodi huo zitakuwa ni pato la Serikali ambayo itaelekeza zitumike kwenye maeneo yatakayopewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa mipango inakamilishwa ili mitambo iliyokwishanunuliwa ya kusindika udongo wenye dhahabu isafirishwe kutoka Afrika Kusini kuja kusimikwa Tembo au Nyamahuna na kuanza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa *hub* hiyo utakwenda sambamba na kampuni ya MEREMETA kuendelea na jukumu lake la ununuzi wa dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo na kuuza dhahabu hiyo baada ya kusafishwa. MEREMETA itaendelea kuwasaidia wachimbaji wadogo wa dhahabu hapa nchini kwa kuwapatia vifaa na huduma mbalimbali za kuongeza ufanisi pamoja na kuendelea na uchimbaji wa mashafti ya dhahabu yaliyoko Tembo na Nyamahuna. Shughuli hizi za MEREMETA zinatarajiwa kuanza katika kipindi cha Septemba na Oktoba, 2003.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeunda timu ya Watalaam ambayo imepewa jukumu la kuhakikisha kwamba mgodi wa Buhemba unatekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kusimamiwa ipasavyo ili mgodi huo ujiendeshe wenyewe kibashara. Timu hiyo ya wataalam pia itaweka mwelekeo ambao utauwezesha mgodi wa Buhemba kujiendesha kama Kampuni inayojitegemea kisheria wakati Kampuni ya MEREMETA inaendelea kutekeleza majukumu yaliyoelezwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Mzinga limeendelea kukabiliwa na uchakavu na teknolojia ya kizamani ya mitambo ya kiwanda chake na hivyo kuathiri jukumu lake la msingi la kuzalisha risasi. Kwa sababu hiyo katika mwaka 2002/2003 Shirika hili limeendelea na utekelezaji wa shughuli mbadala za kutafiti na kuzalisha bidhaa zisizo za kijeshi kama vile baruti za kibashara zinazotumiwa kwenye migodi, baruti maalum za kufukuzia wanyama au ndege waharibifu mashambani, risasi za aina mbalimbali za *shot gun*, breki za gari moshi, mashine ndogo za kupasua, kuranda na kukereza mbao, pamoja na samani za kisasa kwa kiwango cha Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Mzinga pia limeendelea kuagiza kutoka nje silaha, risasi na milipuko aina mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya kiraia. Bidhaa hizo huuzwa kwa wateja wa ndani katika maduka ya Shirika hilo yaliyopo Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga na Arusha. Katika kupanua huduma kwa wananchi, Shirika la Mzinga katika kipindi cha 2003/2004, litafungua duka lake lingine mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mitambo ya kiwanda cha Shirika la Mzinga imechakaa sana na upatikanaji wa vipuri ni mgumu na kupelekea ufanisi na tija kuwa chini mno. Serikali kwa kutambua umuhimu wa kiwanda hiki kwa Jeshi, imeridhia utekelezaji wa mpango wa kukifufua, kukiimarisha na kukiendeleza. Mpango huo utahusisha ununuzi na usimikaji wa mitambo ya kutengeneza risasi za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mitambo hiyo itagharimu shilingi bilioni 7.4 na itakuwa na uwezo wa kuzalisha risasi za aina mbalimbali milioni 42 kwa mwaka ukizalisha kwa utaratibu wa shifti mbili kutoka uzalishaji wa risasi milioni 1.5 wa sasa. Utekelezaji wa mpango huo unategemewa kuanza katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumbu limeendelea kukabiliwa na ukosefu wa mtaji kwa ajili ya utafiti na kuendeleza teknolojia ya magari. Kutokana na hali hiyo, katika mwaka 2002/2003, Shirika limeendelea kutekeleza shughuli mbadala za kutoa huduma za kiufundi kwa viwanda taasisi na makampuni mbalimbali kwa kusani na kutengeneza mitambo.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Shirika la Nyumbu zimekwama kutokana na kushindwa kuhawilisha teknolojia (*Technology Transfer*) ya magari hadi kufikia uwezo wa kuyazalisha kibashara. Programu ya kuhawilisha teknolojia hiyo inahitaji fedha nyingi kwa ajili ya uwekezaji katika mitambo, miundombinu na wataalam.

Mwaka 2002 nililitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imeombwa iishawishi Kampuni ya *First Automobile Works (FAW)* iliyoko China kushirikiana na Shirika la Nyumbu katika programu hiyo. Hata hivyo, nasikitika kueleza kwamba juhudzi za kuishawishi kampuni hiyo zimeshindikana kwa sababu Kampuni hiyo imetoa masharti ambayo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa haikuafikiana nayo. Serikali inaendelea na juhudzi za kumpata mbia wa kushirikiana naye katika kutekeleza programu hiyo na majukumu yanayoambatana nayo.

Mheshimiwa Spika, juhudi zimeendelea kufanywa kuboresha huduma ya maduka ya bei nafuu Jeshini kwa kurekebisha mapungufu yaliyotokea katika uendeshaji wa maduka hayo. Mapungufu hayo yapo katika bei za bidhaa, bidhaa zisizokidhi mahitajio ya walengwa, udhaifu katika uongozi na uendeshaji, kushindwa kuzingatia mikataba iliyowekwa, mitaji finyu ya waendeshaji na kukosekana kwa uaminifu na uadilifu kwa baadhi ya waendeshaji wa maduka hayo.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kudhibiti kuenea kwa Ukimwi ndani ya vyombo vya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekelezwa. Mikakati hiyo inalenga katika kinga, tiba na uhamasishaji wa mashirikiano ya karibu sana na sekta ya afya, Chuo cha Sayansi ya Afya Muhimbili, Kamisheni ya Ukimwi nchini na wafadhili mbalimbali kuhusu utekelezaji wa mikakati ifuatayo:-

(a) Kinga, ziara za mafunzo Uganda kuona na kujifunza mikakati ya nchi ya Uganda ambayo imesifiwa kufanya vizuri katika suala hili. Ziara hii imesaidia kuboresha juhudi zinazochukuliwa Jeshini hivi sasa. Ushauri Nasaha na upimaji wa hiari wa virusi (*VCT*). Wanajeshi na watumishi raia wameendelea kuhamasishwa kwenda kwenye vituo vya ushauri nasaha na upimaji wa maambukizo ya virusi vya Ukimwi. Aliyeathirika anapewa ushauri nasaha wa kuishi kwa matumaini na kushauriwa ni wakati gani aweze kuanza dawa za kuboresha afya na kurefusha maisha yake ya utumishi Jeshini.

Makamanda Jeshini wamefanya warsha kujadili vichocheo vya kueneza Ukimwi Jeshini na jinsi ya kuvikabili vichocheo hivyo pamoja na kuongoza juhudi za kudhibiti Ukimwi. Utooji wa Elimu ya Kinga (filamu ya Ukimwi iitwayo Adui Aliyejificha). Jeshi likishirikiana na Chuo Kikuu cha *Regent, GEO CENTER, INC* na Wizara ya Ulinzi zote kutoka Marekani, wametengeneza filamu ya Ukimwi iitwayo Adui Aliyejificha. Filamu hii ni mafanikio makubwa katika kurahisisha utoaji wa Elimu ya Ukimwi kwa wanajeshi na familia zao. Tayari nakala 300 za filamu hiyo zimekwishatengenezwa.

Kuhusu upimaji wa uambukizo wa Virusi vya Ukimwi, askari wapya wanaoajiriwa, wanajeshi wanaoendelea na utumishi Jeshini na wale wanaokwenda nje ya nchi kwa kozi na kazi maalum wamepimwa uambukizo wa virusi vya Ukimwi na utumiaji wa mipira ya kujamiiana (*Condom*) imepatikana na kusambazwa na wanajeshi wamehamasishwa waitumie ipasavyo.

(b) Kuhusu Tiba ya Magonjwa Tegemezi ya Ukimwi, wanajeshi wagonjwa wa Magonjwa tegemezi ya Ukimwi kama Kifua Kikuu, utando wa mdomoni na kadhalika wameendelea kutibiwa kutegemea na uwezo wa kifedha. Madawa ya kuboresha afya waathirika *ARVS/HAART*. Madawa ya kuboresha na kuongeza muda wa kuishi (*ARVT*) ni ghali sana. Hata hivyo, kwa uwezo mdogo uliopo na kwa ufadhili kama vile wa kupitia *Global Foundation* waathirika mmoja mmoja wameendelea kutibiwa. Juhudi zinaendelea kufanywa ili kupata ufadhili zaidi katika eneo hili kama vile kupitia *Clinton Foundation*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, JWTZ na JKT yameendelea kufadhili huduma ya elimu ya msingi na sekondari katika shule zilizopo katika baadhi ya vikosi. Elimu ya Sekondari inatolewa katika shule za Makongo, Jitegemee, Kigamboni na *Airwing* zilizopo jijini Dar es Salaam, Ruhuwiko iliyopo Songea, Unyanyembe iliyopo Tabora, Kawawa iliyopo Mafinga, Ngerengere na Kizuka zilizopo Morogoro na Nyuki iliyopo Zanzibar.

Aidha, JKT imeendelea kuendesa Vyuo vya Ufundu kwa kutumia mitaala ya *VETA* katika vikosi vya Makutopora, Maramba, Mgulani na Mlale. Shule na vyuo hivyo ni kwa ajili ya watoto wa wanajeshi na watoto wa raia wengine. JWTZ na JKT pia wanatekeleza mpango wa kuwaendeleza wanajeshi na watumishi raia katika majeshi hayo kwa kuwapeleka kusoma katika vyuo ndani na nje ya nchi ili kuinua uwezo wao kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, katika JWTZ na JKT michezo ni suala la kudumu na ni sehemu ya shughuli za wanajeshi ili kuwajengea ukakamavu na nidhamu. Kutokana na utaratibu unaomtaka kila mwanajeshi kushiriki kikamilifu kwenye michezo wanajeshi wetu wameweza kushiriki katika mashindano mbalimbali Kitaifa na Kimataifa na kuliletea Taifa sifa kutokana na ushindi wao.

Mheshimiwa Spika, timu ya JWTZ na JKT zimeendelea kushiriki na zimekuwa zikichuana katika nafasi ya kwanza na ya pili katika mashindano ya kila mwaka katika michezo ya *Netball*, *Handball*, *Volleyball*, *Masumbwi*, *Basketball*, kuogelea na mieleka hapa nchini na nje ya nchi. Mashindano hayo ni Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki na Kati, Klabu Bingwa ya Muungano wa Tanzania na Klabu Bingwa Tanzania Bara.

Aidha, *Ruvu Stars* zinashiriki katika mashindano ya Klabu Bingwa Tanzania Bara katika mchezo wa mpira wa miguu. Timu za *101 KV*, *Kipanga FC* na *151 KJ Hard Rock* zinashiriki katika Ligi Kuu Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2003 ilifanyika michezo ya majeshi ya Ulinzi na Usalama katika Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam ambapo timu mbalimbali za JWTZ na JKT zilifanya vizuri. Michezo hii hutoa asilimia 99 ya wachezaji wanaoliwakilisha Taifa letu kwenye michezo ya Kimataifa kama vile *All Africa Games*, michezo ya *Commonwealth*, *Olympic*, Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (*CISM*) na Michezo ya Bara la Afrika. Michezo hiyo ilifunguliwa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, tarehe 4 Novemba, 2002 na kufungwa tarehe 16 Novemba, 2002 na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume. Mwaka huu michezo hiyo imepangwa kufanyika Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, uongozi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Taasisi zake umeendelea kusimamia utendaji katika Idara na sehemu zote za vyombo hivyo kwa kufuata misingi ya sheria na taratibu zilizowekwa. Misingi hiyo ni pamoja na uadilifu katika kazi, nidhamu na busara katika matumizi ya fedha na mali za umma kwa kuzingatia sheria na kanuni za fedha na ununuzi.

Lengo ni kuleta usanisi katika shughuli za vyombo vya kiulinzi kwa kutumia fedha zinazotolewa. Sambamba na hayo, matumizi ya mfumo wa malipo wa *Intergrated Financial Management System (IFMS)* kuititia katika mtandao wa kompyuta umeendelea kuimarishwa. Mfumo huo ambaeo lengo lake kubwa ni kuleta nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali, ikiwa pamoja na kuepuka kufanya matumizi ya ziada kinyume na bajeti iliyoidhinishwa, sasa unatumika kwenye Makao Makuu ya Wizara, Makao Makuu ya Jeshi na Makao Makuu ya JKT. Jitihada zinafanywa ili kuweka mfumo huo kwenye vituo vya malipo vya JWTZ na JKT vilivyoko Mikoani. Vituo vya malipo ya JWTZ katika Mkoa wa Dar es Salaam vimekwishafungiwa mtandao huo mwezi Julai, 2003 na vinategemewa kuingizwa kwenye mfumo wa malipo wa *IFMS*.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya rushwa, wizi na ubadhilfu wa mali za umma vinaendelea kupigwa vita. Aidha, maafisa, askari na wafanyakazi wameendelea kupatiwa elimu kuhusu ubaya wa adui wa haki na kutakiwa kushiriki katika kudhibiti vitendo vya rushwa. Kwa wale wachache ambao wanabainika kushiriki katika vitendo hivyo au kutozingatia maadili na miiko ya kazi zao wamedhibitiwa na kuadhibiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, juhudu zimefanywa kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa kero mbalimbali Jeshini. Tatizo la likizo lililokuwa kero sugu kwa wanajeshi na familia zao limetatuliwa. Wanajeshi wengi ambaeo walikuwa wakidai kwenda likizo wameeweza kwenda likizo. Wakuu wa Vikosi wameelekezwa kupanga ratiba za likizo kwa wanajeshi bila kuathiri utendaji kazi. Kwa kushirikiana na Hazina madeni na madai mbalimbali yakiwemo madeni ya wazabuni, marupurupu na madai mengine ya wanajeshi yameendelea kulipwa.

Pia Serikali imeendesha programu ya mafunzo mbalimbali, semina na warsha kwa lengo la kuboresha viwango vya utendaji wa wafanyakazi. Mazingira ya kufanya kazi yameendelea kuboreshwa kwa ofisi kuwekewa vitendea kazi bora zaidi na vifaa vya mawasiliano. Baadhi ya majengo Makao Makuu ya Jeshi na Makao Makuu JKT yamefanyiwa ukarabati na majengo mapya yamejengwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 nililieza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaanidaa mpango maalum wa kuyahamishia nchini makaburi ya wanajeshi wetu waliozikwa nje ya nchi wakati wa vita vya ukombozi wa nchi za Afrika kama vile Msumbiji, Zimbabwe na kwingineko ili kuwapa mazishi ya heshima wanayostahili mashujaa hao. Mpango huo utahusisha ujenzi wa mnara maalum ambapo mashujaa

wote waliopoteza maisha yao katika kutetea heshima ya Waafrika na Bara letu yataorodheshwa kwa madhumuni ya kuweka kumbukumbu ya kihistoria kwa vizazi vijavyo.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba umefanyika uchambuzi kuhusu wanajeshi wote waliofariki katika vita nje ya Tanzania. Maandalizi ya kurejesha mabaki ya miili yao yanaendelea. Kamati maalum itaundwa kwa lengo la kuratibu shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utekelezaji wa Mkakati wa Kuimarisha Jeshi, ambao utaingia katika mwaka wa tatu, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2003/2004 itakuwa na mipango ya kuboresha huduma muhimu kwa wanajeshi na vijana wa JKT kama vile sare, tiba na kukuza michezo mbalimbali, kutoa mafunzo na mazoezi ya kijeshi kwa wanajeshi pamoja na mafunzo ya kitaaluma kwa wanajeshi na watumishi raia, kutoa mafunzo ya ukakamavu, ufundi stadi, kilimo na taaluma nyinginezo kwa vijana wa JKT, kufanya matengenezo, kufufua na kukarabati magari, mitambo na vifaa vingine vya kijeshi, kuboresha uwezo wa usafiri na usafirishaji Jeshini kwa kununua Ndege ya Usafirishaji na kulipatia Jeshi magari mapya ya kijeshi, kufanya matengenezo/ukarabati wa baadhi ya majengo katika makambi, kukamilisha baadhi ya viporo vya miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa wanajeshi katika makambi, kukarabati mabweni ya vijana katika makambi ya JKT, kuendeleza utafiti wa Teknolojia ya kijeshi kwa lengo la kuongeza uwezo wa Jeshi kimapigano, kuimarisha mazingira ya kufanya kazi kwa kupata vitendea kazi bora na vya kisasa, kulipia huduma muhimu za umeme, maji na simu, kulipa mishahara na chakula kwa wanajeshi na vijana JKT na watumishi raia na kuimarisha na kupanua matumizi ya Mtando wa *ITN*.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu hii napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake usiroyumbishwa kuhusu suala zima la ulinzi wa nchi yetu. Amiri Jeshi Mkuu amekuwa karibu sana na wapiganaji wake katika kufuutilia maendeleo na matatizo yao. Amefanya jitihada kubwa kuimarisha Jeshi lake pamoja na kuondoa kero zinazowasibu Maafisa na wapiganaji. Sote tunampongeza. Wanajeshi wake wataendelea kuwa watiifu na watakeleza maagizo na maelekezo yake kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwashukuru kwa dhati Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, kwa kuwa kwao karibu na kufuutilia kero na matatizo ya wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Ulinzi chini ya Mwenyekiti wao Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera, kwa kupitia na kuchambua Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuwasilisha taarifa yao kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napenda pia kutoa shukrani kwa Serikali za nchi zifuatazo zilizoshirikiana nasi katika maeneo mbalimbali ambazo ni Jamhuri ya Watu wa China, Shirikisho la Ujeruman, Ufaransa, India, Uingereza, Canada, Marekani, Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Bwana Vincent Mrisho. Shukrani zangu pia ziwaendee Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jeneral George Waitara, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Luteni Jeneral Iddi Gahlu na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jeneral Davis Mwamunyange. Wote nawashukuru kwa msaada wanaonipatia katika kuendesha shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Nawashukuru wafanyakazi wote katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, maafisa na wapiganaji wote wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiano na uhusiano mwema walionipa katika kuongoza Wizara hii pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, mwisho namshukuru Mpiga Chapa wa Serikali na wafanyakazi walio chini yake kwa kuchapisha hotuba hii na kuikamilisha kwa wakati. Navishukuru pia vyombo vya habari hapa nchini kwa kulitangaza Jeshi letu wakati wa mazoezi, sherehe za kijeshi, udhibiti wa wavamizi wa nchi yetu kutoka nje na wakati wa maafa.

Mheshimiwa Spika, mtu akizungumzia amani na utulivu wa Tanzania pamoja na mambo mengine ya maendeleo ya Taifa, hatasita kusema kuwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lina mchango mkubwa katika kulinda na kutetea amani na utulivu tulionao. Mtu akizungumzia historia ya ukombozi wa Bara la Afrika hawezি kuikamilisha historia hiyo bila kuitaja Tanzania na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

JWTZ lilitoa mchango mkubwa kwa kutoa mafunzo, wataalamu katika kambi za wapigania uhuru wa *SWAPO* wa Namibia huru, waliofundishwa Kongwa, Dodoma, wapigania uhuru wa *FRELIMO* wa Msumbiji huru waliofundishwa Mgagao, Iringa na wengine walipata mafunzo katika kambi za Dakawa na Mazimbu pamoja na wapigania uhuru wa *ZANU PF* wa Zimbabwe huru waliofundishwa katika kambi za Dawaka na Mazimbu.

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama wa nchi yetu katika mwaka 2002/2003 ulikuwa imara kutohana na nidhamu, uadilifu, moyo wa uzalendo, ushujaa na utayari wa kulinda na kutetea uhuru na Muungano wetu, na ushupavu wa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, wapiganaji wetu wamedhibiti ulinzi wa mipaka yetu kwa kushirikiana na wananchi na kutohana na kiapo chao hawatakubali ama hawataruhusu nchi au mtu yejote amdhihaki, amdharaau na amtukane Amiri Jeshi Mkuu wala hawatavumilia nchi yoyote au mtu yejote aidhahiki, aidharaau au kuvamia nchi yetu. Wanajua wao ndiyo ngome ya ulinzi na heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kwa Watanzania kujivunia, na kulipatia umuhimu unaostahili Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Amani na utulivu uliopo nchini umeijengea nchi yetu heshima kubwa duniani na umejenga imani kwa watalii, wafanyabiashara kutoka nje, wafanyakazi wa Kibalozi na Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wameendelea kushiriki kwa utulivu katika shughuli za kujiletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo, yatupasa kuelewa kwamba ulinzi ni jukumu lenye gharama kubwa kwa maana ya kujenga uwezo wa kiulinzi ulio madhubuti. Taifa linahitaji kutumia raslimali nyingi kwa ajili ya kulinunulia Jeshi letu vifaa na zana za kisasa pamoja na kuwaajiri vijana ambaao ni nguvu kazi, kuwatunza na kuwafundisha wanajeshi wetu katika fani mbalimbali za kimapigano na kitaaluma ili wawe na ujuzi na maarifa.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tuache utamaduni wa kuamini na kushabikia kila jambo linaloandikwa na vyombo vya habari vya nje kuhusu ulinzi na usalama wa Taifa letu. Tujenge utamaduni wa kuwa na moyo na mtazamo wa kizalendo kutetea maamuzi mazito yanayofanywa na Serikali kuhusu ulinzi na usalama wa nchi yetu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imepewa dhamana na imeelekezwa na Serikali pamoja na wananchi kupitia Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba amani tuliyonayo italindwa kwa nguvu zote, hatutaruhusu maadui kuingiza na kusambaza nchini, sumu inayowasibu majirani zetu na kukaribisha vurugu. Tanzania hatufuati mfumo wa ulinzi, hatufuati maadili, mila, dira ya maendeleo na utamaduni wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, tunao mfumo wetu, mila zetu, dira ya maendeleo na utamaduni wetu. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litahakikisha kuwa mfumo, maadili, mila, dira ya maendeleo na utamaduni wenu unalindwa kwa nguvu zote na unafanikishwa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake iweze kutekeleza majukumu yaliyoelezwa katika hotuba hii kwa mwaka 2003/2004, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadiryo ya Matumizi ya Fedha jumla shilingi 179,088,917,000/= fedha za hapa nchini

ambazo kati yake shilingi 155,078,917,000/= zitatumika kwa ajili ya kulpia mishahara na matumizi mengine na shilingi 24,010,000,000/= zitatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mgawanyo ufuataao:-

Matumizi ya Kawaida, Fungu 38 - Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, shilingi 125,672,448,000=, Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 25,353,594,700= na Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 4,052,864,300=.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Maendeleo, Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 24,010,000,000=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. JOHN S. MALECELA – MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa mara nyingine tena nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunga lako Tukufu, maoni na ushauri wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa Fedha wa 2003/2004, kwa mujibu wa Kanuni ya namba 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo ningependa niwataje wale wenzangu ambao tulishirikiana nao katika kazi hii ya kupitia Makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na Wanakamati ni kama hawa wafuatao, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Omar Mjaka, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Frank Magoba, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Gretrude Mongella, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji na Katibu wa Kamati, Ndugu Angumbwike Ng'wavi. (*MakofiKicheko*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hii kwa kujadili kwa kina masuala mbalimbali yanayohusu Ulinzi na Usalama hapa nchini pamoja na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi na pia napenda kuwapongeza Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na wataalam wake wote, kwa kuiwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Wizara zilizotolewa ndani ya Bunge lako Tukufu na ushauri wa Kamati ya wakati huo ya Kisekta ya Bunge ya mwaka huo yaani Kamati ya Nje, Ulinzi na Jeshi la Kujenga la Kujenga Taifa, pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa Wizara uliotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya Makadirio ya mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili na kuchambua taarifa za Wizara hii pamoja na kujadili Makadirio ya Matumizi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Fungu 38 Jeshi la Kujenga Taifa, Fungu 39 na Wizara (Utawala na Mashirika) Fungu 57 kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati ya Kisekta ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama na wa malengo ya Wizara ya mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa yaani majukumu walivoyatekeleza mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, kama hotuba aliyoisoma Mheshimiwa Waziri hivi punde, alieleza Kamati kuwa katika mwaka wa fedha 2003/2004 Wizara yake imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

Kwa kuajiri watumishi wenye ujuzi, kulingana na mahitaji, kutoa mafunzo ya kijeshi kwa nadharia na vitendo, kununua vifaa vya kisasa, kutengeneza na kukarabati vifaa viliviyopo na kuvihifadhi vizuri na kuboresha teknolojia ya kijeshi kwa kuimarisha utafiti katika mashirika ya Mzinga na Nyumbu.

Pia kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuwaweka Wanajeshi makambini na kuwajengea nyumba za kuishi na kutoa huduma za jamii kama vile matibabu, shule, kumbi za starehe, vifaa vya malazi na kutoa huduma nafuu kwa wanajeshi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilipotembelea vikosi vya Jeshi Mkoani Arusha tarehe 28 hadi 29 Mei, 2003, ilipewa taarifa ya tatizo kubwa la maeneo ya ulinzi na ya mafunzo, narudia tena maeneo ya ulinzi na maeneo ya mafunzo kuvamiwa na watu kwa matumizi ya kilimo, ufugaji na makazi.

Mheshimiwa Spika, matatizo mengine yaliyoelezwa, ni pamoja na ukosefu wa nyumba za kuishi maafisa na wafanyakazi wengine wa vikosi hivyo, upungufu wa maji na ukosefu wa nyumba za kuishi maafisa na wafanyakazi wengine katika vikosi hivyo.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa maji na ukosefu wa Bwawa la Kuogelea kama ni sehemu ya mafunzo katika Chuo cha *Tanzania Military Academy (TMA)*. Matatizo mengine ni ya ukosefu wa umeme katika Kambi ya Oljoro yaani JKT, Chuo cha Uongozi na Unadhimu kuwa pamoja na *TMA* na mipaka kati ya Kenya na Tanzania kutokufyekwa. Hivyo, eneo la mpaka ambalo halipaswi kutumiwa na mtu yeoyote halieleweki.

Mheshimiwa Spika, Wizara, katika kutekeleza malengo waliyojiwekea kwa mwaka 2003/2004, iliomba fedha kwa mafungu yake kama ifuatavyo:-

Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Fungu 38 - Matumizi ya Kawaida shilingi 125,672,448,000/=, Jeshi la Kujenga Taifa, Fungu 39 - Matumizi ya Kawaida shilingi 25,353,594,700/=, Wizara na Mashirika, Fungu 57 - Matumizi ya Kawaida shilingi 4,052,864,300/= na Mipango ya Maendeleo shilingi 24,010,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, jumla ni shilingi 179,088,907,000/=.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti katika vyombo vya ulinzi na usalama. Aidha, napenda kuwapongeza askari wetu kwa uzalendo wao na kwa kuvumilia kuendelea kufanya kazi mara nyingine katika mazingira magumu sana. Tunawapongeza na kuwapa hongera. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa za Wizara na matatizo yaliyojitekeza wakati Kamati ilipotembelea Mkoa wa Arusha, Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze juhudu ya kujenga nyumba za maafisa na makambi kwa ajili ya kuishi askari. Aidha, majengo yaliyopo yawe yanakarabatiwa mara kwa mara. Kwa sababu kwa askari kuishi katika makambi ni njia mojawapo ya kuongeza nidhamu kwa sababu ni vigumu sana kwa viongozi wa Jeshi kuongoza nidhamu jeshini wakati askari wanakaa uraiani. (*Makofî*)

Pia Serikali iiimariske ulinzi katika Ziwa Tanganyika ili kudhibiti matukio ya mauaji na uporani wa mali za wananchi wetu katika ziwa hilo. Aidha, Kamati inashauri kwamba Serikali inunue helikopta kwa ajili ya ulinzi na uokoaji nyakati mbalimbali tunapopatwa na maafa na Serikali iendelee kuwaenzi Majenerali na wanajeshi wenye utaalamu wa hali ya juu walistaafu, na kuwatumia katika shughuli mbalimbali kutokana na ujuziau utaalamu wao au uzoefu wao walionao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ishughulikie mapema migogoro ya ardhi baina ya wananchi na vyombo vya ulinzi na usalama. Kwa sababu kuna mahali tulikuta wananchi wa kawaida wanakaa kama mita 200 hivi kutoka kwenye *radar* za nchi ambayo kwa kweli si jambo zuri. Pia mipaka ya maeneo ya

Majeshi iwekwe wazi na Serikali; hasa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, idhibiti uvamizi wa maeneo hayo. La sivyo tusipofanya hivyo siku za usoni askari wetu watajikuta hawana nafasi za kufanya mazoezi na vyombo walivyonyavyo kutokana na uhaba wa ardhi.

Serikali itafute utaratibu mwininge wa kuwapatia maji raia wanaoishi karibu na maeneo ya Majeshi badala ya kutumia maji ya mabomba ya Jeshi, Serikali iboreshwe utunzaji wa zana za kivita, ivikinge na mvua na mavumbi kutokana na upepo na Chuo cha Uongozi na Unadhimu kitengwe kutokana na chuo cha *TMA*, ili viwe na mahali na uongozi tofauti, Kambi ya Oljoro ipelekewe umeme kwa sababu kama ikipelekewa umeme vijana wetu wanaweza kwa kutumia umeme kujifunza kazi mbalimbali ambazo zitawasaidia katika maisha yao. (*Makofi*)

Pia Serikali ijenge Bwawa la Kuogelea *TMA*. Kama nilivyosema Bwawa kama hilo ni sehemu ya wanajeshi kujifunza kuogelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuwasiliana na nchi jirani ifyeke mipaka kwa upande wa Tanzania na Vituo vya Afya vya jirani na maeneo ya Jeshi viimarishwe ili viweze kutoa huduma bora zaidi na viweze kupunguza msongamano wa raia kufuata matibabu katika Hospitali za Jeshi. Hospitali za Jeshi zihudumie wale tu ambao matatizo yao ni makubwa, lakini matatizo madogo madogo yapelekwe kwenye zahanati ambazo zijengwe na Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Pia ajira mpya za askari katika Majeshi ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Jeshi la Wananchi zizingatie vijana waliopitia katika Jeshi la Kujenga Taifa. Maana hawa vijana waliopitia Jeshi la Kujenga Taifa wamekuwa chini ya uangalizi angalau wa Kijeshi kwa mwaka mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali iimarishe Idara ya Ujenzi ya Jeshi la Kujenga Taifa ili ifikie daraja la kwanza na iweze kushindana katika tenda Kimataifa kama inavyostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali iimarishe Jeshi la Mgambo na sera ya Mgambo iandaliwe ili dira ya Jeshi hilo iwekwe wazi kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inayakubali maombi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2003/2004 yaliyofikishwa mbele ya Kamati. Iliyakubali mapendekezo yaliyofikishwa mbele ya Kamati na iliyapitisha mafungu yote na bila mabadiliko yoyote, yenye jumla ya shilingi 179,088,907,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kamati ingependa ipendekeze kwa Bunge hili kwamba iyakubali Makadirio hayo ya Jeshi letu ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe kwa kunisikiliza na napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Spika, kama kawaida tunawatahadharisha wasemaji wale wa mwanzo ili waweze kujiandaa ni hawa wafuatao, wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, wa pili atakuwa Dr. Lawrence Gama, wa tatu atakuwa Mheshimiwa Shaibu Ahmad Ameir na wa nne Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. (*Makofi*)

Sasa kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, mimi nina Kikao kingine, namwomba Mheshimiwa Naibu Spika, aje anipokee kiti. (*Makofi*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Na.43 (5) (b)(c) toleo la mwaka 2003, naomba kwa ruhusa yako na kwa niaba

ya Kambi ya Upinzani niwasilishe maoni yetu juu ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2003/2004, nikiwa Waziri Kivuli wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa kusimama hapa nimepewa na Waheshimiwa sana wana wa Vunjo, sina budi kuwatanguliza mbele nikiwasalimu na kuwatakia kila la kheri wana wa Vunjo hasa Kata za Kirua, Kilema, Marangu, Mwamba, Mwika, Himo, Makuyuni na Kahe na kuwatakia wafanye kazi kwa bidii na mimi Mbunge wao pamoja na Serikali tutaboresha juhudhi zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa sina nidhamu kama pia sitampongeza Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, kwa kurudi salama kwenye safari yake ya Ulaya na Marekani na manufaa aliyoleta kutoka huko, hakika Serikali itaweza kuyakubali na kuyafanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nichukue nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kwenye uchaguzi mdogo wa mwezi Mei, 2003 ambapo Chama cha *CUF* kikiibuka na ushindi wa hali ya juu wa Wabunge 15 na CCM Wabunge 4 na Wabunge wa hukumu ya Mahakama na ushindi huu ni ushindi wa Wanawake wanenye kutoka chama cha *CUF*. Hongereni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindi wa *CUF* umeongezea nguvu kwa Kambi ya Upinzani Bungeni na kuniimarisha mimi zaidi kuwa Waziri Kivuli wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambapo *NARC* ya 2005 itanifanya mimi kuwa Waziri kamili wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hivi sasa niko kwenye mazoezi makali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mbunge,Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wa sasa, kwa hotuba yake nzuri mno ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2003/2004 ambayo ninaiunga mkono kikamilifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu ni Wizara ya Fedha kutupatia fedha hizo na naamini watakaopokea fedha hizo watazitumia kama ilivyopangwa na ubadhilifu wowote ule napendekeza adhabu yake iwe ni kafilisiwa na kufungwa miaka 30 jela, ili iwe funzo kwa wale wengine amba wana uzembe huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa JKT kuwa wa kwanza kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Saba Saba mwaka huu 2003 katika mazao ya kilimo. JKT imedhihirisha wao wanaweza kuwa walimu wa Kilimo katika Taifa letu na hapo uchumi wetu uweze kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa pongezi kwa kutimiza miaka 40 tarehe 10 Julai, 2003 tangu kuanzishwa kwa JKT. Tunawapongeza sana miaka 40 sio haba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu naomba sasa niingie hatua kwa hatua kuhusu Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni shwari, tulivu, amani na ya kuchapa kazi kikamilifu na kizalendo. (*Makofî*)

(b) Nidhamu ni ya hali ya juu sana na pia Ulinzi wa Viongozi (*VIP Protection*) ni nzuri sana.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Ulinzi wa Ndani ya nchi na Mipaka ya nchi yetu ni imara kabisa, hakuna wa kuichezea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa akifuatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge chini ya Mwenyekiti wake makini Mheshimiwa John Malecela, wamuone Mheshimiwa Rais, wamwombe kufuta Hati Miliki za ekari 32,395 za Mafunzo ya Kijeshi Monduli yaliyochukuliwa kinyemela na raia huku wakijua eneo hilo ni la JWTZ na kubakiza ekari 13,000 tu. Eneo lililobaki la ekari 13,000 halitoshi hata kidogo kwa mazoezi ya kivita hasa *Infantry* kwa mfano, *Advance Attack Defence withdraw and special operations*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika halitoshi kabisa kwa mazoezi ya kivita kwa *Artillery, Micelles, Airforce & Air Defence* kwa kuwa masafa yake ni ya kilomita nyingi sana. Si vizuri kudhuru watu na mali zao kwa kutokuelewa kwao. Kwa hiyo, waondoke kwa usalama wao. Taarifa ya Utekelezaji huo itolewe na Waziri kwenye kikao cha Bunge kitakachoanza tarehe 04 Novemba, 2003. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa *Command & Staff College* iliyojibanza *TMA* Monduli iondoke eneo hilo na kuhamia eneo jingine endelevu kabla ya Bunge la Bajeti 2004/2005. Nitoe pendekezo iangaliwe uwezekano wa kuingia kambi iliyokuwa Chuo cha *TANESCO*, Morogoro. Hilo ni angalizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya *JWTZ Vote 38* ya shilingi bilioni 125.7 imelenga kuhudumia tu ambayo inaitwa *Combat Service Support*. Kila Kasma (*Subvote*) itumike kama ilivyopangwa na kwa ubainifu, lakini kwa kilicho bora, bila ubadhilifu wa aina ye yeyote. Hukumu ya wabadhilifu iwe ni kufilisiwa na kifungo cha miaka 30 jela. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya *Wizara ya Ulinzi Vote 57* kuhusu maendeleo ya shilingi bilioni 24.0 inatosha ikisimamiwa vizuri bila uvujaji au ubadhilifu wa aina yoyote. Hukumu ya ubadhilifu iwe ni ile ya kufilisiwa na kifungo cha miaka 30 jela. Ripoti ya *Controller and Auditor General* ya Oktoba, 2002 inaonyesha upotevu wa shilingi 1,090,945,127/=, uzembe huu ufuatiliwe na ukomeshwe kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya *Zana za Kivita (Combat Support)* haijapewa *Vote Number*, kwa ajili ya *Infantry, Artillery, Air Defence, Micelles, Attack Helicopters, Jet Fighters* na *Navy-War Ships*. *Vote* hiyo isomeke kwa kifupi tu. Kwa mfano, Voti Na. 93 - *Zana za Kivita* - shilingi bilioni 160, basi inatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapojenga Jeshi unatazama Majeshi ya nchi zinazokuzunguka na kwamba kitu mnachoshirikiana kwa pamoja (*In common*) mfano, Mto Nile, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria au Ziwa Tanganyika ina manufaa ya pamoja au kuna utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatarajia kutoa shilingi kwenye Bajeti ya *Ulinzi* na Jeshi la *Kujenga Taifa* 2004/2005 kama *Vote* ya *Combat Support* na *Sub Votes* zake hazitaonyeshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ielevweku kuwa si uvujaji wa siri ila ni kuonyesha Bunge lako Tukufu nia, mwelekeo na hitajio la *Wizara* ili kukamilisha lengo na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya sasa hivi na kabla ya 2004/2005 ni kuongeza *Night Vision Gogos* kwa *Battalion* mbili za mbele. Kila askari apate na kuongeza *Modern Binoculars* zinazoonyesha *Direction, Bearing, Distance* na *Targets* kwa *Forward Obsevation Officers (FOOs)* kwa *Platoon Commanders* wote wa *Battalion* mbili za mbele. (*Makofi*)

Pia kuongeza *Rifle Lessor Beams* kwa idadi ya askari wa *Battalion* mbili za mbele, kuongeza *Modern Radios for Communication and Monitoring* kwa kila Kompania, Makao Makuu ya Kikosi, Makao Makuu ya Brigedi, Makao Makuu ya Division na Makao Makuu ya *JWTZ*, kuongeza Ramani za Kivita za mwaka 2002/2003 toka *Wizara ya Ardhi* za kutosha *Battalion* mbili za mbele na Makao Makuu ya *JWTZ*, *attack Helicopters* idadi ya *Squadron* tatu za kuanzia na kuongeza *Landrover FFR* kwa *Military Intelligence* mbili kila *Battalion* kwa kuanzia ili kupata Taarifa za Upelelezi wa mapema kwani *Intelligence Report Delayed is Report to be Denied*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitajio la mwisho kwa *JWTZ* ni *War Budget Reserve* na ipewe Voti namba yake ikitengewa shilingi bilioni 5 kila mwaka. Hii nitaizungumzia kila Bunge la Bajeti. Hatuna rafiki wa kweli na tuko vitani. Tunachelewesha vita kwa kufanya maandalizi ya vita. Maadui zetu wameshamaliza matayarisho wanatafuta njia nzuri zaidi ya kutuchokoza ili wafanye vita kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa juhudhi zake anazozifanya na kwa hotuba yake nzuri sana ya jana na kwamba ameweza kufanya nchi yetu ielevweke nchi za nje na ioneokane ni nchi ya amani na sio ya fujo na sio nchi ya kibeberu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Kambi ya Upinzani inapendekeza kwa nguvu zake zote kuwa *Sub Vote 260200* ya shilingi 240,000,000/= za Majarida, Maktaba na Michezo zitumike shilingi 40,000,000/= tu na hizo nyingine zinunue *Night Vision Gogos* zenye uwezo wa kuona zaidi ya mita 300 na *Modern Binoculars*.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika *Sub Vote 260300* ya shilingi 297,000,000/= za Takrima ya vikao zitumike shilingi 97,000,000/= tu na shilingi 200,000,000/= zinunue *Night Vision Gogos* na *Modern Binoculars*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ielevweke kuwa Jeshini Michezo, Takrima na Majarida yanaweza kucheleweshwa lakini vita vya usiku havicheleweshwi. Ushindi wa Vita ni Usiku Kuliko Mchana. Historia ya vita vya Iraq vinajionyesha wakati unaskia wako Basra, asubuhi unaskia wamekaribia Baghdad, walikuwa wanakwenda usiku kwa kutumia *Night Vision Gogos*. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inashukuru sana kuwaweka Majenerali Wastaafu Wizarani kwa kutumia Voti 57. Majenerali hawa wapewe majukumu na Ofisi Wizarani kiraia wawe *War Desk Officers*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *War Desk Officers* wamepangwa kwenye ujio wa nchi zinazoambatana na sisi na pia kwenye ujio wa Bahari hao wapewe kuwa ni *War Desk Officers* wafanye kazi hiyo wakishirikiana na Makao Makuu ya JWTZ chini ya Mkuu wa Majeshi (*CDF*).

Pia wapo Maafisa na wapiganaji wa JWTZ waliostaafu kwa Heshima Kuu na ni wataalam wa hali ya juu sana. Kila iwezekanavyo waajiriwe kiraia katika fani mbalimbali kulingana na mahitaji. Wajulikane idadi yao na vyeo vyao waingizwe kwenye voti 38 kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Hii itapunguza wastaafu hao kutoka nchini na kwenda nchi jirani au nchi za nje kuwa Mamluki au Washauri wa Mambo ya Kijeshi ya nchi hizo. Kwa mfano, walioko Uganda na *DRC*. La sivyo tutakuwa tumejiteketeza wenye na hakuna wa kumlaumu. Hawa wana utaalamu wa hali ya juu sana na ndio hao waliokomboa Bara la Afrika. *Tactics* tunazo, hatutaki zivuje ziende huko ziliko, zirudi hapa tufanye nazo kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu JKT, Kambi ya Upinzani inashauri watumie kwa uangalifu kasma yao ya shilingi bilioni 8.1 na atakayefanya ubadhilifu hukumu yake iwe kufilisiwa na kifungo cha miaka 30 jela.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 03 Julai, 2003 Mheshimiwa Rais alihutubia Taifa, Ruvu JKT kuadhimisha miaka 40 ya JKT alitoa agizo kuwa *recruitment* ya Majeshi ya Ulinzi na Usalama itoke JKT na si vinginevyo. Wanaoenda kuruta CCP - Moshi, kuruta JWTZ wachaguliwe toka JKT na si vinginevyo. Faida zake ni nyingi mno. Kamwe wasitoke uraiani moja kwa moja kuingia CCP au JWTZ. Hii ni kudumisha Uzalendo na Ufanisi wa Ulinzi wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Nyumbu Project*, Kambi ya Upinzani inashauri iendelezwne na iwe kitovu cha ubunifu Sayansi na Teknolojia kwa Jeshi letu na vyombo vya Usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha Risasi cha Morogoro, *Mzinga Corporation* kiendelezwne. Risasi na Mabomu ya aina zote na silaha zote ziwe chimbuko lake ni kwenye Kiwanda hicho tuondokane na uagizaji wa silaha ndogo ndogo nchi za nje miaka zaidi ya 40 tangu tupate Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni ya Dhahabu Meremeta - Buhemba, Kambi ya Upinzani inashauri kwa nguvu zake zote hawa wawekezaji wadhibitiwe kufa kupona kwani ndiyo ukombozi pekee wa Taifa kupata zana za Kivita.

Hali kadhalika na machimbo mengine ya *Tanzanite*, Almasi, Rubi, *Green Garnet* na mengineyo. Hawa Wazungu wasipate mwanya hata kidogo wa kupora huu. Ndio Ukombozi wetu peke yake kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mipaka yetu ya nchi kavu, Kambi ya Upinzani inashauri kwa nguvu zake zote kuwa mipaka hiyo ifyekwe mithili ya Gridi ya Taifa ya Umeme (*TANESCO*). Wananchi maeneo ya mpakani tunao ndio nguvu kazi. Mikutano ya ujirani mwema iongezeke na kazi hii ikamilike kabla ya Bunge la Bajeti 2004/2005. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, makaburi ya mashujaa wetu yajengwe kitaalam ukiwepo ukuta ulioandikwa namba za jeshi za shujaa huyo, cheo chake, jina lake na vita alivyopigana. Hii itakuwa kumbukumbu yetu muhimu sana hapa Tanzania. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Kambi ya Upinzani inashauri kwa nguvu zake zote, pindi Waziri mwenye dhamana ya Taifa, anapoenda kuwekeana saini ya Mkataba na Balozi au Taifa jingine, aende na Waziri Kivuli wa Wizara husika. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia sehemu hiyo kwa ruksa yako. Kambi ya Upinzani inashauri kwa nguvu zake zote, pindi Waziri mwenye dhamana ya Taifa, anapoenda kuwekeana saini ya Mkataba na Balozi au Taifa jingine, aende na Waziri Kivuli wa Wizara husika. Hii ni kuimarisha *Democracy and Transparency*. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nikoo tayari kuondoka wakati wowote ule kufuatana na wewe kwa kuwa mimi ni mwanataluma, naomba tiketi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana wewe kwa kunisikiliza. Pia, nimshukuru sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kazi yake nzuri ya kuiongoza Wizara hii. Vile vile, nimshukuru sana Amiri Jeshi Mkuu, ambaye ndiyo mhimili wa kila jambo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na nikiwa na matumaini ya bilioni 5, *War Budget Reserve*.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofsi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama alivyotangaza Mheshimiwa Spika, wale ambao watafuatia kuzungumza ni Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib. Hawa ni wachangiaji watano wa kwanza ambao wataanza kuchangia. Sasa namwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

MHE. ANNE K. KILANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nikushukuru wewe pekee kwa kunipa nafasi ya kuchangia kama mchangiaji wa kwanza kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika chaguzi ndogo, Waheshimiwa Wabunge 15 wa Chama cha CUF, pia niwapongeza Waheshimiwa Wabunge wanenye wa Chama Tawala CCM na Waheshimiwa Wabunge wanenye wa Viti Maalum CUF, kwa kupigania haki yao Mahakamani na kuweza kurudi Bungeni tena. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, kwa hotuba yake nzuri sana. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, nimekuwa naye kwa muda wa miaka mitatu na ni Waziri ambaye anaongoza Wizara nzito bila ya kuwa na Naibu Waziri na kwa kipindi chote amekuwa anafanya kazi nzuri sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nichukue nafasi hii kumpongeza *General* George Waitara na *Lieutenant General* Iddi Gahhu kwa upande wa JWTZ na *Major General* Davis Mwamunyange ambao wanajitahidi sana kuongoza Jeshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia. Kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, naomba nikiri kwamba, ninaifahamu hii Wizara vizuri na aliyoyasoma Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ni mambo ambayo tumeyazungumza wote, lakini naomba nitumie nafasi hii kuongeza tu na kuboresha kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo napenda kuchangia ni kuisihi Serikali kwa nguvu zangu zote kwamba, sasa imefika wakati tufanye kimatendo kabisa kuboresha makazi ya Wanajeshi wetu. Hili jambo tumeliongea kwa muda mrefu sana, ni kweli tunajitahidi, lakini bado naona kama mwendo tunaokwenda ni mdogo. Wanajeshi wetu wengi wanaishi uraiani na hii inatuletea matatizo ya mmomonyoko wa maadili mema ya wapiganaji wetu. Tunaweza tukasema tutawalamikia wao, lakini Serikali inapaswa ichukue jukumu hili la kuwajengea nyumba na kuwajengea makambi bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubali kwamba, tumezungumzia sana suala hili, lakini naomba niisihi Serikali kwa mara nyingine kwamba, ilichukue hili jambo kuwa ni *serious* sana. Iwapo Wanajeshi wetu watakuwa wanaendelea kuishi uraiani, tutaendelea kuwapoteza wengi kwa ugonjwa wa UKIMWI. Kwa sasa hivi sina takwimu maalum ambazo nina uhakika nazo, lakini tuna tatizo kubwa ndani ya Jeshi letu kwamba tunapoteza Wanajeshi wengi kwa ugonjwa wa UKIMWI na hii inachangiwa na kuwa wanaishi uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni kuiomba Serikali iimarishe mafunzo ya JKT kwa kuongeza *intake* za vijana wanaoingia makambini. Ni kweli tumerudisha JKT, lakini kwa sababu ya faida ambazo tunazijua wote, ninaiomba Serikali iongeze *intake* zaidi ili tuweze kupata vijana wengi zaidi ambao watajiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Magereza na Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ninaiomba Serikali kwa kurudia tu kwamba, iendelee kuboresha makambi yetu ya JKT. Tulipokwenda Oljoro tuliona kambi haina hali nzuri, haina umeme na makazi yao si mazuri. Kwa hiyo, ninaisihi Serikali kwa mara nyingine kwamba, iwapo tunataka kupata vijana wazuri ni lazima tuboreshe makazi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba nichukue nafasi hii kuiomba Serikali ijitahidi sana kuhakikisha kwamba, vijana wetu wanaojiunga na Polisi, Magereza na Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanakuwa wamepitia JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuzungumzia suala la Maafisa wanaostaafu Jeshini. Napenda kuzungumzia kwa kutoa mfano, japo suala hili limezungumziwa na Kambi ya Upinzani na tumelizungumzia kwenye Kamati, lakini naomba nitoe mfano wa *General Mboma*. *General Mboma* ni Afisa Mstaafu, alikuwa ni *CDF* ambaye amepokewa na *General* George Waitara. Ukimuangalia *General Mboma* bado ni kijana sana na ana uwezo wa kulitumikia Taifa hili. Kwa hiyo, bado ninaisihi Serikali kwamba, iwe na utaratibu mzuri zaidi wa kuwatumia Maafisa wanaostaafu kutoka Jeshini. Hawa wenzetu wanaume wana bahati sana kwamba, wanachelewa kuzeeka. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wangu niliofa ni wa *General Mboma* na wengine wote. Kwa hiyo, naomba mnielewe kwamba, bado kilio changu ni kwamba, Maafisa wa Jeshi wanastaifu bado wakiwa na uwezo mkubwa. Kwa hiyo, uwekwe utaratibu maalum wa kuendelea kuwatumia kikamilifu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalonapenda kuzungumzia, hiki ni kilio changu hakikuzungumzwa na watu wengine, lakini naomba nikizungumze mimi binafsi. Kwanza, napenda kuishukuru sana Serikali kwa sababu ilishawapa mikopo ya usafiri wa magari wapiganaji wetu. Lakini kwa sababu nimefanya utafiti wa kina na kuona kwamba Askari wetu wanalipwa vizuri sana, niombe tena Serikali kwa mara nyingine iwasaidie wapiganaji wetu mikopo ya magari, pikipiki na baiskeli kwa sababu wapiganaji wetu wanafanya kazi kwa kweli kwa moyo wa Kizalendo. Ninaisihi sana Serikali ikiwezekana

iwafikirie sana mikopo hiyo niliyoitaja pamoja na mikopo ya kujenga nyumba zao za kuishi baada ya kustaaifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na Katibu Mkuu wake, Ndugu Mrisho na Makamanda wote, kwa jinsi walivyoweza kuandaa hotuba hii vizuri sana. Ninakiri kwamba, ni ya kina, *very detailed* na inayoleta matumaini, siyo kwa Makamanda tu au wapiganaji peke yao wa Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, lakini inaleta matumaini kwa sisi Wabunge, pamoja na Wananchi wote. Kwa hiyo, ninampongeza sana Waziri kwa hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda nitumie nafasi hii kulipongeza Jeshi la Kujenga Taifa kwa kutimiza miaka 40 toka lilipoundwa. Miaka 40 ni mingi, wakati huo pia tunakumbuka kwamba, Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania sasa lina umri wa miaka 39 na bila shaka utaweza kushangaa, vipi Jeshi la Kujenga Taifa liwe na miaka 40 na Jeshi la Wananchi wa Tanzania liwe na miaka 39?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wakati wa uhuru tulirithi Jeshi hili kutoka kwa Wakoloni wakati huo likiitwa *KAR* na sisi tulilibatiza tu baada ya kupata uhuru, tukaliita *Tanganyika Rifles*. Lakini lilipofanya maasi mwaka 1964, Amiri Jeshi Mkuu, alilivunja Jeshi lile na ninafikiri alifanya jambo zuri sana, mambo yale yaliyotokea ndio yaliyotusaidia sisi mpaka leo mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuvunja Jeshi lile, sisi Makamanda wa Jeshi la Kujenga Taifa tuliiitwa na Amiri Jeshi Mkuu na akasema: “Sasa nitaunda Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi hili litapita Jeshi la Kujenga Taifa na nitawachagua wale Maaskari walioasi 1,000 na ndio watakaoanzisha Jeshi hili.” Kweli walichaguliwa Askari 1,000 wakaletwa pale Mgulani pamoja na makamanda wao na pale walipikwa vizuri na wakatoka tarehe 1 Oktoba, 1964 na kuanza Jeshi la Wananchi wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania maana yake nini na azma yake ni nini? Jeshi la umma azma yake ni moja kwamba, litapendana na Wananchi na litaandamana na Wananchi kama samaki na bahari au kama pete na kidole. Samaki maana yake ndio wapiganaji na Makamanda na bahari ndio umma au Wananchi. Kwa hiyo, samaki anapoelea ndani ya bahari hawezি kufa, lakini unapomtoea kwenye bahari atakufa! Hiyo ndio maana ya pili ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwamba ni Jeshi la Wananchi na linaandamana na kupendana na Wananchi na linafanya shughuli zake zote kwa kuja kwamba, ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia hiyo limepata sifa kubwa, limefanya mambo ya ajabu sana! Kwa misingi hiyo, limeweza kushinda vita vingi sana, pamoja na Vita vyta Kagera, kwa sababu lilikuwa linaogelea ndani ya umma, ndani ya Wananchi. Wananchi walipigana na makamanda wao bega kwa bega na walishinda.

Vile vile, tarehe 25 Julai tumewakumbuka mashujaa wetu, wale waliokufa vitani, tunawaheshimu na kuwapongeza sana na kusema kweli Jeshi hili ni Jeshi la mfano katika Afrika. Siyo kama Majeshi mengine yanayoua Wananchi. Majeshi mengine yanapigana kuua Wananchi wenzao! Siyo Jeshi la Tanzania, hili ni Jeshi la Wananchi. Tuchukue nafasi hii leo kuwapongeza Makamanda wote wa Jeshi hili kwa kazi nzuri sana waliyoifanya na tunaomba waendelee kufanya hivyo na sisi tutakuwa nyuma yao na tutawasaidia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunaipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa katika miaka hii miwili kwa jinsi ilivyoweza kuliangalia Jeshi letu kutokana na matatizo walijonayo, ya nyumba, vifaa, magari na kadhalika. Ukiangalia Bajeti hii ya Jeshi la Kujenga Taifa haijapata kutokea,

ni karibu asilimia 25! Si rahisi kuongeza Bajeti ya Jeshi kwa namna iliyofanywa kwa miaka miwili! Si rahisi kwa sababu ni fedha nyingi sana. Kwa hiyo, ninaipongeza Serikali kwa hatua hiyo, muendelee kufanya hivyo na sisi tutaunga mkono. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuzungumzia suala moja na nitaomba sana Waziri Sarungi anisikilize. Nataka kuzungumzia juu ya malalamiko ya Maaskari waliopigana katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia, 1939 - 1945. Nakumbuka Decemba, 1998 kuna mtu mmoja anaitwa *Captain Shadrack*, alitangaza katika Taifa hili na Vyombo vya Habari viliandika kwamba, Serikali ya Uingereza itatoa Sh. 8,000/= kwa wapiganaji hao wa miaka hiyo kama kifuta machozi. Dar es Salaam walikwishapewa fedha hizo, lakini walitegemea katika mwaka unaofuata Maaskari wa Mikoa ya Mwanza, Arusha, Tanga na Morogoro wangweza kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri wakati huo nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, habari zilipotoka basi watu wote wakaanza kunitafuta na kuulizia juu ya pesa hizo. Nami kila nilipokuwa naulizia juu ya pesa hizo sikupata jibu sahihi, mpaka nikatoka Ukuu wa Mkoa pale! Sasa niko Mbunge wa Songea Mjini, ninayo makaratsasi chungu nzima yameja hapa na barua chungu nzima, Wananchi hao waliopigana wanaulizia na mara nyingi ni watoto wao, maana wao ni wazee sana, wanasesma hizo fedha ziko wapi, mbona hatuzipati? Nawaambia nendeni mkamwone *DC*. *DC* hatoi majibu sawa sawa! Nendeni mkamwone Mkuu wa Mkoa. Naye hana majibu sawa sawa, Mgambo naye hana majibu ya sawa sawa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelileta suala hili hapa leo, ninaomba Waziri katika *summing up* atoe jibu, awaambie Wananchi wa Tanzania nini kimetokea na fedha hizi, kwamba je, ni kweli Waingereza walitoa hizo fedha na kama walizitoa ziko wapi? Mikoa gani imepata hizo fedha na Mikoa ipi haijapata fedha? Je, kuna utaratibu na mategememo yoyote yale kwamba hizi fedha zitatolewa? Namwomba Waziri Sarungi anipe jibu hili leo ili nikirudi Songea niweze kuwaambia wapiga kura wangu hali halisi hasa ikoje. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo ninapenda nizungumze kidogo juu ya JKT. Jeshi hili ndio Jeshi ambalo mimi mwenyewe nimelianzisha. Waheshimiwa Wabunge wote wanaelewa umuhimu wa Jeshi la Kujenga Taifa, nafikiri wengi wenu mmeピta hapo, mlikuwa *ma-recruit* wangu. Wengi hapa nimewahi kuwafundisha katika makambi mbalimbali. Wakati Jeshi hili limesitishwa, niliona Wabunge wakilalamika humu ndani, wengi tu: "Hili Jeshi litarudi lini, tunataka lirudi mara moja." Kwa hiyo, niliweza kuona kwamba, waliona kuna *gap* kubwa sana. Tangu Jeshi lilipositishwa kulikuwa na *gap* kubwa kwani tabia ya vijana kwa Taifa ilibadilika kidogo. Walikuwa wanavuta bhangi, lakini katikati hapa walikuwa wanavuta bhangi zaidi! Uzururaji ulikuwa ni mwingi zaidi. Vijana kutoka Vijiini wakawa wanakimbilia Mijini kutafuta kazi kwa sababu utaratibu mzuri uliokuwepo wa kuhakikisha kwamba vijana wanakaa kule vijiini ulipotea. Sasa bahati nzuri Serikali ya Awamu ya Tatu imerudisha Jeshi hilo. Tunapongeza sana Serikali kwa hilo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri nilikuwepo kule Ruvu siku ile wakati wa ufunguzi. Nilipoona lile Jeshi linavyofanya mambo yake pale, karibu nitoke machozi kwa furaha. Pia, hotuba ya Amiri Jeshi Mkuu ilinipa moyo sana, ikatamka wazi wazi kuwa: "Sasa nasema kwamba, Jeshi hili la Kujenga Taifa halitasitishwa tena, tutahakikisha kwamba linaendelea." Nafikiri wote tulipata furaha kubwa sana, tena sana. Tunajua majukumu ya Jeshi hili, ndio shule ya vijana wetu wa Tanzania, wanapita hapo kujifunza mambo ya kijeshi kama Askari wetu wa akiba, wanapita kujifunza mambo ya kujitegemea ili waweze kubaki Vijiini badala ya kukimbilia Mijini, pia wanapata mafunzo mbalimbali ya kilimo, ufundi na yale ya kujiamini na kulipenda Taifa letu. Kwa hiyo, tunasema kwamba, Jeshi hili liendelee, tulipe vifaa na tulisaide. Hata hivyo, ninampongeza sana Waziri, Bajeti yake inaleta matumaini kwamba, huenda mambo yakawa ya mafanikio zaidi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuongea juu ya Majenerali Wastaafu. Kwa kweli huwezi kuacha watu kama wale wakazurura zurura hivi hivi tu mradi eti ameshastaafu! Ndio maana Watanzania wanaogopa kustaafu! Mtu anaogopa kustaafu kwa sababu ukistaafu tu unasahauliwa moja kwa moja! Kwa hiyo, unaogopa unataka ubaki humu humu tu, kwa sababu unajua nikotoka hapa basi umekwisha! Sasa, watu kama Majenerali ambao wamejifunza mambo mengi, wenye *experience* kama

akina Gama, wamefanya kazi mbalimbali katika nchi hii huwezi ukawaacha hivi hivi tu wanazubaa zubaa na kadhalika, ni lazima tuwatumie katika maeneo fulani fulani. Kuna maeneo ambayo hawa watu wata-fit na ndivyo dunia inavyofanya. Dunia nzima inafanya hivyo kwamba, huwezi ukawaacha watu kama hawa wanazurura tu hivi hivi, unawapa kazi unawasaidia wanakwenda katika Majeshi wanatoa *lectures*, wanakwenda katika *universities* wanazungumza maneno fulani fulani ya maana na kwa njia hiyo unawapa uhai zaidi na wao wanalipenda Taifa lao zaidi na wanatumikia vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Waziri, amelizungumzia hili neno na ninaunga mkono hotuba ya Mheshimiwa John Malecela, yote ambayo ameyazungumza nayaunga mkono kwa asilimia mia moja. Ni mambo muhimu kabisa ambayo yataweza kutusaidia sisi katika kujenga Majeshi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Baada ya hapo nakushukuru kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Vile vile, ninampongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa hotuba yake nzuri aliyoitao asubuhi hii. Pia, ninawapongeza watendaji wake wakuu katika Majeshi yetu ya Ulinzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 katika Bajeti ya Wizara hii, Wabunge wengi walionyesha imani yao kwa Jeshi lao kwa kutoa kilio chao kuhusu Askari wao kupata chakula bora, yaani walivyopandishiwa *ration allowances*. Tunamshukuru Waziri alipandisha *ration allowances*, lakini alipandishwa kidogo tu, aliwapatia Sh.200/= Kwa hiyo, tunamwomba tena awapatia *ration allowances* kwa kasma hii ili wafikie angalau Sh.2,000/= kwa kutwa kwa wapiganaji wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za *coupon* katika vikosi zilianza mwaka 2002 mwishoni, lakini katika uanzishaji huu kwanza vilanza vikosi vikubwa tu. Kule Zanzibar, ziko kombania nyingine kubwa zilianza kuanzia Januari, lakini huduma kwa vikosi vidogo zilikawia kidogo. Mfumo huu kusema kweli ulikuwa ni mzuri na sasa hivi wazabuni wote wamefurahi kwa sababu wanapata malipo yao bila usumbufu wowote. Hakuna anayecheleweshewa bili yake, kila mwisho wa mwezi ukifika kila mzabuni anapata malipo yake.

Kwa hiyo, kitendo hiki ni cha kufurahisha kabisa, kinyume na zamani ambapo wazabuni wakati mwingine walikuwa wanakaa miezi miwili, mitatu au minne hawajalipwa pesa zao. Lakini hata hivyo, wale waliokuwa wanahudumia kombania katika vikosi, kule chini ya *Brigade* ya Nyuki, bado hawajalipwa fedha zao za miezi mitatu ile ya nyuma kabla ya kuanzishwa *coupon*. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri katika hayo malimbikizo ya madeni, basi waangaliwe kwa jicho la huruma ili nao walipwe fedha zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuongelea kuhusu Hospitali ya Bububu. Ni kweli Mheshimiwa Waziri, ametekeleza yale yote aliyosema, lakini bado kazi ipo. Zile *ward* nne amezimaliza, bado nafikiri kuhamiwa tu, lakini vinatakiwa vifaa vya ndani, nafikiri vitanda bado, halafu na mambo mengine ya kitaalam hayajawekwa. Lakini hata hivyo tunamshukuru sana kwa kufikia hatua ile na tunamwomba lile jengo walilokusudia kulifanya liwe la *x-ray* nalo walimalize kwa sababu ile hospitali inafanya kazi za kila aina. Hospitali hasa ni lazima ipate *x-ray*. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atuwekee *x-ray* pale ili huduma ziweze kuboreka.

Vile vile, *mortuary* pale hakuna, kuna ofisi ya *Company Sergeant Major* tu! Tunaomba ile *mortuary* airekebishe katika kipindi hiki ili tupate huduma za kuweka maiti wetu wanaofariki katika hospital ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hospitali ya Bububu tunajua kwamba, ina *cost sharing*, lakini baadhi ya matibabu yamekuwa ghali sana. Mfano, mgonjwa mwenye kutaka kwenda kufanyiwa *operation* ya *hernia* au *hydrous* bei imekuwa kubwa na sisi ndio tunawapeleka wagonjwa wetu, wale ni wapigakura

wetu kutoka katika Majimbo yetu. Mgonjwa mmoja utaambiwa utoe Sh. 50,000/= ukiwa una wagonjwa kama watatu ni Sh.150, 000/=.

Kwa Mbunge kama mimi nashindwa sana na huduma zile ni lazima niwapatие wapigakura wangu. Kwa hiyo, ningombia hizi za matibabu zingekuwa zote sambamba katika hospitali zetu kwa sababu tunajua Hospitali ya Bububu ni Hospitali ya Serikali, siyo ya mtu binafsi kama tukitaka huduma apate fedha nyngi. Pale ni sehemu ya kutoa huduma muhimu.

Sasa tunaomba tungewekewa angalau unafuu kidogo ili matibabu unapokwenda pale tuweze kuyamudu sisi na unyonge wanaoishi katika Majimbo yetu hawawezi kumudu gharama hizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za madawa vile vile katika mahospitali *Unit Aid Station* zote dawa hazitoshi wala hazikidhi kwa sababu wanapata mgao wa dawa katika Kanda ya kule inakuwa *quarterly* yaani kila baada ya miezi mitatu ndiyo wanapata mgao. Sasa hizi dawa zikifika pale vile vile zinagawiwa kwenye *Unit Aid Station* na vikosi vya pale ni vingi. Kwa hiyo, askari ikifika baada ya mwezi mmoja utakuta wanahangaika sana dawa zimekwisha. Wanapita kununua dawa kwa fedha kutoka mifukoni mwao wenyewe na hawamudu gharama. Kwa hiyo, ningombia ungewekewa utaratibu kama imefika *term* moja wapelekewe *kits* zile *Essential Drugs* yaani kila *Unit Aid Station* ipelekewe *kits* kila mwezi, hiyo ingeweza kusaidia kuliko mfumo unaotumika sasa yaani dawa zinafika katika Kanda zinagawiwa tena. Sasa hela nyngi zinakwisha zinaishia mikononi hazifiki kwa walengwa. Kwa hiyo, utaratibu wa *Essential Drugs* kama ingeanzishwa basi ingesaidia sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Makambi mengi tumeona Kambi nyngi sana hazina uzio. Huwezi kutofautisha baina ya anayekaa ndani ya Kambi au wa nje, uraiani kabisa. Nyumba zimezunguka Kambi sasa hivi utakuta kilio cha wapiganaji wanasesma sisi tumezungukwa na raia kila upande. Hata maeneo ya kufanya mafunzo vile vile sasa hivi yamekuwa fujo kabisa. Sasa tunaomba hizi Kambi Mheshimiwa Waziri, angefanya utaratibu angalau kila baada ya muda akaweka uzio kwa Kambi moja moja ili Kambi zote ziwe ndani ya uzio kwa sababu ziko nje kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ulinzi bila kuwa na *fence* unakuwa hujui lile lindo unalolilinda ni lipi. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atuwekee uzio kwenye Makambi ili tuweze kutofautisha baina ya nyumba za kiraia na *fence* ya kuingia Kambini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kabla hatujaja huku nilipita Makao Makuu ya *Brigade Headquarter 101 KV*. Mheshimiwa Waziri, amejenga barabara nzuri, ile barabara lakini kajenga kwa upendeleo kwa sababu pale *Brigade Quarter* kuelekea *Bavuai Camp*, hasa hizi Kambi nyngine zina barabara mbovu kabisa. Hii barabara ya kwenda Bububu ni mbovu zaidi na umbali wake ni nusu kilometra. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri na ile barabara ingetazamwa kwa jicho la huruma akaitengeneza kwa sababu ile Hospitali ndiyo Hospitali ya kanda na ndiyo sisi wote tunakwenda pale kupata huduma. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri aitengeneze barabara hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba kuzungumzia kuhusu kozi za kitaalam. Vikosi vya SMZ vinahitaji vipatiwe msaada wa kitaalam kwa sababu huku Bara Askari wa Jamhuri ya Muungano, tunasema sisi ni Chuo Kikuu hata Jeshi lake limekuwa ndiyo lina taaluma kubwa zaidi. Kwa hiyo, tukitazama kama Vikosi vya KMKM na JKU, wanaweza kupatiwa msaada mkubwa sana kitaalam. Kwa hiyo, tunaomba hizi kozi za kitaalam zinapotokea basi na sisi tupatiwe mgao. Mfano, kama JKU wanakwenda sambamba na JKT na hapo zamani walikuwa na ushirikiano mkubwa sana. Sasa katika kozi za kitaalam basi wanapoendesha zile kozi na JKU ipatiwe mgao wake uwewe maalum ili washirikiane pamoa uende sambamba kitaalam maana lengo la Majeshi haya yote ni kujenga uchumi lakini yote ni sawa kabisa.

Halafu kuhusu *Navy* na KMKM vile vile wote ni walinzi wa bahari. Kwa hiyo, hizi kozi za kitaalam zikiendeshwa basi na KMKM nao vile vile wapewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache mimi sina zaidi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. (*Makofî*)

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, asubuhi ya leo kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kabla sijaendelea mbele, namshukuru sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na watendaji wake wote, Makamanda wake wote ambao wamemsaidia katika kufanikisha shughuli hii na leo kuiwasilisha kwa ufasaha na majigambo mazuri kujua Jeshi linafanikiwa katika Bajeti hii. Katika mchango wangu nitajikita katika sehemu kuu mbili. Kwanza, shukrani na pili, malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumshukuru sana Waziri kwa haya aliyozungumza. Lakini vile vile nataka kusema kwamba, katika suala zima la Ulinzi ni suala nyeti halafu liko katika pande mbili za Muungano, yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Lakini Taarifa ya Kamati nayo naipongeza sana, ilivyokuwa inatoa maelezo au taarifa yake, imejielekeza sana katika sehemu moja tu ya Muungano. Kwa hiyo, niliona kama walifanya ziara au kutembelea sehemu basi wangetembelea sehemu hizo na kuona hali halisi ya matatizo yaliyopo baina ya pande zote mbili. Hili niliona na taarifa hii ikazungumzia Makambi ya sehemu tu. Lakini hata hivyo, kwa vile matatizo yanaoana au yanalingana pande zote kwa hiyo, sina shaka yale yaliyozungumzwa upande mmoja yataondoshwa yapelekwe upande mwagine ili yahakikishe kuwa yanaondolewa matatizo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu JKT. JKT kwa kweli ni chombo kizuri, kimeanzishwa na ukweli hivi sasa Wabunge wengi wanapata kulenga shabaha kwa kupitia JKT Makutopora. Suala zima hivi sasa jinsi ya kuingiza hao vijana wanaoingia katika Makambi ya JKT, kwa kule Zanzibar tunazo nafasi chache sana ambazo ni 50 tunazopewa kila *intake* inapoingia. Lakini ukiangalia hii Wizara ni ya Muungano na kinachotakiwa hivi sasa tuweke mikakati kuwa vijana ambao watatoka kwenye Makambi ya JKT ndio waajiriwe. Sasa suala hili halitaathiri sana upande wa Zanzibar? (*Makofi*)

Halafu suala jingine kwa nini kusiwe na utaratibu mzima wa kuweka Kambi za JKT, Zanzibar, ambazo zitakusanya vijana wale na tukitaka Maaskari Polisi, tukitaka Wanajeshi, tunakwenda katika Makambi yale tunawaleta huku ili kuhakikisha kuwa zile taratibu na Kanuni wanazifuata katika mfumo mzima wa kupata Wanajeshi au Askari? Kwa hiyo, sasa hivi tunasumbuana sana kwa sababu sifa zilizopo huku Zanzibar hakuna, ukienda Zanzibar huku hakuna kwa hiyo, hili ni suala ambalo linaleta usumbufu wakati mwagine. Lakini kwa nini tusianzishe Kambi wakati hii ni Sekta ya Muungano? Tuantzishe Makambi kule tuwaingize vijana halafu wale wale tuwachukue katika ajira za Muungano kutakuwa hakuna matatizo yoyote ambayo tayari sifa walizoingia nazo ndizo wanazotumia katika kuajiriwa. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kushauri hivyo tu Mheshimiwa Waziri, kama upo uwezekano basi tuweke kitu kama hicho ili kitusaidie hapo baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu suala jingine ambalo nataka kulizungumzia, Mheshimiwa Waziri, alijipigia kifua sana kuhusu michezo. Kwa kweli michezo nchi yetu ilivyo na amani ni mizuri sana kwa Wanajeshi, ambayo inaleta hadhi na heshima kwa vikosi vyetu hivi sasa. (*Makofi*)

Kwa kweli michezo Wanajeshi ndio iliyobakia kwa sababu vyama vingi vya michezo sasa hivi vina migogoro ya nidhamu au ukosefu wa fedha. Lakini sasa suala zima la Wanajeshi kwa hivi sasa nidhamu bado ipo, nafikiri kila wanachotenga kuhusu michezo kinatumika vizuri. Kwa hiyo, michezo bado inaendelea katika Majeshi. Kwa hiyo, ninachoomba waongeze motisha na kuhakikisha kuwa wanapatiwa vifaa vya kileo ili wahakikishe kuwa michezo katika kazi zetu za majeshi nafikiri baada ya miaka mitano au kumi ijayo, timu zote zitakuwa hazipo isipokuwa Jeshi tu kwa jinsi migogoro inavyoendelea Tanzania. Kila siku kupambana Mahakmani. Kwa hiyo, masuala kama haya kwa kweli nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, kuhusu michezo na leo hii Zanzibar, tayari wanaanzisha Michezo ya Majeshi ambayo inaanza leo Kanda ya Zanzibar, sijui kama Waziri unayo habari?

Nafikiri nayo haiwezekani kufanyika Wanajeshi walivyo na nidhamu bila kukutaarifu. Kwa hiyo, inafanyika hivi leo ambayo tunahakikisha kuwa michezo hii baadaye kama nilivyosema ya Kitaifa itafanyika Zanzibar mwaka huu. Wao wanaanza ya Kanda, Kanda ya Zanzibar ambayo inaanza leo. Kwa

hiyo, nawapongeza sana kwa masuala kama haya ambayo tayari tunajisifia na timu ambazo umezitaja ni nzuri zinafanikisha malengo ya michezo ambayo inaleta hadhi na heshima katika michezo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu suala zima ambalo hivi sasa linatusumbua ambalo juzi mlisikia katika vyombo tukitoa kauli, namsifu sana Jenerali wa Jeshi ambaye alikwenda kuwaona wale vijana ambao wanataka kuajiriwa hivi sasa kupimwa Ukimwi. Ni suala kwa kweli hivi vijana wetu katika Kambi za Kijeshi lazima wawe na afya kwa sababu huwezi kuwa Wanajeshi, halafu ukawa ni mtu ambaye ni mgonjwa au mbovu, huwezi kufanya kazi ya Ulinzi. Masuala kama haya kwa kweli yanasiskitisha, ni juzi tu Mheshimiwa Chiligati, Polisi wameondoa vijana kule Moshi 103 ambao afya zao siyo nzuri. Kwa kweli hili linasikitisha sana, naona wakati wa kupimwa sijui uangalifu ulikuwa mdogo au ni kwamba nenda tu mtoto wa mjomba au shangazi bila ya uangalifu wowote na ikatoka hali hiyo.

Kwa hiyo, ni hasara kwani baada ya miezi mitatu unawaondoa vijana warudi majumbani kwa ajili ya magonjwa mbalimbali. Kwa hiyo, hii ilitakiwa kabla hawajaingia kwenye Makambi ilikuwa ni lazima wapimwe afya zao kabla ya kuajiriwa. Kwa hiyo, nashukuru Wanajeshi wanafanya hivyo nafikiri kila baada ya muda wanaangalia afya zao hususan janga la Ukimwi. Kwa hiyo, hili nawashukuru sana kwa masuala kama haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu suala jingine ambalo nataka kulizungumzia sana, ambalo ni kilio, mimi hufikiria wakati wote, Rais, Waziri au Kiongozi yeoyote anapotembelea sehemu, mahali hapo lazima panatokea faraja. Waswahili wanasema mkaa chini ya muasumini haachi kunukia. Lakini tatizo kubwa lililotokea, Waziri ulikuja Kambi ya Potoa na ukaitembelea vizuri sana, tukatembea wote kwa kujigamba. Lakini suala zima ambalo pamoja na unene wote linanikondesha kulisikia kuwa mpaka leo bado Kambi ile hajifanyiwa ukarabati, wala fedha iliyotengwa hajjakwenda kwa wakati, kama ilipelekwa hajifanya kazi ambayo imekusudiwa. Kwa hiyo, suala hili kwa kweli linanisikitisha sana. Kambi ya Potoa kila siku Mheshimiwa Waziri, hata mimi kusimama leo hasa nia na madhumuni siyo kuchangia mada nyingine isipokuwa ni hii.

Nimetumwa na Wanajeshi wa kule kwa sababu wao kusema hawawezi. Hata mkienda ninyi viongozi wanaogopa hata kusema. Lakini wanatukonyeza Wanasiaya ili tuhakikishe matatizo yao tunayasema. Kambi imeanza mwaka 1970 mpaka leo hajjakarabatiwa. Kambi kaazisha Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, lakini kambi hiyo imeshindwa hata kuongeza kibanda cha mgongo. Yaani mpaka leo majengo ni yale yale machakavu, ambayo hayana ukarabati, hayajaongezwa, wamechukua eneo kubwa hivi sasa lakini hakuna kilichoendelea. Kwa hiyo, kwa hili naomba kupatiwa maelezo.

Lingine ni umeme. Nashukuru Zanzibar ina maji mengi na uhakika ni masafa mafupi ambayo unaweza ukaingiza umeme na maji. Lakini tatizo linakuja pale pale, mawasiliano bado hayajawa mazuri baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wanajeshi wenyewe. Lakini suala hili kwa kweli lazima tufikie mahali tulione kama ni aibu na fedheha kuwa wananchi Zanzibar hivi sasa mwanzo mpaka mwisho wana umeme, Makambi ya Jeshi yanashindwa umeme ambapo haifiki gharama ya shilingi milioni tano. Nafikiri hivyo na pale mimi nimehesabu hazifiki nguzo sita, majenereta yale tangu tumekwenda tulienda kuyaangalia majenereta sita aliyoacha Mchina mwaka huo mpaka leo yamebakia mawili ambayo yanafanya kazi. Kwa hiyo, ni kitu ambacho kinasikitisha. Wale Wanajeshi wanafanya kazi katika mazingira magumu, yaani yanawashwa mpaka ikitokea *emergency*. Lakini wanatumia koroboi na chemli. Mafuta ambayo wanapelekewa ni kidogo, hayo hayo yanatumika kwenye magari, hayo hayo kwenye *generator*. Mpaka Mkubwa afanye ziara ya kwenda Zanzibar, *SAO* ndiyo apewe mafuta, la sivyo abakie nyumbani kulala. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hili namwomba Waziri awaangalie kwa jicho la huruma Wanajeshi wale, aangalie ile Kambi ifanyiwe ukarabati ambao unastahili na mazingira tuliyonayo ya leo, la sivyo watabakia nyuma na kujisikia kama wameachwa nyuma. Mimi nilifikiri Kamati, ikitembelea kule Zanzibar isimalizie tu migombani bali ifike vijijini hasa ikaone hali halisi za Kambi zetu zilivyo za vijijini wasimalizie pale wakanyweshwa soda na bia wakamalizia pale *no*, twende vijijini tukaone hali halisi iliyoko vijijini kwa kweli kambi inasikitisha, tunasikitika sana mpaka leo hazijafanyiwa ukarabati. Mimi tokea nasoma shule mpaka leo kambi ile ukienda haina ukarabati wa aina yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo naunga mkono hoja lakini kwa kweli suala hili Mheshimiwa Waziri, aje tena kuangalia kama fedha amezituma zilitumikaje, kama hazikutumika basi zipelekwe nytingine zikatumike kwa suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mchana huu na vile vile nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mkuu wa Majeshi, Makamanda wote wa Majeshi, wafanyakazi wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na JKT. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu nitaelekeza katika maeneo karibu matatu hivi. Lakini nataka nianze na hili linalonikereketa zaidi. Mimi nataka nizungumzie nyumba za wafanyakazi wa Jeshi pale Vitongoji Pemba. Wakati tulikuwa tunatembelea pale Vitongoji nyumba za Askari ni mbovu sana. Sasa kama alivyosema mwenzangu aliyetangulia kuzungumza, Wanajeshi wenyewe kuja kusema hili suala siyo rahisi kwa sababu hawawezi kuja hapa Bungeni na inawezekana pengine wakati wa ziara ya Wakuu wa Majeshi au Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wao hawana nafasi ya kusema. Lakini sisi kama ni wawakilishi wao, tuna haki na wajibu wa kusema hapa Bungeni. Sasa nasema kwamba, nyumba hizi ni mbovu kwa hiyo, Wizara ifanyie kazi ya kuzikarabati. Siyo kuzikarabati tu pia hazitoshi. (*Makofî*)

Kuna Mbunge mwenzangu mmoja, alisema kuwa siyo vema Wanajeshi kukaa uraiani. Kwa maana hiyo na mimi nasema hivyo hivyo si vizuri Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kukaa uraiani pengine wengine wanakaa mbali, Mwanajeshi anafanya kazi Vitongoji lakini anakaa Mtambile. Hawezi kufika kazini kwa muda unaotakiwa. Kwa hiyo, naomba nyumba hizi zikarabatiwe na zingine ziongezwe kujengwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka niliongee ni suala zima la mafao ya Wanajeshi wakati wanapostaafu. Hii kero hata Jimboni kwangu pale Mkanyageni ipo, kuna Wanajeshi huu ni mwaka wa nne wamestaafu lakini mafao yao hawajalipwa. Lakini mbaya zaidi wakati wa kufuatilia mafao yao, wanalahimika wafuatilie Dar es Salaam. Ukishafika pale Dar es Salaam inachukua muda mrefu hujalipwa. Unaweza kwenda mara ya kwanza, mara ya pili, mara tatu, mpaka utarudi kwenu hayo mafao hujayapata, mstaaafu yule anafika mahali kukata tamaa na akikata tamaa ndiyo vurugu inaanza sasa hapo. Anaweza akaona Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haina maana na kwa misingi hiyo hiyo, kama alivyosema Mbunge mwenzangu aliyetangulia, ndipo ugomvi unapoanza kusema kuwa afadhali nifie humu humu Jeshini. Wengine wanakuwa wako tayari kustaafu, lakini anajiuliza mimi nikistaafu maafao yangu nitayapata wapi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba sasa kabla Mwanajeshi hajastaafu, atayarishiwe mafao yake mapema sana. Akistaafu tu apewe *cheque* yake na mafao yake arudi nyumbani kwao. Hapo watu watakuwa na imani na Jeshi lao, lakini tabia hii ya kumstaafisha Mwanajeshi halafu hana uhakika na mafao yake, kwa kweli itatuweka mahali pabaya sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Waziri kuanzia sasa achukue hii kazi ya kuhakikisha kwamba, Wanajeshi wanaostaafu wanalipwa maafao yao mapema sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wanajeshi waliofariki muda mrefu, kipindi cha Bunge kilichopita niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Waziri, kuhusu Askari waliofariki kwa nini hawajalipwa mafao yao? Mimi Jimboni kwangu ninaye Mwanajeshi mmoja pale Mkanyageni, huu ni mwaka wa saba amefariki dunia, sasa ameacha watoto hawapungui saba, ana mke ana familia, hivi familia yake hii itakuwa na imani na Serikali hii? Kwa hiyo, naomba kwamba, wale waliofariki dunia akiwemo na yule Askari kutoka Jimboni kwangu, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa akitaka hiso taarifa hapa siwezi nikazisema, lakini nitamwambia ni Mwanajeshi gani amefariki wapi na nambari zake za kazi halafu tuhakikishe kuwa analipwa. Naamini kuwa siyo huyu tu, inawezekana wako wengi. Kwa hiyo, naomba wale Askari waliofariki basi warithi wa marehemu wapewe mafao yao, wasiichukie Serikali, Serikali hii

nzuri bwana. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanye kazi ya kuhakikisha kwamba, Wanajeshi wanaofariki wanalipwa mafao yao mapema sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Askari Mwanajeshi na Askari wa JKT, wakistaafu kwa kawaida hutegemea warudi nyumbani kwao, siyo wengi wanaostaafu kazi wakakaa pale pale wanapofanyia kazi, wengi wanapenda wakimaliza muda wao wa kazi warudi majumbani kwao. Hapa nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuwakopesha hii mikopo. Lakini sasa tunachopata shida usimamizi, unaweza ukamkopesha Mwanajeshi fedha za kujengea nyumba kumbe akafanya mambo mengine. Sasa naomba Serikali mnapowakopesha hawa vifaa vya kujengea, mhakikishe kwamba, hizi fedha za kujenga na vifaa vya kujengea kweli wanajengea nyumba makwao. Hili linaweza likatusaidia sana. Lakini ukimkopesha mtu fedha ukamwambia basi nenda kajenge, wengine wakishazipata tu pale pale ukimkopesha saruji anakwenda kuiuba anatafuta fedha anaweka mfukoni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ni vema hizi fedha za mkopo mnazozitoa mhakikishe Wanajeshi wanajenga majumbani kwao, wakimaliza muda wa kazi warudi kwao wale wanaopenda kwao, vinginevyo mnaweza mkalaumiwa bure hamkopeshi fedha za ujenzi kumbe mnajitahidi kukopesha, lakini fedha za ujenzi hawafanyii hiyo kazi ya kujenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli maelekezo yangu hasa yalikuwa hayo, sitaki nichukue muda mrefu kwa sababu muda wenyewe ni mdogo. Nimemaliza ya kwangu halafu nikiongeza kuchangia mengine naweza nikayaharibu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi nachukua nafasi hii kwa mara ya mwisho, kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Wakuu wa Majeshi kwa hotuba hii nzuri na ili nisije nikasau naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe mionganoni mwa watu watakaochangia katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii. Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza Kiongozi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Mkuu wa Jeshi na Wasaidizi wake, Mkuu wa JKT na Watumishi wote katika Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimevutiwa sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Lakini kabla sijaanza kuchangia, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, nimpongeze kwa uchambuzi wake katika hotuba yake. Mengi kabisa ambayo tulikusudia kuyasema, ye ye ametusaidia ameyasema kwanza. Lakini nimpongeze zaidi Mzee huyu kwa kupata jiko kipindi hiki. Huyu Mzee kadri mnavyomwona na uzee wake, lakini ni kijana wangu. Tumembariki na tunamwombea kila la kheri katika jiko lake hili, Mwenyezi Mungu, awaepushie kila aina ya shari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze na mimi kwa kuungana na wenzangu amba o wamechangia hapa katika suala zima la vyombo vyetu vya Ulinzi hususan katika kuyaangalia Makambi ya Jeshi, Nyumba zao wanazokaa, Kambi zenye zilivyo, jinsi nyingi zilivyozeeka. Kwa mfano, Kambi ya Mtoni pale Zanzibar, mwaka 2002 nilisema na mwaka huu nitasema na mwakani ikiwezekana nitasema. Kwa Zanzibar ile ndiyo Kambi ya mwanzo ya jeshi ambayo tangu ukoloni ilikuwepo. Majengo yaliyopo katika Kambi ile sasa yamezeeka, ipo haja ya kufanya kwa makusudi, ukarabati katika Kambi ya Mtoni. (*Makofi*)

Lakini si Mtoni tu, Kambi ya Welezo Zanzibar na yenye ukiangalia ukienda ukiona vijana wetu wanakaa, juu bat, ndani bat, mpaka leo bado juhudhi hajijachukuliwa kurekebisha Kambi ile. Ukienda kwenye Kambi ya Ubago, zilijengwa nyumba miaka zaidi ya 15 hakuna ukarabati wowote, yale majengo sasa hivi wanaishi tu wale vijana. Sasa naiomba Serikali ichukue juhudhi za makusudi za kufanya ukarabati katika Kambi na si hizo tu ni Kambi zote za Jeshi. Kwa bahati mbaya sana Wanajeshi siku hizi wana kazi kubwa sana na wana bahati nyingine kwamba, wamewekewa wigo, Viongozi wa Siasa hawaruhuswi kuingia katika Makambi wakatoa jasho lao. Mle anaingia Waziri wa Ulinzi, amejikaza Mkuu wa Majeshi,

wakifika mguu sawa, yanayosemwa ni hayo hayo hakuna la ziada, hawana uhuru wa kusema matatizo. (*Makofî*)

Nashangaa sana sioni sababu ya msingi ya kumfanya Mbunge wa Jamhuri ya Muungano asiingie katika Kambi ya Jeshi, kuwasikiliza matatizo yao, sioni sababu. Nahisi Viongozi kama Wabunge kutokwenda katika Kambi za Jeshi ni kuwapunguzia haki Wanajeshi ya kusema matatizo walijonayyo. Vijana hawa wanafanya kazi vizuri na wana nidhamu nzuri, lakini hawana pa kupumulia mengi sana. Ningemwomba Serikali katika siku zijazo, waangalie upya sheria ile kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kidogo nimemsikia Mheshimiwa Waziri, anazungumzia Hospitali ya Bububu. Mheshimiwa Waziri, anapoizungumzia Hospitali ya Bububu na Bunge hili akileleza unaweza ukasema hiyo Hospitali labda ukifika ni sawa na peponi. Lakini katika eneo ambalo Hospitali ile watu wanatibiwa katika hali ya mazingira ambayo siyo mazuri ya kihospitali ni ile. Ni eneo ambalo kwa kweli majengo yake yanatia aibu, haidhuru Mheshimiwa Waziri, kajitahidi kiasi cha kutosha, ningemwomba Serikali ichukue jitihada za makusudi za kuijenga ile hospitali angalau iwe hospitali ya kisasa pale Zanzibar. Hospitali ya Bububu ndiyo kubwa katika Hospitali za Jeshi pale Zanzibar. Lakini si hiyo tu, tuna Hospitali ya pili ya Uelezo pale. Hospitali ya Uelezo tumeifungua vizuri na kila kitu, lakini ukienda kuiona sasa hivi imesharudi katika hali mbaya na vifaa hakuna. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, hospitali zote mbili hizi aziangalie kwa jicho zuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ana sifa nzuri sana. Unapomwambia jambo hawezi kukubishia, atakukubalia tena vizuri, atakunyenyekea, lakini njoo kwenye utekelezaji wa kazi. Sasa tungemwomba katika kipindi hiki, maana huu mwaka wa 2003 ndio tunaambizana yatekelezwe haya mambo. Mwaka 2004 hatuambizani. Ukiangalia katika *Hansard*, mimi ndiyo nilikuwa mtu wa mwanzo kwenye mwaka 1987 kutoa Shilingi ya Jeshi na ilitoka nikapumzika tukaja tukairudisha usiku, nadhani unakumbuka. Sasa tusije tukafika huku katika masuala mengine haya. Nataka nieleze tu hiyo kwa ufupi.

Lingine ambalo hawa Wanajeshi wanانung'unika ni suala la mikopo ya vifaa vya ujenzi. Wanajeshi wanakopeshwa magari aina ya Hyundai. Kwa nini mnawakopeshwa Hyundai na kuna magari mazuri? Wakopeshwe magari yanayoweza kuwasaidia kwenda kazini na kufanya shughuli zao nyininge. Wakopeshwe vifaa vya ujenzi ili wanapostaafu wawe na nyumba zao za kuishi. Tuna Wanajeshi pale Zanzibar wamestaafu, ukimwona alikuwa Kanali, ni aibu! Utamkimbia! Hana uwezo wa kuishi, hana nyumba, hali yake hohehahe. Sio kosa lake, ni kwa sababu *system* haikumsaidia wakati anafanya kazi. Mshahara wanaopata huu ni wa kula tu. Huwezi ukapata mshahara halafu ukasema utajenga kwa mshahara wa Kijeshi. Mwanajeshi pia ana masharti yake, kwanza awe *smart*, halafu kuna zile dabliyu lazima zikamilike. Ndio Mwanajeshi! Sasa leo unamsema mshahara huo anaopata kidogo, basi aishi, ningemwomba Serikali iwe na mikakati wa makusudi wa kuwapa mikopo ya ujenzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumzia kuhusu wastaafu. Mwanajeshi anastaafu mwaka immoja kutoka Zanzibar kule, kwanza akishastaafu, akishavua yale magwanda, ana nidhamu ya Kijeshi na haki yake anakaa mwaka mzima hajaipata, mwaka wa pili hajapata, thamani ya pesa inateremka, ikiteremka anahangaika, akija akiipata thamani imekwisha, anadaiwa *fees* ya watoto na hali yake inakuwa mbaya. Ningesema kwamba, Serikali yetu hii ambayo ni nzuri iwe na mkakati kwamba siku mtu anayostaafu na *cheque* yake anaipata. (*Makofî*)

Niliwaona juzi *Ma-Brigadier*, wale *Ma-General* wanasingidikiza na *cheque* yake anaondoka nayo! Sio tena anaanza kurudirudi Ofisini anambembeleza, anaambiwa lakini wewe bwana ulikuwa Askari zamani, sasa hivi Afande ni mimi. Kwa hiyo, mguu sawa, geuka nyuma tutazungumza baadaye. Sasa hili Mheshimiwa Waziri, ni la kwetu sisi wanasiisa, kujenga mazingira mazuri katika Jeshi na kujenga mazingira mazuri katika Jeshi ni kuhakikisha wale wastaafu wanapata haki zao mapema iwezekanavyo. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la elimu, nataka niipongeze sana Serikali hii kwamba, ina Shule za Sekondari ambazo wanasona Wanajeshi na inawaendeleza Wanajeshi kielimu mpaka Chuo Kikuu. Kwa hiyo, nashauri utaratibu huu uendelezwe maana sasa yameshakuwa tayari yanaanza mazonge kwamba aah, maana yake sasa hivi tuna watu wengi wa Chuo Kikuu wanataka, kwa hiyo, tutakuwa

tunawaajiri tu, hapana. Utaratibu wa kuwaendeleza Wanajeshi kielimu wakiwa kazini uendelee. Tena uendelee kwa nguvu zote kwa sababu wapo Wanajeshi walijirijiwa wakiwa Darasa la Saba sasa hivi wana taaluma ya Chuo Kikuu na wanafanya kazi nzuri sana. Naomba sana Serikali kwa nguvu zake zote iendelee na utaratibu huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo, kama utaratibu huu unaendelezwa, nilikuwa naiomba Serikali kwa bidii yote kwamba, iendelee na utaratibu wa mwanzo wa kuwaajiri vijana wanaomaliza Darasa la Saba ndani ya Jeshi na wakiwa ndani ya Jeshi watapata taaluma. Kwa kule Zanzibar waajiriwe vijana waliomaliza Darasa la Kumi ndani ya Jeshi. Wakiwa ndani ya Jeshi watapata taaluma mpaka watajiendeleza huko wanakofikia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninao Ushahidi, mfano Uingereza pale, mmoja katika Mawaziri Wakuu wanaopendwa sana na historia nzuri ni Mr. Churchill. Churchill taaluma yake ni Darasa la Nne. Mpaka leo ikiwa utatoa hoja nzuri katika Bunge la Uingereza na ikapendeza, basi unakimbia mbio kwenda kugusa lile sanamu lake, unagusa mguu wake maana yake wewe una falsafa kama yule, hata kama wewe ni *graduate*. Kwa hiyo, binadamu tusiwapuuze kwa sababu wana taaluma ndogo tukaanza kujenga tabaka la wasomi na wale wengine wakawa hawana haki katika nchi hii. Ni vizuri vijana wetu wa Darasa la Saba na Darasa la Kumi waajiriwe katika Jeshi lakini waendelezwe kitaaluma. Naomba kupendekeza hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa pia nasema kwamba, Jeshi la Kujenga Taifa, linafanya kazi nzuri sana na humu katika Bunge ukija ukiwahoji, ukiwadodosa, karibu wengi wamekwenda JKT. Wale waliokwenda JKT ndani ya Bunge na nje, nidhamu zao zinakuwa nzuri zaidi. Nilitaka niseme, hili Jeshi liendelee. Lakini wazo langu ni kwamba, JKT na JKU umefika wakati sasa wa kuunganishwa Jeshi likawa moja. JKT na JKU ya Zanzibar likawa Jeshi moja tukaungana. Kwa hali hiyo hiyo, siku za nyuma katika Muafaka tulizungumza kwamba, KMKM badala ya kufanya kazi Zanzibar sasa ifanye kazi Tanzania nzima. Sijui utekelezaji huu umekwenda wapi mpaka leo? Nani anazungumza? Zaidi ya miaka mitano mambo hayo yamekaa kimya, hakuna msemaji, tunasikiliza tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jeshi, nilitaka niseme tu mipaka yetu iangaliwe vizuri. Mipaka ni pamoja na bahari. Bahari ya Zanzibar ile, Tanzania yote imekwenda mpaka Mombasa, hivi kuna chombo gani? Nasikia tu Serikali inanunua ndege, kwa nini isinunue manowari? Sasa hivi imeshafikia nchi hii ina miaka 40 ya uhuru lazima tuwe na manowari ambayo inalinda mipaka yetu. Inalinda na kuangalia mambo yote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sitaki nigongewe kengele ya pili, nataka nimalizie tu kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Awali ya yote naomba nitamke tu moja kwa moja kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Makamanda wote, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kwa kipindi cha muda mrefu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Waziri kwa kusoma hii hotuba yake Kijeshi. Maana nilikuwa naona anasoma kama Askari Jeshi. Lakini nadhani pia ukifanya kazi na Wanajeshi unakuwa kama Mwanajeshi kabisa. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu kwa makusudi kabisa iliamua kuchukua uamuzi wa kuuza nyumba za Serikali kwa Maafisa wake wa Serikali na nadhani ilifanya hivi kwa nia njema kwa sababu ya kutaka kuondoa adha ya Makazi kwa ajili ya Maafisa wake. Mimi nimekuwa nikijiuliza kwamba, wale wafanyakazi ambao hawapo ndani ya Serikali Kuu, wao watanufaika vipi na

mpango huu wa kukopeshwa nyumba au kujengewa nyumba hasa wafanyakazi ambao wako kwenye Taasisi hizi za kijeshi likiwemo Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa, Polisi, Magereza na Kadhalika?

Kwa hiyo, nilichotaka kushauri ni kwamba kuna umuhimu sasa wa Serikali kuwa na mpango wa jumla wa kuondoa tatizo la Makazi kwa wafanyakazi wake na hasa tatizo la ujenzi wa nyumba za Askari katika Makambi ya Jeshi. Lakini tunachozungumzia hapa ni vitu viwili kwamba, kuna ujenzi wa nyumba za Makazi ndani ya Makambi yetu ya Jeshi. Lakini pia tuangalie kwamba, kuna umuhimu wa kuzungumzia ujenzi wa nyumba kwa maana ya nyumba binafsi kwa hawa Wapiganaji baada ya kuwa wamestaifu kazi. Kwa hiyo, nilichokuwa nashauri ni kwamba, pamoja na kwamba tunazungumzia ukamilishaji wa nyumba hizi ambazo ziko ndani ya Makambi, lakin tuangalie ni utaratibu gani ambao unaweza kutumika, Serikali iandae mpango mahsusii kuwa na Mfuko Maalum wa ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kuwakopesha Maaskari waweze kujijengea nyumba katika maeneo wanayokusudia kuishi baada ya kustaifu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie nyumba za Makazi kwa Wanajeshi. Katika kipindi kilichopita cha Bajeti, nilizungumzia kuhusu kusuasua kwa ukamilishaji wa nyumba za Makazi ya Askari kwenye Kambi ya Jeshi Makoko Mjini Musoma. Katika kuzungumzia hilo pia kulikuwa na kutokukamilishwa kwa nyumba nyingine kwenye Kambi ya Makambako kule Njombe Iringa. Nakumbuka Wizara ilitoa ahadi kwamba, kwenye Bajeti ya mwaka huu, zingetengwa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa nyumba hizo za makazi katika Kambi za Makambako, Njombe na Makoko, Musoma Mjini. Sasa nimejaribu kupitia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na nimejaribu kupitia Kitabu cha Bajeti ya Maendeleo, sijaona sehemu ambapo zimetengwa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo ya nyumba za Askari pale Makoko katika Jimbo langu la Musoma Mjini. Sasa sikusudii kuondoa Shilingi wakati tukiingia kwenye Kamati ya Fedha ya Bunge, lakin natumaini kwenye fedha ambazo nimeziona zimetengwa kwa ajili ya ujenzi, kwenye Kitabu cha Maendeleo zipo takriban Shilingi bilioni 1.5 na hazijaelezwa *construction* ambayo imetajwa mle ndani ni kwenye Kambi zipi. Kwa hiyo, nategemea wakati Waziri aki-wind up ataelea kwamba, ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha nyumba za Wanajeshi katika Kambi ya Makoko pale Mjini Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikusudia kuzungumza ni kuhusu hii Taasisi ya Nyumbu. Kama kuna vitu ambavyo kwa kweli vinasikitisha au vinatia huzuni katika miradi ambayo ilikuwa ni ya muhimu sana kuendeleza Sekta ya Sayansi na Teknolojia ni ile Taasisi ya Nyumbu pale Kibaha. Maana tunapozungumzia mabadiliko ya kiteknolojia kwamba tunataka kulifanya Jeshi letu liwe Jeshi la kisayansi zaidi na Jeshi ambalo linachukua teknolojia mpya, sidhani kwamba, tutakuwa kwenye nafasi nzuri ya kukamilisha azma hiyo kama hatuna Taasisi ambazo zitajihusisha moja kwa moja kwenye hiyo Sekta. Sasa Taasisi hii wakati inaanizishwa na Marehemu Baba wa Taifa, wakati wa Awamu ya Kwanza, ilitaka ku-transform Jeshi liwe la kisayansi, ambalo linaweza kuwa na ubunifu na wale wabunifu wakapata sehemu ya kwenda kufanya ubunifu wao. Lakini Taasisi hii imeachwa, kila mwaka tunaambiya fedha hazikupatikana za kutosha kuweza kuendeleza utafiti na kuendeleza kazi katika Taasisi ile. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kitu kimoja ndani ya Bunge lako Tukufu kwamba, kwa wale ambao wanafika pale *Dar es Salaam International Airport*, kuna gari moja la kuzima moto ambalo limetengenezwa na Taasisi hii na ni moja ya sifa ambazo lazima tujivunie kwamba tuna vitu vyetu wenywewe. Sasa, hivi ndio vitu vya kuangalia tunapozungumzia mabadiliko ya kulifanya Jeshi hili liwe la kisayansi zaidi. Kama hizi Taasisi hatuwezi kuzipa fedha kufanya kazi, hivi tutalibadilisha hili Jeshi letu liwe la kisayansi kwa kutumia utaratibu upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, katika fedha ambazo Serikali inaweza kutenga kwa ajili ya kufanya *research* na hii Taasisi iwe ni moja ya Taasisi ambazo zitapewa fedha kwa ajili ya tafiti na ugunduzi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Majeshi ya wenzetu wakati wa kipindi cha amani, yanajihuisha na vitu vya ugunduzi, yanatengeneza silaha na yanaauza na inakuwa ni moja ya vitu ambavyo vinatengeneza uchumi wa nchi zao. *South Africa* sasa hivi wanaauza silaha kama zilivyo nchi nyingine za Ulaya. Sasa wenzetu hawa wa nchi zilizoendelea hawatakubali kuona Taasisi kama Nyumbu au Mzinga zikiendelea kwa sababu wanajua tutaondoilea ile dhana ya kuwa tegemezi kwao. Kwa hiyo, pendekezo langu ni kwamba,

kwa kuanza basi, Waziri alichukue hili kwamba, inapokuja kwenye Bajeti ya Wizara yake mwaka ujao wa fedha, aangalie ni namna gani atazisaidia hizi Taasisi mbili. Taasisi hii ya kwanza ya Nyumbu na Mzinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Jeshi letu lianze kwa mtindo huo, mimi nilikuwa nashauri kwamba, kwa mfano, pale ambapo tumeanzisha tena Jeshi letu la Kujenga Taifa kwamba, tumeanza sasa kuchukua vijana, nilikuwa nashauri kwamba, Wizara ya Ulinzi kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara kuititia *SIDO*, basi *SIDO* ione namna gani inaweza kuwekeza ndani ya Kambi zetu za *National Service* miradi midogo midogo ambayo tayari JKT wamekwishaianzisha, ipate msukumo, ipate uwezo wa kifedha na utsaalamu kutoka *SIDO* ili miradi ile iweze kuwa endelevu na iweze kuendeshwa kitaalamu zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Kwa sababu madhumuni sasa ya kuwaweka wale vijana wetu pale ni kuwafundisha namna ya kuzalisha na wazalishe kitaalamu. (*Makofi*)

Lakini lingine pia nilikuwa naishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kuititia tena Taasisi nyingine ya *VETA* kwamba, Wizara ishirikiane na *VETA* kuhakikisha kwamba, *VETA* inapeleka uzoefu wake ndani ya Kambi hizi za Jeshi la Kujenga Taifa, ili vijana wetu wanapokuwa pale wajifunze kazi za ufundi stadi na wakitoka pale wawe na Vyeti vya kuwawezesha kuweza kujajiri au kuajiri na Taasisi zozote katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kitu kimoja ambacho nadhani sio vizuri nikaacha kukizungumza. Mwaka 2002 nilizungumzia kwamba, Wizara ya Ulinzi ikishirikiana na Wizara ya Afya waangalie ni jinsi gani Hospitali Kuu ya Jeshi ya Lugalo inaweza kusaidiwa na ikaendelezwa ikawa hospitali ya kuweza kushughulikia matatizo ya viongozi wa nchi hii kwa maana ya tiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi viongozi wanatibiwa kwenye Taasisi za Afya ambazo ziko chini ya Jeshi. Kwa hiyo na mimi naishauri Wizara ya Ulinzi ilitazame hili kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kwamba, Hospitali ya Lugalo izidi kuendelezwa, ipewe raslimali za kuiwezesha kufikia mahali ambapo inaweza kuwa hospitali kubwa ya kisasa kuliko hapo ilipofikia. (*Makofi*)

Napenda niishukuru sana Serikali ya Ujerumani, kwa msaada ambao wametupa kuboresha huduma za afya katika hospitali zetu za Jeshi. Lakini niseme, jirani anapokusaidia na wewe onesha ile nia ya kujisaidia mwenyewe. Kwa hiyo, siyo tu kwamba tumesaidiwa, basi tubweteke tuishie hapo, lakini kuna umuhimu wa Serikali kuweza kuzisaidia hospitali zetu za Jeshi hizi zisifike mahali zikakwama baada ya wafadhili kujiondoa. (*Makofi*)

Nadhani mengine mengi yamezungumzwa. Lakini kama nilivyosema, sikusudii kuondoa Shilingi, ni matumaini yangu Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, atanipa taarifa ni kiasi gani cha fedha ambacho kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha nyumba za Makazi kwenye Kambi ya Kikosi cha Makoko pale Mjini Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba niwapongeze sana Wapiganaji wetu kwa kuwa Taasisi ya mfano kwa maana ya nidhamu na kwa kuwa Taasisi ya mfano kwa maana ya uadilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja wa wapiga vita wakubwa wa rushwa. Kama kuna Taasisi ambayo ni mfano, nadhani basi ni hii ya Jeshi la Wananchi na *National Service*. Ningombaa basi na sisi wengine uraiani tuige mfano huo wa kuwa waadilifu ili tuweze kuitumikia nchi yetu, tuweze ku-deliver yale ambayo wananchi wanakusudia kuyapata kutoka kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib kwamba, angechangia, lakini alitoka. Amesema dakika zilizobaki zinamtosha tu. Kwa hiyo, nakuita Mheshimiwa Mohamed Khatib, uweze kuchangia. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuhitimisha sehemu hii ya asubuhi ya kikao chetu. Napenda nichukue nafasi hii kwanza,

kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Wasaidizi wake wote. Kabla sijaendelea kusema, nasema kwamba, naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

Mambo mengi yamezungumzwa hapa na mojawapo likiwa ni hili la nidhamu ya Jeshi letu. Hata mimi napenda nichukue nafasi hii kwa kweli kuwapongeza sana Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi la Tanzania, kwa nidhamu yao kubwa wanayoionesha daima ambayo imesaidia katika kile kielelezo kinachoonekana kwamba, Tanzania ni Kisiwa cha amani. Vurugu nyingi kwa kweli zinazofanywa katika nchi mbalimbali zinaonekana kwamba, huu mkono wa Jeshi uko usoni kwa sababu daima vurugu haziwezi kufanywa na mtu mnyonge. Mtu mwenye nguvu, mwenye mabavu akiamua kufanya vurugu, basi nafasi ya kufanya vurugu anayo. Lakini Wanajeshi wetu pamoja na fursa yote tuliyowapa, silaha zote wanazo wao, wanazijua wapi zinapokaa na nguvu zake, lakini bado wanazitumia kwa kupambana na maadui wa nje na sio kupambana na wale waliokuwa wakionekana kama ni maadui wa ndani na tokea hapo hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema tu kwamba, kama nilivyo sema awali, sikuwa na dhamira ya kusema maneno mengi, isipokuwa tu kwa sababu katika Bunge hili tumo Wabunge tunaowakilisha Vyama mbalimbali, basi ni wazi kwamba na mawazo yetu pia na maoni yetu yatakuwa yanaendana kulingana na hili Bunge letu linavyowakilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kama nilivyoichukua wakati wa kuchangia katika Wizara ya Mambo ya Ndani kusikitikia jambo moja tu, nalo ni hili la uajiri wa Wanajeshi. Napenda kumwarifu Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamba, sisi kule Pemba kwa kweli tuna masikitiko makubwa katika hii shughuli ya kuwaajiri vijana wetu kuingia katika Jeshi la Wananchi. Hapa kwa kweli pana mtihani. Shughuli hii inafanyika kwa njia ambayo hairidhishi. Jeshi hili tunaliita ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Watanzania wote wanao-*qualify* kazi hii kwa uwezo, akili na maadili, wanapaswa kuajiriwa katika Jeshi hili. Sasa tatizo tunalolipata sisi kule Pemba ni kwamba, tumebaani kwamba, panafanyika ubaguzi mkubwa katika kuwaajiri hawa wanajeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ubaguzi unaofanyika ni kwamba, wanatumia itikadi za kisiasa. Vijana wote ambao wanaonekana kuwa wanaipendelea *CUF*, hawapati kabisa nafasi ya kujiunga na Jeshi hili.

WABUNGE FULANI: Waongo.

MHE. MOHAMED JUMA KHATIB: Kuna ushahidi, kuna wakati mmoja Bwana mmoja ambaye ni Sheha, mjukuu wake alikuwemo katika *list*, alikwishapenya. Lakini akaenda mahali ambapo ndio kwenye *control* ya uajiri akaenda akasema hasa, kwamba, “huyu mimi namfahamu ni mjukuu wangu na huyu ni *CUF*. Atolewe! Akafutwa. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wasioelewa madhara ya ubaguzi ambao sisi Watanzania kwa kweli ulitugharimu sana, nasema tena kwamba, ulitugharimu sana, tulipeleka Wanajeshi wetu nje ya mipaka ya nchi hii kwenda kupigania haki na umoja. Sasa inatia aibu kweli kweli kumwona Mbunge anashabikia suala la ubaguzi. Sheria Na.5 ya Usajili wa Vyama vya Siasa, haikutaka kabisa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama viingizwe katika ushabiki wa kisiasa na hili liko hata katika uajiri. Mimi nasema ni hatari kwa kweli kwa sababu ukisema kwamba, sasa hivi mtu tunayemshuku kwamba, ni *CUF* au aliyemo katika Chama chochote kile cha Upinzani hatutaruhusu kumwajiri katika Jeshi, tuna hakika gani kwamba, hao Wanajeshi waliopo sasa hivi...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):
Kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni Na.50(1), inamzuia Mheshimiwa Mbunge kusema uongo ndani ya Bunge. Sisi tunaamini kwamba, Jeshi letu linafanya kazi kwa mujibu wa Katiba na Majeshi yetu yote ya Ulinzi na Usalama hayana ubaguzi wala Serikali haina ubaguzi. Ningetaka Mheshimiwa Mbunge, afute maneno aliyoyasema kwamba, Jeshi linafanya upendeleo katika ajira kwa mujibu wa kisiasa au upo ubaguzi ndani ya Jeshi au atoe Ushahidi. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa unataka kufanya nini? Ametoa kuhusu utaratibu na wewe unataka kutoa mwininge? Hapana imetosha hii mpaka itolewe maamuzi. Sasa Mheshimiwa Msemaji, una njia mbili za kufanya, ama kusisitiza unalolisema ili utakiwe ulete ushahidi ama kuondoa maneno yako.

MHE. MOHAMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikusema kama Jeshi lina ubaguzi, hapana. Nimesema kwamba, hawa watu walio na dhamana ya uajiri wanafanya ubaguzi na ninaweza nikwambie kwamba, kule kwetu wanaopewa dhamana ya kuajiri hawa ni Masheha. Masheha ambao ile ajira yao haipati mtu yeoyote kama hajakuwa anatoka kwenye Chama cha Mapinduzi, huyu Sheha asili yake anatoka kwenye Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, katika kuajiri hawa Wanajeshi, nimesema hapa Jeshi letu ni safi halina tatizo, halina ubaguzi, lakini hawa walio na mamlaka ya kuwachukua hawa vijana kuwaingiza katika Jeshi, ndio wanaotupa matatizo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Alichosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba, Mheshimiwa Mbunge, amelisingizia Jeshi kwamba, linaajiri kufuatana na itikadi ya mtu. Mheshimiwa Mbunge, anasema mimi sikusema Jeshi, nimesema sijui cheo gani huko, Sheha. Kwa hiyo, sasa ni juu ya Mto hoja. Unasemaje? Mimi nadhani maadamu amefuta hilo, badala ya kuliendeleza mimi nafikiri tuamini kwamba, amefuta. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge, muda umepita, tuko saa 7.00 sasa napata taabu kukupa muda kwa sababu muda umepita. Lakini mchana tutaendelea na mimi nitakupa tena dakika tano kama utahitaji ambazo zimetokana na *interaction* hii. (*Makofi*)

Baada ya kusema hivyo, kipindi cha mchana ataanza kuchangia Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, kumalizia dakika tano, halafu tutakuwa na Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Magayane, Mheshimiwa Msafiri na Mheshimiwa Faida Bakar, ndiyo watakuwa wachangiaji. (*Makofi*)

Baada ya hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

MHE. MOHAMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa ahadi yako. Lakini niseme tu kwamba, namtakia kheri Mheshimiwa Waziri, aendelee vizuri na shughuli zake na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza, kukupongea wewe na kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika usimamizi wa kisiasa. Mheshimiwa Profesa Sarungi, raia mwenzetu lakini anaendesha vizuri jeshi hili na utaratibu wa Wizara yenyewe na amekuwa mzoefu katika masuala haya. Nimeona mabadiliko kadhaa katika uchangiaji wa Waheshimiwa Wabunge na wana sifa kemkem zinawendea, kwa hiyo, hii ni dalili nzuri tu kwamba anaendesha vizuri. (*Makofi*)

Baada ya shukrani naanza na mara nyingi naanza kutoa historia ndogo kuhusu mambo ya ulinzi na usalama wa nchi yetu. Kwanza, dunia inaitambua Tanzania katika ramani ya dunia kwamba, kwa sababu ya mshikamano wake na majeshi yetu, taarifa iliyotolewa na Kitabu kinachoitwa *World Almanac* katika ukurasa 269, katika nchi zote toka Afghanistan mpaka Zimbabwe, zikiwemo nchi nyingi tu ambazo zinaambiwa majeshi yao yamechemsha. Nchi kama Singapore, Silvania, Quatar, Estonia, zimeonyesha kipaumbele katika kumuweka Mungu mbele, umma kati, majeshi yakabaki nyuma katika kulinda nchi zao.

Tanzania katika upande wa majeshi, wameandika sifa zake lakini kilichonifurahisha katika ukurasa huo mkiupata katika Kitabu, wameandika “*It is active troop*”. Hiyo peke yake ni sifa kubwa sana kwa nchi hii. Nitasoma ukurasa 664 unaitwa, “*World Almanac*, Toleo la mwaka 2000”. Pale ndiyo sifa za nchi zote duniani, zilizochemsha na zinazofanya vizuri. Tanzania katika upande wa jeshi ni *active*. Tumeambiwa ni *active* sisi. Ila tu kwenye sifa ya dunia huambiwa kwamba Watanzania mara nyingi nchi

kama hizi huwa hazijaribu dhambi kwamba tuna majeshi ambayo yana utaratibu. Inaonekana kwa utaratibu na ustaarabu wake kutokana na nchi zilizotengemaa.

Tanzania ni kwamba, tumetoka mbali, watu wanasesma kwa nini mmetoka mbali kwa nini hamjamfika. Safari ya kuongoza haina kufika. Ukipika ndiyo umefika unawaachia wenzio wanakwenda. Kwa hiyo, ndiyo tunakuambia tumetoka mbali, hivyo sifa zake na historia yake. Kwa hiyo, Tanzania inastahili sifa hiyo, tumeenda kuwaelezea ulinzi wetu katika mwaka 1971 kwa Mwongozo wa TANU, halafu tukafanya tathmini katika ulinzi na usalama na mazingira ya maendeleo ya nchi hii katika mwongozo wa Chama Cha Mapinduzi mwaka 1981.

Halafu baada ya hapo, nilitaka nitoe tathmini mwaka 2001 baada ya miaka 10, tukaona hakuna haja ya kufanya hivyo. Kwa sababu chama tawala kimeunda utaratibu mpya wa kuwa na vipindi nya miaka mitano mitano katika utaratibu wa Ilani na Uchaguzi ya mwaka 1990. Tathmini ya wananchi ya mwaka 1995 kuipa kura asilimia 75 chama kinachotawala tayari kimefanikiwa maana yake Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 1990. Mwaka 2000, tathmini iliyo fanywa ya wapiga kura kupata kura asilimia karibuni 37.9 ndiyo maana yake tumetekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 1995. Mwaka huu tumelamba dume, tumeenda kutekeleza kabla ya wakati. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, tathmini kwa kweli itakuwa Watanzania wanaona hakuna ya kuwafanyia tathmini. Kwa vile karibu mambo mengi yamejitokeza katika upande wa ulinzi na usalama wa nchi yetu na wanajeshi wetu wametulia. Mwaka 2002 nilitoa mfanano mmoja kwamba, mbuzi alikosa mkia kwa sababu ya kelele. Jeshi letu halina kelele. Wakati wakipanga foleni wanyama wapewe mkia na Mwenyezi Mungu, kutofautisha na binadamu, basi mbuzi alianza makelele kwenye foleni pale pale.

Mungu alipoulima kwamba je, hizo kelele nani anapiga, wakasema mbuzi mliyemleta, akatoa mkia wake mapema. Lakini wanyama walitulua kama kondoo, wale wanyama walitulua kama ng'ombe, simba, walitulua wakapata mikia mirefu. Jeshi letu na nchi yetu ikapata mikia mirefu kwa kutulia kwetu. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, kabla hujaingia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya 9, ibara ya 144, 147, inaingiliana huko juu na Wabunge wanazo na Watanzania waliokuwa nazo, nitanukuu, sitafanya kazi hii ya kunukuu. Someni ibara hizo mtaona, kwamba jeshi lililokuwa limeundwa na taratibu zake na haki zinazopewa na majukumu iliyopewa. Sasa mimi nasema kuna viongozi ambao wamepata *license* hizi. Nalisema kwa mujibu wa ibara ya 101 ya Katiba na itahojiwa huko nje ya Bunge.

Kuna baadhi ambao hawana madaraka hata katika Serikali, wanakuwa na madaraka kwenye Chama kimoja cha Upinzani na siyo *NGO*. Anakwenda nchi za nje anawadanganya Watanzania kwamba, amefuata kuhusu misaada ya umeme Marekani. Labda anasema umeme wenyewe hauna nguzo wala waya, basi hiyo radi. (*Kicheko/Makofi*)

Mimi nimesoma vitabu vyote, hakuna umeme ambao hauna waya kwa kweli. Labda kuna *Wireless Local Loop* wa simu, kweli inaweza ikafanya hivyo. Lakini umeme ambao hauna waya wala nguzo hiyo ni radi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ina mwelekeo tulivu, halafu kuna maelezo ambayo yametathminiwa lakini yamekuwa yanashika nafasi nzuri Kitaifa, ni Taifa lililokomaa ambalo halina utaratibu wa kujigamba. Mara nyingi watu wanajigamba kutokana na taratibu na mafanikio yale. Lakini viyi tunaamua kwamba, tutekeleze wajibu wetu. Hotuba yako imetoa michanganuo mbalimbali katika maeneo 13 kwa kueleza maeneo, mikakati, utekelezaji na uwajibikaji wa maeneo hayo. Lakini ningeomba Mheshimiwa Profesa Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuna mambo mengine ambayo yanakuponza ni mambo ya kuahidi mtu mmoja mmoja, kwamba kila kitu, huna *negative answer*.

Jifunze kusema mambo mengine *no!* Ndiyo maana unapata lawama mambo mengine. Ujifunze kusema *no!* Mtu anakuambia unaitwa, unasema hiyo nitaangalia. Kwa hiyo, kwa Waheshimiwa Wabunge tunachukua kama ahadi. (*Kicheko/Makofsi*)

Kwa hiyo, ndiyo maana wanapata matatizo mengi ya ahadi, maana zipo ahadi za Wizara. Wajifunze kusema hapana kwa mambo ambayo hayana mwellekeo. Mambo ambayo hayamo kwenye Bajeti, atasema hili halimo kwenye Bajeti, Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli tutalishughulikia hali itakapokuwa nzuri. Inaweza wakati mwingine ukipata *positive* unasifiwa. Lakini *positive* ambayo *negative* utapata matatizo. (*Kicheko*)

Hotuba ya Waziri imetoa mchanganuo mzuri tu kwamba, nchi inajilinda katika miongozo, inasema nchi na *gender* iwe sawa! Mtu anaweza akajilinda mwenyewe lakini lazima awapate wataalam kama wanajeshi wajifunze, walinde nchi. Kuna vitu vingine vinalindwa kama nanasi. Linalindwa kuanzia shina mpaka tunda, lakini linaliwa. (*Kicheko/Makofsi*)

Lazima umpate *watchman* alinde. Kuna mti unaolindwa kama mchungwa lakini unaibiwa. Sasa lazima kuwepo na *watchman* pale. Sasa wataalam lazima wawepo ambao wanajua mambo ya kulinda, ni wana jeshi ambao wanajifunza mbinu mbalimbali ya nchi na kujuvitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kuliongelea ni hili la ushirikiano wa majeshi yetu kikanda. Huu ni utaratibu mzuri. Nchi inapotulia lakini tusiwe na mikanda kama nchi kama jirani yao, lakini kuna jirani ukiwapenda tabia zao ni mbovu kwa kweli. Tutawapenda tukiamini kwamba, kuti kavu. Tutawapenda majirani ambao wanapenda ujjirani mwema. Lakini wale majirani ambao wana matatizo kwa sababu adui ye yeyote lazima ni adui tu, mpake rangi simba, mpake wanja machoni, mpake rangi vidoleni, lakini ukimkaribia lazima atakutafuna. (*Kicheko*)

Adui ni adui hata ukimlemba. Kwa hiyo, nchi ambazo zipo jirani tutawapenda kama wenzetu lakini wanapoleta chokochoko watapata majibu bila kuwasamehe, mpaka nchini kwao. Uwezo huo tunao na tumefanya hilo. Unavumilia mtu mpaka unachoka na kwa kweli tunasema masuala haya ya nchi chokochoko ambazo ni nchi zinataka kutugombanisha kati ya nchi na nchi. Mafanikio haya ni ya kwetu na asije mtu akadandia kusema kwamba, haya ni mafanikio ya mtu mmoja, hapana. Isiwe tabia ya kurumbizi. Kurumbizi ana tabia mbovu kweli kweli. Siku moja alikuta Mto Ruvu umefurika kama mafuriko, mbuyu ukaanguka ukawa unaelea, ye ye kapanda juu akasema, kumbe anakwenda na maji. (*Kicheko*)

Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inapeleka lile, maji ya Mto Ruvu yakapanda, ukaambwiwa utapanda mpaka wapi? Akasema mpaka baharini. Sasa wakamfuatilia wakamwambia atapelekwa yule baharini. Kuja Mto Ruvu pale kuna daraja likakwama tapu. Akasema hapa ni mapumziko chuchchu napumzika. Kumbe hana uwezo wa kulirudisha kule ndani. Sasa msidandie haya mafanikio yanayojitokeza, mtu akajitokeza akasema haya mafanikio ni ya kwetu. Ni ya Watanzania kwa ujumla na Sera Safi za Chama Tawala zimeyaweka mambo haya ndiyo maana utulivu na mshikamano unakuwepo. Ndiyo maana na hiyo Sera ya kusema kwamba, majeshi yasiingie katika chama chochote niliwaeleza wakati tulipokuwa tunapitisha mfumo wa Vyama Vingi, niliwaambia hata Mwenyezi Mungu alipoumba binadamu akamwambia kuna vitu vinane *delicate*, lazima vikae ndani. Kwa sababu vikikaa nje vikining'inia vitapata matatizo. Hivi *delicate* akaulizwa vitu gani, moyo ukae kwa ndani. Kibofu kikae ndani, utumbo, ini, vitu vingine hata kuna vingine *delicate* ukivigusa unatoa jicho. Ni jicho ambalo ni *delicate*. Sasa *delicate* akasema vitu *delicate* kwa *formula* ile ile ya kusema kwamba, viwekwe ndani, jicho lingewekwa ndani ya mapafu, lakini sasa litaonaje? Ni *delicate* lakini ni *sensitive*. (*Kicheko/Makofsi*)

Sasa kwa jicho ambalo ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania ukiliweka ndani ya *theatre* tu litaleta matatizo katika nchi. Hilo likae nje ya mwili ili liangalie, kuna kipindi ambacho linaweza likakaa ndani ni kwa kutuliza, kutengeneza wakati wa utulivu ndiyo hapo tukaleta kope, wakati wa kufunga, linafunga macho na kufumbua. (*Kicheko/Makofsi*)

Kwa hiyo, jeshi linakuwa nje ya vyama ili lidhihirike. Kwa hiyo, hizi ni dalili kwamba, kuna watu wa vyama fulani wanaingia kwenye jeshi, kwa kweli itakuwa vyama vile, jeshi likiwa na chama cha utawala sidhani kama watu wangeishi katika nchi hii.

Tuliweka jeshi nje kwa sababu ni jicho la nchi na pamoja niseme ni *sensitive*, ni *delicate* lakini ni *sensitive*. Kwa hiyo, mwisho napenda kupongeza yale mashirika ya Nyumbu, Suma, Maduka ya Kambini, ambayo yanaleta bidhaa nafuu ndani ya Kambi za Jeshi. Lakini pelekeni vifaa ambavyo wanavipenda. Msipeleke vifaa ambavyo vinakaa pale *idle*, vikikaa pale kama havitakiwi katika Kambi hiyo basi viondolewe ili walete vifaa ambavyo vinanunuliwa na wananchi.

Kwa mfano, vinakaa kwa muda mrefu pale Kambini ambavyo havitakiwi kuleta kama makarai, ma-wheel barrow, majembe, wanataka vifaa ambavyo ni vya bei nafuu vinavyotumika na familia. Lingine kuhusu wakati huu wa mshikamano ambaao ni wa hali ya utulivu wa nchi yetu ni kwamba, majeshi haya yatumike katika ujenzi wa nchi, katika sehemu ambazo zinazalisha mali, basi vyombo hivyo viongezewe mitaji ili kuongezea, kwa mfano, maeneo ya Meremeta, Nyumbu, Suma na Maduka basi yaongezewe ili yaendeshe uchumi katika kuzalisha katika kuziba pengo la maeneo ambayo Serikali imeshindwa kuyaendeleza.

Lingine ni magari ya mikopo ya majeshi. Kuna baadhi ya wanajeshi wanakatwa magari yale yaliyokopeshwa miaka mitano ya nyuma, lakini yale magari yamechakaa nadhani naweza kusema hayapo sasa hivi. Kwa vile vikosi vya kule kwangu vikosi nyeti, sitataja eneo, kwamba askari ambaao ni wa ngazi za chini wamekopa magari yale na bado hayafanyi kazi sasa hivi lakini bado wanakatwa mishahara. Tukifikiria kwa kweli hapo wangesamehewa hiyo mikopo kwa sababu magari yale ni *useless* sasa hivi.

Kwa hiyo, wayatumie kwa kazi zao zingine kwa ajili ya kazi za kusaidia familia kwa vikosi vile vingesaidia. Kuna majumba ya batii kwa batii, yamepitwa na wakati. Kuna baadhi ya wanajeshi wetu wanakaa kwenye mabati, *temperature* ya ya maeneo hayo kwa kweli wale watu wanaiva kweli. Mimi sijawahi kuona mwanajeshi mweupe. Lakini sasa hivi unawakuta weupe lakini kwa sababu ya *temperature* ile ya mle ndani. (*Kicheko/Makofi*)

Mimi nilikuta watu weusi kule Nigeria, mimi nilikuwa naitwa cheupe, ni Mtanzania mweupe mweupe. Wako Waibo na Wayoruba, sasa hivi Nigeria iko pamoja na Profesa Topowola, Profesa Aboyomi Satowola, Profesa Adebeji Adebayoi, wale niliokuwa nao pale, sasa utakuta wengine weupe si wa kawaida, pengine ni yale majumba ambayo tunasema ya mabati yale, yanaweza yakawa *temperature* inakuwa kali sana mle ndani.

Kwa hiyo, naomba tafadhali sana tumieni vikosi vile, ili watengeneze majengo ambayo ni ya afya kwa wananchi wale, maeneo kama ya vikosi nyeti kule, maeneo ya Jimbo langu ambayo najua Profesa Sarungi ulikuja kule, ulikuja timu yangu ya *Super Mkong'oto* ukakabidhi jezi pale ile timu juzi ilifungwa kwa tabu sana goli 9. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu wa amani, majeshi kama ya vikosi nyeti cha Uhandisi cha maeneo ya Jimbo langu wangesaadia katika kujenga barabara zile. Kwa kweli tunahitaji fedha kwa ajili ya barabara ya Mkulazi kwenda Kidunda, ulikuwa barabara ya kisiasa. Sasa hivi tumepata fedha kwa ajili ya barabara hiyo. Kwa hiyo, hii barabara ya kule kama Kidunda, Mkulazi, Chanyumbu na maeneo mengine ya Usungura ni ukombozi.

Kwa hiyo, jeshi lingepewa kule kutengeneza barabara. Sasa hivi tumeshaweka watu wanafyeka na Jumapili hii naenda kupeleka mwanajeshi kule Ngerengere na nitakwenda kuzungumza na majeshi pale Sanga Sanga, ninaongea saa hizi mnanisikia, Jumapili nitakuwa pale. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, nitakuwa ninasimamia barabara, mtengeneze wakati huu wa utulivu. Hivi kengele tayari? Bado!

Mwisho, jeshi letu linapenda kufanya kazi, siyo yule Binti Mfalme Mpenda Raha. Ni majeshi ambayo yanapenda kujituma na kufanya kazi. Binti Mfalme Mpenda Raha, aliudanganya ukoo fulani wa mfalme mwingine wa kiume mpaka akaolewa kwa kutumia utapeli. Lakini jeshi letu siyo mpenda raha. Ni watu ambaao wanajituma.

Binti Mfalme Mpenda Raha alikwenda kwenye nyumba moja akasema, eee! Binti Mfalme, kwa bahati nzuri alikuta mwanaume wa mfalme, mtoto wa mfalme naye akataka aoe mtoto wa mfalme. Akamwambia sawa. Tupige miziga ili umuo. Akasema hapana, mpaka tukufanyie majoribio. Ilibidi waweke choroko. Choroko mnazijua? Choroko kidogo tu, wakaweka kwenye kitanda au kwenye magodoro 12, wakamwambia alale kwenye chumba hicho, halafu wakamtandikia vizuri, lala humu. Kulala asubuhi ilibidi mfalme alikuwa amejiandaa kwa ajili ya harusi, ni kama mtihani atashinda. Kwenda chumbani akamkuta yule binti analia. Wakasema unalilia nini? Akasema, sikulala baba kitu kilikuwa kinanifinya. Kwa hiyo, wakasema sema kweli, huyu mtoto wa mfalme. Wakasema wewe choroko godoro 12 juu mpaka zikamfinya. Huyu anapenda raha kwa kweli. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, ikapigwa mizinga kule kwa Binti Mfalme na si kweli kwamba Binti Mfalme choroko ataifika kule juu kwa zile godoro 12, lakini aligundua ule mtihani. Kwa hiyo, alioa mwanamke feki. Kwa hiyo, jeshi letu siyo mpenda raha, ni jeshi ambalo lina msimamo, limeshikamana na raia wa Tanzania katika kuimarisha uchumi wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pili namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na uongozi wake wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Jeshi la Ulinzi ni kazi nyeti sana na inahitaji wanaoajiriwa wawe watu waaminifu, wa kweli na wawe na imani ya nchi yao. Vijana kama hao ndiyo watakaotufaa kwa wakati huu. Jeshi halajiriwi kutokana na chama, ikiwa mwanachama wa CCM, ikiwa mwanachama wa CUF wakati nidhamu yake ni nzuri, hakuna tatizo lolote, ajira anapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hujaajiriwa na wewe hivi leo unataka kupindua Vituo vya Polisi, kweli kijana kama huyu atatufaa kwamba tumwajiri katika jeshi na zana hana? Akipewa zana atafanya nini mtu kama huyo? Wanafika kuua mtu kama kuku kumchinja. (*Makofi*)

Jeshi hili halajiriwi kwa chama, lakini lazima vijana wetu tuwaangalie kama kweli wana imani ya nchi hii? Kweli watulivu? Kweli wana usalama? Hili lazima lipite, hatuvezi kuliepuka na hasa kwa Zanzibar. Zanzibar sisi hatukupata kwa kalamu nchi ile. (*Makofi*)

Wazee wetu wamepoteza roho zao, wamekufa, kwa hiyo, lazima tujitahidi tuhakikishe kwamba, tunadumisha mapinduzi ya Zanzibar. Naendelea kutokana na ajira. Najua kuna matatizo yanayojitokeza. Mara nyingi wakati zinatokea ajira za kijeshi hususan Zanzibar, wenzetu huku mnatupa matatizo, maana hata ile mvua huonyesha wingu, lakini kule mnatuleeta taarifa ghafla mnataka watoto na mnakuja kupima mara moja mnasema mnaharaka. Mimi nahesabia ule ni ujanja wa ajira kutukosesa nafasi Wazanzibar. (*Makofi*)

Mara nyingi kama wanatakiwa watu, basi ukija huku hawatimii watu wale, haya ni matatizo yaliyojitokeza. Uwepo wakati, tupewe muda tutafute vijana wetu, ili waje wapimwe kikamilifu, tuwe na uhakika kwamba, vijana wetu wamefanikiwa na kama wanapimwa UKIMWI tunasema na kule vyombo viko Zanzibar. Hatari iliyoko baada ya kuleta huku unasikia wengine hawafai, wanarejeshwa. Sasa hii inakuwa tatizo kubwa sana, wakati kule mnahakikisha vijana ambapo hawakutimia basi mnachukua wale Zanzibar. Tusije tukafanya jeshi hili likawa kama Burundi baina ya Watutsi na Wahutu, tusije tukafika hapo. (*Kicheko*)

Kwa sababu tuna sehemu zetu mbili, Zanzibar na Tanzania Bara, sasa isije kuwa jeshi hili tunajua kwamba *population* ya Tanzania Bara ni kubwa haiwezi kukiukwa. Lakini tusije kukosa vijana wetu wakaonyesha kwamba hafifu sana ikiwa jeshi letu limetawaliwa na wenzetu wa Tanzania Bara ikiwa sisi haki yetu inapotea. Suala hili ningalipenda lichukuliwe hatua kikamilifu. Hayo nayaeleza kwa sababu yanajitokeza. Utamkuta kijana amechukuliwa kule miezi mitatu, minne, huku yuko mara anarejeshwa. Sasa kule vyombo viro, mtoto ana tatizo, tupate nafasi tuingize mwininge. Lakini awe mtoto yule anatoka kule. Tunajua sasa hivi ajira ngumu. Tanzania Bara bila ajira matatizo. Tanzania Visiwani pia matatizo.

Lakini kama haki yetu lazima tuhakikishe hawa Wazanzibari arubamia siyo tunakuja kujaza huku, msiweke vijana wenu. Nafikiri ujumbe umefika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu safari za nje. Mara nyingi hizi la safari za nje zinakuja ghafla. Mnaleta taarifa kule tunataka vijana kwenda nje kwa masomo fulani awe na sifa fulani. Lakini mnashtukia kama mauti au mauti mtu huumwa kwanza. (*Kicheko*)

Wakileta taarifa kule Tanzania Visiwani, mnasema bila shaka nafasi hakuna wamechelewa, wasichelewe vipi na nyie mmepeleka taarifa ghafla. Sasa ndiyo yale ninayosema kwamba, mnatuletea matatizo na kule wako vijana, sifa zile wanazo. Hata kama huku mmechukua watatu japokuwa mmoja mchukueni kule na mhakikishe kwamba ni Mzanzibari. Hili jeshi tumeungana sote kwa pamoja. Sasa isionyeshe kwamba, sehemu moja tu ndiyo inayosonga mbele na ile sehemu nyingine hakuna. Hili nafikiri itakuwa ni dosari kubwa sana. Kwa hiyo, nategemea ujumbe huu viongozi mpo kule mbele na ninategemea kwamba mtafanikisha.

Hivi sasa tunachukua miaka sita ndipo mtu aweze kupata, lakini kupata *rank* inafikia kiwango sehemu zote amekwisha askari huyu kuzimaliza. Amekwenda kozi, mitihani amefanya *part one* na *part two* amemaliza. Lakini kama haijatimia ile miaka sita kwa kweli hawezi kupanda *rank*. Hili suala hebu nahisi kama limepitwa na wakati. Tunamhisni Askari yule anastahili na amefanikisha vizuri, basi tusiwe tunasubiri na ukaona kwamba, vijana wetu hawa kwa sababu jeshi wanastaifu vile vile kutokana na umri, sasa unakuta vijana wetu wengi wanakuwa bado wangali vijana lakini utaona kwamba, yuko nje. Sasa kama tutafanya kama hivi nilivyooleza kwamba, miaka sita mmingi basi tutawakuta bado vijana wetu wangali vijana wako jeshini na bado wana-trot na uwezo wanao.

Jambo lingine ni kuhusu ndugu zetu vile vile wanajeshi. Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa wakati umebadilika, sasa hivi kuna maradhi na sheria asioe mpaka itimie miaka sita. Hebu tuijulize kweli Askari anakula, anashiba, miaka sita na wakati huu tulionao atakaa kweli asile? (*Kicheko/Makofî*)

Hapa ndipo tunaposema kwamba, Askari wetu wanapata UKIMWI, sasa tutazame mambo gani yanasaababisha, lazima tuangalie kitu gani kinasababisha na njia gani tunaweza mambo haya kupekuna nayo kwa sababu aliyenacho si asiyenacho. Kama unaye basi kidogo matatizo yatakuwa hajjambo. Lakini kama kabisa hutakubali uwe peke yako, utataka uwe naye. Sasa hii italeta matatizo, sasa sheria hii imepitwa na wakati kutokana na hali ya maradhi yalivyo sasa. (*Makofî*)

Maana hapa Askari unamwambia moja kwa moja kwamba katafute. Kwa sababu pale watoto wanakwenda shababi, kijana amewiva, hawezi kustahimili. Tufanye utaratibu wa kuweza kustahimili miaka sita ni mmingi, muweze kuifupisha ili hawa watoto wapate kuoa na wawe na wenzao labda kidogo itastiri kutokana na matendo haya. Kwa sababu wakati ule itakuwa wanaokota okota tu. Kwa hiyo, utaona kwamba, maradhi haya yanaweza kuzidi itakuwa hakuna mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, hapa wamesimama vijana mara nyingi hutaka watoto wetu labda darasa la saba, darasa la kumi. Mimi nasema twendeni na wakati, pale wakati tunataka nchi tu, hata kule Zanzibar viongozi walikuwa hawakusoma. Kwa sababu lile jambo lilikuwa mwanzoni, lakini leo tumeishi miaka 40 bado tumchukue mtu wa darasa la saba na sisi kweli tunataka maendeleo, nahisi si mahali pake. Lazima tupate watoto waliokuwa *capable*, waliosoma, ndiyo watafanikisha. (*Makofî*)

Tusirudi nyuma, asiyeridhika na jamii yake kule, ndiyo tutazorota akaona labda ndipo mahali, hapana! Lazima tupate vijana waliosoma, huu ndiyo wakati. Mtoto akiwa *graduate*, mtoto akiwa ana *Masters*, lakini lazima tupate vijana waliosoma ndiyo tuweze kuwaajiri kufanikisha jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kutokana na jitihada zake wanazofanya. Kwa hiyo, bado tunaomba uwepo ushirikiano zaidi na haya tunayoyeleza tunataka yachukuliwe hatua kwa sababu mnatupa dhiki sisi tulio kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nasema naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

MHE. BEATUS R. MAGAYANE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hotuba ambayo kwa kweli ni nzuri, yenye mwelekeo na yenye kutia matumaini. Kabla sijasahau, naomba kusema kwamba, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilipongeze Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kutimiza miaka 40 ya kazi ambayo imetukuka. Niipongeze Serikali kwa kweli kwa kurudisha mafunzo ya JKT kwa sababu JKT ndiyo kiwanda cha kuweza kufunza Uzalendo na Utaifa. (*Makofi*)

Niungane na Amiri Jeshi Mkuu kwa yale aliyosema na kuagiza kwamba, wale watakaoajiriwa katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama watoke JKT. Huu ni mtazamo sahihi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Wanajeshi wote, Maafisa na Wapiganaji, kwa kazi nzuri ambayo mpaka hivi sasa wameifanya tangu tupate uhuru ya kulinda nchi na mipaka yake na kwa kweli kwa kutuletea amani na utulivu katika nchi yetu. Tunawatakia kila la kheri katika kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya jeshi wakati wa utulivu ni kufanya kazi za kiraia na wamefanya kazi nzuri sana hasa wakati wa maafa, tunawapongeza sana kwa yale waliyofanya. (*Makofi*)

Lakini kazi yao muhimu Mheshimiwa Naibu Spika, ni ile ya kulinda mipaka ya nchi yetu ili tusipate watu wa kuja kutacheza na kucheza amani yetu. Wameifanya kwa ufasaha na wametuhakikishia amani mipakani kwa kiwango kikubwa na kwa kweli wameiwezesha Serikali kuwa na uhalali wa kuendelea kutawala.

Maana yake Serikali kama haiwezi kuwashakikishia wananchi wake na mali zao usalama, watakuwa hawana uhalali wa kutawala. Jeshi letu linaihakikishia Serikali ya Chama cha Mapinduzi uhalali wa kuendelea kutawala, tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie suala la mpaka wetu na nchi jirani ya Burundi hususan kwetu sisi ambao tunatoka Mkoa wa Kigoma. Mheshimiwa Waziri, amesema kumekuwa na utulivu katika mpaka wa Tanzania na Burundi hasa kwa sababu mapigano sasa yako ndani ya Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ambao tuko katika maeneo hayo tumeshuhudia uvamizi wa mara nyingi sana wa Askari wa Burundi wakiingia katika Vijiji vya Tanzania. Tumeshuhudia uporaji mkubwa wa mali hasa mifugo ya Watanzania, tumeshuhudia mauaji ya baadhi ya raia na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, jana aliwataja watu saba na kwangu wako watu wawili. Mara nyingine tumeshuhudia hata utekaji nyara wa wananchi. Katika hali kama hii, inakuwa vigumu kusema kwamba, kuna utulivu. Bomu lilipigwa kutoka Burundi likapiga katika Kituo cha Polisi cha Mnanila na wananchi wakakimbia na Maaskari waliokuwepo hapo, hiyo huwezi kuiita ni hali ya utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanne wametekwa katika Kijiji cha Kibande na kupelekwa Burundi na mmoja akauawa, hiyo haiwezi kuitwa ni hali ya utulivu. Wananchi zaidi ya 26 katika Kijiji cha Rumashi wameporwa mifugo yao mara nyingi sana na Askari wa Burundi, huo huwezi kuuita kwamba ni utulivu. Imebidi tuwahamishe wananchi, familia zaidi ya 600 katika Kijiji cha Malenga ili kuwaondoa mpakani wasiendelee kuvamiwa na Maaskari wa Burundi na tukaiomba Serikali itusaidie walau shilingi milioni tano kwa ajili ya kuwa-resettle, bahati mbaya hatukupata. Juzi Jumapili, Maaskari wa Burundi wamekivamia Kijiji hicho hicho cha Malenga na watu wakarushiana risasi na wapiganaji wetu walikuwepo hapo na wananchi watatu wako mahututi, hiyo huwezi kuiita kwamba ni hali ya utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hapo tu ila kuna uvamizi katika Vijiji vya Bukiriro, Kasuga, Kabale, Kibande na hata Kitanga katika maeneo ya Kasulu. Tunapenda kuiomba kwa dhati kabisa Serikali na hasa Wizara hii kwa makusudi, iwhakikishie wananchi wanaoishi mipakani hali ya amani na utulivu ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Nimekuwa nikiuliza maswali hapa Bungeni na swali langu la kwanza nililoliuliza humu Bungeni lilikuwa ni juu ya uvamizi wa wanajeshi wa Burundi. Mara ya kwanza nikajibiwa kwamba, uvamizi huo haupo, nikamwambia Mheshimiwa Waziri, uvamizi huo upo kwa ushahidi. Mara ya pili nikaambiwa hatuwezi kudai fidia kwa sababu Burundi hakuna Serikali na juzi katika kikao hiki hiki

tukaambiwa hatuwezi kupata fidia kwa sababu hatuko vitani na Burundi. Kwa matukio haya sisi ambao tuko kule tunajiona tuko vitani kwa sababu hatukutulia. Sasa suala la kusema kwamba, tuko vitani au hatuko vitani, inawezekana kama nchi hatuko vitani, lakini wananchi wa maeneo yale wako vitani na Jeshi la Burundi. Ni vema Serikali ikalitambua hili na kwa kweli ikaweka kila msaada katika Vijiji hivyo vya mpakani ili wananchi waweze kuishi kwa amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua si rahisi kupata fidia ya mifugo ambayo imechukuliwa na pia si rahisi kupata fidia ya watu wetu waliouawa lakini ni vema Serikali ikatambua kwamba, kuna umuhimu wa kuongeza ulinzi na wanajeshi katika maeneo hayo ambayo mara nyangi yanavamiwa. Lakini ni vema pia Serikali ika-*register* Umoja wa Taifa kwamba, Serikali ya Burundi kwa makusudi imekuwa inavamia ardhi ya Tanzania na kuwaua watu wake. Tusipo-*register* tutakuwa tumewakosea haki wananchi hawa ambao wanaumia kila siku. Utakuwa ni Baba mbaya ambaye mtoto wa jirani kila siku anamkung'uta mwanao wewe unakuja kusema kwamba, mtoto hajapigwa, hata ule U-baba unakuwa huna uhalali nao tena. Sasa tusifikie mahali hapo Serikali hii ikawa na utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili ili Serikali iache kutoa majibu kama ya Yesu wa Nazareti. Unajua Yesu wa Nazareti alikuwa akiwakuta watu wanalia, anawaambia mnalilia nini? Huyo hakufa amelala. Sasa hii inakuwa si nzuri, inakuwa ni *mockeryn*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwamba, amewachagua wanajeshi kuwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa katika eneo la Kigoma. Dhana ni nzuri lakini kwa bahati mbaya hawa pamoja na kwamba wako kule kwenye *field* na ni wanajeshi, hawana *command* yoyote kwa wale wanajeshi ili wawaamrishe waweze kupiga. Mheshimiwa Waziri, labda angelitazama akashauriana na Amiri Jeshi Mkuu ili kuona ni namna gani yanawenza kukasimiwa haya madaraka ya kuamrisha pale pale kunapotokea mapigano ili tujibu mapigo pale pale yanapotokea. Kwa sababu mtu akipiga Malenga wakafa, mpaka kuja kupata kibali cha kujibu mapigo ni mpaka urudi Dar es Salaam, sasa watu wanakuwa wamekwishaumia na ile dhana nzima ya kuwaweka wanajeshi katika Mkoa wa Kigoma tena Makanali watupu inakuwa haina maana. Hilo ni la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tungelipenda kuiomba kabisa Serikali kwa dhati, itambue kwamba kwenda katika hivyo Vijiji vya mpakani ambapo tunashambuliwa kila siku na wanajeshi wa kutoka Burundi, barabara ni mbaya sana. Sasa tungependa kuiomba Serikali kwa makusudi kabisa, kwa ujumla wake kwamba, barabara za mpakani izione kwamba ni barabara za ulinzi na usalama wa nchi, zitengenezwe na Serikali Kuu badala ya kuiachia Halmashauri ya Wilaya ambayo haina uwezo wa kuzitengeneza hizi barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashukuru kwamba, tumeanzisha majadiliano na Serikali ya Burundi mpaka kwenye ngazi ya Tarafa. Lakini hawa watu hawasikii, ndiyo yale yanayozungumzwa ya jirani mbaya. Sasa mimi nafikiri wangepewa fundisho kidogo, wakachapwa. Ili kwa kuwa wanakataa kwamba si wanajeshi wao, wale tutakaowakamata basi tuweze kuwaonyesha kwenye vyombo vya habari vya Kimataifa kwamba, hawa walituvamia ndiyo maana tumewateka na tukawapiga na ikibidi tuwachape mpaka tujue mwisho wao ni wapi, kama mwisho ni Bujumbura basi tujue kwamba ni Bunjumbura wametoka huko. Lakini tukiwa tunanyamaza namna hii inaonekana kwamba Tanzania sasa ndiyo mchokozi wakati sisi ndio tunaochokozwa na ndio tunaoumia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda hautoshi, namwomba Mheshimiwa Waziri, ashauriane pia na Serikali Kuu kwa ujumla kwamba, Vijiji vya mpakani ni vema vikapewa mawasiliano ya uhakika hasa ya simu. Mtu anayetoka Nyabibuye kuja kutoa taarifa Kibondo inamchukua siku mbili kwa sababu hakuna usafiri. Lakini pia gharama yake ni Sh. 6,000/=, hivi ni mtu gani atakayejitolea kila siku kuwa analipa Sh. 6,000/= kwa sababu hatuna simu kwenye Tarafa na pia hatuna simu kwenye Vijiji ni mpaka ufile Makao Makuu ya Wilaya na ni kilomita 106 kutoka huko. Sasa ningependa kuiomba Serikali kwa ujumla wake, iangalie kwamba kuna haja ya kuimarishe ulinzi kwa ujumla katika Vijiji vya mpakani, kuongeza miundombinu na ku-*improve* na kuhakikisha kwamba, kuna mawasiliano ya uhakika ili wananchi wanaokaa mpakani nao waweze kufurahia amani ambayo Watanzania wengine wanafurahia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, napenda kusema tena kwamba, nawatakia kila la kheri Maafisa na Wapiganaji, Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nianzie kuchangia katika eneo hili la majukumu ambayo Wizara inakusudia kuyatekeleza katika kipindi kinachokuja. Pia napenda nizungumzie vile vile hili eneo la pili ambalo Wizara imekusudia kuendelea kuwaandaa vijana wa Taifa hili la Tanzania ili wawe raia wema watakaosimamia umoja, Utaifa na watakaokuwa na silika ya kufanya kazi za mikono na kujitegemea kwa kuwapatia mafunzo ya Uzalendo, ukakamavu, ulinzi, ufundi stadi na uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimependa kuanzia hilo nikiwa ninakusudia kuzipeleka salama zangu za shukrani sana na pongezi kwa Mheshimiwa Amiri Jeshi Mkuu, mpendwa Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa jinsi ambavyo ye ye mwenyewe kwa kauli yake wakati akizindua sherehe za miaka 40, alitoa kauli kwamba, "Jeshi la Kujenga Taifa litadumishwa kwa sababu ni kwa faida ya vijana wetu wa leo na ni kwa faida vile vile ya vizazi vijavyo". (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi tulifurahia sana tuliposikia JKT imekubaliwa kurejeshwa katika mwaka 2001, nina hakika matunda yake tumeweza kuyaona, kwa jinsi ambavyo baada ya vijana hawa kuhitimu vyombo vingi sana vya ulinzi viliwakimbilia kwa mfano Jeshi la Wananchi, *TANAPA*, Polisi na hata Magereza, kwa sababu wanaukiri umahiri wao ambao wameupata baada ya mafunzo yao katika Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofî*)

Ukiangalia hili nimeona kwamba, vile vile Watanzania walikuwa na kiu kubwa sana ya chombo gani ambacho kingweza kikawaunganisha Watanzania wote bila kujali misingi ya kisiasa, bila kujali misingi ya ukabila, bila kujali misingi ya rangi, udini, jinsia ama tofauti ya namna yoyote ile. Kwa upande wa vijana na hata kwa Watanzania tumekiunga mkono chombo hiki ambacho ni cha Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uthibitisho huu tunaupata katika takwimu pale kwenye ukurasa wa 29 mpaka ukurasa wa 30. Unakuta takwimu zake zinaonyesha kwamba, tangu JKT ilipoanza jumla ya vijana 770,000 walijitokeza kuwania nafasi hii. Lakini kutokana na ufinyu wa nafasi tulizokuwa nazo na Bajeti tuliyonayo na kwa sababu ni mwanzo ni vijana 5088 tu ndio walioweza kupata nafasi ya kuijunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa msingi huo, bado kiu ya vijana hawa na Watanzania kuona kwamba, wanawenza kuijunga katika Jeshi la Kujenga Taifa ni kubwa mno. Kwa msingi huo ninashauri suala zima la kutoa masomo ya ulinzi wa Taifa na usalama vile vile yaende yakazingatie masuala yanayohusu ujenzi, kilimo na miundombini mbalimbali itakayowawezesha vijana hawa ambao hawataweza kupata nafasi kwenye vyombo hivi vya ulinzi na usalama, waweze kwenda kuwa ni vijana bora na raia bora kwa kuweza kuanzisha vikundi mbalimbali vitakavyoweza kujitegemea na ambapo itakuwa ni mahali pazuri pa Serikali kuweza hata kutoa mikopo kwa sababu watakuwa wanawafahamu vijana hawa ni vijana ambao wamefundishwa nidhamu, utiifu, Uzalendo na pia wamefundishwa kufanya kazi kwa muda mrefu sana bila kulalamika na wakiwa kazini wanaifanya kwa ukamilifu kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, vijana wanaopita katika Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Wananchi, ni vijana ambao wanakuwa na nidhamu kubwa sana. Hata katika taaluma ya kazi pale inapotokea akapata nafasi ya kazi ama akarudi katika maisha ya uraia, anakuwa ni kijana mwema, ni kijana mwenye nidhamu na kazi anaitenda bila kuwa na manung'uniko wala matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo ni vizuri kabisa mimi kwa ushauri ambao ninao, kwamba katika Taifa hili ambalo ni Taifa la Vyama Vingi, Taifa ambalo lisipoangaliwa vizuri Vyama

Vingi vinaelekea kupenda kuleta mgawanyiko na mtafaruku, ni vizuri kabisa tukarejea katika mfumo wetu ule wa kila anayekwenda kulitumikia Taifa kwa utaalam wowote ule ama wa Ualimu, Uduktari, Uhndisi na wa namna nyingine yoyote ile, basi tukarejea walau wakapata hata miezi mitatu ya kwenda katika Jeshi la Kujenga Taifa ili kuweza kumuweka mtu moyo wa Uzalendo, moyo wa kulitumikia Taifa na moyo wa kutoa huduma bila kutanguliza au kupata chochote, bila kutanguliza kujipenda yeze mwenyewe, akawa ni kijana ama Mtanzania aliyejenga mazingira ya kupenda kuwatumikia wenzake bila kuwaliza wenzangu mmenipa nini, bali apende kuulizwa kwamba yeze ametoa nini kwa wale ambao wamekwenda kupata huduma yake. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Makutopora. Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakitupatia nafasi sisi Wabunge ya mafunzo mafupi katika kipindi cha Bajeti, tunaweza kwenda pale kujifunza kulenga shabaha za kupiga bunduki za namna mbalimbali, kitu ambacho kinatuwezesha na sisi kujikumbusha enzi zetu ama zile za *National Service* ama zile ambazo na sisi tulikuwa tunaweza kuva kama wao vijana wa siku hizi wa JKT, basi yale mazingira tunayapenda sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi tunapata nafasi ya kutembelea mazingira walipo vijana wetu kuona wanafanya kazi gani. Naomba nitumie nafasi hii kuipongeza kazi nzuri inayofanyika katika Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa cha Makutopora na kazi nzuri ya kuwaelimisha vijana. Kuna kazi nzuri ya bustani na kutokana na bustani wameweza kununua mpaka hata malori ya Isuzu makubwa kabisa kwa shilingi milioni 25, kwa pesa ya bustani tu. Ni suala ambalo linastahili kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile niombe kwamba, kufanyike utaratibu wa kuongeza idadi ya vijana wanaokwenda JKT. Idadi hii wakati inapokwenda kuongezwa iangalie idadi ya vijana wengi wanaotamani kwenda kule Jeshini, si pekee kwa suala la kutamani ajira. Wengi sana huwa wanaogopa JKT hata ambao walikuwa wanakwenda kwa Mujibu wa Sheria, walikuwa wanatafuta kila sababu wasiweze kwenda lakini naona kwamba, moyo wa Uzalendo chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi unavyozidi kujengeka, vijana wetu wanatamani sana kwenda kulitumikia Taifa kuliko kubaki hawana shughuli ya kufanya. Lakini ninachoshauri ni kwamba, ninaomba na idadi ya vijana wa kike iongezwe. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama katika mabweni mengi yaliyoko katika Jeshi la Kujenga Taifa la Makutopora utakuta mabweni ya vijana wa kike ni machache, kwa hiyo, inashiria kwamba, hata idadi yao vile vile ni ndogo. Nilikuwa naomba nishauri kwamba, kwa sababu akina mama wameonyesha uwezo mkubwa sana katika kazi mbalimbali naamini hata kazi hii pia wanaiweza. Nafasi zao ziweke ulingano unaweza kuwapa nafasi ya kuweza na wenyewe kuonyesha umahiri na ujuzi wao. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie katika eneo la pili. Pia napenda nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Jeshi letu la Ulinzi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa jinsi linavyofanya ulinzi mahiri wa nchi yetu. Katika Ibara ya tatu, ukurasa wa pili, Wizara inaendelea vile vile kututhibitishia kwamba, moja ya shughuli zake za msingi ni kwamba, Wizara inadhibiti ulinzi wa mipaka ya nchi yetu dhidi ya uvamizi wa maadui kutoka nje ili Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iendelee kuwa na amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pasipo na amani na utulivu hakuna chochote kinachoweza kufanyika. Kwa msingi huo ni kwamba, Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana. Ninapenda kuungana moja kwa moja na wale ambao wameeleza ya kwamba, Jeshi letu linafanya kazi kubwa sana. Lakini pia ni Jeshi ambalo halina kelele na hakika halijui hata kung'ang'ania, kudai vitu ambavyo wakati mwininge ni stahili yao lakini hawana *style* ya kudai haki zao kwa kupiga kelele, bali wanatumia msingi wa nguvu ya hoja. Napenda kuwapongeza sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wamekuwa maarufu kwa jina la vijana wa kazi. Ni kwa sababu pale wanapotokea kufanya kazi wanayopewa, wanaifanya kwa moyo bila kudai kwanza wapate nini na wako tayari saa 24 kufanya kazi bila matatizo ya namna yoyote. Ninapenda kuwapongeza sana kwa hali hii ambayo wameonyesha na ninazidi kuwaomba waendelee kuwa na moyo huu chini ya viongozi wao walionao. Ninawapongeza sana na kuwatakia mafanikio makubwa, huko mbele wazidi kujengwa matumaini

ya Taifa letu, amani na utulivu ndiyo hazina ya Taifa letu na bado tunapenda iendelee kuwepo kwa sababu ndiyo msingi wa kila jambo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niwapongeze vijana wa kazi kwa jinsi walivyofanya kazi ya kupambana na majambazi katika Mkoo wa Kagera walipounda hii *Operation KAMAKA*, Kamata Majambazi Kagera. Kazi hii ilifanyika kwa umakinwa hali ya juu sana na mimi nashukuru sana jinsi ilivyonisaidia kuwaondoa majambazi, yalikuwa yanawasumbua sana wananchi katika Jimbo langu katika Kata ya Ngenge, Kijiji cha Rutoro, Kyobuheke na Kyarutare ambavyo vilikuwa vimevamiwa na majambazi na wananchi walikuwa hawawezi kufanya kazi yoyote. Kwa sasa hivi hali ni shuwari na wananchi wanafurahi sana, kazi hii ilifanywa na vijana hawa wa kazi. Ninapenda kuwapongeza sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nilizungumzie hili suala la Jeshi la Wananchi Kaboya maarufu kwa 21KJ. Tulipopata uvamizi wa Idd Amin, tuliwapoteza vijana wetu nasi tulikiri kwamba vijana waliorudi walirudi kishujaa na wale waliokufa walikufa kishujaa. Ukiwa unapita pale kwa wale wenyeji mazingira ya pale Kaboya hayajakaa vizuri kuonyesha kwamba pale ni mahali tulipoweka bustani ya vijana waliokufa kishujaa. Ninapendekeza kwamba, Zahanati ya Kambi ya Kaboya kwanza ijengwe baada ya Zahanati iliyokuwepo kupigwa mabomu tangu kipindi kile cha vita. Sasa hivi huduma inatolewa katika nyumba za watumishi pale pale Kikosini, kuna jumla ya vitanda sita mpaka nane kwa kulazimisha ili kuweza kuwalaza wagonjwa kama ni dharura, wanaye Mganga mmoja wa Kikosi na Nesi mmoja. Wakati Zahanati hii inategemewa na wananchi wa Vijiji kumi, Kata ya Mayondwe, Kata ya Muhutwe na Kata ya Izigo. Kwa msingi huo, unakuta kwamba, huduma ile inayotolewa pale inakuwa ni kama huduma ya kwanza tu lakini huduma yao ni nzuri na inapendwa lakini haiwezi kukidhi haja. Ninashauri suala hili liangaliwe ili waongezwe wataalam, madawa kwa ajili ya huduma pale na vifaa vya kufanyia kazi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile mahali hapo kuna hii barabara ya kutoka Ntungamo - Kantinya inayokatisha katikati ya kikosi kile. Barabara ile inapita karibu kabisa na hii bustani ya mashujaa. Ninaomba barabara hii Wizara ione uwezekano wa kuiwekea lami. Tusiendelee kuwa tunawawekea pale vumbi, tunapita kwa kasi isiyokuwa ya kawaida na utaratibu usiokuwa wa kawaida mbele ya vijana wetu waliokufa kishujaa. Barabara ile ninaomba iangaliwe na iweze kuwa ni ya lami na pale kwenye lile eneo kuwekwe eneo la kutoa heshima ili kila anayepita pale ajue kwamba anapita mbele ya vijana ambaa walikufa kishujaa na hakika tunaendelea kuwaenzi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia na suala la kuelezea kiasi walichotengewa Wizara hii. Mimi napenda kusema kwamba, kwa haya niliyotangulia kuyaelezea ,hoja ya JKT na Jeshi la Wananchi, mimi naridhika kabisa kusema kwamba, pesa hizi ni kidogo sana. Kwa msingi huo ninapendekeza Bajeti ijayo Wizara ya Fedha, ione uwezekano wa kuwaongezea fedha hizi ili waweze kumudu kazi kubwa wanayopambana nayo na iliyoko mbele yao na ambayo ni ya manufaa makubwa sana kwetu, bila wao sisi hatuwezi kupata amani. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, ninapenda kurudia kusema kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofsi*)

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa nafasi hii ya mwisho katika kuchangia hotuba ya Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Wawi, wakiwemo Wapiganaji wa Kikosi cha 151KJ na 141KJ, napenda kutoa shukrani zangu za dhati na pongezi kubwa kwa Amiri Jeshi Mkoo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake usiroyumbishwa kuhusu suala zima la ulinzi wa nchi yetu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, kwa kazi yake nzuri ya kuiongoza Wizara hii akishirikiana na viongozi wenzake, Katibu Mkoo wa Wizara, Bwana Vincent F. Mrisho, Mkoo wa Majeshi ya Ulinzi, Jeneral George M. Waitara, Mnadhimu Mkoo wa Jeshi, Luteni Jeneral Iddi S. Gahhu, Mkoo wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Davis Mwamunyange, Mkoo wa Jeshi Zanzibar na Ma-CO wote wa Vikosi

vyote vya Tanzania, pamoja na Makamanda na Wapiganaji wote, kwa ushirikiano wao katika kufanya kazi ya ulinzi kwa nidhamu kubwa sana na pia kwa ushirikiano wao kwa raia. Naomba waendelee na nidhamu hiyo hiyo kwa sababu Watanzania wote tunawategemea sana katika ulinzi wa Taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pongezi za pekee ziwaendee Jeshi la Kujenga Taifa Makutopora, kwa kazi zao nzuri katika utendaji wao wa kila siku wa kuwafundisha vijana wetu maadili mema ya ulinzi wa nchi yao na vile vile kutufundisha sisi Waheshimiwa Wabunge, upigaji wa shabaha na ukakamavu mkubwa.

Nina ushahidi kamili kwa sababu hivi karibuni tu katika kipindi hiki Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tunaenda kule kupiga shabaha mimi nikiwa mmojawa. Vijana wale kwa kweli huwezi kuamini, hajjawahi kutokea, ni wazuri, wanafanya kazi vizuri, wanatufundisha vizuri upigaji wa shabaha na wengi wetu tulishinda katika kupiga shahaba. Kwa hiyo, nawapongeza sana na waendelee na kazi hiyo hiyo katika kuelimisha vijana na sisi Waheshimiwa Wabunge. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nisije kusahau, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii katika maeneo yafuatayo. Eneo la kwanza ambalo mwaka wa kwanza, wa pili na huu mwaka wa tatu, nalizungumza ni kuhusu ujenzi wa nyumba za Askari na Mheshimiwa Sarungi ananisikiliza, lazima tutambue umuhimu wa Maaskari na Maafisa wetu. Ingawa tunasema Bajeti ni ndogo iongozwe ili wapiganaji wetu wajengewe nyumba za kukaa kwa sababu wanaishi maisha duni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utamkuta Afisa mzima wa Jeshi, achilia mbali Askari mdogo, anakaa uraiani kwenye nyumba ya kukodi! Zile pesa zinazolipa nyumba ile ni nyingi zaidi kuliko ambazo wangejengewa nyumba ya vyumba japo viwili na watakodiwa nyumba mpaka lini? Hasa kule kwangu Jimbo la Wawi, Askari na Maafisa wengi wanakaa uraiani, ni hatari.

MBUNGE FULANI: Sana.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Kwa maisha ya leo, Maafisa kukaa nje ya kambi ni hatari. Likitokea jambo atatafutwa saa ngapi? Kama jambo lenyewe lipo katikati ataenda vipi kule kambini?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaambia hawa wapiganaji wa kule Jimboni kwangu waelewe kwamba, kila siku nawatetea lakini mpaka leo bado Waziri hatekelezi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri, kilio changu ukisikilize, Askari wetu wana hali mbaya, wanakaa nyumba za toka hata hatujazaliwa, za toka Ukoloni, zinatakiwa zifanyiwe ukarabati. Maafisa wengine wanakaa mbali na kambini, kwa kweli ni hatari, naomba sana nyumba za Askari zitiliwe maanani. (*Makofî*)

Suala lingine ni tatizo la mipaka kwa sababu hata katika hotuba hii limo. Katika Jimbo langu la Wawi kama tunavyoolewa kuna zile kambi karibu na raia. Kuna sehemu kubwa sana ambapo Wizara ilito fedha kununua sehemu ile lakini sasa yanakuja maneno, maneno, kwa kweli sio mazuri yatauharibia hata katika siasa. Wanasema raia wamechukuliwa sehemu zao, Askari pale wanasema aah sehemu hii ni ya kwetu. Kwa hiyo, suala hili Mheshimiwa Waziri, kama limeshakufikia naomba ulishughulikie yizuri ili hali kule isiharibike ili tujue haki hii iko kwenye Jeshi au wananchi kwa sababu tunashirikiana isije kutokea matatizo ya kugombania ardhi kwa sababu hivi sasa tunaishi kwa uzuri na usalama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia sehemu ya kupambana na umaskini Jeshini. Katika Majeshi au vikosi vingi vya Majeshi, Askari huwa wanajishughulisha na biashara mbalimbali ama kilimo chao binafsi kama ukulima wa mbogamboga au ufugaji. Katika Kambi za Wawi, Maaskari wengi na familia zao ndio wanaolisha Chake Chake nzima kwa mbogamboga kwa kweli nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi karibuni limetokea tatizo fulani wamekatazwa kulima wakaambibi aah mnaharibu mazingira. Kwa sababu eneo lenyewe ndio hilo ninalozungumzia wameshapata lakini limekaa hivi hivi, kwa hiyo, hawawezi kujua kama eneo hilo ni lao au si lao. Naomba Askari hawa waruhusiwe kujilimia mbogamboga na kufuga katika yale yale maeneo yao ili wajipatitie riziki kwa sababu mshahara hata wafanye nini hautoshi na wao wana familia kubwa. Hizi fedha ambazo wanazipata kutokana na kulima mbogamboga na ufugaji zinawasaidia. Naomba sana suala hili Mheshimiwa Waziri alifuatilie na awape ruhusa walime himo mbogamboga, waendelee kutulisha na wao kujipatitie mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiondoka hapo naenda moja kwa moja kwenye suala la kuwekewa duka la vifaa nya ujenzi Jeshini, hili ni suala nyeti sana. Sasa hivi Mwanajeshi hana nyumba ya kukaa kesho kutwa atakapostaafu hana nyumba lakini Jeshi *okay* linalimpaa, ni vizuri kile kitu kiwepo pale Jeshini, wawekewe duka maalum la kuchukua vifaa kama vile saruji, mabati, nondo, ili waweze kujenga na Maafisa wawe wanawafuatilia wasiachiwe tu. Kama alivyozungumza mwenzangu asubuhi wameshachukua saruji wanakwenda kuiiza lakini wakisimamiwa wataweza kujenga nyumba zao baada ya kustaafuli watakuwa na sehemu ya kukaa. Mheshimiwa Waziri, naomba ulichukue suala hili kwa sababu hii ni mara ya tatu nalizungumzia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuchangia kuhusu mafao ya Askari. Askari anaweza kufanya kazi miaka yote lakini kazi ipo hapo anapostaafu au kazi inatokea pale Askari huyo anapopata maafa pengine ya kifo. Nina ushahidi kamili katika kile Kikosi cha 151KJ na 14KJ, kuna Askari ambaye amekufa mwaka 2001, mke wake akafuatia mwaka 2003 na hawa wameacha watoto wa nne na huyo mtoto wa mwisho sasa hivi yuko mahututi, sijui ni maradhi gani, sipendi kusema hapa lakini kwa kweli wamekufa na mpaka sasa hivi maslahi yao hawajapata mpaka wakaja kwangu mimi kunilalamikia.

Kwa hiyo, suala hili naomba Mheshimiwa Waziri, ulifuatilie sio kwa kule Wawi tu, bali kwa Tanzania nzima, Askari wanapata tabu wakifika na matatizo kama hayo, familia zinapata tabu, tuisiwapende Maaskari wakiwa na uwezo tu wa kufanya kazi wakifa au wakipata matatizo au wakistaafu tunawadharua, tuwapende kama wanavyoipenda nchi yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu mishahara ya Maaskari. Kama alivyozungumza mwenzangu hapa ni kwamba, Bajeti hii tunasema ni kubwa lakini mimi nasema ni ndogo kwa sababu Wanajeshi wana kazi kubwa sana ya kulinda nchi hii. Kwa hiyo na wale vile vile wanapenda wakifanya kazi na wao watunzwe, wapewe mishahara mizuri. Kwa hiyo, naomba kila mwaka kama inawezekana kwenye Bajeti mishahara iongezwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu Hospitali ya Jeshi 14 KJ, Hospitali ile ina Madaktari wazuri sana lakini hii ni mara ya tatu nasema haifanyiwi ukarabati, haiboreshwii. Naomba Hospitali ile kwanza ipatiwe madawa. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, nikiondoka hapa Bungeni huwa ananisaidia kipeleka madawa lakini naomba wapelekewe mgao *special*. Pia naomba ifanyiwe ukarabati halafu iwekwe jokofu kwa sababu Maaskari wanatokea sehemu mbalimbali wanapopata maafa ya kufa wanapelekwa Hospitali nyingine ya mbali ambayo pengine umeme sio wa uhakika, lakini wakipatiwa jokofu na jenereta, basi hata akifa anaweza kuwekwa hata wiki nzima akasafirishwa. Kwa hiyo, naomba sana Hospitali hii 14 KJ itazamwe kwa jicho la huruma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuzipongeza timu za mpira za Jeshi *Hard Rock* na Kipanga kwa sababu hizi Mheshimiwa Waziri mwenyewe alizisifia ziko katika *premium*. Lakini Maaskari hawa walioko katika *football* hawajui hatma yao. Ni Maaskari lakini huoni hata kuongezwa vyeo, wanaongezwa vyeo wengine lakini wao hawaongezwi na wao waongezwe vyeo kwa sababu ya kazi yao, kwa sababu ya muda wao mwingi wanaopoteza kutokana na kulisiaidia Jeshi katika masuala ya michezo. Naomba sana timu hizi zisaidiwe na vile vile wanamichezo watazamwe vizuri, wasaidiwe kwa kila hali, wasidharauliwe kwa sababu aah wao ni wanamichezo, wao pia ni Askari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini safari hii Mheshimiwa Waziri, atahurumia vikosi vile vya 14 KJ na 151KJ atamfuata Waziri mwenzake wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi alivyowajengea

nyumba Askari wake katika Jimbo la Wawi. Kwa hiyo, mwaka 2004 aweke kwenye Bajeti ili awajengee nyumba Askari wake wa 14 KJ na 151 KJ. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja.
(*Makofî*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. TALALA B. MBISE: Mheshimiwa Naibu Spika, *military science* imechangia kwa kiasi kikubwa kwenye maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa upana wake, ikiwa ni pamoja na sayansi ya jamii na uchumi. Kwa mfano, chanzo cha dhana *Strategic Management, Strategic Partners.* Neno *strategy* limetokana na dhana za kivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa utafiti (*Research*) kwenye Jeshi hauna haja ya msisitizo. Ili kuendeleza *research* kwenye Jeshi letu, elimu ya juu na *specialized education* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wanajeshi waliobahatika kupata elimu ya juu sana. Wengine walipata elimu kwenye maeneo *specialized* na adimu Tanzania. Kuna mifano hai, bahati mbaya hawa hawajatumika ipasavyo, wengine wamewekwa kwenye maeneo ya kazi ambayo yana uhusiano mdogo sana na *professional* ya Jeshi. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wale wote wenye *specialized education* na elimu ya juu wanatumika ipasavyo kwa manufaa ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza yafuatayo: Utafiti kwenye Jeshi uimarishwe kwa kupatiwa Bajeti ya kutosha kwa elimu ya juu na kutafuta jinsi ya kuwatumia walio na *specialized education* na utafiti upanuliwe ku-include *economic intelligence*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Philemon Sarungi na timu yake na Wizara nzima, kwa kazi nyeti na inayofanyika vizuri na kwa ufanisi wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu tatizo la vijana wa Vijijini kujiunga na Jeshi. Vijana wa Vijijini hasa wa wafugaji hawana vyeti vyaa kuzaliwa kutopteka na mazingira yao. Mara nyingi habari/taarifa za nafasi za ajira zitokeapo Jeshini haziwafikii kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira kama haya, vijana hawa wenye sifa za kujiunga Jeshini waruhusiwe kujiunga na Jeshi kwa wao kuapa kwa njia za *affidavit* na viapo hivyo kuthibitishwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili limewanufaisha vijana wanaokuwa katika Makao Makuu ya Wilaya na Mijini (wengine ni wale wanaoitwa watoto wa kijiveni), wakati vijana *unpolluted* wa Vijijini huachwa kwa kukosa vyeti vyaa kuzaliwa. Athari nyingine ni kwamba, vijana watakaopata nafasi Jeshini ni wale tu ambaa wazazi wao ni watumishi na wafanyabiashara wa Mijini.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara hii kununua *helicopter* zaidi ili ziweze kutoa huduma zaidi katika uokozi. Mapema mwaka huu ilitokea ajali ya boti iliyokuwa inatoka Tanga kwenda Pemba, ambapo Watanzania 36 walikufa maji. Kama kungekuwa na *helicopter* za kutosha za Jeshi, Watanzania hawa wangeweza kuokolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado hospitali zetu za Serikali kule Pemba zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa madawa iko haja kubwa kwa hospitali za Jeshi kuongezwa madawa ili Wananchi wengi zaidi waweze kupata huduma katika hospitali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kijana wangu ambaye alikuwa mwanjeshi, kwa bahati mbaya amepata ugonjwa wa muda mrefu na hadi sasa yuko kitandani karibu miaka miwili na nusu na Jeshi

halijachukua hatua yoyote ya kumsaidia huyu kijana! Naomba Mheshimiwa Waziri, ashughulikie suala hili ili huyu kijana aweze kupata msaada kutoka Jeshini. Kijana mwenyewe anaitwa Said Abdallah Bakar, ambaye ni mkazi wa Ziwanji, Chake Chake Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa upande wa Jeshi iangalie sifa na uwezo wa mwombaji na si kwa Itikadi ya Chama fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la UKIMWI limekuwa ni tatizo sugu katika nchi yetu. Naishauri Wizara kuchukua hatua za dharura katika kukabiliana na ugonjwa huu hatari. Pia, naishauri Wizara ifanyi utaratibu wa kuwapima Wanajeshi wote kila mwezi ili kuwa na hakika ya Wanajeshi walio safi.

MHE. GEORGE F. MLAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mkuu wa Majeshi na Makamanda wote kwa kazi yenye viwango vya juu vya ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu mdogo kwanza, ningependa kutoa ushauri kuhusu usafiri na usafirishaji Jeshini. Ninapongeza mpango wa kulinunulia Jeshi la Wananchi wa Tanzania ndege mbili kubwa za usafirishaji. Pamoja na hayo, ili kukabili vema majukumu ya dharura na maafa ni vema sana kuwa na *helicopter* kubwa zinazoweza kusafirisha Askari na vifaa na kutua hata kwenye maeneo yasiyokuwa na viwanja vya ndege. Vile vile, kwa hali ya leo tunahitaji pia *helicopter* za kivita, *Helicopter Gunship*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo naomba nichangie kwa ushauri ni juu ya shughuli za ulinzi wa umma (Mgambo). Maafisa wa Jeshi na Askari amba wanakuwa wamestaifu wanabaki katika Jeshi la akiba (*Reserve Army*). Lakini kwa kawaida, Maafisa na Askari hawa hawatumiki ipasavyo wakiwa wanaishi mitaani na Vijijini katika ushiriki au kushauri juu ya ulinzi wa umma. Siku hizi hali ya usalama wa raia imezidi kuwa mbaya sana. Majambazi amba ni *trained* katika matumizi ya silaha wanazidi kuongezeka. Vile vile, silaha za kivita kutoka nchi jirani zinazidi kuingizwa mitaani na Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri sana ya Jeshi la Polisi, hali inaonyesha wazi kuwa kazi ya ziada inahitajika sana. Hawa Maafisa na Askari Wastaifu wanaweza kusaidia kwa namna moja au nyingine katika kudumisha usalama kwa raia. Kwa mfano, Maafisa wa ngazi za juu wawe wanaalikwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa na Wilaya, wao wakiwa wamestaifu na kuishi katika Mikoa au Wilaya hiyo. Hawa Maafisa wa ngazi za juu amba wamestaifu wanaweza kutoa ushauri muhimu katika kubuni mbinu za kupambana na majambazi walio na ujuzi wa mapambano ya kivita na pia walio na silaha kubwa. Kwa upande wa mfumo wa ulinzi wa umma mitaani na Vijijini Maafisa wastaifu wa ngazi za chini na wale amba walikuwa *Non-Commissioned Officers* ni vema wawe Viongozi wa Askari Mgambo au washauri. Hata iweje ni muhimu sana Maafisa wa Jeshi Wastaifu na Askari Wastaifu, wawe *very actively involved* katika kudumisha usalama wa raia katika maeneo wanayoishi.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri na mandalizi ya hotuba nzuri ya Bajeti ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za pekee kwa jitihada za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mkakati na utekelezaji wa ujenzi wa nyumba kwa ajili ya wapiganaji wetu kwa mwaka 2002/2003 na mpango wa kuendeleza jitihada hizo kwa mwaka huu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili za Jeshi imara ni pamoja na kuwa na uwezo na vifaa vya kisasa. Dalili hizi zipo wazi katika mpango wa Wizara hii katika mikakati yake ya miaka iliyopita na katika mwaka huu wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, Jeshi linawajibika kuboresha mahusiano mazuri na jamii inayowazunguka na hasa katika maeneo yanayopakana na kambi za wapiganaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001/2002, nilimwandikia barua Mheshimiwa Waziri juu ya kuwepo dalili za mgogoro wa eneo la ardhi kati ya Jeshi na Shule ya Sekondari ya Wananchi ya Songa, Kata ya Songa, Jimbo na Wilaya ya Muheza. Jeshi limewahi kudai kwamba, eneo hilo ni mali yake na kwamba Wananchi wamewaingilia. Kauli na hisia hizo ni vizuri zikapatiwa ufumbuzi ili kuepusha migogoro inayoweza kuwafanya Wananchi kupoteza nguvu na fedha zao katika kuendelea na ujenzi wa Shule hiyo ambayo inalenga kutoa huduma kwa watoto wakiwemo pia watoto wa wapiganaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mbunge kuomba msaada wa Jeshi kama jirani wa Shule hiyo ya Sekondari ya Songa kusaidia hata kwa utaalam tu Wananchi hao katika ujenzi wa Shule yao, bado hakuna ushiriki na pengine Wananchi wana hofu ni kutokana na mgogoro huo. Hata hivyo, Wananchi wana imani kwamba Jeshi litaona umuhimu wa Shule hiyo na kuwapa moyo Wananchi kuendelea na jitihada zao kuikamilisha. Kazi za Wananchi zinaendelea kukamilisha ujenzi wa madarasa, hosteli, maabaraa na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Muheza imekuwa na bahati mbaya kwani hata katika kipindi cha mwaka 2001/2002, wakati Jeshi letu lilipofanya mazoezi ya pamoja na Majeshi ya nje yaliyofanyika Tanga, licha ya baadhi ya Askari hao kuweka kambi yao ndani ya uwanja wa mpira pale Muheza, Wilaya haikupewa msaada wowote kutoka katika Jeshi kama ilivyofanya kwa Wilaya ya Tanga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya maelezo hayo ni kuonyesha jinsi ambavyo Jeshi letu linaweza kuujenyea uhusiano mzuri na wa karibu na raia, badala ya Wananchi kuliona Jeshi kama chombo cha kuogopwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuboresha huduma za afya kwa wapiganaji wake na kutoa huduma kwa Wananchi wanaoishi jirani na kambi za Majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake safi sana na napenda vile vile kuwapongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii na watendaji wake kwa ujasiri na uwezo wao mkubwa walionao wa kusaidia nchi yetu hii kuweka mazingira ya usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri bila ya usalama hakuna utulivu na bila utulivu hakuna uchumi na kwa maana hiyo ni vurugu tupu. Kuwepo kwenu ni kuwepo kwa Serikali na kudumu kwa Taifa hili. Nawapongeza kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wazo la Mheshimiwa Waziri kuwa, kwa utaratibu mzuri wa Jeshi hili ni sahihi kabisa uajiri wa vijana wetu Polisi, Jeshi Wanamaji (Jeshi la Majini), lazima watolewe kutoka JKT au JKU. Huko ndiko utakapopata vijana wenye maadili, vijana safi na wenye upeo na uchungu wa nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile naomba yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kambi za vijana zipanuliwe kwa kupunguza umaskini. Hapa nina maana kambi za vijana ziwe na mtazamo wa kupunguza tatizo la ajira tulilonalo. Nazo zielekezwe katika kilimo kwa dhana ya kuongeza uwezo ili kilimo kiwe ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, endapo tutapanua kambi za vijana kwa upande wa kilimo tutapunguza tatizo la ajira, watakaomiliza muda wao pale wataweza kuujajiri, tutakuza uchumi wa nchi na kupunguza watu vijiweni na kungoja ajira Serikalini, tutawajengea Uzalendo wa kupenda nchi yao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi tutakuwa na raia (Uongozi wa baadaye) utakaojali maslahi na dhana ya Utaifa wa nchi hii na Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wanajeshi (Viongozi). Wanapostaafu wajengewe mazingira ambayo watadhibitiwa na watakuwa ni sehemu ya hazina ya nchi hii. Nakubaliana na dhana kuwa hawa (wastaafu hasa Viongozi kama Majenerali kuwaacha mitaani ni kosa kubwa kwani wanaweza kutumiwa na maadui zetu wanapowahitaji na kuhatarisha usalama wa nchi yetu. Kuwashifadhi ni jambo jema kwani tunaweza kuwatumia hata kwa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa usalama wa Taifa, nadhani umefika wakati tuwe na watumishi wa Serikali watakuwa *attached* na *system* kwa kuwafuatilia au kufanya kazi pamoja na Wakuu (wageni) wa vitengo mbalimbali vya uchumi vinavyokuja kuwekeza hapa nchini. Hili ni suala kubwa na ni muhimu sana kuwaachia wageni kuja kuwekeza. Lakini tukiwaamini moja kwa moja, ni udhaifu ambao gharama yake ni kubwa sana na ambayo hatuimudu. Hili nalo lina haja ya kufikishwa na kufikiriwa hata kule kwenye Vyombo vya Habari, wawekezaji na hata Vyama vya Siasa.

Nina wasiwasi kuwa baadhi ya Vyama vya Siasa vinatumiwa na kwa lugha nzuri walizonazo, demokrasia wanayohubiri, sura zao nzuri ndani yake kuna utashi wa madaraka na wao hawatishiki na lolote lile ilimradi dhamira zao zinatimizwa. Kwa maana hii hata wakorofi wa Mataifa ya nje watakubali kuyakumbatia na hawatajali usalama wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri alitazame suala hili zaidi kwa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano, Zanzibar.

- Kwa uwazi nchini sasa unatumika ukabila, ujimbo, rangi zao na kadhalika.
- Hawa wapo tayari hata kumwaga damu, lakini kiu ya utawala walijonayo kwenye dhamira yao ipatikane.
- Watu weusi kama chungu wao watajiita Waarabu ukikutana nao maneno yao matamu undani wao shubiri.
- Hawapendi Muungano, hawa hawawapendi Waafrika.
- Wakiwa Bara, Watanzania, wakiwa Zanzibar, Wazanzibara, wakiwa Pemba wao ni Wapemba, wakiwa Wete wao ni Waarabu, wakiwa Mkoani wao ni Wahadimu (kwa maana ya kuwa siyo wao).

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Vyama vya Siasa kwa usalama wa Taifa hili ni lazima idhibitiwe. Haitakuwa busara mambo haya kuyaacha hohehahe. Nchi hii itavunjika.

MHE. HADIJA K. KUSAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ninampongeza sana Waziri Sarungi kwa kazi nzuri anayoifanya, ameleta mshikamano sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuzungumzia Jeshi la Kujenga Taifa. Toka Serikali irejeshe mafunzo ya JKT kwa vijana wetu, mpango ambao ulisimama kwa karibu miaka saba, tunaishaukuru sana kwa uamuzi wake mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri ufuatao: -

- Kutokana na uzoefu ambao tumeupata toka mpango huu wa *Operation Mkapa* uanze, Serikali iangalie uwezekano wa kutoa kipaumbele kwa vijana waishio karibu na kambi hizi badala ya kuwatoa mbali.
- Kutoa kipaumbele kwa vijana walioishia darasa la saba ambao hawana uwezo wa kuendelea na Elimu ya Sekondari kutokana na sababu mbalimbali, kwani vijana waliofika darasa la 12 - 14 wanayo nafasi ya kuchukuliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwani wao wameshatangaza kuwa

hawataajiri tena vijana wa darasa la saba. Hivyo, Wizara hii isaidie kuwachukua ili wakajiendeleze na hatimaye waweze kuajiriwa ama kujajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwininge ni kuhusu lile ambalo limezungumzwa na Kamati kifungu na. 4.2.4. Migogoro ya ardhi baina ya Wananchi na Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Mwaka 2002 nilizingumzia kuhusu eneo la Jeshi lililoko Buza. Napenda kuiomba Serikali itoe eneo hilo kwa Wananchi wa Buza kwani limekuwa karibu na makazi ya Wananchi, lakini haya zaidi eneo hili hutumika kuficha vitu vinavyoibiwa kama vile magari. Eneo hili limekuwa ni kero kubwa kwa wakazi wa Buza, Wilayani Temeke, Kata ya Yombo Vituka. Naomba Waziri anisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni kuhusu mikopo ya vifaa vya ujenzi kwa Maaskari wetu, niliwaombea viwanja vya kujenga nyumba na wamepata. Hivyo, naomba Serikali iwawezeshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Profesa Philemon M. Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Ndugu Vincent Mrisho, Katibu Mkuu wake pamoja na Makamanda, Wapiganaji na Viongozi wengine wa Vikosi, Asasi na Vyuo vya Wizara hii, kwa hotuba nzuri sana. Aidha, kwa utekelezaji bora na majukumu ya Ulinzi na Kujenga Taifa pamoja na kuziboresha shughuli na vitendea kazi vinavyohusiana na majukumu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha upya na kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa, hatua hiyo siyo tu itasaidia kuimarisha ukakamavu, Uzalendo na Umoja wa Kitaifa, bali pia itasaidia kuchangia katika Pato la Taifa, kuwapatia vijana stadi mbalimbali na hatimaye kuongeza Jeshi la Viongozi bora, wafanyakazi bora na kupunguza uzururaji na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafarijika sana kwamba, Wilaya yetu ya Muheza hususan katika Jimbo la Mkinga tumebahatika kuwa na Kambi kubwa ya JKT kule Maramba, kwa jumla kambi hiyo ya JKT imefanya kazi nzuri. Zaidi ya kutoa mafunzo ya kijeshi na ya stadi mbalimbali, kambi hiyo imefanya juhudhi kubwa kubuni miradi maalum ambayo inawasaki sana Wananchi hasa vikundi vya akina mama na vijana. Vile vile, kambi hii imo mbioni kutafuta Mbia, ambaye watashirikiana naye katika kuendeleza uzalishaji wa kakao na mazao yake. Pia, kambi hii ina mradi wa kuzalisha miche ya mikakao kwa madhumuni ya kusambaza na kuwahamasisha Wananchi kuendeleza zao hili. JKT Maramba vile vile imeshiriki katika ujenzi wa madarasa na majengo mengine kwa huduma za jamii kwa bei nafuu. Hali kadhalika Zahanati yao inahudumia Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri yote hayo zimekuwepo dosari ambazo zinastahili kurekebishiwa ili Wananchi wasiione JKT Maramba kama kero kwao. Baadhi ya dosari hizo ni pamoja na baadhi ya Wanajeshi wa kambi hiyo kuwadhalilisha Wananchi kama vile kuwanyanyasa na hata kuwapiga isivyostahili. Kero nyingine ni pamoja na: -

- Kuwanyima Wananchi sehemu za ardhi zilizo wazi kwa ajili ya kilimo au kuwatoza ada kubwa na kuwatumikisha bila mapato. Napenda kueleza hapa kwamba, Kata ya Maramba, Muhinduo, Kigongoi na Gombero, zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa ardhi kutokana na ardhi kubwa kuwa chini ya JKT Maramba, hifadhi za misitu, shamba la mbegu la Mwele na mashamba makubwa ya mkonge. Hivyo, kuwanyima Wananchi fursa ya kulima katikati ya safu za mazao ya kudumu na kuwanyima fursa ya kupata maji kutoka maeneo ya karibu, hii ni kero kubwa kwa Wananchi kama ilivyoshauriwa na Kamati ya Bunge.

- Kuwanyanyasa wanafunzi wa kike wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya Maramba. Baadhi ya Askari huwachukulia wanafunzi hao kama wake zao na kuwaweka vimada.

- Mara nyingine huilingilia kazi za Polisi na kuwanyanyasa Polisi wachache sana waliopo katika Kituo Kidogo cha Polisi kilichopo Maramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari hizi chache nilizozitaja na nyinginezo, sio tu zinaharibu sifa nzuri za JKT Maramba, bali pia zinapaka matope Serikali pamoja na Chama. Hapana budi kero hizi zikemewe na hatua za nidhamu zichukuliwe kwa watakaobainika kuhusika na kusababisha kero hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine pia ingesaidia iwapo JKT Maramba itapata Kiongozi aliyethibitishwa badala ya kuwa Kaimu Kamanda kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. ELISA D. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kuchangia machache kwa nia ya kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Prof. Phillemont Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Watalaam pamoja na Watendaji wake, kwa kutayarisha hotuba hii ya kina na ambayo inaridhisha. Aidha, nitamke kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamba, licha ya kuendeleza na kutekeleza majukumu yake mazito ya Ulinzi wa Taifa letu, Wizara pia imejitahidi kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa kuwawekea Wanajeshi makambi na kuwajengea malazi bora ya kuishi. Aidha, Wizara inatoo huduma za jamii kama vile matibabu na elimu hasa Shule za Sekondari katika sehemu mbalimbali za Majeshi ya Ulinzi wa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kuboresha huduma za jamii katika Majeshi yetu ni dhahiri zinawanufaisha pia na raia wetu. Tunashauri Wizara iendelee na juhudhi hizi kwa nguvu zote na Serikali iware msaada na ushauri pale inapobidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mikakati mbalimbali ya kuimarisha ulinzi katika nchi yetu. Hali ya ulinzi katika mipaka yetu na nchi za jirani imeendelea kuwa shuwari licha ya ukosefu wa amani katika nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majeshi yetu ya Ulinzi yanapaswa kupewa kila ushirikiano katika mafunzo ya kila wakati, huduma bora za jamii ikiwepo tiba, malazi na elimu katika ngazi zote, pamoja na zana za kisasa za kuwawezesha kujifunza na kutekeleza majukumu ya ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Taifa ya kusambaza huduma ya umeme katika Kambi ya JKT Oljoro, iliyoko Arusha. Umeme huu ni muhimu sana siyo kwa matumizi ya Jeshi la Kujenga Taifa peke yake, bali pia kwa Wananchi na jamii inayozunguka Kambi za JKT Oljoro, hasa kwa kuwa pale Oljoro kwa sasa kuna Kituo cha Afya cha Oljoro ambacho kinafaa kuwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie mgogoro uliopo kati ya Wananchi wa Jimbo langu la Arumeru Magharibi, Kata ya Oldonyosambu na JWTZ, Kikosi cha Rada Oldonyosambu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgogoro huu Wananchi wa Oldonyosambu wametakiwa kuhama kwa agizo la Serikali kuwa sehemu hii sasa ni ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Sasa wamepewa hadi tarehe 31 Julai, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Oldonyosambu wamekubali agizo la Serikali, lakini wanaomba kabla ya kuondoka wapatiwe ufanuzi katika haya yafuatayo: -

(i) Wapewe fidia inayolingana na hali ya sasa. Fidia hiyo ijumuise ardhi, nyumba na usafiri kwenda pale Serikali itakapowaweka.

(ii) Suala la watoto wa Shule za Msingi na watoto walioko Sekondari liwe limefanyiwa maandalizi kule waendapo.

(iii) Walipwe fidia ya miundombinu ya jamii kama vile Shule za Msingi, Shule za Sekondari walizochangia.

(iv) Wawe wameandaliwa huduma za jamii kama maji, Shule za Msingi na Sekondari, Hospitali na Vituo vya Afya kule wanapopelekwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi hawa wanaiomba Serikali iwafikirie, iwasaidie wapate fidia inayowastahili kabla ya kuondolewa na kupewa makazi mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, atakapokuwa anahitimisha majibu yake kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge, alizungumzie suala hili nyeti kwa Wananchi wa Arumeru Magharibi, Kata ya Oldonyosambu.

Narudia kutamka kuwa baada ya haya machache, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali George M. Waitara, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Luteni Jenerali Iddi S. Gahhu na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Davis Mwamunyange, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kuimarisha ulinzi wa nchi yetu na Wananchi. Askari wetu wameshiriki *operation* mbalimbali kama vile kusindikiza meli za kiraia na kufanya doria katika Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi na *Operation* Kamata Majambazi Mkoa wa Kagera (KAMAKA), nikizitaja chache tu. *Operation* hizi zimeongeza imani ya Wananchi kwa Jeshi lao na Serikali yao. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilibahatika kushiriki katika uzinduzi wa sherehe za miaka 40 ya Jeshi la Kujenga Taifa. Wakati wa sherehe hizo nilishuhudia ari ya Askari na vijana wetu, mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali za mafunzo kwa vijana wetu kama vile ulinzi, uchumi, ufundi, michezo na utamaduni. Ni dhahiri kama Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alivyosema katika hotuba yake ya uzinduzi wa sherehe hizo kwamba, kuna sababu za msingi kudumisha Jeshi la Kujenga Taifa kwa faida ya vijana wetu wa leo na kwa faida ya vizazi vijavyo. Mimi binafsi maisha yangu na tabia yangu kwa kiasi kikubwa yameboreshwa na mafunzo niliyopapatna kushiriki kikamilifu kuwafundisha vijana wenzangu pale Oljoro Arusha kuanzia Januari, 1977 hadi Januari 1978. Kwa hiyo, nasubiri kwa shauku kubwa, pamoja na Wananchi wa Kanda ya Ziwa, uanzishwaji wa Kambi ya JKT huko Muleba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Jenerali George M. Waitara na Luteni Jenerali Iddi S. Gahhu, kwa kusimamia vizuri shughuli zote Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara pamoja na Kurugenzi za Michezo kwa kutuletea ushindi kwenye aina zote za michezo. Pia, naishukuru Wizara kwa kuleta michezo ya Bara la Afrika kufanyika Zanzibar. Michezo hiyo imeleta msisimko kwa Wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa 49 amezungumzia kwamba, kutakuwa na michezo mingine mwezi ujao. Je, maandalizi yamefikia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa nini Timu ya Jeshi ya Soka haifanyi mazoezi na Timu yangu ya Mlandege katika kipindi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Waziri hatusaidii kwenye kesi ya Mlandege na Ruvu wakati Ndolanga, Wambura, BMT hadi leo wameshindwa kutatua tatizo lao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali iwaenzi Majenerali na Makanali wastaafu kwa kuwapangia shughuli mbalimbali wenyewe uujuzi nazo.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Wataalam wake wote, kwa hotuba nzuri pamoja na kazi nzuri ambazo wanazitekeleza kila siku na kazi walizozifanya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuzungumzia Hospitali ya Bububu. Hospitali ya Bububu imekuwa kila mwaka tunaelezwa kuwa ujenzi wake utakamilika, lakini bado haujakamilika. Kwa hiyo, namwomba Waziri katika Bajeti hii, achukue umuhimu wa hospitali hiyo iimarishwe kwa sababu ni hospitali ambayo inatoa msaada mkubwa sana kuanzia kwa Viongozi Wanajeshi hadi kwa Raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu Kambi ya Welezo ambayo iko ndani ya Jimbo langu la Mwera. Kambi hii ni ya Kikosi cha Missile pia ina hospitali ambayo sasa imechakaa kabisa. Pia, ofisi ya kambi hiyo ni nyumba ya mbao na ambayo imechakaa kabisa kabisa haifai hata kutumika. Naomba Mheshimiwa Waziri, afanye ziara ya makusudi ili atembelee Kambi hiyo ya Welezo, akiiona labda anaweza kuwa na moyo wa huruma na kushughulikia ukarabati wa hospitali na ujenzi wa ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu michezo. Michezo kwa Wanajeshi ni jambo muhimu sana. Katika Kambi hii ya Welezo kuna Timu inayoitwa Missile, lakini kusema kweli ina uhaba wa vifaa. Kwa hiyo, timu za Jeshi hasa za kambini ziwezeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu matatizo ya tenda ya chakula cha Wanajeshi huko Zanzibar. Hivi sasa Wananchi waliochukua tenda hiyo wanasisitika sana kwa sababu ya kazi nzito isiyo na faida kwao. Hivi sasa wenyewe tenda hiyo wanatakiwa wahudumie upishi, vifaa vya jikoni, bidhaa, kuni na vyombo vya kutolea huduma. Sasa, kule Zanzibar bidhaa kama mchele, sembe na sukari bei zake huwa hazitulii, mara kwa mara huwa zinabadilika na kuwa juu, lakini waletaji wa tenda hizi malipo yao huwa yale yale! Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kuwa, ni vema hivi sasa Jeshi lichukue hatua ya kujipikia wao wenyewe ili kupunguza gharama na kupunguza matatizo kwa hawa wenyewe tenda ili wawe wanapeleka bidhaa tu. Natumaini Wanajeshi wana uwezo mzuri tu wa kupika na kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, kwa hotuba nzuri na pia ninampongeza Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote waliohusika katika maandalizi ya hotuba hiyo nzuri.

Awali ya yote ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara kwa jumla, kwa kutekeleza kwa kiasi kikubwa yale yaliyokusudiwa katika Bajeti ya 2002/2003. Aidha, nampongeza kwa hatua zinazochukuliwa kuboresha mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wengi sana wa Vijijini wakiwemo wale wa Jimboni kwangu Liwale wana nia ya kuijunga na JKT, lakini kutokana na uchache au upungufu wa nafasi, hawajafanikiwa. Ninashauri Wizara ifanye kila linalowezekana kupanua mafunzo hayo ya JKT ili vijana wengi zaidi wapate nafasi ya kuijunga na JKT. Ninapendekeza kuwa utaratibu unaotumika wa kuwapata vijana wanaopenda kuijunga na JKT au JWTZ kuititia Wilayani uendelee na pia uboreshwe kwa kusimamia vizuri ili kuwapata vijana halali wa maeneo hayo, vinginevyo nia nzuri ya Serikali ya kutaka kujenga Jeshi kutokana na Wananchi wake kote nchini itapotoshwa na wajanja wanaotafuta ajira kwa ndugu zao na maraffiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata vijana wa kila Wilaya kujiunga na JWTZ au JKT, ninashauri Mbunge wa eneo husika awe mionganoni mwa Kamati itakayopitia maombi ya vijana wanaoomba kujiunga na JWTZ au JKT. Kazi hii hivi sasa inafanywa na Kamati ya Usalama ya Wilaya ambayo Mbunge siyo Mjumbe. Lakini anayeweza kutambua uhalali wa vijana wanaoomba nafasi hizo ni Mbunge wa maeneo hayo ya waombaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hatua zinazochukuliwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya kuweka mikakati ya kuimarisha Jeshi la Mgambo ambalo mafunzo yao hutolewa na Wanajeshi, Makamanda wa Mgambo walioko Wilayani. Napendekeza Sera ya Mgambo iandaliwe ili Dira ya Jeshi hilo muhimu iwekwe wazi. Nilipochangia Bajeti ya Ulinzi mwaka 2002/2003 nilielezea kwamba, Jimboni kwangu Liwale zaidi ya Wananchi 300 walihitimu mafunzo ya Mgambo hawajapata vitambulisho. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, atekelезaji ufanyike mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kazi nzuri na ninamalizia kwa kusema tena ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuwasilisha hotuba nzuri na yenye dira ya ulinzi na usalama wa nchi hii. Aidha, maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri ni ya kina sana na kwamba sasa Watanzania tujue historia na mikakati ya Wizara hii. Pamoja na pongezi hizi bado napenda kuridhika na utaratibu wa kuliimarisha Jeshi la Kujenga Taifa kuwa ndicho kiimi cha amani, malezi na stadi mbalimbali kwa vijana wetu. Sisi sote tulipotitia Jeshi hili tunajivunia hadhi hii na mbinu za kukabiliana na maisha.

Mwisho, naomba sana Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo ya kina kuhusu tatizo la Ndugu Gabriel Yohana, mpiganaji JWTZ, mwenye Na. MW 43040. Mpiganaji huyu kama ilivyoelezwa kwenye barua ya Mkuu wa Wilaya - Magu, mimi mwenyewe nimemuona mara kadhaa japo mpaka sasa Wizara bado haijamtatulia tatizo lake. Hivyo, katika maelezo yake, naomba Mheshimiwa Waziri, anipatie majibu sahihi ili nami niweze kumuwasilishia kikamilifu. Ahsante.

MHE. KHADIJA SALEH NGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichangie hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuipongeza hotuba hii nzuri na ya kutia moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi ni jeshi imara lililoandaliwa kuwa Jeshi la Wananchi. Kweli sina budi kulipongeza jeshi hili pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa asilimia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hotuba hii kwa kikitaja Kituo cha Jeshi Potoa (*Navy*) kuwa askari wa kituo hicho bado ni watiifu, waaminifu kwa muda wote watakaolitumikia jeshi hilo. Ukweli ni kwamba askari hao bado wanaishi katika mazingira magumu kwa muda wote tokea kituo hicho kilipojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alifanya ziara mwaka jana 2002 na alijionea mwenyewe hali halisi ya kituo hicho kilivyo na mapungufu muhimu yaliyopo kama ukosefu wa umeme, simu na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ziara ya Waziri kutembelea kituo hicho kwa kuuona umuhimu uliokuwepo katika kituo hicho, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 Wizara yake ilitenga kiasi cha shilingi milioni 15 (15,000,000) kwa ajili ya upatikanaji wa mahitaji hayo muhimu hapo kituoni ikiwa ni pamoja na ukarabati wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aje tena kituo cha Jeshi Potoa kwa mara nyingine aje aone ni kwa nini mahitaji hayo muhimu katika kituo hicho muhimu kwa upande wa Zanzibar utekelezaji wake unavyoendeshwa taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu askari waliostaafu. Tunao askari waliostaafu ambao bado wana nguvu za kulijenga, kulilinda na kulitetea Taifa lao. Hivi Wizara yako haioni iko haja ya kuwaajiri japo kwa mkataba kulingana na sifa zao au utendaji kazi wao mzuri waliozifanya wakati wakiwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Kujenga Taifa, ukweli ni kwamba vijana hawa wanastahili pongezi za pekee kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya hasa kazi za mikono. Mfano hai tumeuona wakati wa Maonyesho ya Sherehe za Saba Saba Dar es Salaam.

Samani walizotengeneza ni nzuri sana kiasi kwamba wananchi waliotembelea banda hilo watakubaliana nami kuwa, bidhaa zao zilikuwa nzuri kiasi kwamba hazikukidhi mahitaji ya wateja kwa sababu, vijana wa jeshi hilo hawakupata muda mrefu wa utengenezaji wa vifaa hivyo. Miezi miwili haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi hili litenge askari maalum wa jeshi hili kwa kazi hiyo tu ya utengenezaji wa samani hizo ili wananchi wafaidike na huduma hizo siyo kusubiri wakati wa Saba Saba. Na hii pia itasaidia kutunisha Mfuko wa Jeshi hilo.

Naomba kuunga mkono hoja hii asilimia kwa mia.

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wapiganaji wote wa jeshi letu kwa kuimarisha na kudumisha ulinzi na usalama wa nchi yetu na kuwa ni mfano wa kuigwa katika Afrika. Mimi katika hali hii nzuri inayojenga imani na matumaini makubwa kwa wananchi inanilazimisha kuunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa iliyoko mipakani kuna barabara za ulinzi na barabara hizo zinatambuliwa na Wizara yako ya Ulinzi. Kwa mikoa wetu wa Ruvuma kuna barabara mbili zinajulikana kama ni barabara za ulinzi, nazo:-

- (a) Barabara ya Songea hadi Mitomoni; na
- (b) Barabara ya Lituhi, Liuli, *Mbamba Bay* hadi Chiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kufahamu Wizara ya Ulinzi inaitunzaje hizi barabara za ulinzi? Inakuwaje barabara ya ulinzi haipitiki kabisa muda wote, na kwa nini barabara hizi hazitunzwi ipasavyo? Ikiwa barabara ya ulinzi inapitika, basi inapitika kwa taabu wakati wa kiangazi na wakati wa masika hazipitiki kabisa. Kama barabara ya Lituhi, Liuli, *Mbamba Bay* hadi Chiwanda. Naishauri Serikali yetu Tukufu, iangalie na itunze barabara zote za ulinzi hapa nchini ili zipitike vizuri wakati wote masika na kiangazi. Ahsante sana.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja bila mashaka yoyote. Baada ya hapo napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

1. Naishauri Serikali kuimarisha upya suala la mafunzo ya Mgambo nchini. Askari wa Mgambo walisaidia sana vita dhidi ya Nduli Iddi Amin. Ni askari wazuri sana wa akiba wanasaidia sana usalama wa raia.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani kuimarisha mafunzo ya Mgambo na kuwatumia askari hao katika ulinzi wa nchi na wa raia?

(b) Serikali ina mpango gani kuimarisha Ofisi za Washauri wa Mgambo Wilayani kwa kuwapa usafiri wa gari au pikipiki ili kurahisisha kazi?

2. Kwa kuwa askari wapiganaji hustaa fu mapema kulinganisha na watumishi wengine Je, Serikali ina mpango gani wa kuwakopesha wapiganaji vifaa vya kujenga nyumba ili mara wanapostaafu wawe na mahali pa kuingia?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo yako.

3. Kwa kuwa Serikali iliamua kununua Rada kwa faida ya maendeleo yetu na usalama wa nchi yetu. Je, rada hiyo ilishanunuliwa? Je, inaendeshwa na wageni au wapiganaji wazalendo? Na inasaidiaje?

4. Nataka kujua hospitali ya Jeshi ya Lugalo ina sifa gani hasa vifaa, majengo, Madaktari, na kama raia wa kawaida wanatibiwa kwa masharti gani?

Je, wapiganaji wanachangia matibabu na raia je?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba nzuri na mipango kabambe ya kuendeleza jeshi letu la Ulinzi. Mimi, naunga mkono hoja hii bila kuhoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuelezea furaha yangu binafsi na furaha kubwa ya wananchi wa Mwanga kwa kutembelewa na Wahandisi wa Jeshi. Wahandisi hao walikuja kutathmini ugumu wa kuzikamilisha barabara 3 zilizochimbwa na wananchi lakini zimeshindikana kukamilika kwa sababu ya vikwazo katika maeneo korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wahandisi wa Jeshi walotembelea Mwanga walitoa ripori yao nzuri. Sasa tunangojea kwa hamu, waje watusaidie kuzikamilisha barabara hizi tatu. Ahsante sana.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu, Makamanda wa Majeshi, wataalam na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kulinda Taifa letu. Hongera sana. Pia nawapongeza kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kueleweka na kuandaliwa kisayansi. Mchango wangu ni kuishauri tu Serikali katika nia ya kupata ufanuzi wa maeneo machache tu. Ushauri wangu ni kuwa wale wapiganaji waliopata ulemavu wakiwa katika shughuli za kuikomboa Afrika na Tanzania kwa ujumla wanasaidiwaje katika Taifa hili? Nina taarifa kuwa baadhi ya wapiganaji hao wamewekwa kwenye Kambi huko Lugalo. Lakini nimepata taarifa kuwa matunzo ya hapo si mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo ndivyo, naishauri Wizara itupie macho Kambi hilo ili hawa wapiganaji wamepata ulemavu huo wakiwa katika harakati za ukombozi, hivyo watunzwe vizuri sana kutokana na mchangwo na damu kwa nchi. Baada ya ushauri huu naunga mkono hoja.

MHE. REMIDIUS EDINGTON KISSASSI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kuwa nampongeza sana Waziri Prof. Sarungi na wanajeshi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda nchi yetu. Nasema naiunga mkono hoja hii. Pamoja na hayo, napenda kuchangia machache yafuatayo:-

(i) Naomba Mheshimiwa Waziri ashughulikie matatizo ya mgogoro wa mipaka katika kambi ya Chukwani Zanzibar niko tayari tushirikiane kwa hilo.

(ii) Kutokana na matatizo makubwa ya umeme na maji katika kambi za Chukwani na Kisakasaka pamoja na Vijiji vya jirani, nashauri Mheshimiwa Waziri tushirikiane ili huduma hizi ziwepo; hasa kwa vile huduma hizo zipo karibu na kambi hizo.

(iii) Pamoja na pendekezo zuri la Kamati kuwa ajira katika vikosi vya ulinzi watoke JKT lakini mmesahau na JKU. Hili ni muhimu sana kwa maslahi ya Muungano wetu.

(iv) Wizara iendelee kuhimiza michezo jeshini ili wawe nyota wa kuwakilisha nchi yetu katika michezo ya Kimataifa.

Baada ya kusema hayo naiunga mkono hoja tena. Ahsante.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba nzuri, makini na iliyoeleza mambo yote ambayo mtu wa kawaida angependa na anayostahili kuyafahamu. Napongeza pia wote walioshiriki kumsaidia Mheshimiwa Waziri katika kuandaa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2002/2003 zinatia moyo sana. Kazi za ujenzi na ukarabati wa nyumba za wanajeshi inaonyesha mwelekeo mzuri.

Napenda kupongeza JWTZ kwa kushiriki katika *operation KAMAKA*. Mafanikio ya operation hii yameleta nafuu kwa wananchi angalau wameweza kupata usingizi. Tunaomba *operation* hii iwe ya kudumu ili kuzidi kuwabaini majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa ni muhimu sana hasa kwa wakati huu ambaa vijana wengi wanakosa mwelekeo, maadili yanamomonyoka ajira hakuna. JKT iwe na malengo ya kuwapa vijana mwelekeo kuwaimarisha kimaadili lakini pia iwapatie mafunzo yatakayowasaidia vijana hao kujajiri mwenyewe hasa katika maeneo ya kilimo.

Nampongeza Mheshimiwa Meja J. J. Makundi kwa hotuba yake ingawa katika baadhi ya maeneo alikuwa anaeleza kana kwamba kuna vita tayari. Tuna haja/sababu ya kuwatilia mashaka majirani zetu?

Namaliza kwa kuunga mkono hoja.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa leo asubuhi. Hotuba hii imejaa uchambuzi wa kina na hekima na busara za hali ya juu. Pongezi sana Mheshimiwa Waziri. Katika jimbo langu la Siha kuna wazee ambaa walipigana katika vita kuu ya pili ya dunia ya 1939 - 1945. Wananchi hawa wamenilalamikia mara kwa mara wakiuliza mbona fidia ambayo waliahidiwa mpaka leo hajatolewa?

Katika Kijiji cha Ngaronyi - Kata ya Siha Kaskazini mwananchi mmoja - Mzee Elirehema Ngowo alinikumbushia kwa mara nyingine katika mkutano wa hadhara kuhusu fidia zao. Naomba nipate majibu leo ili nikirudi Jimboni niweze kumpelekea majibu. Naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Naipongeza hotuba hii kwa juhudini zinazofanywa na Wizara hii kwa kudhibiti hali ya usalama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali mambo yafuatayo:-

1. Nafasi za vijana wanaoingia jeshini ziongezwe zaidi ili kupata idadi kubwa ya vijana wanaopata nafasi na kupata hasa stadi na utaalamu wa kuwawezesha kujajiri ili kupunguza vijana wanaozurura.
2. Nafasi za vijana wa kike ziongezwe zaidi ili kwenda sambamba na azima ya Serikali ya kuelimisha wasichana.
3. Taaluma na stadi ipanuliwe jeshini zikiwa taaluma ya kompyuta, *Engineering*, simu za mikononi, umeme na kadhalika;
4. Utaratibu wa kuwasaili vijana wanaochaguliwa kwenda JKT ufanywe na Wilaya moja kwa moja na mkoaa upitishe tu sio tena kuchuja.

5. Pamoja na juhudi za Wizara kujenga nyumba za wapiganaji na juhudi hizo ziendelezwe ili kuwawezesha wapiganaji kuishi pamoja, ili kujenga nidhamu.

6. Wizara iongezewe fedha ili kuwezesha Wizara kuimarisha shughuli zake hasa katika eneo la mafunzo ya JKT kwani inafanya kazi kubwa ya kuwezesha vijana wa nchi kuwa na shughuli na kupunguza wimbi la majambazi.

7. Naishauri Serikali kumrudisha ule utaratibu wa vijana wanaomiliza *High School* na Vyuo mbalimbali waende JKT bila kujali wataajiriwa au hapana. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi, Katibu Mkuu, Amiri Jeshi Mkuu Jeneral George M. Waitara pamoja na wakuu wote wa Jeshi la Wananchi, Meja Jeneral Davis Mwamunyanga, na askari wote wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri ambayo jeshi letu linafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mapendekezo machache kuhusu hoja hii nazo ni kama zifuatazo:-

* Utaratibu unaotumika kwa kuwachukua vijana wetu wa JKT inaonyesha una walakini na upendeleo mkubwa. Kwa vile bado vijana wa vijijini wengi hawapati nafasi:-

*	<i>Selection</i> ya kwanza	-	Kijiji;
*	<i>Selection</i> ya Pili	-	Kata;
*	<i>Selection</i> ya tatu	-	Wilaya;
*	<i>Selection</i> ya nne	-	Mkoani;
*	<i>Selection</i> ya tano	-	Taifa.

Ni sawa lakini kusiwe na upendeleo wa wazi. Vijana wasio na mtu wa kuwasimamia wamekuwa hawapati nafasi katika eneo hilo lote la usaili. Hasa wale wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mkuu wa Jeshi na yule wa JKT wasimamie kwa karibu uteuzi wa vijana mara baada ya kumaliza Jeshi. Wanaojiunga na Jeshi na JKT kwa mkataba vijana wachache wamekuwa hawapati nafasi hizi kwa visingizio mbalimbali. Afya mbaya na kadhalika ninayo mifano ya vijana walirudishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hii ikisimamiwa vizuri hakutakuwa na upendeleo wowote JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa jimbo langu wanapenda sana kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa nimejaribu sana kutafuta nafasi walau chache kwa vijana wa jimbo langu imekuwa ngumu kwa sababu ya urasimu. Wilayani na Mkoani *something should be done*, ili wote tupate nafasi sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jeshi litumike kwa ulinzi wa uvamizi wa wananchi nyakati za usiku hasa kwa wasafiri. Mimi sioni sababu Mabasi yasitembee usiku wakati nchi nyingi Mabasi yanatembea usiku na mchana hata nchi jirani wanatumia Jeshi na Polisi katika eneo hili na hakuna tatizo lolote lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kama upo uwezekano wa Kampuni ya Meremeta kukopesha vijana wangu pale Mkwajuni kupata *Detectors* za kutafutia madini. Mikopo imekuwa vigumu au jambo zuri ni kuleta vifaa vidogo vidogo kwa ajili ya suala hili. Mara nyingi upatikana kwa vifaa hivi ni vigumu kwa kutumika kama vile vya ku-*detect*, mabomu ya ardhini. Nitafurahi sana kwani Kampuni hii ya Meremeta ina machimbo, jimboni kwangu Songwe. Naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. BALOZI GERTRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu na wapiganaji wote kwa kazi nzuri. Ninayo maoni yafuatayo:-

1. Ipo haja ya kulitumia jeshi la JWTZ na JKT kujenga, uwezo wa nchi wa Sayansi na Teknolojia kwa kutumia wataalamu walioko ndani ya jeshi. Jeshi pia linaweza kufuatilia vijana wenye vipaji maalum walioko shulenii vyuoni na katika maeneo mengine ili waingie jeshini ili watumie vipaji hivyo kujenga uwezo wa Sayansi na Teknoloji. Jenerali George M. Waitara kwa kukaa India anao uzoefu wa nchi hiyo.

2. Napongeza jeshi kwa kuanzisha Mashirika ya uzalishaji mali, chini ya uzalishaji mali kama vile SUMA JKT, TANZANSION, MEREMETA LTD. ninapendekeza jeshi lianzishe Mashirika mawili katika maeneo yafuatayo:-

(a) Mawasiliano - Jeshi liweze kuwa na simu za mtandao kwa kutumia satellite iliyowekwa kwa msaada wa Belgium. Wataalamu wa jeshi wapo na pendekezo hilo lilikwishesanyiwa mchanganuo. Kwa kufanya hivyo wataalamu hao wanetumiwa kikamilifu na gharama za simu hasa zile za mkono zingepungua. Jeshi pia lingepata mapato makubwa ambayo sasa inachukuliwa na watu binafsi hasa kutoka nje.

(b) *Manufacturing Company*, jukumu lake liwe ni uzalishaji wa vifaa vya jeshi kwa mfano nguo, viatu, "housewife" na kadhalika Kampuni hii ingeweza kuzalisha ziada kwa soko la ndani na masoko ya nje kama vile *Agoa* na masoko ya majeshi jirani.

3. Ombi:

(a) Kwa hali ya visiwa vya Ziwa Victoria mafunzo ya Mgambo yaelekezwe kwa wavuvi wenyeji ili waweze kujihami na kulinda maeneo yao kwa kuanzia na Ukerewe ambako majambazi wa majini wanatishia maisha ya wavuvi.

(b) Nakumbushia ombi langu la kuanzisha *JKT Day* Ukerewe kama kuanzishwa kwa kambi ya kawaida ya JKT haiwezekani. Hii itaondoa vijana kuwa wazururaji na kuwapa uwezo wa kuzalisha mali kwa kuvua, kuanzisha bustani na mashamba ya matunda kwa utaalamu JKT inaweza kuwafunza vijana useremala, ushonaji, ujenzi na kuanzisha viwanda vidogo hasa kwa kuzingatia uhaba wa ardhi na wingi wa watu walio katika eneo hili. Ombi lizingatiwe na nitaendelea kukumbushia.

Mwisho, Jeshi liendelee kudhibiti usambazaji wa silaha ndogo zinazosababisha ujambazi. Kutokana na kuzungukwa na jirani amba wamekuwa na vita nchini mwao kwa miaka. Uwepo udhibiti wa silaha zinazopitia nchini mwetu kwenda nchi hizo.

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri anazozifanya kwa Wizara yake kwa mafanikio makubwa. Hakika hotuba amewasilisha vizuri na malengo yake yanaashiria maendeleo kwa Taifa letu. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii Bajeti ya 2003/2004 mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii nachangia mambo muhimu yafuatayo:-

1. Vijana wanaojiunga na JKT Wananchi wamehamasika sana kuurudisha mpango wa mafunzo ya JKT kwa vijana wao, kwa sababu vijana wengi waliopitia JKT wamemudu kuishi kwa kujitegemea, kuwa na nidhamu ndani ya jamii na uaminifu katika usalama wa nchi yetu. Kwa manufaa hayo vijana wengi wamejitokeza wenyeve katika kujiunga na mafunzo ya JKT. Tatizo lililojitokeza katika utaratibu wa sasa ni kama ifuatavyo:-

(i) Nafasi zinazotolewa ni ndogo sana hadi kuleta kutolewana kwa maafisa wanaoteua vijana Wilayani na Mikoani na wazazi wa vijana hao. Tunaomba nafasi ziongezwe.

(ii) Masharti ya kuwa na vyeti vya kuzaliwa inakuwa ni ngumu kwa vijana wanaotoka vijiji kwa sababu wazazi hawana mwamko wa kuandikisha vyetu vya kuzaliwa kwa watoto wao tangu wakiwa watoto. Kwa hiyo, nashauri Wizara itoe elimu kwa njia ya *Radio juu* ya umuhimu wa kuwa na vyeti vya kuzaliwa kwa vijana wanaotaka kujiunga na JKT kuanzia mwaka 2004. Na kwamba wale amba wale hawana

vyeti Serikali ya Vijiji itoe uthibitisho wa kuzaliwa kijijini vijana husika badala ya kuwafukuza na wakati huo huo utaratibu wa kupata yeti unafanywa na wazazi wao. Nasema hivyo kwa sababu wananchi wanapata hisia kwamba JKT ya sasa ni ya watoto wa wakubwa tu. Kwa hali hii naiomba Serikali iongeze fedha maalum kwa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili idadi ya vijana waongezewe huduma zao wakiwa kambini.

2. Wanajeshi wanaostaafu kazi chini ya umri wa miaka 60:

Kutokana na amri ya kazi za Jeshi, watumishi wake wengi hustaa fishwa kazi na matokeo yake wanahangaika kimaisha kwa vile wanastaafu kwa mshahara mdogo hawakuwa na muda wa kujiaadaa kimaisha kama kujenga nyumba, kulima mashamba ya mazao ya kudumu kwa sababu hawana kituo cha kudumu cha kazi. Kwa hiyo, wanastaafu kazi wakiwa wanaelekea kwenye maisha ya umaskini kuliko mkulima. Kwa hali hiyo naomba kuwepo na utaratibu wa kuwezesha watumishi husika kujenga nyumba kabla ya kustaa fu na watoto wao wasomeshwe bure kwenye shule zao za Kijeshi, na tatu wapewe kazi za mikataba ya muda kufundisha vijana wa JKT, Mgambo kwa kulipwa posho kidogo. Kwa sababu wanaweza kuwa raia wana vijiji, bila kupata vishawishi vibaya kutokana na shida ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa hoja nilizochangia, natumaini Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Kujenga Taifa atazitolea ufanuzi atakapo jibu hoja zote ndani ya Bunge letu Tukufu.

MHE. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake wote wakiwemo watendaji wa Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo ninatamka mwanzoni kwamba ninaunga mkono hoja ya Wizara hii asilimia kwa mia. Pamoja na uzuri na ukamilifu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ninaomba kuchangia sehemu chache ambazo naamini zitasaidia kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Silaha za Ulinzi, ninaomba kabisa kutilia mkazo katika kupata silaha za kileo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge lako Tukufu. Aidha, mimi ni Kanali wa Jeshi Mstaafu, nimetembelea makambi yetu hivyo baadhi ya mambo ya ulinzi nakiri kuyaelewa kwa kiasi. Kwa maana hiyo ninatilia mkazo lazima tukubali kuligeuza jeshi letu liwe safi na kileo kufuatana na Teknolojia ya kileo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya jeshi letu la Bahari (*Navy*) hali yake si nzuri. Vyombo vyake ni vya zamani sana na vimezeeka. Kwa kweli haviwezi kukabiliana na vyombo vya Teknolojia ya kileo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa mara nyingine twende na wakati, lazima tupate vyombo vya kisasa vyenye uwezo mkubwa wa kupambana na adui ye yeyote. Vita vya Baharini ni vita ngumu sana tena vya kitaalam ya hali ya juu sana, lazima tuijandae vizuri sana. Tukubali kwamba tuna eneo kubwa la impaka wa mwambao wa Bahari ya Hindi, Kaskazini tumepakana na Jamhuri ya Kenya na Kusini tumepakana na Jamhuri ya Watu wa Msumbiji lakini kwa Mashariki yetu ziko nchi za Sheli Sheli na visiwa vya Komoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bahari ya Hindi ni kubwa na ni bahari inayohitaji vyombo vikubwa na vya kileo. Madola Makuu ya ulimwengu yanaichezea sana bahari yetu katika upande wa Mashariki na wanathubutu kutaibia rasilimali (utajiri wetu wa baharini) kama samaki na mali za bahari. Wakati wa amani ndio wakati mzuri wa kuyaandaa vyema Majeshi yetu, katika hali zote. Mafunzo ya mbini mbalimbali aidha kuzizoea silaha mpya na utaaliam wake ulivyo. Mazoezi maana yake ni kupunguza vifo na maafa makubwa wakati wa vita halisi. Mazoezi ndio kazi kubwa ya Majeshi kwani jukumu lake ni kuweka amani na utulivu wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za wapiganaji, ninashukuru kwa juhudzi za kuimarishwa majenzi hayo, kwani mpiganaji lazima awe kambini mwake, hiyo inajenga heshima ya jeshi, nidhamu na wakati wowote anapohitajika anapatikana. Aidha, mambo yote ya kijeshi yanabaki kati hali ya siri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, ninaomba kutamka kwa mara nyingine tena kuiunga mkono hoja hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. Ahsante.

MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na wataalam wasaidizi wao wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika mwaka wa fedha uliopita na kwa kutayarisha hotuba nzuri ya Bajeti ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni moja kati ya Wizara nyeti katika nchi yoyote. Majeshi ya nchi yakinumika vibaya inaweza kusababisha hali ya machafuko makubwa nchini au hali mbaya ya ulinzi, na hii itakuwa na matokeo ya kufanya nchi kwa ujumla ishindwe kufanya shughuli za maendeleo kwa wananchi. Kazi za dola zinaweza zikakwama kabisa. Tunayo mifano mingi katika Bara letu la Afrika kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Majeshi yetu kwa kuwa na uzalendo wa hali ya juu na kusimamia katika maslahi ya Taifa na siyo maslahi binafsi. Majeshi yetu ya ulinzi yamekuwa na msaada na ushirikiano wa hali ya juu. Hospitali za Kijeshi zimekuwa mstari wa mbele katika kutoa huduma za afya na matibabu kwa raia. Askari wamekuwa wanatoa huduma za dharura kila walipoona kuna haja ya kufanya hivyo. Ninapongeza Madaktari, wauguzi na wahudumu wote wa Hospitali za Jeshi amba wamekuwa wanafanya kazi yao kwa nidhamu ya hali ya juu. Pia ninawapongeza na kuwashukuru askari wote amba wamekuwa wakitoa misaada kwa raia bila kujali shughuli zao nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hata hivyo, kumekuwa na matatizo yaliyo wazi kwa askari wetu. Hali ya nyumba za makazi kambini ni mbaya sana. Ninampongeza Mkuu wa Majeshi kwa hatua alizochukua za kuanza kukarabati nyumba za aksari na kuboresha mazingira ya nyumba hizo. Eneo la kambi ya Lugalo, Dar es Salaam, ni mfano mzuri. Pamoja na ushauri hii kazi nzuri iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kasi ya ujenzi wa nyumba mpya kwa ajili ya askari wetu ni ndogo mno. Hii inasababisha askari wengi sana pamoja na familia zao kuishi uraiani, tofauti na mategemeo yetu kuwa askari wanaishi kwa pamoja makambini. Matokeo ya hali hii ni kuwa kuna askari wachache amba wamepotoka na kushirikiana na raia wabaya katika kufanya vitendo ya uhalifu. Hawa wachache wanakuwa doa bayaa kwa Jeshi ambalo lina nidhamu ya hali ya juu. Ninashauri kasi ya ujenzi wa nyumba za askari iongezwe, na pale inapobidi, Kikosi vya Ujenzi vya JWTZ na SUMA JKT vitumike katika kazi hii ili kuhakikisha kuwa kazi hii inatekelezwa kwa haraka na gharama ndogo kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nieleze hofu yangu juu ya fujo zinazofanywa na askari wachache wanaopiga raia kwenye maeneo hayo. Fujo zilizotokea Kunduchi Mtongani na Kigamboni, Dar es Salaam ni mfano mzuri. Ninaupongeza uongozi wa jeshi kwa jinsi ulivyojitalidi kuzituliza. Ni matumaini kuwa wale waliohusika wamejulikana na wameshughulikiwa ipasavyo. Ninaomba jitihada zifanywe kuzuia fujo hizo kujirudia. Fujo za namna hii zinakuwa na matokeo ya kusababisha mahusiano mabaya sana kati ya jeshi na raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 1996 nimekuwa nikilalamika juu ya uwanja wa shabaha ulioko Kunduchi, Dar es Salaam. Nimekuwa ninasema kuwa sasa uwanja huo umezungukwa na makazi ya raia, na shughuli za shabaha zinazofanywa hapo zinahatarisha usalama wa raia. Matukio ya raia kuumizwa na risasi zilizopigwa wakati wa mazoezi ya kulenga shabaha yamedhihirika huko Ukonga Dar es Salaam. Nilikuwa nimependekeza kuwa shughuli za mazoezi ya shabaha katika viwanja vilivyo mijini au sehemu ambazo viwanja hivyo vimezungukwa na makazi ya raia zisitishwe na viwanja hivyo vitumike kwa ujenzi wa makazi ya askari. Ningependa Mheshimiwa Waziri aeleze kwa nini jambo hili linachukua muda mrefu hivyo kutekelezwa, licha ya ahadi za Serikali mara nyingi tu kuwa hili jambo lingeshughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wa kawaida na wa vyeo vya chini na kati amba wamestaafu wanayo matatizo makubwa sana ya maisha. Hii imesababisha baadhi yao kwenda nje ya Tanzania kuajiriwa katika Majeshi tofauti katika maeneo yenyе machafuko, na wengine wamefia huko. Siku hizi sio

ajabu kumkuta askari aliyekuwa officer akifanya kazi za ulinzi uraiani. Wengine wanalazimika kushiriki kwenye vitendo vyta uhalifu ili waweze kukidhi haja zao za maisha. Ninashauri utaratibu wa mafao ya askari wastaa fu uangaliwe upya ili kuwapunguzia hawa askari walotumikia Taifa kwa uaminifu wa hali ya juu makali ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kurejesha shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa. Kama mmoja wa waliopitia JKT, ninatambua umuhimu wa JKT kama kisima cha ujenzi wa nidhamu kwa vijana wetu. Ningeshauri kuwa wigo wa vijana amba wanaochukuliwa na JKT upanuliwe ili tuwe na vijana wengi zaidi JKT. Hii ni moja kati ya njia za kutumia nguvu kazi ya vijana ambayo kwa sasa haitumiki. Pia itapunguza uwezekano wa uhalifu wa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima na taadhima, ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mia kwa mia. Ahsante sana.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza kabisa naunga mkono hoja asilimia mia na nawataki Wizara utekelezaji mwema wa malengo waliojiwekea kwa Bajeti ya mwaka 2003/2004. Wazungu wanasema: “*If you want to be left in peace, you should be able to defend yourself*” na “*if you want peace you must prepare for war*”. Nchi za Rwanda, Burundi na Uganda wameingia kiulaini nchini DRC zaidi ya kilomita 100 ndani ya DRC sababu DRC haikuweza kujilinda. Kwa hiyo, naunga mkono kwa Serikali kuongeza Bajeti hii kuwezeshwa jeshi letu kuwa na vitendea kazi vinavyofaa kwa kikabiliana na wanaoitazama nchi yetu kwa jicho la husuda. Ukisoma Biblia, *Ancient and Modern History* hakuna mahali palipoongelewa amani kwa hiyo ni vyema tukajiandaa vyema katika suala la ulinzi na kuwaandaa vijana wetu kwa kupitia JKT.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana kambi zetu za Shinyanga za *Old Shinyanga* na Kizumbi, nyumba za Jeshi ziweze kukarabatiwa na kujenga nyumba zao.

Ombi Maalum ni kwamba naiomba Wizara itoe msaada kwenye ujenzi wa Shule ya Sekondari ya *Old Shinyanga* inayojengwa kwa wapiganaji na wananchi wa Kata ya Chibe fedha hata Tshs. 20 milioni ili kuikamilisha ujenzi huo. Shule hii itasaidia sana watoto wa wanajeshi kusoma karibu. Kwa sasa kila siku wanasona kilomita 15. Kutoka *Old Shinyanga* hadi Mjini Shinyanga. Naomba sana jeshi lisaidie ujenzi huo.

Pia naomba jeshi wawapatie wapiganaji wetu wa Kambi ya *Old Shinyanga* Mabasi ya kutosha na kwa kuwa hakuna nyumba za kutosha pale *Old Shinyanga* wapo wapiganaji wengi wanaishi mjini Shinyanga. Naomba Serikali ikamilishe ujenzi wa shedi za kuhifadhi mizinga pale *Old Shinyanga* ili kulinda na kuhifadhi mizinga na vitendea kazi za jeshi letu. Shedi hizi zilianza kujengwa miaka ya 1979 na hazikumalizika utaratibu wa kufunika kwa turubai wakati mwinci ya maisha mapema na hasa wakati wa mvua mizinga hii inaweza kuharibika.

Magari makubwa na *Lowloader* pale *Old Shinyanga* ni vyema vikawepo vyta kutosha. Vita havina macho na wala huwezi kujua adui anaweza kushambulia lini. *Lowloaders* na magari makubwa ni vyema vikawepo vyta kutosha. Vitendea kazi vya majini ni vyema vikaimarishwa, kwa kuwa nchi yetu imezungukwa na bahari na maziwa, ni vyema kukawepo vitendea kazi vya kutosha (Meli) kwa maziwa yote pamoja na bahari zetu zote. Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi. Suala hili ni muhimu sana. Pamoja na kuwa viongozi wetu wanaweka ujirani mwema katika majira yetu lakini ni sharti tuijandae kikamilifu kuweka mikakati, misingi na vitendea kazi vya kijeshi vya kuweza kujikumu endapo tutashambuliwa.

Mikopo na mafao ya wanajeshi ni muhimu sana. Kila wakati Serikali inapopata fedha ni vyema kuboresha mapato (mishahara) ya wapiganaji. Pia mikopo ya magari na vifaa wakapewa wapiganaji wetu kwa bei nafuu na kadhalika. Aidha ninaipongeza Serikali Wizara kwa kututakia suala la unifomu kwa ujumla kwa kudhibitiwa ninaamini ni vyema suala hili likazidi kuboreshwa.

Mheshimiwa Waziri nimeandika barua mara nyingi kuhusu mafao ya Mwanajeshi mstaafu. Naomba usaidie hata majibu. Naunga mkono na Mola awabariki kwa kutekeleza malengo mloliojiwekea katika Bajeti yenu ya mwaka wa fedha wa 2003/2004.

MHE. BEATUS R. MAGAYANE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamba kumetokea mapigano katika kijiji cha Malenga Wilayani Kibondo kati ya wanajeshi wetu wamerushiana risasi na wanajeshi wa Burundi tarehe 27 Julai, 2003, watu watatu wamejeruhiwa sana.

MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Prof. Phillemont Sarungi, Mbunge, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, hasa kwa kuwa karibu na sisi Waheshimiwa Wabunge. Nampongeza sana Jeneral George Waitara Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Pongezi kwa ndugu yangu Comrade Vincent Mrisho Katibu Mkuu, kwa uzoefu alionao katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza mno Serikali hii ya awamu ya tatu, kwa kurudisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa JKT. Ni chombo muhimu sana kwa Taifa letu kwani kinaleta umaja, huleta Utaifa na kuondoa udini. Kwa muda tulioondoa mafunzo ya JKT Taifa lilikwenda kombo. Naomba usawa kwa mgao wa nafasi za kujunga na JKT zitolewe kwa usawa kila Wilaya, kila Mkoa na msisitizo uwe ni huo. Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wawe mbele kulinda umaja wa Taifa letu.

MHE. FRANK M. MUSSATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Prof. Phillemont Sarungi, Mbunge, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu, Bwana Vincent Mrisho, Jeneral George Waitara, Makamanda na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri iliyofanyika katika kipindi cha 2002/2003. Ninawaombea mfanikiwe zaidi mwaka 2003/2004. Hata hivyo, ninaomba Wizara izingatie yafuatayo:-

Uimarishaji wa ulinzi mipakani, hususani Mkoa wa Kigoma kuna Vituo kadhaa mpakani Mkoani Kigoma ambavyo vinasimamiwa na Askari wa *TPDF*. Vituo hivi vina kazi kubwa kiulinzi na kiusalama, lakini havina Askari wa kutosha na vitendea kazi kama vyombo vyaya usafiri na mawasiliano. Ni vyema Serikali ikahakikisha kuwa mipaka inalindwa vyema kwa kupeleka Askari wa kutosha na kuwapa hao Askari vitendea kazi ili waweze kutimiza wajibu wao. Uchache wa Askari mpakani ni moja ya sababu inayofanya watu wabaya kutoka nchi jirani za Kongo na Burundi kuingia nchini kwetu wakiwa na silaha nzitonzito.

Katika kuwezesha mradi wa Nyumbu, Serikali ichukue hatua za makusudi kuwezesha kituo hiki muhimu kutimiza malengo yake ya kiutafiti katika suala la magari. Hii ni moja ya Taasisi alizoanzisha marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na hivyo Serikali lazima iiwezeshe kwa kuipatia fedha za kutosha ya utafiti ili kutambua na kuenzi mambo mazuri aliyooyafanya huyu muasiswa, Marehemu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utulivu, Tanzania ni tulivu kutokana na tabia ya raia. Jeshi tulivu lenye utii na nidhamu kwa Serikali yake. Pongezi nyingi zitolewe kwa wana JWTZ nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi na majukumu wakati wa amani. Kipindi hiki suala la uzalishaji mali lichukue nafasi kubwa. Jeshi la JWTZ na JKT, Idara za ushirikishwaji vyombo vyake vyenye sura ya uimarishaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutoa vifaa vya ujenzi na ukarabati. Vikosi vya Uhandisi mfano KJ 121 wakiwezeshwa kwa vifaa vya ujenzi wa barabara. Hivi sasa wanajitolea sana kujenga barabara zao kule Ngerengere. Naomba sana Mheshimiwa Waziri ukisaidie kikosi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za vikosi vya Ngerengere, Kidugallo, na Kinonko. Nyumba za juu bati chini, bati zimepitwa na wakati. Naomba tutumie vikosi vya ujenzi vijengee nyumba za vikosi. Nyumba za mabati zote zibomolewe kesho na ujenzi uanze mara moja.

MHE. SUMRI A. S. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na naunga mkono kwa asilimia mia moja Makadirio ya Bajeti yake kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyejua kuwa hii Wizara ni nyeti na yenyе maadili ya uaminifu, inayolinda mipaka yetu na watu wake. Pongezi tele kwa Wizara na wanapiganaji wetu. Mimi binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Mpanda Magharibi tunajua vizuri sana umuhimu wa majeshi yetu, hasa kwa wanavijiji wa kando ya Ziwa Tanganyika, katika vijiji vya Karema, Ikola, Kasanga Tongwe, Isengule na Kaselamyange.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa shukrani za dhati kwa kikosi kidogo cha Askari wetu wa JWTZ waliopo Ikola; lakini tunazidi kuiomba Wizara iongeze idadi ya Askari na kutupa msaada wa speed boat ili waweze kupambana na ujambazi uliokithiri kuititia Ziwa Tanganyiaka toka *DRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni juzi juzi tu, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa kuna wananchi walipigwa risasi na majambazi ndani ya Ziwa hilo. Bi Elizabeth Samwel mwenye umri wa miaka 26 aliuawa, nahodha wa boti Festo Chunda alipigwa risasi. Wengine ni Anastazia Christopher na mtoto Paulo Chunda mwenye umri wa miaka miwili wamejeruhiwa. Tukio hilo ni la tarehe 23 Julai, 2003, wakiwa safarini toka Kabwe kuja Karema. Hivyo tunazidi kuomba boti kwa ajili ya Patrol.

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu za awali kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Makamanda wa vikosi mbalimbali wanaoviongoza vikosi vya ulinzi, wataalamu na watendaji wao wote wanaoshirikiana nao katika utendaji wao wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa pongezi za pekee Mkuu wa Jeshi la Ulinzi hapa nchini Generali George M. Waitara na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jeneral Davis Mwamunyange kwa utulivu wao wa hali ya juu na kutekeleza wajibu wao katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maaskari wetu wengi wanapata usumbufu wa makazi ya kikambi na nyumba za kuishi, lakini kwa jitihada zilizofanywa na Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi imeweze kukamilisha ujenzi wa nyumba za kuishi zisizopungua familia 90. Hili ni jambo la kujivunia sana kwa kuweza kukamilisha hatua hiyo ambayo ni kubwa sana katika utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ulinzi wa nchi yetu ni suala ambalo halitaki mzaha kwani hivi sasa nchi yetu imezungukwa na nchi ambazo zimo katika migogoro ya wenywewo kwa wenywewo, lakini hatma yake wananchi wao huanza kukimbilia kwenye nchi yetu na si hao raia tu bali hata baadhi ya Askari hao wa nchi jirani huingia nchini kwetu na kuanza kupora mali za raia, bila ya kuwa na uwezo na utekelezaji mzuri basi panawenza kutokea mapigano yasiyo na ulazima kama jeshi halitokuwa makini kutuliza hali zilizomo mipakani mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira mara nyingi ajira za Jeshi zinafanya Tanzania Bara tu kama vile Tanzania Visiwani hakuna vigezo vya kuwaandikisha Askari kwa upande wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufanywe utaratibu wa kuweza kuwaandikisha Askari kule kule Zanzibar kwani ni rahisi zaidi kwa vijana wetu kuweza kutekeleza yale yote ambayo atatakiwa ayafanye kuliko kumuweka ugenini wakati wa kuandikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Prof. Phillemont Sarungi Mbunge, na watalaam wake kwa kutayarisha hotuba hii nzuri. Naanza kwa kuunga mkono hoja, na kuchangia au kupongeza juhudhi zifuatazo:-

- (a) Ulinzi wa mipaka yetu yote, juu ya kuwepo kwa upungufu wa vifaa vya kutendea kazi.
- (b) Nalipongeza Jeshi letu kwa namna linavyohakikisha kuwa amani na utulivu unakuwepo nchini na kulinda uhuru wetu ni dhamana kubwa waliobeba.
- (c) Waasi kutoka *DRC* na Burundi wanaoingia nchini wanadhibitiwa na *JWTZ*, ninawapongeza kwa hili.
- (d) Ninawapongeza kwa juhudhi za ulinzi wa mipaka yetu pamoja na eneo la Bahari ya Hindi.
- (e) Huduma zinazotolewa na Hospitali za Kijeshi zimewanufaisha wengi, naipongeza Wizara kwa kuziangalia vizuri.
- (f) Ununuzi wa ndege mbili aina ya *Y-8* ni hatua kubwa ya kimaendeleo. Vilevile kuna umuhimu kuwa na *helicopter* kwa ajili ya shughuli mbalimbali.
- (g) Ninaipongeza Wizara kwa kujenga muundo mbinu wa Serikali Elektroni(*E - Government*). Ni hatua kubwa kwani (*E - Government*) nchi za Magharibi nyingi kwa sasa wana paperless office hawatumii mafaili badala yake wanatumia computers kwa mawasiliano na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusambazwa kwa kondomu isiwe ndio licence ya kufanya ngono nje ya ndoa. Tuepukane na zinaa ni njia mbaya ya kupita. Ningelishauri Kiwanda cha Madawa cha *TANZANSINO* kutengeneza madawa ya kurefusha maisha ya walioathirika na UKIMWI Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Askari wetu sana kwa uzalendo na subira walionayo. Ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. BERNARD K. MEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Phillemont Sarungi pamoja na watalamu wake kwa kazi nzuri sana walioifanya ya kuleta hotuba yenye uchambuzi yakinifu. Napenda niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu ni nguzo kuu ya heshima ya Taifa letu. Usalama, amani, utulivu na ulinzi wa nchi yetu unalitegemea Jehsi letu la Ulinzi. Lakini Jeshi imara lazima liwe na vifaa vya kisasa vinavyokwenda na wakati. Tumeanza kuona jinsi *Air Force* inayotakiwa kuwa na *helicopters* za kisasa za kivita. Pia tunajifunza umuhimu wa kuwa ni *fighter planes*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Jeshi letu lipewe fedha za kutosha za kununua vifaa na zana za kivita vinavyofanana na wakati tulionao. Katika kipindi cha miaka 40 iliyopita, Jeshi letu liliweza kuipa heshima nchi hii, heshima ya kuogopesha Bara zima la Afrika na dunia kwa ujumla lilishuhudia ushujaa wa jeshi letu lilipoyaondoa majeshi ya Iddi Amin kutoka Tanzania na kusambaratisha Serikali yote. Dunia haiwezi kusahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tulijenga Jeshi letu upya, ndivyo inavyokuwa popote pale duniani. Kila baada ya vita, jeshi halina budi kujengwa upya. Hatujalijenga Jeshi letu upya, tulijenge

Jeshi letu upya. Tufanye kila linalowezekana kulifanya Jeshi letu upya. Tukifanya hivyo, Taifa litakuwa salama majirani hawatatushokoza, na heshima ya nchi yetu itakwendā juu. Naunga mkono hoja hii.

MHE. EDWARD N. LOWASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na pia naipongeza Wizara kwa kazi nzuri. Kipekee napongeza hatua yenu ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za Asakri pale Sofa Monduli. Hongereni sana, maana jambo hili lilikuwa kero ya muda mrefu sana.

Pili, nampongeza Meja Jenerali Kimonge wa *TMA* kwa jinsi walivyosimamia suala la maji ya *TMA* na sasa hali imekuwa ahuensi. Hata sisi wakazi wa Monduli sasa tunapata mgao wetu. Tafadhalii Mkuu huyu apongezwe sana, maana hili nalo lilikuwa kero ya muda mrefu.

Mwisho, kuna mgogoro unaonukia juu ya ardhi ya JWTZ katika Jimbo langu. Jambo hili ni la muda mrefu na pengine makosa yapo pande zote kwa wanavijiji waliovamia maeneo ya JWTZ na kwa viongozi wa Jeshi ambao ama walishiriki au walikaa kimya! Kwa hiyo nashauri jambo hili lishughulikiwe kwa maelewano na mashirikiano bila raia kutishwa, kuonewa maana JWTZ ni Jeshi la umma na nchi yetu inaheshimu sana haki na wajibu wa raia wetu.

MHE. ABU T. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa ningeomba niipongeze Serikali yetu kwa kujizatiti kwake kurejesha Makambi ya JKT. Naamini sasa nidhamu ya Taifa letu na uzalendo sasa utarudi kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kuzorotesha kwenye miaka ya 80, 90 na mapema miaka ya 2000. Ulinzi sasa kikaya hadi kitarafa utarejea kwa ubora wake kama ilivyodhihirishwa kwenye vita ile iliyomng'o Nduli Iddi Amini madarakanii.

Ni mategemeo yangu ya dhati kabisa kuwa sasa kwa kujizatiti zaidi kwenye kambi zetu za JKT tabia mbaya ya vijana wetu kuingia kwenye madawa ya kulevyia na uhalifu kwenye jamii pamoja na kuwaelimisha katika makambi hayo nguvu kazi, basi utulivu, amani, upendo na mashirikiano kwenye Taifa letu vyote hivyo vitaendelezwa na kudumishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa na Elimu Kazi inayotolewa na JKT, kama ilivyodhihirishwa kwenye sherehe zile za miaka 40 zilizofanyika JKT Ruvu ambapo mimi pia nilishiriki. Kikosi cha ujenzi pamoja na kile cha kilimo kilinipa faraja sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ajira kubwa iko kwenye ardhi, hususan kilimo ambapo asilimia 80 ya watu wetu wako kwenye kilimo, nashauri hivi sasa JKT, ingetumia nyenzo, mali na uhusiano wake wote, na asilimia kubwa zaidi ya uwezo wake kwenye sekta ya kilimo, kambi zetu nyangi ziwe za kilimo, kambi hizo zipewe hadhi kamili ya Vyuo vya Kilimo na angalau kambi hizo zitoe vyeti vya kilimo *Certificate in Agriculture and Animal Husbandry*. Ili wahitimu waweze kutumia Elimu hiyo moja kwa moja baada ya kuhitimu. Baada ya hilo basi emphasis ielekezwe kweney elimu ya Viwanda vidogo vidogo. Ni muhimu JKT na Wizara nzima ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kujenga ushirikiano kamili na Wizara zingine, kama vile Wizara ya Kilimo na Chakula, *VETA* Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Wizara ya Ujenzi. Kwa kujiwesha kutekeleza malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Prof. Phillemon Sarungi, Mbunge pamoja na safu yake nyote ya uongozi kwenye Wizara yake kwa maandalizi mazuri ya hoja yenye uwazi wa kufungua jicho kwa wananchi kwa jumla na umahiri na umuhimu mkubwa wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. LEPHY B. GEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwa kweli kuna matatizo ya Bajeti kuwa finyu. Hivyo, kusababisha mambo mengi kukwama yanayohusu maslahi ya wapiganaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa Jimbo langu. Katika Jimbo langu la Mapanda kati ninao wastaafu wengi waliokuwa wanajeshi katika ngazi mbalimbali, na wamestaafu katika miaka mbalimbali. Kinachosikitisha ni kwamba toka walivyostaafu wameendelea kudai kiinua mgongo chao, lakini hakuna mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili lilifikishwa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hili la Mpanda Kati Mheshimiwa Mbogo na mimi vilevile nimeliendeza. Nilimwandikia Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Prof. Philomen Sarungi alijibu barua hiyo yangu ya kwanza na kuahidi kwamba angeweza kulishughulikia suala hilo mapema sana mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoona muda unazidi kwenda niliamua kumkumbusha kwa barua ya pili, kumbukumbu ninazo. Cha kusikitisha Mheshimiwa Waziri hakutaka kujibu wala kujali kuniarifu kuwa aliipata barua, nilimkumbusha tena lakini hakuna mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielewe hivi ndiyo utendaji na utawala bora huu! Naomba Mheshimiwa Waziri atoe maeleo nini hatma ya wanajeshi wastaafu wa ngazi mbalimbali ambao wameendelea kuumia muda mrefu bila kulipwa wanachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natarajia kama suala hili halitatolewa maeleo ya kutosheleza, nitamwomba Mheshimiwa Waziri akubali kwa gharama zangu niwalete wastaafu wote katika Ofisi yake ili aweze kuzungumza nao, pengine hii itasaidia kwa sababu Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu wa angalau kutoa majibu kwa njia ya barua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu zote zipo na Makao Makuu ya Jeshi kumbukumbu hizo wanazo. Naomba Mheshimiwa Waziri suala hili alipe umuhimu wake unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuchangia katika hoja iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda nichukue fursa hii kwa moyo wangu wa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Prof. Phillemont Sarungi Mbunge, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu wa JWTZ, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, na Makamanda wote pamoja na wasaidizi wao walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa makini na umahirini mkubwa. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Sasa naomba kutoa mchango wangu kwa lengo la kuboresha na kujenga katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya Jeshi la Ulinzi. Tuanfahamu kuwa mipaka yetu na anga zetu ni mikubwa. Kwa hiyo huwezi kusema kuwa kuna wakati wa amani, hasa ikizingatiwa kuwa tumezungukwa na nchi zenye migogoro ya kupigana wenyewe kwa wenyewe. Hata hivyo, wakati ambapo hakuna mapambano ya moja kwa moja, uwanja wa matumizi ya jeshi letu bado ungeweza kupanuliwa zaidi ili Jeshi hili lijiingize zaidi katika maeneo ya uzalishaji, hasa viwanndani, ujenzi wa barabara, madaraja na majengo mbalimbali kwa kutumia uzoefu wao. Fedha zinazotumika kuwalipa wakandarasi wanaodai hongo ya asilimia kumi zingetumika kuwapa kazi za kutosha wanajeshi wetu. Nashauri kufanyike utafiti kuona na kubaini maeneo ambayo wanapiganaji wetu wanaweza kuzalisha mali kwa lengo la kuuza humu nchini na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ninalopenda nichangie ni lile la kubadili utamaduni wetu. Kwa ujumla Watanzania tunalo tatizo la ujumla la kupungukiwa na *maintenance culture*. Hali hii tuliiiona katika baadhi ya majengo mengi ya jeshi tulipotembelea Chuo cha Kijeshi Monduli, ni vyema majeshi yetu yakawa chachu ya kubadili utamaduni huo usiokuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwenye Chuo cha Monduli yapo majengo ambayo yalibomoka kutokana na tetemeko la ardhi, nashauri na ingekuwa jambo la maana kama wataalam wa masuala ya Giolojia ya tetemeko la ardhi wangekuwa wanashauriwa kabla ya kuamua maeneo ya kujenga majengo mazito, kwa lengo la kuepusha madhara kwa watu na mali. Ikumbukwe kwamba maeneo ya Bonde la Ufa yana mikondo mahsusisi inayothiriwa kila mara na tetemeko la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya majeshi yetu ni hazina kubwa sana ya uhai wa Taifa hili. Nchi zote duniani hususan uheshimu na kuogopa kuingilia maeneo ya mafunzo ya kijeshi kwa sababu ya unyeti wake. Maeneo hayo ni muhimu kwa ajili ya mafunzo na mazoezi ya kila aina ya wapiganaji. Sasa kuna maeneo haya yanamegwa na kupewa matumizi mengine, hali hii ni sawa na kuamua kuondoa shughuli za mafunzo na mazoezi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili ni kubwa kule Monduli, hata hivyo, kuna tatizo la kuvamia maeneo ya majeshi na lipo pia katika sehemu nyingi hapa Tanzania. Nashauri Serikali ifanye tathminni kuhusu hali ya uvamizi na hatimaye kuchukua hatua za kudhibiti hali hiyo.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu JKT. Jeshi hili linafanya kazi nzuri na limeanza kurudisha kwa kasi imani ya Watanzania kuwa mawazo na fikra za waasisi wa Taifa hili zinaendelezwa. Ili jeshi hili liwe Jeshi la Kujenga Taifa kwa vitendo, inabidi lipanuke kutoka kwenye makambi na kwenda ngazi za vijiji ili kujenga nidhamu ya kazi katika ngazi hiyo. Vijijini ndiko kwenye shughuli nyingi na vijana wengi wasio na kazi wanaishi huko, wanachohitaji ni oganaizesheni, uongozi na uelekezwaji mambo ambayo yanakosekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia Jeshi hilo lianze kuwashirikisha wanavijiji waliopo karibu na makambi hayo kufanya yale ambayo yanatakiwa katika ujenzi wa Taifa. Kwa hiyo nimefurahishwa na hatua ya JKT, Kambi ya Makutupora ya kushiriki katika kuweka Mji wa Dodoma katika hali ya usafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, JKT washirikiane kwa karibu sana na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ni vyema pakawepo na utaratibu wa pamoja katika maeneo yanayoingiliana. Vilevile sera za asasi hizo zihuishwe ili kuleta ufanisi.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri na Makamanda wake kwa kazi nzuri ya kuimarisha Jeshi. Nadhani miaka 15 ijayo itakayotumika kutekeleza uliyoyaandaa ni mingi sana. Nakuomba Mheshimiwa Waziri iwepo mipango ya muda mrefu na muda mfupi. Tunahitaji vifaa bora sasa na kesho ili kazi ziendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya kuboresha Hospitali ya Jeshi ni muhimu. Nakupongeza sana. Lakini naomba hospitali ya Lugalo iwe nje ya eneo la *Barracks* katika eneo hilo hilo, lakini si kama ilivyo. Hii iliyopo ibaki kwa wanajeshi peke yao. Ile ya nje iimarishwe kama Jeshi ya rufaa kwa wanajeshi na wananchi hasa viongozi wake. Mipango ya ujenzi ielekee na Waheshimiwa Wabunge tutakuunga mkono. Uadilifu wa Askari utasiadia kutiba wananchi ambaa huenda wangekwenda nje. Tafuta msaada nje na omnia Serikali ianze kazi njema hiyo. Wananchi wamejenga imani kwa Madaktari wa Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha makazi ya Askari ni muhimu. Naomba JKT kikosi cha ujenzi waanze kujenga nyumba chache chache kwa kujitolea. Utapata kazi ndogo za kununua vifaa vya kumalizia nyumba. Tumia ujuzi na nguvu za vijana wa JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya diplomasia yafundishwe kwa Majenerali wote wasome wafuzu. Ni akiba kwao wakiwa nje ya Jeshi baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maaskari wa vikosi vya majini wapate vifaa vya kisasa ili kazi yao iwe rahisi majini, sote tunajua adha ya ujambazi wanaoufanya wabaya wetu majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana 1611 waliojiunga na JKT ni wachache mno. Mmomonyoko wa maadili ni mkubwa. Dawa ya kuwaponya vijana wetu ni JKT. Naomba Serikali iongeze vijana wengi zaidi kuokoa nchi yetu. Serikali iangalie umuhimu wa kuongeza vijana JKT kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu wa kuwafundisha kuzalisha mali naomba wafundishwe namna ya kutafuta masoko ndani na nje ya nchi. Ushindani wa siku hizi ni mkubwa. Vijana hawa wanaweza kuandika Tanzania katika ramani ya dunia kwa mazao yetu mazuri.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa maendeleo ya shule ya Makongo. Shule hiyo ni nzuri inafundisha vizuri. Upungufu kwa Taasisi hiyo ni kawaida ikiwezekana ianzishwe shule nyingine Makambi kidogo kidogo. Naunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Prof. Phillemor M. Sarungi, Katibu Mkuu, Mkuu wa Jeshi la Ulinzi na Watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba ya bajeti hii yenye mwelekeo wa kuimarisha Jeshi la Ulinzi nchini kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niitumie pia nafasi hii kuwapongeza vijana wote nchini hususan vijana wa Mkoa wa Singida waliojitolea kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa bila kujali kuwa watapata ajira au sivyo. Kitendo hiki kimeonyesha uzalendo wa hali ya juu kwa kuongeza nguvu na idadi ya wanajeshi wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uzalendo huu walioonyesha vijana wengi, kumekuwa na vikwazo vidogo vya kuwafanya vijana wengi kutokuchaguliwa pamoja na sifa nyingi kuwa nazo kutokuchaguliwa kwa sababu eti umri umezidi kwa mwezi mmoja, kikwazo ambacho kinawavunja moyo vijana wengi. Naiomba Serikali iondoe masharti yasiyokuwa ya muhimu ili Taifa lipate mashujaa wenye moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa utaratibu wake wa zamani ambao uliwataka vijana wote waliomaliza mafunzo mbalimbali au kozi mbalimbali kijiunga na JKT, lakini baadaye ukasitishwa. Naiomba Serikali irudishie mpango huu kwani ulikuwa unawaandaa vijana kwa ulinzi wa familia zao hapo baadaye na Taifa kuwa na walini wengi waliopata mafunzo kwa maslahi ya nchi na kuwa na watumishi wakakamavu na tayari wakati wowote kwa lolote ambalo linaweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda nizungmzie suala la wanajeshi kuoa ama kuolewa kwa kufuata taratibu za Jeshi. ; mwanajeshi huoa ama kuolewa baada ya miaka sita, utaratibu ambao unamnyima haki ambayo tulipewa na Mwenyezi Mungu. Naiomba Serikali ilegeze sheria hii wanajeshi waruhusiwe kuoa ama kuolewa baada ya miaka mitat kwa kuwa kipindi tulichonacho sasa hivi ni kigumu kutokana na janga la UKIMWI ni vigumu sana vijana kutawala nafsi kwa kipindi chote hicho cha miaka sita. Kwani ibilisi wa mtu ni mtu inawezekana vijana (wanajeshi) wengi wakapata maambukizo kwa ajili ya kukosa unyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi mkubwa na utoaji wa sare za wanajeshi kwa sababu mara nyingi majambazi yanapokamatwa huwa wameva sare za Jeshi. Je, huwa yanapata wapi? Naomba ulinzi wa utoaji wa sare uimarishwe na adhabu kali itolewe kwa ye yeyote anayepatikana na sare za Jeshi kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niungane na wenzangu waliochangia kwa mazungumzo kwa kuiomba Serikali iboreshe mazingira ya Wanajeshi mfano ardhi pana ya kufanya mafunzo yao, nyumba za kuishi, kujengwa zaidi au kukarabatiwa na bila kusahau suala zima la maji na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ikumbukwe wanajeshi hawa kazi zao ni ngumu sana hazilingani hata na mishahara yao. Naiomba Serikali itazame upya viwango vyao vya mishahara kwa lengo la kuboresha pamoja na posho zao ninaamini itakuwa ni changamoto kubwa sana kwa wanajeshi kuipenda kazi yao. Wasiwasi wangu wako wanajeshi wanaojiunga na vitendo vibovu kwa sababu ya ukata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna habari za kuaminika kuwa majambazi wengi hukamatwa wakiwa na silaha za Serikali suala ambalo linadhalilisha Jeshi letu, naomba Serikali iweke mikakati mikali na adhabu kali kwa yejote anayekutwa na silaha ya Serikali kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanajeshi wastaaafu ambaao bado wanaidai Serikali mafao yao baada ya kustaafu. Naiomba Serikali iwawekee mazingira mazuri ya upatikanaji wa mafao ya wanajeshi mara wanapostaafu. Ninasema hivi, kwa sababu wapo wastaaafu ambaao bado hawajalipwa mafao yao mpaka leo suala ambalo limekuwa kero kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu ambaao nina hakika Mheshimiwa Waziri Mzee wangu Prof. Phillemon Sarungi atanijibu wakati wa majumuisho yake, nitamke rasmi kuwa naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Nawatakia utekelezaji mwema na maisha marefu wakidumisha mshikamano.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimi Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya ya Wizara hii nyeti ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwanzo nauelekeza katika kikosi cha wanamaji, kikosi ambacho tunakitegemea sana katika fani zao za kiufundi, naomba kikosi hiki kiongezewe nyenzo hasa mtaji ili kiweze kupiga hatua zaidi ya kilipo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Radar vya Kikosi hiki viimarishwe zaidi hasa katika huduma nzuri ya vyakula, lakini pia vingeboreshwa zaidi katika mitambo ya kisasa katika Karne hii ya 21. Ninamaanisha kurutubisha zaidi ulinzi wa uchunguzi wa baharini kuna umuhimu mkubwa sana, hasa kwa kuzingitia jiografia yetu. Suala la umeme katika Kituo cha 2 na Radar Station cha Potoa Zanzibar, sielewi kwa nini halipatiwi ufumbuzi. Kwani kutumia jenereta ni ghali zaidi ukilinganisha na kuvuta umeme ambaao haupo mbali na Kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Wizara tuipongeze sana katika kuboresha huduma za afya ndani ya Jeshi letu, kwani sio siri kazi inaonekana bayana, hata kwa kuwa na Madaktari wenye ujuzi wa juu, pamoja na sifa hizi lakini huduma ya kusambaza madawa katika hospitali uongezwe kwani raia pia wamekuwa wanakimbilia huduma nzuri za Jeshini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hekima ya Jeshi itapanuka zaidi pale ile hospitali ya Bububu Zanzibar itakapokuwa imepanuliwa na kufikia kiwango cha Kitaifa hasa ukizingatia inategemewa zaidi na viongozi wa Kitaifa. Jeshi letu limejitahidi sana katika upande wa sare, tunalipongeza, lakini pia liangalie upande wa wanajeshi katika huduma za usafiri, hivyo naishauri sana Serikali itenye fedha kwa makusudi katika ununuzi wa magari hasa mabasi kwa ajili ya wapiganaji. Jeshi letu limepata sifa kubwa katika mazoezi ya pamoja na Ufaransa. Hii inaonesha vijana wetu wanavyowajibika upande wao, hivyo nampongeza Jeneral George Waitara na maafisa wote na wapiganaji kwa jumla kwani wametuwalisha vizuri katika medani ya kivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi katika Jeshi kuna mpango maalum wa kustaafu kwa umri, hivyo wapo Maafisa wenye hekima kubwa wanakwenda uraiani. Mimi naishauri Serikali pamoja na kustaafu kwao lakini waangaliwe sana kwa kuwatumia kama hazina za nchi kwani utaalamu wao mkubwa ipo siku tutauhitaji. Lakini bado namshauri Mheshimiwa Waziri awaandalie klabu yao ambayo itawakutanisha mara kwa mara. Nachukua fursa hii kuwatakia maisha mapya ya uraiani wale wote walioagwa hivi karibuni. Jeshi lazima likae pamoja na kuandaa makongamano ya kuelimishana juu ya gonjwa la UKIMWI kila baada ya muda mfupi, kwani imekuwa pigo kwa Jeshi kwa kupoteza wataalamu muhimu sana.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kauli, maandishi na wote

waliochangia kwa kutoa ushauri na mapendekezo nje ya Bunge, michango yao imezingatiwa kwa umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Semindu Pawa kwamba unapofanya kazi katika taasisi fulani lazima uendane na hali ya taasisi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijeshi mkubwa wako akikuambia kitu lazima useme: “Ndio Afande” na akikutuma fanya kitu fulani: “Ndio Afande” maelezo ni baadaye. Kiraia ni tofauti kwanza utafute maelezo mengi ndipo ufanye. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kusema kwamba ninatoa ahadi ambazo hazitekelezeki, nafikiri hapo ameongeza chumvi kidogo na nia yake ilikuwa ni nzuri. Mimi kama kiongozi, kama Mbunge mwenzenu ninayeongoza Wizara hii ni watumishi wa wananchi, Waheshimiwa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi na wananchi ndio waajiri wetu. Kwa hiyo mkituambia kitu ama mkituuliza maswali hakuna negative, hapana kwanza unakubali “Ndio Afande” baadaye uthalifanya kazi na tulilifanya kazi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijitabu hiki...

(Hapa Kitabu Husika Kilionyeshwa kwa Wabunge Kama Kielelezo)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Majibu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujensga Taifa, hoja na maswali mbalimbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kila Mbunge mmoja mmoja tumeeleza na sababu yake. Sasa sijui mwenzangu amesoma lakini nasema bahati mbaya kama imetokea kuna kitu ambacho tulitoa ahadi hatujatekeleza basi tuonane.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kuhusu hilo, suala la Jeshi la Ulinzi unakwenda na utaratibu, sheria na kanuni zake. Unaweza kukubali kwa mfano Mheshimiwa Semindu Pawa alinialika kwenda kutembelea makambi yake sikuwa na nafasi ningesema hapana lakini baadaye ningepata nafasi niseme ndio angeniona ni mtu wa ajabu sana. Kwa hiyo, kwanza nakubali, nakwenda kuandaa baadaye ndio nakwenda. Kwa hiyo, naomba anielewe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kuwa michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge itaimarisha na kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kuliwezesha Jeshi letu liwe la kisasa na kuweza kutimiza majukumu yake kulingana na hali ya maendeleo duniani kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamechangia lakini michango hii ya Waheshimiwa Wabunge inashiria jinsi Waheshimiwa Wabunge wanavyothamini na kuwa na imani kubwa na Jeshi hili kwa kupitia Wizara. Kwa hiyo, nawapongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba niwatambue waliochangia kwa kauli. Naomba kwa heshima na taadhima nimirambue Mzee wangu, mwenzetu, mzalendo, kiongozi wetu aliyebobea, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ulinzi na Usalama, Dr. John Samwel Malecela. Mimi mzee huyu alikuwa Waziri wangu Mkuu nimefanya naye kazi nilikuwa chini yake kama Waziri amenilea vizuri sana na kati ya watu 10 mashahuri duniani ye ye ni mmojawapo. Kwa hiyo tuna hazina kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwininge ni Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waziri Kivuli, Mheshimiwa Anne Kilango (Malecela), Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Khamis Aweso Aboud, Mheshimiwa Juma Suleiman N’hunga, Mheshimiwa Ibrahim W. Marwa, Mheshimiwa Omar Juma Khatib, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa, Mheshimiwa Beatus R. Magayane, Mheshimiwa Ruth Msafiri na mwisho kwa uzito na umaarufu wake ni Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Abu Kiwanga,

Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Fatma Said Ali (Mchumo), Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro.

Wengine ni Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Kanali Feteh Mgeni, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Paul Ntwina; Mheshimiwa Mariam Faki, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Khadija Ngozi, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa Khatib Ameir, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Sumri Mohamed, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Abdullatif Esmail na Mheshimiwa Bernard Membe. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa nchi ni jukumu lenye gharama kubwa sana kwa maana ya kujenga uwezo wa kiulinzi ulio madhubuti na Tanzania tumejinyima sana, Jeshi letu lina heshima kubwa sana, nitasema baadaye. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa linahitaji kutumia rasilimali nyingi kwa ajili ya kununulia Jeshi letu vifaa, zana za kisasa pamoja na kuajiri vijana amba ni nguvu kazi. Lakini la muhimu ni kuwatunza na kuwafundisha Wanajeshi wetu katika fani mbalimbali za kimapigano na za kitaaluma ili wawe na uujuzi na maarifa kulingana na hali halisi ya dunia. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa : "Kupanga ni kuchagua", tuchague kujenga nyumba haraka haraka haya mambo mengine tuyaweke pembeni, tuko tayari? Kwa hiyo, mmenielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mzee wangu, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi, Mheshimiwa Malecela kwa sababu amekuwa mstari wa mbele kutetea Jeshi hili. Kuna wakati hata bajeti imeshapita amehakikisha tunapata fedha za ziada, Mzee nakushukuru sana. Maelezo na mapendekezo ya Kamati yake tumeyazingatia na ndio yatakuwa dira ya utekelezaji. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Majenerali Wastaafu, napenda kuliarifu Bunge lako kwamba suala hili litajumuishwa katika mijadala ya Sera ya Ulinzi ili utaratibu mzuri na unaoeleweka utolewe na kutekelezwa na utolewe tamko. Hatuwezi kujibu hapa kwa sababu hiyo ni sera. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ardhi, namshukuru sana Mheshimiwa Lowassa, sijui yupo, ametusaidia sana kule Monduli na Jimbo lake sasa Wanajeshi wanapata maji na aliwaahidi atashirikiana na sisi atawapelekea maji na maji yamekwenda, huyu ni Askari wa Mwavuli, nakushukuru sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la ardhi, malalamiko hayo tumeyapocea na Wizara italifanya kazi suala hili tutakaa pamoja na mamlaka zote zinaohusika kuna Mikoa na Waziri wa Ardhi. Jeshi halitaki kugombana na wananchi lakini wakati huo huo na wananchi pia waelewe ardhi ya Jeshi ni eneo la Jeshi. Lakini tutakaa pamoja hili ni Jeshi lenu la Wananchi wa Tanzania sio Jeshi la watu, sio Jeshi la kukodisha, ni Jeshi linalojali maslahi ya wananchi. Tutakaa kama tulivyofanya kwa Mheshimiwa Halinga sijui yupo na tumemaliza tatizo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya bomba la maji, utaratibu uliokubalika awali kati ya Wizara na wananchi ambao bomba la maji linapita limeonekana kuleta kero na usumbufu kwa Kambi ya *TMA* ambao ndio walengwa. Wizara inaangalia uwezekano wa kupata utaratibu muafaka kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ili kuondoa kasoro zilizojitokeza. Kulikuwa na hoja pia ya kuboresha utunzaji wa zana za vita. Wizara imezingatia, utekelezaji wake utakwenda hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha. Chuo cha Uongozi na Unadhimu kutengwa na *TMA*, uamuzi wa

kutenganisha Chuo hicho na *TMA* umekwishafanya na eneo lake limepatikana. Wizara inatafuta uwezo wa kifedha wa kujenga Chuo hicho sehemu mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuamua Chuo kiende wapi Morogoro au wapi ni la Wanajeshi wenyewe. Wameshaamua basi tuwaachie na mimi nikiwaingilia watashangaa sana watasema Profesa mzima hajui hata kufuata taratibu, sheria na kanuni? Sijui Mheshimiwa Lwakatare yeze atasemaje? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maombi ya kupeleka umeme katika Kambi ya JKT Oljoro. Napenda nimpongeze Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa kufutilia mambo kwa karibu sana. Waliandikiwa barua na Meneja wa Mkoa Arusha, naisoma: "Shirika la Umeme Tanzania. Aione Dr. Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Upelekaji umeme Oljoro JKT."

Ifuatayo ni taarifa fupi ya kupeleka umeme kituo cha Oljoro JKT. Mkao ulishafanya *survey* ya kupeleka umeme kwenye mradi huo laini ni ya msongo wa 33kv, urefu wa laini ni kilomita 10, gharama za mradi huo ni Sh.110,708,381.00 kutokana na makadirio ya mwaka ya 2002. Mradi huu haukuweza kufanyika kutoka na ufinyu wa bajeti. Mradi wa kupeleka umeme Oljoro sasa umewekwa kwenye mradi wa *Electricity Power IV phase II* ambao unategemewa kuanza mapema mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bwawa la kuogelea *TMA*, ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge ni mzuri na wa msingi, Wizara yangu itaufanyia kazi. Kuhusu kufyeka barabara za mipakani, Wizara yangu inafahamu umuhimu wake na kwa kushirikiana na Wizara nyininge husika zitashughulikia suala hili. Hoja nyininge iliyotolewa ni kuimarishe Vituo vya Afya jirani na maeneo ya Jeshi. Ushauri huo unakubalika na Wizara yangu itashirikiana na vyombo husika kuona uwezekano wa utekelezaji wake bila kuathiri huduma za walengwa ambaa ni Wanajeshi. Kuhusu JKT kuwa chimbuko la ajira kwa vyombo vya ulinzi na usalama. Kama nilivyosema hilo ni agizo la Amiri Jeshi Mkuu na lazima lитеkelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza malipo ya *Ration Allowance* kwa wapiganaji, Serikali inatambua kuwa kuna upungufu unatokana na malipo ya *Ration Allowance* yanayotolewa hivi sasa. Wizara yangu inafuutilia suala hili ili kupata ufumbuzi kulingana uwezo wa kifedha wa Serikali. Kuhusu Serikali kuimarishe Idara ya Ujenzi JKT ili kufikia Daraja la I. Nawapongezeni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua uwezo wa JKT hasa SUMAJKT. Ushauri uliotolewa ni mzuri na unazingatiwa na Wizara yangu na tutahakikisha kwamba tutawasiliana na wahusika na kusaidia SUMAJKT kupanda daraja kutoka Daraja la III hadi la I. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarishe Jeshi la Mgambo, Wizara yangu imekamilisha rasimu ya pili ya sera ya Mgambo. Vitambulisho vya Mgambo vitaanza kutolewa mwakani. Hoja nyininge ambayo ametoa kwa kauli Mheshimiwa Anne Kilango (Malecela) ni kuhusu ukarabati wa Makambi, ushauri huo kama nilivysoma katika hotuba yangu unakubalika na Wizara yangu inaendelea na jitihada za kuboresha makazi ya wapiganaji wake kwa kutumia uwezo wa kifedha uliopo kukarabati majengo na miundo mbinu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa miaka mingi suala hili lilisaulikia tulianza mwaka jana na Ihumwa sasa tuko Sopa na tunakwenda kukamilisha nyumba 331 na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ametusaidia sana. Sasa tumefikia ukingoni kukamilisha mazungumzo na *NSSF* kupata Sh.20 bilioni ili tuweze kuwarudisha Wanajeshi wengi sana katika Kambi. Jitihada zinafanywa lakini kama mnataka tutaacha hilo tutahakikishe kwamba Wanajeshi wanapata zana na vifaa waendelee kuishi uraiani...

WABUNGE FULANI: Aaah!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Ndio! "Kupanga ni kuchagua". Tunakwenda taratibu lakini hata hivyo mngetupongeza kwa sababu kuna jitihada. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo ya vyombo vya usafiri na vifaa vya ujenzi, mikopo hutolewa na vyombo husika kwa makubaliano kati ya vyombo hivyo na mkopaji. Wizara ina jukumu la

kuthibitisha uwezo wa kifedha wa mkopaji kwa kuzingatia mshahara wake kutoka dhamana. Ni jukumu la mkopaji na vyombo vilivyokopesha kuhakikisha mkopo unatumika kwa lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niwahakikishieni kwamba pamoja na hayo yote maduka yetu na mimi nimetembelea maduka yote mpaka Makambako kama Makambako kuna duka nimefika, Mheshimiwa Nyimbo, ndiyo, tumeagiza kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha tutahakikisha kwamba maduka ambayo hayatazingatia maagizo tunavunja mikataba na maduka hayo kwa kuwa tunesema walete vifaa nya ujenzi ambavyo vitasaidia Wanajeshi.

Mheshimiwa Lawrence Gama amenipa agizo kwamba nitamke jinsi Askari walioigana Vita Vikuu katika Jimbo lake jinsi watakavyosaidiwa na pesa walizopata. Kuna kitabu, Serikali ilitoa tamko tulieleza na ninamuomba sana tusiendeleze mjadala nitamkaribisha, nitamwonyesha kwa sababu ya muda. Lakini suala hili sio la Wizara ya Ulinzi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa Waziri Mkuu aliagiza mambo ya kufanya na aliagiza kutokana na uamuza wa Rais wa Awamu ya Pili na tumetekeleza mengi lakini tatizo la malipo haya ni matatizo katika uongozi. Wanagombana na wangemaliza ugomvi hata fedha ambazo zilikuwa zimekusudiwa zingeshaletwa. Mimi nimefanya jitihada kukutana nao mara kwa mara. Sasa nitamwomba tu tusaidiane katika suala hili maelezo yote ninayo, nilitoa tamko hapa Bungeni na hata mimi katika Jimbo langu kuna malalamiko kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shaibu Hamad Zubeir alizungumzia kuhusu matengenezo katika hospitali ya Bububu. Sasa nataka kusema pamoja na wale waliochangia kwa maandishi, hatubagui Jeshi upande wa Zanzibar. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni Jeshi la Jamhuri ya Muungano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1964 baada ya Muungano jeshi lilizaliwa na kutokana na historia aliyosema Mheshimiwa Lawrence Gama vijana wa *Afro Shirazi* na vijana wa *TANU* na wale wanajeshi wachache ambao walichaguliwa ndiyo walianzisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Pia siku Jeshi la Ulinzi lilipozinduliwa waasisi wa Taifa letu Mzee Amani Abeid Karume na Mwalimu walikuwepo. Sasa Jeshi la Ulinzi halina Tanzania Bara wala Tanzania Zanzibar. Viongozi wa Zanzibar wapo huku, wengine wameshaoa huku na hawataki kuondoka wamebaki hapa Tanzania bara. Ni utaratibu wa kijeshi, unapandishwa cheo kutokana na utaratibu na vigezo. Sasa kama ingekuwa hivyo kiholela holela jeshi hili lingekuwa ni jeshi la ajabu hata Idd Amini tusingeweza kupambana naye. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa fedha zilizokwenda Zanzibar na Mheshimiwa Nhunga naomba unisikilize, Bububu walipelekewa shilingi 11,000,000/= na Potowa walipelekewa shilingi 6,600,000 kwa ajili ya ukarabati wa majengo na uwekaji wa umeme. Lakini tatizo hawaajaleta taarifa. Fedha za kijeshi huwezi kupelekewa hivyo. Ndiyo, usipoleta taarifa utaulizwa. Kama fedha zimepotea utaadhibiwa. Bububu mwaka huu wa fedha wametengewa shilingi 20,000,000/= wameshapelekewa shilingi 5,000,000/= mwezi Julai, tarehe 3 ili kuendelea na ukarabati na ujenzi. Potowa wameshapelekewa shilingi 500,000 licha ya kwamba hawaajaleta taarifa ya shilingi 6,600,000=/. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mzee Zubeir tulikwenda na wewe kutembelea pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, akaniahidi tatizo la maji atalisaidia na wewe ulikuwepo. Sasa mimi ambalo naweza kufanya ni kufuatilia, nipo tayari na hii itakuwa ni safari ya sita natembelea Zanzibar (Unguja na Pemba). Kuhusu malipo ya wazabuni wahusika. Malipo yao yanashughulikiwa kwa kufuata taratibu zilizowekwa lakini kama kuna mtu amepunjwa na wengi nimeshawalipa, walete taarifa maana jeshi lina utaratibu wake. Mimi nitakukubalia ndiyo nitatekeleza, lakini lazima utaratibu wake nitafuata mkondo wake na nikisema hapana nitaonekana mtu wa ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama za tiba katika hospitali ya Bububu. Hii ni sera ya Taifa kuhusu kuchangia gharama za tiba. Lakini uwezo wa kumudu gharama hizo za tiba, majibu haya yanahitaji ufanuzi kutoka kwa Wizara kadhaa. Hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge anione kabla ya kikao kwisha kwa maelezo zaidi, aidha twende naye ama mimi mwenyewe nitafuatilia kuona naweza kulimaliza vipi tatizo hili. Kuhusu uhaba wa madawa katika *Unit Aid Station*. Mfumo wa kutoa madawa katika *Unit Aid Station* unaeleweka na unakidhi mahitaji. Lakini kama kuna matatizo tutafanya tathmini. Kuhusu kuweka uzio katika maeneo ya makambi. Utekelezaji wa kuweka uzio katika maeneo ya makambi

upo katika mipango yetu ya maendeleo ya uboreshaji jeshi wa miaka kumi na tano, ni distance kweli kweli. Kuhusu ujenzi wa barabara ya Bububu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge italifuatilia suala hilo ili kutafuta ufumbuzi muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa vikosi vya SMZ. Upo ushirikiano mzuri kati ya JKU na JKT katika mafunzo mbalimbali. Hivi sasa wapo Maofisa wapiganaji kutoka JKU wanajifunza taaluma mbalimbali katika makambi ya JKT. Mafunzo mengine kwa majeshi kama KMKM na Navy yanahitaji kuangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Sera juu ya uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la umeme katika Kambi ya Potoa nimeshalizungumzia. Baada ya kusema hayo sasa nataka nizungumzie

WABUNGE FULANI: Toa hoja, toa hoja.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Naomba mniruhusu nizungumzie hili kwa sababu jinsi lilivyosemwa, nikiwa kama Waziri wa Ulinzi na Mtanzania na Waziri mwenye dhamana nisiposema nikiulizwa na Amiri Jeshi Mkuu sitakuwa na maelezo.

Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib amezungumzia mengi kuhusu kubaguliwa kwa vijana wa CUF. Lakini nakubaliana naye kuwa kazi ya jeshi letu ni kulinda kwa silaha kwa lengo la kupambana na maadui wa nchi. Yeye pia anatambua hilo kwamba ni kazi ya jeshi. Jukumu lake la msingi ni kupambana na maadui wa nchi kwa maana hiyo jeshi hili halitekelezi majukumu yake kwa msingi wa itikadi ya kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ielewewe kuwa lina kanuni, sheria na utaratibu na mpangilio wa majukumu yake kwani kazi ya jeshi ni kulinda, kutekeleza na kudumisha utiifu kwa mambo yafuatayo:-

- * Kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)
- * Kulinda Muungano. (*Makofi*)
- * Kulinda Umoja wa Taifa. (*Makofi*)
- * Utiifu kwa Amiri Jeshi Mkuu na wasaidizi wake wote na wananchi kwa ujumla hiyo ni kazi ya jeshi bila kujali wewe ni Mpinzani au Chama Tawala. Kiongozi Lwakatare analindwa, kama mtu atakayemchezea, analindwa hata mpaka kule kwake Kagera, analindwa. (*Makofi*)
- * Ni jeshi la ulinzi ambalo linalinda mipaka ya nchi yetu, uhuru wa nchi yetu na watu wake wote, ulinzi wa viongozi wakuu na mali ya umma na ulinzi wa zana za kivita na vifaa vyote vya kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira jeshini. Jeshi la Ulinzi linapokea vijana walioteuliwa na mamlaka husika kuanzia Vijijini, Kata, Wilaya hadi Mkoani baada ya kuchujwa ipasavyo. Wanachujwa kuhusu tabia, uzalendo, uraia, uaminifu, ukakamavu na hali ya afya.

Baada ya hapo hupokelewa jeshini kama kuruta, wanaendelea kupikwa kweli kweli na wale ambaao hawafai wanaachwa. Sasa hili jeshi letu halina siasa, lakini linamtambua Amiri Jeshi Mkuu, Rais wa nchi wanamtii na viongozi, lakini kwa sasa viongozi hao ni wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA
FUNGU 38 - NGOME

Kif. 1001 - *Administration and General ...* Shs. 125,672,448,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge nimewaona wawili sasa naomba radhi sana ni yale yale ambayo mmeyafanya kwa Waziri yule. Unapomwambia kwamba omnia fedha, kaa, *you are being unfair to him*. Ana muda amba amepangia saa nzima ya kueleza na kutoa majibu. Sasa unapomwambia nenda kakae, omnia fedha, *we are being unfair* kwa kweli kwa hawa watu. (*Makofî*)

Lakini kwa sababu wameshasimama Waheshimiwa Wabunge wawili naomba niwape nafasi ili waweze kutoa hoja zao. Mheshimiwa Dr. Lamwai, utafuatiwa na Mheshimiwa N'hunga.

MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mshahara wa Waziri. Naomba nianze kwa kusema kwamba sina haja ya kumnyima mshahara hata senti tano.

MWENYEKITI: Kifungu gani Mheshimiwa?

MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI: Kifungu 1001.

MWENYEKITI: Hebu, kuna mshahara wa Waziri hapo?

MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI: Samahani kifungu 1001 *Administration and General*. Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Kama unataka kuhoji ...

MHE. MASUMBUKO R.M. LAMWAI: Nahoji as if question?

MWENYEKITI: Mheshimiwa hii ni Ngome Waziri hayumo humu. Kuna Majenerali wa Ngome tu humu.

MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI: Sawa, basi nitasubiri.

MHE. JUMA S. N'HUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 1001, kifungu kidogo cha 250100....

MWENYEKITI: Mshahara wa nani?

MHE. JUMA S. N'HUNGA: Majenerali.

MWENYEKITI: Wa Mkuu wa Jeshi?

MHE. JUMA S. N'HUNGA: Ndiyo.

MWENYEKITI: Haya endelea.

MHE. JUMA S. N'HUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba niulize maswali madogo mawili. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja alisema kwamba hospitali ya Bububu imepelekewa fedha lakini majibu hayajaja. Je, jukumu la kuleta majukumu ni la nani, la Wabunge ama la Wizara kufuatilia? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, milioni ishirini zilizotolewa Mheshimiwa Waziri atalihakikishia Bunge hili kwamba ukarabati wa Hospitali ya Bububu utamalizika kwa sababu suala la Hospitali ya Bububu tumekuwa tunazungumza kila Bunge zaidi ya miaka mitano sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ningeomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli kuhusu ukarabati wa kambi ya Mtoni hali ikoje na atasaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Nitampa nafasi lakini nishauri tu, nilidhani ungebakiza hiyo kwenye mshahara wa Waziri, je, unaonaje? Lakini ni ushauri tu nitakupa bado nafasi.

MHE. JUMA S. N'HUNGA: Nakubali Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitakuwa nishauliza, sitauliza tena. Kwa hiyo, likifika *automatic* Mheshimiwa Waziri aanze kujibu.

MWENYEKITI: Haya ikifika kwa Waziri basi atajibu.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 39 - JESHI LA KUJENGA TAIFA

Kif. - *The National Service Force* Shs. 25,353,594,700/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamatibila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 57 - WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

Kif. 1001 - *Administration and General* ... Shs. 3,848,797,800/=

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa N'hunga alishaeleza, kwa hiyo sasa nimpe nafasi Mheshimiwa Waziri kujibu yale ya Mheshimiwa N'hunga, halafu nitakupatia nafasi Mheshimiwa Dr. Lamwai.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba radhi sana Mheshimiwa Mbunge N'hunga, fedha ambazo zilikuwa hazijatolewa maelezo ni fedha za Potoa siyo Bububu. Fedha za Bububu zimetumika vizuri na tunawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kumhakikishia ye ye anajua mwenyewe, mimi nimeshakwenda Bububu mara nne kukagua ujenzi na nitahakikisha kwamba fedha hizo zinatumika ipasavyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuhusu suala la ukarabati wa Mtoni, nimesema Jeshi limeweka mikakati ya mpango wa kuimarisha jeshi wa miaka 15 na *book* hili ni kubwa sana. Kwa hiyo, kila kitu ambacho kilisemwa na Mheshimiwa Major Jesse Makundi tutaweka kwenye maandishi, nikitaka kueleza nitachukua muda mpaka kesho asubuhi. Sasa nitashughulika na wataalam na tutawaleteeni jibu kwa kila swali ambalo mmeuliza na hatua ambazo tutazichukua. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wakubali kwa matuamini hayo. (*Makofî*)

MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu uwanja wa kulenga shabaha uliopo Kunduchi Dar es Salaam. Mwaka wa 1996 nililalamika hapa Bungeni juu ya huo uwanja kuwa katika maeneo ambayo wanaishi raia na nimekuwa naendelea kulalamika katika maswali kadhaa ambayo nimeuliza hapa Bungeni. Leo pia katika mchango wangu nimekumbushia haja ya kuhamisha huo uwanja kwa sababu upo eneo ambalo ni hatari sana kwa usalama wa raia wakati askari wanalenga shabaha na tumeshakuwa na mifano Dar es Salaam kwamba risasi zimetoka kwenye uwanja wa shabaha na zimeuwa wananchi.

Sasa muda wote jibu lililokuwa linatolewa ni kwamba ni ukweli tazito hilo linatambuliwa na Serikali itachukua hatua za kuhamisha uwanja huo na badala ya kuwa na uwanja pale wajenge nyumba za Askari. Sasa imepita karibu miaka sita. Leo sikusikia jibu la Waziri kuhusiana na hoja hiyo. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli juu ya ule uwanja ambao ni mtego mkubwa sana kwa raia pale Kunduchi. (*Makofî*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza nilipokuwa najibu baadhi ya hoja na ninajieleza kijeshi huwezi kutoa kauli. Kuna utaratibu wa utekelezaji mambo katika jeshi, tutatoa maelekezo na amri kwa wanaohusika na tatalifanyia kazi. Lakini pamoja na hayo napenda kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dr. Lamwai kwa kazi nzuri aliyofanya japokuwa yeze hakutambua kuwa baadaye atakuja kuwa mwanachama wetu wa Chama cha Mapinduzi na Mbunge Mteuliwa wa Chama cha Mapinduzi, nampongeza sana. (*Makofi*)

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia kwamba eneo limeshapatikana. Sasa hayo ndiyo mambo ambayo nimesema hatuwezi kuyajibu hapa, lakini aniamini kama alivyoniamini nilipokuwa Mkuu wake wa Mkoa na nilipokuwa na Mzee wake. Kwa hiyo, hili tutawasiliana naye na siku uwanja utakapohamishwa yeze ndiye atakuwa wa kwanza kwenda kushuhudia na tutamwalika. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri je, kwa kuzingatia hatari iliyopo katika matumizi ya uwanja ule. Je, siyo jambo la busara matumizi yake yakasimamishwa kwa ajili ya kulenga shabaha kwa sababu ya usalama wa raia? Kwa sababu Jeshi pamoja na utaratibu wake pia lina wajibu wa kuhakikisha kwamba raia ni salama.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja na watu ambao waliojenga pale ni wavamizi. Eneo lile lilikuwa ni la Jeshi.

Sasa kutokana na kilio cha wananchi ndiyo hilo tunataka kufanya, lakini kusema kwamba tusitishe mazoezi ya jeshi kwa kutokupiga shabaha kwa ajili ya uvamizi, tunachoweza kufanya ni kuwaambia wananchi wakati wa mazoezi wasifike huko.

Namwomba sana Mheshimiwa Mbunge aeewe suala la jeshi siyo suala la mzaha. Leo tukisema kwamba tunasitisha, kesho tutasitisha kila mahali. (*Makofi*)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Shs. 62,094,600/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Shs. 23,047,000/=
Kif. 2001 - <i>Industries, Construction and Agriculture</i>	Shs. 118,924,900/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 57 - WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

Kif. 2001 - <i>Industries, Construction and Agriculture</i>	Shs. 24,010,000,000/=
--	-----------------------

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kuketi kama Kamati ya Bunge Zima na kupitia Kifungu kwa Kifungu Makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2003/2004 kwa ajili ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote, sasa naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubalike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kwa Mwaka 2003/2004
yalipitishwa na Bunge)*

(Saa 12.55 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 31 Julai, 2003 Saa Tatuu Asubuhi)